

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Nane - Tarehe 25 Mei, 2016**

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

**D U A**

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Maswali, tunaanza na swali la kwanza linalekezwa kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na linaulizwa na Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi.

Na. 229

### **Ujenzi wa Daraja Kata ya Ruhembe**

**MHE. JOSEPH L. HAULE** aliuliza:-

Serikali ilifanya tathmini na kuona umuhimu wa kujenga daraja kwenye Kata ya Ruhembe kwa shilingi milioni mia sita lakini mpaka sasa shilingi milioni 100 tu zimepelekwa kwenye Halmashauri ya Kilosa.

Je, ni lini kiasi cha shilingi milioni 500 kilichobakia kitapelekwa ili kukamilisha daraja hilo na kuwasaidia wananchi wa Ruhembe wanaozunguka umbali mrefu ili kupata mahitaji yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
aliijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizoidhinishwa na Serikali katika bajeti ya mwaka 2014/2015, kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Ruhembe ziliwa ni shilingi milioni 300 fedha zilizopokelewa hadi Juni, 2015 ziliwa shilingi milioni 100 ambazo zilitumika kwa ajili ya usanifu wa ujenzi wa daraja hilo. Mkandarasi aliyeomba fedha hizo anahitaji shilingi milioni 600 na hivyo kusababisha mradi huo kutotekelzeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2016/2017, zimetengwa shilingi milioni 700 ambazo zitatumika kujenga daraja hilo na kuchonga njia inayounganisha daraja hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Haule!

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naishukuru sana Serikali kwa kutenga bajeti ya daraja hili la Ruhembe kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017. Hata hivyo, kutokana na kilio na mateso makali pamoja na vifo vya watu wa Ruhembe ambao wamekuwa wakilia kwa muda mrefu, Serikali ipo tayari kuleta pesa hizi kule Mikumi katika robo ya kwanza ya mwaka 2016/2017?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari kutenga?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nimesema hapa tumetenga shilingi milioni 700 na hii milioni 700 Mheshimiwa Joseph Haule anachosema ni kweli, katika lile daraja tumpoteza watu wengi sana, takribani watu wanane hivi kwa mujibu wa takwimu nilizopata na mtu mmoja ambaye tumempoteza pale ni mtumishi wa Serikali katika Ofisi yetu ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, jambo hili sisi wengine tunalifuatilia na tunalijua vizuri sana. Ndiyo maana tumeona katika suala zima la bajeti, mwaka jana waliomba shilingi milioni 600, lakini kilichopitishwa Hazina ilikuwa ni shilingi milioni 300 na ilikuja milioni 100 peke yake. Katika msisitizo mwaka huu tukaona ile milioni 700 lazima irudi katika bajeti kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linatugusa sana kwa sababu, wananchi pale wakitaka kuvuka kufika ng'ambo ya pili ni mpaka watembee au wazunguke karibu kilometra 20. Tatizo ni kubwa, ndiyo maana ofisi yetu sasa imefanya harakati za kutosha kuhakikisha tunawasiliana na wenzetu wa TANROAD na hivi sasa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunapewa daraja la mudam lile la chuma kupitia ofisi ya TANROAD, si muda mrefu sana angalau liweze kufungwa wakati tukisubiri mpango mrefu kuhakikisha daraja lile linajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo sasa angalau tutapunguza kilio cha watu wa eneo lile na imani yangu kubwa ni kwamba, watu wa TANROAD kuanzia wiki hii sasa muda wowote watakwenda kulifunga ili kuondoa tatizo kwa wananchi wa eneo lile.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje swali moja la nyongeza.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali ya nyongeza. Kwa kuwa katika kipindi hiki cha mvua barabara nyingi sana zimeharibika, mfano, Wilaya ya Mpwapwa; Kata za Matomondo, Lembule, Mlima, Bereje, Mkanana, Londo, Chamanda, Majami mpaka Nana kule. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa kutenga fungu la kutosha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizo kwa sababu zinapitika kwa shida?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAMISEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na Mheshimiwa Lubeleje hivi karibuni tumekwenda Wilaya ya Mpwapwa pale kutembelea kuangalia baadhi ya huduma zikiwemo huduma za afya, huduma ya shule, takribani wiki mbili na nusu zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nimeona changamoto ya barabara katika maeneo yale, lakini nimesema katika kila mgawanyo wa halmashauri una fungu lake. Jukumu letu kubwa ni hii bajeti iliyotengwa, ikishapatikana basi iende kuweka miundombinu, kwa sababu utengaji wa bajeti ni jambo moja na utekelezaji wa bajeti ni jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutajielekeza kuhakikisha pesa yote iliyotengwa angalau iweze kufika katika maeneo kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu inarekebishwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lubeleje kwa sababu na mimi nilifika kule nimeona hali jinsi gani ilivyo naomba tushirikiane kwa pamoja kuangalia kile kitakachowezekana tuweze kukifanya ili mradi wananchi wa Mpwapwa waweze kupata huduma ya miundombinu ya barabara.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa sababu ya muda tunaendelea na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa.

Na. 230

### **Ujenzi wa Daraja Kata ya Ruhembe**

**MHE. DEOGATIAS F. NGALAWA** aliuliza:-

Serikali ilitoa ahadi ya kutengeneza barabara ya lami toka Itoni – Njombe – Manda na upembuzi yakinifu tayari umeshafanyika.

Je, ni lini ujenzi huo utaanza hasa ikizingatiwa kuwa barabara hiyo imekuwa kero kubwa hasa kipindi cha masika lakini pia ni muhimu kwa sababu ya ujilio wa miradi ya makaa ya mawe Mchuchuma na chuma cha Liganga?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa barabara ya Itoni – Ludewa hadi Manda yenye urefu wa kilometra 211.4 kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa barabara yameshaanza ambapo kwa sasa barabara inafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, usanifu wa kina kwa sehemu ya barabara yenyeye urefu wa kilometra 50 kuanzia Kijiji cha Lusitu hadi Kijiji cha Mawengi umekamilika na taratibu za kumpata mkandarasi wa kujenga sehemu hii ya barabara zipo katika hatua za mwisho. Ujenzi wa kiwango cha zege wa sehemu ya Lusitu hadi Mawengi umepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usanifu wa kina wa sehemu ya barabara iliyobaki, unatarajiwa kukamilika Julai, 2016. Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara hii kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngalawa.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Juu ya suala la upembuzi yakinifu wa barabara hii limeshakuwa ni la muda mrefu sana. Bahati nzuri tayari hata Mkandarasi alishapatiwana na tayari hilo tangazo lilishatolewa toka Desemba, 2015. Sasa leo hii mnapozungumza kwamba, process za kumpata mkandarasi zinaendelea ni mkandarasi gani tena mwingine huyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, imeshakuwa ni kawaida kwa Serikali kuwa inatoa utaratibu wa kwamba hiki kitu kitashughulikiwa muda fulani, lakini matokeo yake muda unapita na hicho kitu kinakuwa hakijafanyika. Sasa ningependa kujua kwa sababu 2016/2017 ni muda mrefu, ni muda ambao unachukua miezi 12, wananchi wa Ludewa wangependa wajue ni lini hasa itaanza?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa nilizonazo kama ambavyo nilisema katika jibu la msingi mkandarasi yupo katika hatua ya mwisho kupatikana. Vilevile ujenzi wa barabara hii atakumbuka kwamba, alisaidia sana Bunge limepitisha bajeti ya Wizara yetu na katika bajeti ile kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii, kwa hiyo, ujenzi utaanza katika mwaka ujao wa fedha unaoanza tarehe Mosi, Julai.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali moja la nyongeza Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Huko nyuma takribani kama miaka sita sasa kumewahi kutolewa ahadi ya kujengwa baadhi ya barabara katika Mji wa Karatu kwa kiwango cha lami na ahadi hii imekuwa ni ya muda mrefu na mara nyingi tumeuliza hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ituambie ahadi ile ilikuwa tu ni kuwahadaa wananchi ili watoe kura au mmeshindwa kutekeleza? Tunaomba jibu. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi zote za Serikali zinaonyesha dhamira ya dhati ya viongozi wote wanaotoa ahadi ya kutaka kujenga hizo barabara. Kinachotukwamisha zaidi ni uwezo wa kifedha na naomba nichukue fursa hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hicho kipande chake kitashughulikiwa kama ambavyo viongozi wetu waliahidi. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ritta.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa muda mrefu sana Serikali iliahidi kujenga barabara inayokwenda kwenye hifadhi la Ruaha National Park na nakumbuka nilishawahi kuleta swali hapa Bungeni na Mheshimiwa ambaye sasa hivi ni Rais alikuwa Waziri alijibu kwamba, kuna pesa zinatoka Marekani kwa ajili ya ujenzi wa hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mheshimiwa anijibu ni kwa nini, kwa sababu barabara hii ni muhimu sana kwenye Mkoa wetu wa Iringa.

**MWENYEKITI:** Uliza swali sasa.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba anijibu kwa sababu katika tengeo la bajeti ya safari hii sijalelewa vizuri, sasa atuambie ni lini barabara ile itajengwa inayokwenda kwenye Ruaha National Park?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, lini lini, lini!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, barabara hiyo hatujaiweka katika mwaka huu wa fedha unaoanza Julai, lakini namhakikishia ahadi hii kama ambavyo ilitolewa na Mheshimiwa Rais na viongozi wengine itatekelezwa kama ilivyoahidiwa kabla ya kipindi hiki tulichopewa cha uongozi kwisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, linalizwa na Mheshimiwa Emmanuel Papian John, Mbunge wa Kiteto.

Na. 231

### **Migogoro Mingi ya Ardhi Huko Kiteto Bainya ya Wakulima na Wafugaji**

**MHE. EMMANUEL P. JOHN** aliuliza:-

Kwa kipindi kirefu sasa kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi huko Kiteto baina ya wakulima na wafugaji:-

(a) Je, ni lini Serikali itaipatia Kiteto Mahakama ya Baraza la Ardhi ili kesi nyingi ziweze kusikilizwa hapo Kiteto?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupima ardhi yote ya Kiteto ili kila mtu afahamu mipaka ya eneo lake ili kuepusha mwingiliano wa maeneo usio wa lazima, itafanya hivyo lini?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali namba 231 la Mheshimiwa Emmanuel Papian John, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu naomba nifanye sahihisho dogo kwenye jibu la msingi isomeke mwaka 2015/2016 na siyo 2016/2017 kama ilivyoandikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu sasa Wabunge wafahamu kuwa lengo la Serikali la kuunda Mabaraza ya Ardhi katika kila Wilaya ni kusogea huduma za utatuzi wa migogoro karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara iliahidi kuunda Mabaraza nane likiwemo Baraza Nyumba katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kiteto ametoa jengo ambalo tayari limeshafanyiwa ukaguzi ili kubaini mahitaji. Wizara imekwisha nunua samani za ofisi na hata sasa inaendelea na taratibu za upatikanaji wa watendaji. Taratibu hizo zitakapokamilika baraza litaanza kazi mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, Novemba, 2014, kikosi kazi cha kushughulikia mipaka ya maeneo katika Wilaya ya Kiteto kiliundwa. Kikosi kazi hicho kilijumuisha wataalam kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI; Ofisi ya Takwimu; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na wataalam kutoka Halmashauri ya Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizofanyika zilikuwa ni kurekebisha mipaka ya vijiji 10; Kijiji cha Loltepes, Emart, Enguserosidan, Kimana, Kinua, Nhati, Nemalock, Ndirigishi, Krashna na Taigo) katika eneo lililokuwa limegombewa kuzunguka hifadhi ya Emboley Murtangos kukamilisha mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 10 ni pamoja na kupima mashamba 2,110 katika vijiji vitatu, Kijiji cha Loltepes mashamba 385; Kimana mashamba 1,250; na Nemalock 475 na kutoa elimu iliyolenga kutatua migogoro ya ardhi katika Wilaya ya Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii ni kazi endelevu na itakamilika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Emmanuel Papian.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kutokana na hali ya Kiteto ilivyo na wote mnafahamu, ningependa Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini angeweza kufika Kiteto na kuzungukia hayo maeneo kama Waziri wa Ardhi, aweze kuona na kufanya mikutano ya hadhara ili aweze kuzungumza na wananchi wamweleze kero zao zaidi ya hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naomba Wilaya ya Kiteto ipimwe maeneo yote kwa maana ya kila mtu ajue kipande chake cha ardhi ili kuepusha ile migogoro inayoendelea kwa sababu leo tunaendelea, lakini bado kuna vuguvugu la migogoro inayoendelea. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBANI NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ameuliza ni lini tutazungukia Kiteto na kufanya mikutano ya hadhara. Naomba nimhakikishie tu kwa sababu zoezi hili la migogoro utatuzi wake utafanyika kwa nchi nzima na kama ambavyo Wizara imeshatoa kitabu cha migogoro, hivyo, muda unakapowadia katika suala zima la kuanza kuzungukia maeneo hayo na Kiteto pia tutafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameulizia ni lini sasa ardhi yote ya Kiteto itapimwa. Kama Waziri alivyotoa kwenye bajeti yake tumeanza na wilaya tatu ambazo ni wilaya za mfano ambazo tunakwenda kuanza nazo kazi na wameshaanza katika Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la upimaji ni suala ambalo linagharimu pesa nyangi na kama tulivyoeleza wakati tunatoa maelezo wakati tunamalizia bajeti, tulisema kwamba, halmashauri pia zinapaswa kutenga pesa kiasi kidogo ili kuweza kuanza upimaji katika maeneo yake, wakati Wizara pia inajipanga katika kuhakikisha kwamba ardhi ya nchi nzima inapimwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa sababu ya muda tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Salma Mohamed Mwassa, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 232

### **Kumaliza Migogoro ya Ardhi Nchini**

**MHE. SALMA M. MWASSA** aliuliza:-

Kumekuwa na Migogoro mingi ya ardhi mjini na vijiji inayotokana na kutopima na kupanga matumizi bora ya ardhi:-

(a) Je, Serikali imejipangaje kupunguza au kumaliza migogoro ya ardhi?

(b) Je, lini Serikali itaandaa mipango Kabambe (*Master plans*) mijini na vijiji lili kuainisha matumizi bora ya ardhi na kuondoa migogoro ya ardhi nchini?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Mohamed Mwassa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Salma Mohamed Mwassa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b), napenda kutoa maelezo mafupi ya vyanzo vya migogoro kama ifuatavyo:-

Utwaaji wa ardhi bila fidia stahiki; taasisi za umma na binafsi kuwa na maeneo au mashamba makubwa bila kuyaendeleza na kuyalinda; utata wa mipaka kati ya vijiji na wilaya pamoja na hifadhi; uvamizi wa viwanja na mashamba; kutokuwepo kwa mipango ya matumizi ya ardhi; ongezeko kubwa la idadi ya watu na shughuli mijini na vijiji katika ardhi ile ile na kutoheshimu sheria na mipango ya matumizi ya ardhi na shughuli za makundi ya watu wengine kama vile wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza na kutatua migogoro ya ardhi, Wizara imekuwa ikitekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuandaa kitabu cha orodha ya migogoro ya Nchi nzima kinachoainisha vyanzo vyake ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa;

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu.

### **NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

- (ii) Kuwasiliana na Wizara zinazohusika na kilimo, mifugo na uvuvi; maliasili na utalii pamoja na TAMISEMI ili kutatua migogoro mtambuka;
- (iii) Kuandaa matumizi ya ardhi katika vijiji na miji ambako migogoro ya ardhi imekuwa ikijitokeza na kusambaza miongozo inayohusu sera na sheria za ardhi;
- (iv) Halmashauri zote nchini zimeelekezwa kuainisha viwanja na mashamba yasiyoendelezwa ipasavyo ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa;
- (v) Kuimarisha mfumo wa ki-electronic katika kutunza kumbukumbu;
- (vi) Kuimarisha ofisi za kanda ili kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi;
- (vii) Kuanzisha Mfuko wa Fidia ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utayarishaji wa mipango kabambe ya miji, Wizara imekuwa ikitekeleza mambo yafuatayo:-

- (i) Kuunda na kukamilisha program ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi Tanzania itakayotekelawa katika kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2015 mpaka 2025;
- (ii) Wizara inasaidiana na Halmashauri za Wilaya na miji 18 kwenye program ya *Urban Local Government Supporting Program* katika utayarishaji wa mipango kabambe; na
- (iii) Kujadiliana na Benki ya Dunia ili kuharakisha zoezi la utayarishaji wa mipango kabambe katika miji mingine 30 ya Tanzania bara.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwassa.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Pia nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuna migogoro ambayo hasa inatokana na tatizo la usimamizi mbovu wa sera. Kwa mfano, kuna matatizo yanayotokana na hawa Viongozi wa Serikali za Mitaa kuuza maeneo ya umma kama shule, zahanati, majeshi na hiyo inatokana na kwamba Serikali haijaweka zile demarcation au kutoa hati miliki katika maeneo hayo, kwa hiyo, hicho ni chanzo cha migogoro. Je, ni lini Serikali itapima haya maeneo ya umma ili kuondoa migogoro hii hasa kwa Jiji la Dar es Salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, fidia ni tatizo pia, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wanaanzisha Mfuko wa Fidia. Kuanzisha Mfuko wa Fidia tu sio suluhu ya mgogoro. Mgogoro wa fidia unatokana hasa na yule mlipaji kutokuwa na hela stahiki wakati anafanya uthamini. Je, ni lini sasa Serikali itasimamia kabla ya *schedule* ya kwenda kuthaminiwa na Mthamini Mkuu wa Serikali yule mlipaji wa fidia awe tayari ameshaweka hizo hela kwenye Mfuko wa Fidia? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza ameulizia suala la tatizo la watu kuvamia maeneo ya Taasisi. Hata kabla ya upimaji ambao unatakiwa kufanyika kwa nchi nzima, Wizara ilishaelekeza kwa halmashauri zote kuhakikisha kwamba, maeneo yote ya umma yaweze kupimwa na hii inafanyika katika Halmashauri zenyewe husika kwa sababu ni maeneo ambayo wako nayo na wanayatambua katika maeneo yao. Kwa hiyo, haya hayasubiri ule upimaji wa Kitaifa ambao unaendelea kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa ni Halmashauri zenyewe ziweze kulinda maeneo yake na kama hiyo haitoshi, tumekwishaanza zoezi kwa Dar es Salaam ambapo Wenyeviti wa maeneo husika wamepewa ramani za maeneo yao kuweza kutambua maeneo yapi ya wazi, yapi ya umma na yapi ambayo yanatakiwa kuangaliwa ili yasiweze kuvamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwakumbushie tu kuititia katika swalii la Mheshimiwa Mwassa, halmashauri zote zihakikishe kazi ya upimaji maeneo yanayomilikiwa na Taasisi mbalimbali ifanyike ili kuepusha migogoro ambayo inaendelea kutokea siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, ameongelea suala la fidia, nadhani tulishalijibu katika hotuba wakati tunazungumzia na bado nitaendelea kulijibu tu. Ni kwamba, Mfuko wa Fidia umewekwa pale ili kuweza kukaa tayari katika kuititia yale masuala ambayo yatakuwa yana migogoro ambayo haijatatuliwa katika ukamilifu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Wizara kazi yake siyo kulipa fidia katika maeneo ambayo yanatwaliwa na Wawekezaji au na watu binafsi katika maeneo hayo. Ni jukumu lao kuona kwamba analipa fidia, Wizara imetoa maelekezo, haitaweza kuitisha uthamini wowote utakaletwa, yale majedwali yatakayoletwa, kabla ya kujiridhisha kwamba kuna pesa ambayo imeshatengwa na ndiyo maana Mfuko huu utakuwa na bodi yake ambayo itafanya kazi zake katika kuhakikisha pia wanajiridhisha na kile ambacho Wizara

imeelekeza kabla ya fidia kulipwa au kabla ya watu kuondolewa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishawaelekeza kama Wizara, hakuna mtu kuondolewa katika eneo lake kabla hajalipwa fidia. Kwa hiyo, hilo ni lazima lizingatiwe kwa wale wanaokuwa na mawazo ya kutwaa ardhi za watu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea kwa sababu ya muda, swali linalofuata ni la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti, kwa niaba yake linaulizwa na Mheshimiwa Zainabu Matitu Vulu.

Na. 233

### **Upatikanaji wa Hati za Kimila na Hati Miliki za Ardhi**

**MHE. ZAINAB M. VULU (K.n.y MHE. ALLY S. UNGANDO)** aliuliza:-

Kuendana na kasi ya Mheshimiwa Rais kutaka kumaliza kabisa urasimu wa upatikanaji wa hati za kimila na hati za ardhi mpaka sasa bado ni tatizo kwa Wilaya ya Rufiji:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Afisa Ardhi Mteule?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba ina kila sababu ya kupeleka vifaa vyta kisasa vyta kupima viwanja na mashamba?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Wizara hiyo hiyo ya Ardhi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Jimbo la Kibiti, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kawaida, Afisa Mteule na ni Mwajiriwa katika halmashauri husika. Kabla ya kuteuliwa kuwa Afisa Ardhi Mteule, mapendekezo ya uteuzi huanzia katika halmashauri husika kutoa pendekoz ambalo linawasilishwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa husika ambaye na yeye ataliwasilisha pendekoz hilo kwa Kamishna wa Ardhi. Pendekoz litakapowasilishwa kwa Kamishna wa Ardhi, Kamishna atafanya uteuzi wa Afisa Mteule

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji afuate utaratibu huo nilioueleza hapo awali ili halmashauri yake iweze kupata Afisa Mteule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inatambua umuhimu wa kupima viwanja na mashamba hapa nchini. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imekuwa ikiziagiza halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya upimaji. Aidha, katika kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa vifaa hivyo, Wizara kuititia Benki ya Dunia ipo katika mchakato wa kununua vifaa vya upimaji ambavyo vitasambazwa katika Kanda nane za Wizara yangu ili halmashauri zote zilizopo ndani ya kanda hizo ziweze kunufaika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Vullu.

**MHE. ZAINAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

La kwanza, kufuatana na maelezo ya Wizara husika kwamba mashamba yasipimwe viwanja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Je, hawaoni kwamba wananchi watanyimwa haki zao kwa sababu mtu anapokuwa na mashamba yake ana ndugu zake, ana watoto wake, ana wake zake atataka awagawie maeneo ya kuweza kuijendeleza na kukwepa ujengaji holela katika miji yetu, Serikali haioni kwamba itamnyima haki huyo mhusika wa hilo shamba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kutokana na tatizo la mgogoro wa mipaka kati ya Ikwiriri na Nyamwage kwa maana ya Kata ya Mbwara na ni wa muda mrefu. Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuutatua mgogoro huo na kuwawezesha wananchi wa Wilaya ya Rufiji kuweza kuwa na mji mdogo katika Jimbo la Rufiji? Naomba majibu na tuambiwe lini wananchi hao watatatuliwa mgogoro huo na kupewa majibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kulingana na swali alilouliza kwamba mashamba yasipimwe, kutopimwa mashamba hayo kufanywa viwanja kutanyima haki ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuelewe kwamba tamko la Wizara lililotolewa ni kwa ajili ya faida na manufaa ya halmashauri zetu wenywewe kwa sababu watu wamekuwa wakitumia njia hiyo kujinufaisha katika kupima, kununua mashamba baadaye wanapima viwanja na wanaviuza katika bei

kubwa sana, square meter moja inauzwa 20,000 na kuendelea na ni baadhi ya Wabunge pia wamelalamika katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na wakati mwingine pia unaporuhusu hiyo, watu wanaanza kuanzisha miji ambayo haiko katika utaratibu wa mipango miji kulingana na mipango kabambe ambayo imewekwa katika maeneo hayo. Kwa hiyo, hatuwezi kuruhusu hilo liendele, kama kazi hiyo itakuwa iko ndani ya mpango wa Halmashauri inaweza ikafanyika hivyo ,lakini suala kubwa hapa ni kwamba, halmashauri zetu zinaibiwa au Serikali inaibiwa na haipati pesa. Hakuna tatizo lolote la yeye kupeleka mpango wake halmashauri na halmashauri ikafanya kazi hiyo ya ugawaji viwanja na mapato ya Serikali yakaingia kuliko yeye kudanganya kwamba anataka shamba baadaye anapima na kupunja wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı lake la pili, kuhusu mgogoro wa Kijiji cha Ikwiriri na Nyamwage, samahani Mheshimiwa kama nitakuwa nimeatajiba vibaya. Nyamage?

**WABUNGE FULANI:** Nyamwage.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Nyamwage! Naomba niseme migogoro hii iko mingi kama ambavyo tumeelekeza sasa inakuwa ngumu sana kwenda leo, kwenda Ikwiriri, kesho unarudi unaitwa tena kulekule katika eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunafanya uratibishi kama Wizara kuweza kujua migogoro yote hii ili timu inapokwenda kufanya utatuzi wa mgogoro huu wa Ikwiriri ikatatue na migogoro mingine katika maeneo hayo badala ya kwenda mgogoro mmoja baada ya mwingine ambayo inagharimu Serikali pesa nydingi ya mtu kwenda na kurudi kwa hiyo tutafanya utatuzi huu katika migogoro yote kama jinsi ambavyo tutakuwa tumeikusanya ambavyo tumeleta kitabu na bado mnaendelea ku-update taarifa zilizoko humu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mnaona muda, tunaendelea na swalı linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua, kwa niaba yake Mheshimiwa Riziki Mngwali.

Na. 234

**Athari Zinazosababishwa na Milipuko ya Baruti Inayofanywa  
na Kampuni ya CHIKO**

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI (K.n.y MHE. MAGDALENA H. SAKAYA)** aliuliza:-

Wananchi wa Kitongoji cha Twende Pamoja, Kijiji cha Igwisi, Wilaya ya Kaliua wamekuwa wakipata athari kubwa za kiafya kutokana na milipuko ya baruti inayofanywa na Kampuni ya CHIKO, kupasua mawe na kokoto kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Kaliua mpaka Kigoma:-

(a) Kwa nini Serikali isiwalipe Wananchi hao stahiki zao ili waondoke sehemu hiyo na waende kuishi maeneo mengine ambayo ni salama?

(b) Kijiji cha Igwisi kinanufaikaje na Machimbo haya ya Mawe ambayo yapo kwenye eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya CHICO inatekeleza mradi wa ujenzi wa barabara wa kilometra 56 kuanzia Kaliua hadi Kazilambwa. Kipande hiki ni sehemu ya barabara kuu inayounganisha wilaya ya Kaliua, Mkoa wa Tabora pamoja na Mkoa wa Kigoma. Ili kupata madini ya ujenzi wa barabara, Kampuni ya CHICO inachimba mawe na kokoto katika leseni ya uchimbaji mdogo PML namba 001290CWTZ iliyopo katika Kijiji cha Igwisi iliyotolewa na Wizara ya Nishati na Madini tarehe 12 Aprili, 2013 kwa TANROADS Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya uchimbaji wa mawe na kokoto inahusisha ulipuaji wa baruti inayoweza kusababisha madhara katika maeneo ya jirani. Ili kuepusha madhara kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo, tathmini hufanyika na kwa sasa tathmini ya wananchi 71 imefanyika na kati ya hao, wananchi 34 ni kwa ajili ya mazao na wananchi 37 ni kwa ajili ya makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya CHICO iliwapa fidia waathirika 71 jumla ya shilingi milioni 473.9 chini ya usimamizi wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuititia TANROADS.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Igwisi kinanufaika na Mradi huu ambapo kwa sasa eneo lao linapitika kwa kipindi cha muda mrefu bila kuwa na matatizo yoyote. Sababu nyingine ambazo zinachangia ni pamoja na kunufaika na uchimbaji huo kwa wannchi kuweza kufanya biashara katika maeneo hayo, lakini pia kwa Halmashauri kulipa service levy. Hivi sasa TANROADS inakusudia kulipa shilingi milioni 23 inachodaiwa kwa kipindi cha Aprili hadi Desemba, 2014.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mngwali .

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Pamoja na majibu hayo, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, ni kwamba kwenye jibu lake la msingi la (b) anazungumzia malipo haya ya 2014, ni lini basi atatuambia pesa hizi zitalipwa ili Halmashauri ya Kaliua iweze kufanya shughuli zake kwa kutumia fedha hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni la ujumla, kwamba miradi kama hii inafanywa katika sehemu nyingi za nchi, lakini mara nyingi pamoja na kufanya social na environmental impact assessment bado wananchi huachwa mpaka wakapata mateso ndipo Serikali ikaja kuwalipa baadaye. Je, Serikali inatuambia nini kwamba sasa watakuwa wanafanya malipo kabla ya athari kupatikana kwa wananchi? Atupe majibu ni lini. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya, yote ni lini lini. Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa malipo ambayo yalitarajiwa kulipwa kwa kipindi hiki cha 2014 yangekuwa yameshafanyika hadi sasa, lakini hadi sasa hayajafanyika. Napenda nimpe uhakika Mheshimiwa Mbunge kwamba, TANROADS imeshafanya mahesabu na imeshamwandikia sasa mkandarasi kwa ajili ya kuanza malipo. Kwa sasa tumejipanga TANROADS pamoja na wenzetu, wataanza kulipwa kuanzia Agosti hadi Septemba mwaka huu kulingana na upatikanaji wa fedha

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili kuhusiana na malipo kufanyika mapema. Kwa mujibu wa Sheria ya Madini ni kwamba kabla ya shughuli za madini hazijaanza kufanyika, kazi inayotakiwa kufanyika kwanza ni kufanya tathmini na tathmini ikishafanyika na malipo yakakubalika na wadau wakakubaliana kuhusiana na malipo ya fidia, kawaida malipo huwa yanafanyika kabla ya shughuli kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiri tu kwamba kwa sababu wakati wanaanza uchimbaji wa kokoto wa kwenye barabara hii, tathmini zilichelewa kukamilika, kwa hiyo, malipo hayakuanza kufanyika mapema. Hata hivyo, kwa taratibu

ambazo tunaanza kuanzia sasa, malipo yatakuwa yanafanyika kabla ya wananchi kuathirika. Kwa hiyo, malipo ya fidia yatakuwa yakianza kufanyika kabla ya shughuli za uchimbaji wa kokoto kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi hatuwezi kusema zitaanza lini kwa sababu walishaanza kuathirika na malipo hayajafanyika, lakini malipo yote ambayo hayajafanyika kwenye barabara hii, yatafanyika kati ya Septemba hadi Oktoba mwishoni mwa mwaka huu bila kuchelewa kwa ushirikiano wa wadau, TANROADS pamoja na Halmashauri ya Kijiji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwijage haraka swalii moja la nyongeza.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana. Kwa kuwa milipuko hii inaleta matatizo ya afya ya wananchi walioko karibu na sehemu ya mashimo hayo na kuacha mazingira yakiwa na mashimo. Je, ni lini Serikali itakuwa inahakikisha afya za watu hao zinakuwa sawa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa kifupi sana, lini mtahakikisha afya za wananchi haziathiriki.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane nae kwanza, kwamba, shughuli za madini hufanyika na kuacha madhara kiafya. Kuhusu ni lini, ni wakati wote shughuli za madini zinapofanyika tunatakiwa tuhakikishe kwamba afya za wananchi pamoja na wachimbaji zinabaki salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, swalii linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 235

### **Wanafunzi Kutojua Kusoma na Kuandika**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Matatizo ya wanafunzi kutojua kusoma na kuandika pamoja na kutofanya vizuri katika mitihani yao mara zote lawama zinakwenda kwa Walimu.

Je, Serikali imefanya utafiti wa kina na kuona kama Mwalimu peke yake ndiye anayeweza kumfanya mwanafuzi aweze kufanikiwa katika masomo yake?

## **WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufuatiliaji unaofanyika kupitia Wadhibiti wa Ubora wa Shule na wataalam mbalimbali wa elimu, imethibitika kwamba Mwalimu ana nafasi kubwa katika kumwezesha mwanafunzi kumudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu ili aweze kufanya vizuri zaidi katika masomo yake ya baadaye. Hata hivyo, ili Mwalimu aweze kufanya kazi yake kwa ufanisi na kumsaidia mwanafunzi ipasavyo, masuala mengine yanayopaswa kuzingatiwa ni pamoja na:-

Uwiano wa Mwalimu kwa wanafunzi katika darasa, upatikanaji wa vitabu, vifaa na zana stahiki, ushirikiano wa wazazi na jamii pamoja na mazingira rafiki ya kujifunzia na kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hayo, Serikali inachukua hatua mbalimbali za kuimarisha ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

Kwanza, kutoa mafunzo kazini kwa Walimu, Wadhibiti Ubora wa Shule na Wakuu wa Shule; kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara; kuhakikisha upatikanaji wa vifaa mbalimbali vyta kujifunzia na kufundishia kwa wakati; na kuweka mazingira mazuri ya shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa wazazi na jamii kwa ujumla kuwapa ushirikiano wa kutosha Walimu ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, napenda kutumia nafasi hii kuwashimiza Waheshimiwa Wabunge amba ni wawakilishi wa wananchi kuweza kuwashamasisha wazazi/walezi na jamii kwa ujumla kuhakikisha wanafuatalia maendeleo ya watoto wao mara kwa mara ili waweze kumudu stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu na kufanya vizuri zaidi katika masomo yao. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa majibu ya Serikali yanaeleza wazi kuwa kufaulu kwa mtoto kunategemea mwanafunzi mwenyewe, Mwalimu, mazingira ya kufundishia pamoja na wazazi. Sasa, je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba mazingira ya kufundisha na kufundishia yanakuwa bora na pia kutoa elimu bora kwa wazazi kwamba wao ni wajibu wao pia kuwasimamia watoto wao?

Swali la pili, kwa kuwa hakuna Mwalimu anayefanya kazi kubwa kama Mwalimu ya KKK wa darasa la kwanza na la pili kwani yeye ndiye anayetoa msingi wa elimu au mwelekeo wa mtoto wa maendeleo yake ya baadaye. Je, Serikali imejipanga vipi kuwapa motisha Walimu wa KKK kutokana na kazi kubwa wanayoifanya?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi kwa ufuatiliaji mzuri. Anawajali sana Walimu na ndiyo maana maswali yake kila siku yanalenga katika kuangalia Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia na ndiyo maana katika majibu yangu ya msingi nimeeleza kabisa kwamba, Serikali imekuwa inatoa mafunzo kwa walimu kazini na tumetoa mafunzo kwa walimu 22,697 kwa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu, hii yote ni katika kujenga mazingira mazuri na kumwezesha mwalimu. Vilevile Serikali imeandaa vitabu na iko inasambaza vitabu katika kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kwamba Serikali inafanya nini ili wazazi waweze kutambua wajibu wao. Serikali imekuwa ikihamasisha wazazi na ndiyo maana hata kupitia Bunge lako naomba pia Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono katika maeneo yenu tuhamasishe wazazi ili watambue kwamba elimu ndiyo kila kitu katika maisha ya watoto wao na hivyo Serikali itaendelea kutoa uhamasishaji kwa wazazi ili waendelee kutambua wajibu wao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la mwisho la nyongeza anauliza kwamba, Serikali imejipanga vipi kutoa motisha kwa walimu wa darasa la kwanza na la pili ambao wanakuwa na mzigio mkubwa wa kufundisha watoto. Serikali inatambua mchango wa walimu na naiyo maana nasema ukiangalia vipaumbele vyetu katika mafunzo kwa Walimu kazini tumejikita zaidi kwa Walimu hao kwa sababu tunatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nitumie nafasi hii kusema kwamba tunakusudia na kesho nitasimama hapa mbele yenu kueleza mipango yetu ijayo lakini tunakusudia kuweka utaratibu wa kuweza pia kuwatambua Walimu wa darasa la kwanza na la pili wanaofanya vizuri kwa sababu tumekuwa na utamaduni wa kuwatambua kwenye darasa la saba, kidato cha nne, lakini tunaweka utaratibu mahsus wa kuweza pia kuwatambua kwa sababu nayo pia ni motisha. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naelewa swali hili la msingi, swali moja tu la nyongeza Mheshimiwa Ester Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na uwepo wa Tume ya Vyuo Vikuu yaani TCU (*Tanzania Commission for Universities*), lakini tumekuwa na changamoto kubwa sana ya kuzalisha wahitimu wasiokuwa na uwezo wa kutosha katika mustakabali wa ujenzi wa uchumi wa nchi ya Tanzania. Swali, je, Serikali imejipangaje katika suala zima la kuzalisha wahitimu wenyewe uwezo, weledi wenyewe tija na maarifa kazini? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Serikali imejipanga vizuri kabisa kuhakikisha kwamba watu wasiokuwa na uwezo wanachukuliwa hatua stahiki na katika hili niseme tu wazi kwamba, Serikali itafanya uhakiki wa wanafunzi au tunaangalia upya vigezo vya wanafunzi kujiunga na vyuo vikuu ili tuweze kuchukua hatua mahsus.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kesho nitakuwa nawasilisha hotuba yangu, haya yote nitayaeleza kwa kina, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Ester upokee hili jibu lakini tumejipanga vizuri na mikakati yote nitakuja kuieleza hapa kesho.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini.

Na. 236

### **Kibali cha Kuvuna Msitu Sao Hill**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Wavunaji na watumishi wa msitu wa Taifa Sao Hill wanapata huduma za kijamii na mahitaji yao katika Jimbo la Mafinga Mjini na kwa kuwa msimu uliopita hakuna kijiji au mtaa hata mmoja uliopata kibali cha kuvuna msitu katika Jimbo hilo:-

(a) Je, Serikali iko tayari kutoa kibali cha kuvuna msitu kwa kila kijiji au mtaa ili fedha zitakazopatikana kutohana na vibali hivyo ziweze kusaidia shuguli za kuboresha huduma za jamii kama vile kuchonga madawati na kumalizia ujenzi wa zahanati?

(b) Je, Serikali iko tayari kutoa vibali vya kuvuna misitu kwa vikundi rasmi vya wajasiliamali ili kuwasaidia kukuza mitaji yao na kujipatia maendeleo ya kiuchumi?

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetolewa kama sehemu ya kurejesha hisani kwa jamii kutoka kwa kampuni ya misitu na viwanda vikubwa vya mazao ya misitu vilivyopo kwenye Jimbo la Mafinga na maeneo ya jirani?

### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugawaji wa malighafi kutoka katika mashamba ya miti unaongozwa na Mwongozo wa Uvunaji wa mwaka 2007 uliofanyiwa mapitio mwaka 2015. Aidha, Wizara yangu kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania imekuwa ikipokea na kuyafanya kazi maombi mengi ya vibali vya uvunaji vyenye uhitaji wa mita za ujazo nyingi kuliko kiwango kinachoruhusiwa ikilinganishwa na uwezo wa mashamba wa kutoa malighafi kwa viwanda vya uchakataji wa mazao ya misitu kwa mwaka. Kwa mfano mwaka 2015/2016, jumla ya maombi 4,986 ambayo yalihitaji mita za ujazo 15,454,214 yalipokelewa na kufanyiwa kazi. Hata hivyo, ni maombi 1,030 pekee yenye jumla ya mita za ujazo 740,800 yaliidhinishwa, ambacho ndicho kiwango cha ukomo kulingana na uwezo wa mashamba katika mwaka huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchache wa malighafi, Wizara imekuwa inatoa kipaumbele cha vibali vya uvunaji miti kwa viwanda vyenye mikataba na Serikali, mionganoni mwao ni baadhi ya viwanda vya Serikali vilivyobinafsishwa, viwanda vingine vikubwa na vya katil, ikifuatiwa na wavunaji wadogo wadogo, vikundi na taasisi za watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa ikitoa vibali pia kwa wadau na vijiji vinavyopakana na misitu kwa ajili ya shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa madawati. Kwa mfano, katika shamba la miti la Sao Hill katil ya mwaka 2010/2011 na 2015/2016 vibali vya uvunaji kwa vijiji 183 vyenye thamani ya sh. 2,820,000,000 vilitolewa. Vile vile, shamba la Sao Hill lilihifadhili miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi milioni 880 ikiwemo utengenezaji wa madawati katika vijiji 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uzoefu wa hivi karibuni Wizara yangu imeona haja ya kupitia upya mwongozo wa uvunaji wa mwaka 2007 kwa namna ambayo itazingatia manufaa kwa jamii jirani na misitu hiyo kama ilani ya CCM inavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu haina takwimu zinazohusu kiasi cha fedha zilizorejeshwa kama hisani kwa jamii kutoka kampuni na viwanda vikubwa vya mazao ya misitu vilivypo kwenye Jimbo la Mafinga Mjini na maeneo ya jirani. Aidha, ushauri unatolewa kwa Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafinga ili aweze kupatiwa takwimu hizo.

**MWENYEKITI:** Enhee! Swali la nyongeza, nadhani la msingi hapo kupitia upya mwongozo wa uvunaji misitu.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali inawauzia kiwanda cha Mgololo nusu ya bei 14,000 badala ya 28,000; je, Wizara iko tayari sasa kuwauzia pia wavunaji wadogo wadogo wa Mafinga na Wilaya ya Mufindi kwa ujumla nusu ya bei kama inavyouzia MPM?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa kumekuwa na ujanja ujanja mwangi katika suala zima la utoaji vibali na kama nilivyo sema jana tuko karibu na waridi lazima tunukie waridi; je, Wizara iko tayari sasa katika kutoa vibali, *itoe by name and by location* ili kusudi wakazi wanaozunguka msitu waweze pia na wenyewe kunufaika kwa kupata vibali hivyo badala ilivyo sasa orodha inaonesha kuna watu wanapata vibali lakini majina ya watu hao sio wanaozunguka msitu. Ahsante. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Engineer.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kuhusu nusu bei kwa kiwanda cha Mgololo na uwezekano wa kuuza kwa bei hiyo hiyo bidhaa hiyo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo au mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili hoja yake ni mionganoni mwa hoja kubwa, nzito zilizotolewa wakati wa mjadala wa bajeti jana na kwa sababu hiyo maandalizi ya majibu ya kina yapo kwenye majawabu ya ufanuzi wakati Mheshimiwa Waziri atakaposimama na nitakaposimama mimi. Sasa kwa kuokoa muda namwomba Mheshimiwa Mbunge asubiri wakati tutakapokuwa tunahitimisha hotuba jioni. Atapata majibu ya kina kuhusu swali hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili la ujanja ujanja na uwezekano wa kutoa vibali kwa majina na kwa maeneo; jawabu ni kwamba jambo la msingi hapo linalohitajika ni uwazi. Wananchi wangependa kuona uwazi zaidi kuliko ilivyo sasa kwamba tutakapotoa takwimu kwamba watu gani

wamepata mgao, basi ni vyema watu hao wakaonekana mionganii mwa jamii wazi wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nimetembelea kwenye shamba la msitu la Sao Hill moja ya mambo ambayo nilisema ni kwamba, kuanzia baada ya ziara yangu wakati utakapofika licha ya ule utaratibu wa kusubiri kuititia mwongozo mzima, hili moja ni la wazi kabisa kwamba tunakwenda kushirikisha Serikali tangu kwenye ngazi ya vitongoji na vijiji si tu kwamba kumtaja mtu mmoja mmoja lakini Serikali kwa ujumla wake kwa kutumia mfumo wake utashirikishwa katika zoezi zima la ugawaji wa malighafi hizi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa sababu ya muda tunaendelea Waheshimiwa, mengine mtaendelea kuchangia kwenye Wizara hii. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Engineer Justus Nditiye, linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mwamoto.

Na. 237

### **Kuboresha Chuo cha Wauguzi Muhamwe**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)**  
aliuliza:-

Katika Jimbo la Muhamwe kuna Chuo cha Wauguzi (MCH) ambacho ni muhimu sana katika sekta ya afya, lakini hakiko katika hali nzuri.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukiboresha chuo hicho na vingine vya aina hiyo ili viweze kuijendesha na kulipa wazabuni wengi amba wanawadai?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Atashasta Justus Nditiye, Mbunge wa Jimbo la Muhamwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Uuguzi na Ukunga Kibondo kilichopo Jimbo ka Muhamwe, ni kati ya vyuo sabini na saba ambavyo vinamilikiwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Vyuo hivi vilijengwa kwa nguvu ya Serikali na wadau wa maendeleo miaka michache baada ya uhuru, kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa watumishi wa afya na kipaumbele ikiwa ni afya ya msingi kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Wizara kujikita katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) mwaka 2007, tumekuwa tukitenga fedha za maendeleo kwa ajili ya kufanya ukarabati na upanuzi ili kukidhi ongezeko la udahili wa wanafunzi kwa lengo la kufikia udahili wa wanafunzi 10,000 kwa mwaka na pia kushirikisha sekta binafsi katika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili la udahili limeongeza mahitaji ya kupanua miundombinu na pia kufanya ukarabati wa mara kwa mara kukidhi ongezeko hilo. Wizara imekuwa ikitenga fedha za ukarabati kupitia Mfuko wa Fadhili wa Pamoja yaani Basket Fund hadi mwaka 2006/2007. Kutokana na kusitishwa kwa fedha za basket mwaka 2006, majengo mengi ya Wizara hayakukamilishwa na kubakia magofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali imejikita katika kutenga fedha zake za ndani kukamilisha majengo hayo kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa mwaka wa 2016/2017, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni nane kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Vyuo vya Afya vya Serikali, ambapo Chuo cha Uugazi na Ukunga Kibondo kimetengewa Sh. 630,000,000)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya wazabuni, ni kweli Wizara inadaiwa na wazabuni mbalimbali ambao wamekuwa wakitoa huduma za vyakula vibichi, vya kupikwa na huduma zinazoendana na ukamilishaji wa huduma hiyo, ambapo malimbikizo ya madeni kuanzia mwaka 2009 hadi 2015 yalifikia jumla ya sh. 6,859,299,159.05. Madeni yote hayo yamehakikiwa na yanashiri upatikanaji wa fedha toka Serikalini ili yaweze kulipwa. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kuanzia mwaka wa masomo 2015, huduma hii haigharamiwi na Serikali tena bali sekta binafsi imepewa fursa kutoa huduma kwa kuzingatia taratibu zilizopo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swal, Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Kibondo ni Wilaya ambayo ilikaliwa na wakimbizi na kwa kuwa kuna majengo ambayo yamekaa kwa muda mrefu ya IOM ambayo Serikali ya Wilaya na Mkoa ilisharidhia kwamba yatumike kwa ajili ya chuo hicho. Je, Waziri haoni sasa ili kubana matumizi ya Serikali afike na kutoa ushauri ili yale majengo yatumike kwa ajili hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti swali la pili, kwa kuwa makampuni mengi ya ujenzi baada ya kujenga barabara yamekuwa yakiacha miundombinu ya majengo mazuri. Sasa haoni ni wakati muafaka wa kupunguza upungufu wa

wauguzi zikiwepo Wilaya nyingi pamoja na Kilolo kwa kuweza kuyatumia yale majengo vizuri ili Serikali iweze kupata manufaa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwamba nifike Kibondo ili nikashauriane na Serikali ya Mkoa ambao wameshapitisha azimio la kutaka kutumia majengo yaliyoachwa na IOM namwahidi nitafika mara baada ya Bunge la Bajeti kukamilika ili nishirikiane na Serikali ya Mkoa nione kwa ushirikiano na Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo wana dhamana ya mali na maeneo yote ya wakimbizi, ni nini Serikali itafanya ili kuwezesha azimio lao hilo mkoani kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusiana na majengo yaliyoachwa na miradi mbalimbali ya ujenzi; taratibu kwa kweli zimekuwa ni hivyo kama anavyopendekeza Mheshimiwa Mbunge. Hivyo, wafuate taratibu za kuzungumza ndani ya vikao vyao vya kufanya maamuzi kwenye halmashauri husika, ili walete mapendekezo Serikali Kuu tuone kama yanaweza yakapitishwa na wanaohusika na mradi huo kutumika kwa ajili ya shughuli ambazo wanazipendekeza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda haupo rafiki tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo, ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe.

Na. 238

### **Marekebisho ya Sheria ya Ndoa**

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE (K.n.y. MHE. TASKA R. MBOGO)**  
aliuliza:-

Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 inaanisha kuwa, mtu akifika umri wa miaka 18 huyo ni mtu mzima na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, Ibara ya 13 inasema umri wa msichana kuolewa ni miaka 15 na mvulana kuo ni miaka 18:-

Je, ni lini Serikali itafanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa, ili watoto wa kike wasiolewe na umri mdogo kama ilivyo sasa?

## **NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** ali jibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kumekuwa na mkanganyiko kati ya Sheria hizo mbili, hususan kuhusu umri wa kuolewa, kwani Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009 katika Kifungu cha nne imetafsiri mtoto kuwa ni mwenye umri chini ya miaka 18, ingawa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, Kifungu cha 13, kinaruhusu mtoto wa chini ya miaka 15 kuolewa. Serikali ilishaanza kufanya kazi marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 baada ya kupokea taarifa ya Tume ya Kurekebisha Sheria ya mwaka 1996 kuhusu sheria kandamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya kazi zilizofanyika ni pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria kuandaa Waraka Maalum wa Serikali (*White Paper*) kwa lengo la kukusanya maoni ya wananchi kuhusu marekebisho ya Sheria hiyo. Kwa sasa Waraka huo Maalum upo katika ngazi ya Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hii, Serikali pia, imefanya juhudzi nyingine, kama vile kutungwa kwa Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009, iliyofuta vipengele vya 161 mpaka 166 vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971. Ili kuweka tafsiri moja ya mtoto kuwa ni chini ya umri wa miaka 18. Hatua hii inaifanya sasa Sheria ya Mtoto kutumika katika mashauri mengi yanayohusu haki za mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa kutambua thamani na haki za makundi yote katika jamii Serikali imeweka Ibara Maalum ya 57 inayohusu Haki za Watoto katika Katiba inayopendekezwa. Hivyo, endapo Katiba inayopendekezwa itapitishwa basi taratibu zitafuata za kufanya marekebisho Sheria zote kandamizi kwa wanawake na watoto.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa, suala hili ni nyeti na linagubikwa na mambo mbalimbali ndani ya jamii ikiwemo imani mbalimbali za kidini, mila na desturi. Je, ni lini sasa *White Paper* hiyo itapitishwa katika makundi mbalimbali ya jamii, ili iweze kupata maoni yake mbalimbali na kuweza kutungwa Sheria inayoweza kumlinda mtoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali langu la pili; chini ya llani ya Chama cha Mapinduzi, kwa kuwa, mpaka sasa hivi elimu yetu ya mpaka sekondari ni bure. Je, Serikali sasa haioni kuna umuhimu wa kuongeza elimu ya kidato cha bure ikawa mpaka *form six* ambayo ni elimu ya lazima, ili tuweze kuvuka ule umri wa miaka 18 ukizingatia sasa hivi watoto wameanza kusoma wakiwa chini ya miaka minne mpaka mitano? Je, Serikali inasema nini kuhusiana na hilo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Elimu majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru kwa swali alilouliza Mheshimiwa Mbunge, napenda kumjibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba, kila safari tunaanza kwa hatua kwa hiyo, Serikali imeanza kutoa elimu bure na hatua ya kwanza tumeanza na elimu msingi mpaka kidato cha nne. Kuna changamoto ambazo zinajitokeza katika kutekeleza hii, kwa hiyo, tupate nafasi tutatue changamoto, lakini mawazo na mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge ni jambo la msingi ambalo Serikali italiangalia baada ya kuwa tumeweka vizuri hii ambayo tumeanza nayo kwa awamu ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bulembo!

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Ni lini Serikali italeta marekebisho yaliyoahidiwa na Mheshimiwa Mwakyembe wakati wa bajeti yake ili kuzuia ndoa za watoto wa shule?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa...

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu moja halijajibiwa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nayaunganisha yote mawili kwenye jibu langu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza mchakato wa white paper toka mwaka 2008 na lengo likiwa ni kutafuta namna ya kuwashirikisha wananchi kwa ujumla wao kwenye kufanya maamuzi juu ya suala hili ambalo limegubikwa na misingi ya dini, lakini pia limegubikwa na misingi ya mila zetu kwenye makabila mbalimbali hapa nchini. Kwa maana hiyo, suala hili Serikali imeonelea

isilichukue kwa haraka haraka na ndiyo maana ikaanzisha mchakato wa *white paper*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa bahati mbaya mwaka 2010 Mheshimiwa Rais, niseme kwa bahati nzuri pia, aliamua kuanzisha mchakato wa Mabadiliko ya Katiba na ndani yake akidhani kwamba, ile Tume itakapokuwa inakusanya maoni ingewezekana kupata maoni ambayo yangethusisha nia ya wananchi ya kutaka kufanya mabadiliko kwenye sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya baada ya mchakato ule kukamilika, maoni yanayohusiana na suala hili hayakuonekana kama ni miongoni mwa mambo ambayo yalipendekezwa na wananchi. Hivyo, sasa hivi Serikali kuitia Wizara ya Sheria na Katiba imeamua kuanza upya jitihada za kuipeleka mbele *white paper* ili kupata maoni ya wananchi na hatimaye tuweze kuchukua maamuzi kama Serikali.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Nina swalii dogo tu, nawaunga mkono wanaharakati wote kuhusu suala hili muhimu, sasa nauliza Serikali, je, itakuwa tayari kuingiza kipengele kwenye sheria ambacho kinazuia kuzaa kabla ya kufikisha miaka 18? Maana wapo watoto wanazaa wana miaka 13 au 14, lakini hawachukuliwi hatua yoyote. Je, Serikali itaweka kipengele kuzuia? Ahsante sana. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangala.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala lenye utata kidogo na katika hatua hii kwa kweli, hatujalifirkiria hilo. Naomba tuchukue wazo lake tulifanyie kazi tuone kama ni jambo ambalo angalau linaweza hata likafikiriwa kwa sababu lina utata sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge muda wetu wa maswali ndiyo huo. Basi, niende kwenye matangazo, nitaanza na matangazo ya wageni halafu ya kazi za leo. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; kwa upande wa wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Tuna wageni 18 wa Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe ambaao ni wanafunzi wa UDOM kutoka Mkoa wa Katavi, wakiongozwa na Ndugu Evaston Daniel, wako wapi? Haya karibuni sana. (*Makofij*)

Wapo wageni 25 wa Mheshimiwa Elias John Kwandikwa ambaao ni wanafunzi wa UDOM kutoka Ushetu, Mkoa wa Shinyanga, wakiongozwa na Ndugu Isangura Baraka. Karibuni sana wanafunzi. (*Makofij*)

Kundi la tatu ni wageni wawili wa Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, ambao ni Watumishi wa Ofisi ya Mbunge, kutoka Mkoa wa Kagera, ambao ni Ndugu Suleiman Bunzia, Katibu wa Mbunge na Ndugu Isaya Kazimoto, Dereva wa Mbunge. Karibuni sana. (Makofi)

Kundi la nne ni wageni 16 wa Mheshimiwa Esther Michael Mmasi, ambao ni Marais na Viongozi Waandamizi wa Serikali ya Wanafunzi Vyuo Vikuu vya Mkoa wa Dar-es-Salaam, wakiongozwa na Ndugu Leon Erasmo, Rais wa Serikali ya Wanafunzi *University of Dar-es-Salaam* na Ndugu Ignathio Mkumbo, Spika wa Bunge la Wanafunzi wa Chuo Kikuu, Ardhi. Wako wapi! Hawapo humu ndani!

Kundi la tano ni mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, ambaye ni Julius Moses kutoka Chunya. Karibu sana. (Makofi)

Pia kuna wageni tisa wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge, ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha UDOM. Karibuni sana. (Makofi)

Kundi la saba ni wageni watatu wa Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge, ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Saint John kilichopo hapa Dodoma wakiongozwa na Lukashinje Joseph. Ahsante. (Makofi)

Kundi lingine ni wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo hapa Bungeni. Hawa ni wanafunzi na Walimu 43 kutoka Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii Stadi – VETA, Mkoa wa Dodoma. Wako wapi! Enhee, hawa hapo! Karibuni sana. (Makofi)

Wageni watatu ambao ni Mawakala wa Kampuni ya Maji ya Udzungwa hapa Mkoani Dodoma, Udzungwa! Ahsanteni. (Makofi)

Mheshimiwa Keissy ana mgeni wake ambaye ni Mwalimu, Ndugu Abdallah Fungo anatoka Kirando, Nkasi. Karibu sana Mwalimu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio Wageni wetu, kama nimepitiwa na wengine mtanikumbusha kwa haraka haraka, lakini twende kwenye shughuli zetu za kazi kwa leo.

Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Wajumbe wake wanatangaziwa na Mwenyekiti wao Dkt. Mary Nagu kwamba, leo tarehe 25, saa nane mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo, chumba namba 229, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala.

Tangazo la pili la kazi, Kamati ya masuala ya UKIMWI, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo,

kwamba, leo saa saba mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo na kitafanyika katika Ukumbi wa Msekwa D, pale juu.

Halafu kuna hili Tangazo muhimu sana. Mheshimiwa Joseph Selasini, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote ambao ni Wakatoliki na wasio Wakatoliki kwamba, leo tarehe 25, saa saba mchana, baada ya kuahirishwa Shughuli za Bunge, kutakuwa na Misa Takatifu kwa Wakristo wote na hiyo itaongozwa na Paroko wa Kanisa Kuu Dodoma, mnaombwa kuhudhuria.

Hayo ndio Matangazo. Enhee! Mwongozo!

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Ngoja kidogo, maana! Enhee, Mwongozo! Mheshimiwa Matiko!

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) pamoja na Kanuni ya 47. Naomba nisiisome ili kuokoa muda!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba, Jeshi la Askari wa Magereza ni muhimu sana kwenye nchi yetu. Hivi ninavyoongea na wewe Askari hawa hawajaweza kupewa posho yao ya chakula ambayo ilikuwa ni 180,000/= ikasogezwa kuwa 300,000/=, posho hii ya chakula inatakiwa itoke tarehe 14 mpaka tarehe 16! Kwa mwezi uliopita walipewa mwezi huu tarehe tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba, hawa Askari Magereza wana matatizo mengi sana na mengine mliyashuhudia juzi ya makazi mabovu. Askari Magereza hawa hawapewi hata ile posho ya pango! Askari Magereza hawa hata wakistaifu hawawezi kuzawadiwa vile vyeo ambavyo wanapewa Maaskari wa Jeshi la Polisi na Wanajeshi kuwa Wakuu wa Mikoa au Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba, hawa Askari Magereza wakigoma wale wahalifu ambao mmewaweka kwenye Magereza mle Tanzania nzima, wakiamua kugoma na wale wahalifu wakatoka tutakuwa ni nchi ambayo haina amani sasa hivi. Leo hatuwathamini hawa Maaskari! Askari wa Polisi wameshalipwa, lakini Askari Magereza mpaka leo hawajaweza kupatiwa hiyo posho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetaka kupata Mwongozo wako Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali na nilishamwambia Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani takribani wiki sasa! Ni kwa nini hawaoni umuhimu wa kuhakikisha wanawapa Askari Magereza hawa posho ambayo ni haki yao tarehe 14 mpaka tarehe 16?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nami naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Bungeni kila Mbunge anaongelea tatizo kubwa sana la Walimu, hususan Walimu wa Sayansi na ndiyo sababu mwaka jana tulianzisha programu maalum ya Walimu wa Sayansi katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapoongea Walimu hao wameshindwa kuingia madarasani na leo ni wiki ya saba ambapo walitakiwa wafanye mitihani, wameshindwa kwa sababu Wakufunzi wao wamegoma kuwafundisha na hii ni kwa sababu hawajalipwa fedha kama Mkataba wao unavyosema. Jana wamefanya Kikao na Utawala wa Chuo bado tatizo liko palepale na hivi leo wameona kilio chao hakiskilizwi wakawa wanaandamana kuja Bungeni, wamezuiwa na Polisi pale UDOM. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili mimi kama Waziri Kivuli wa Elimu, niliongea na Waziri wa Elimu kumweleza tatizo hili toka wiki jana na akasema analifuatilia, lakini jambo hili halijapata ufumbuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kujua ni kwa nini Serikali haiwalipi Wakufunzi hawa ili waweze kuwafundisha watoto wetu amba ni Walimu wa kesho? Tunatarajia kupata Walimu wa namna gani kama Walimu hawa hawaingii madarasani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. (Makofi)

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) pamoja na Kanuni ya 69 ambayo nitaisoma:

“Mbunge anayependa mjadala unoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja “kwamba mjadala sasa uahirishwe” na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mjadala tunaoendeleanao uahirishwe tujadili jambo la dharura ambalo ni ukosefu wa sukari mtaani na Serikali imekuwa ikitoa kauli kila siku humu ndani, lakini hazitekelezeki. Sasa nawaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono kwa sababu, Bunge ndiyo chombo kwa ajili ya kuisimamia Serikali; wajadili jambo hili na watoe maelekezo kwa Serikali ni lini sukari iingie mtaani na wananchi waanze kutumia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche, hebu niambie Kifungu chako?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba Mwongozo kwa 68(7) pamoja na Kanuni ya 69 na ya 47, zote unaweza kusoma ziko sawa. Zote zinaweza ku-direct kwenye hili nililolisema! (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa maombi ya mwongozo. Nianze na Mheshimiwa Matiko na kwa kiasi fulani Mheshimiwa Lyimo, yanahusu watumishi wa umma kwa stahiki zao. Ninaposimamia kanuni nataka wote tuwe tunakwenda pamoja, jana Spika, alitoa mwongozo kwa yale ambayo yanafanana fanana na hii. Kanuni ya 68(7) ni vizuri tukaisoma, kanuni hiyo huwezi ukaiunganisha na kanuni nyininge.

Wewe unachotaka kuomba kwa Kiti, unataka ujue jambo ambalo limetokea mapema na mapema tumeshalitolea mwongozo mapema siku hiyo. Tusianzishe haya kusema ni shughuli muhimu hapana, mapema siku hiyo ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni au taratibu za Bunge na majibu ya Spika, yatatolewa hapa hapa au baadaye.

Sasa kwa yote haya nataka nilisaidie Bunge na Wabunge wengine ambaeo watapenda siku za usoni kutumia kanuni hizi. Unaweza ukaingia kupitia kanuni ya 50 ukatoa maelezo binafsi kwa suala hilo kama linakusumbua sana au ukatumia kanuni ya 28(11) wakati wa adjournment motion jioni, unatoa tu hoja kama mlivyoona juzi Mheshimiwa Chumi aliitumia vizuri sana fursa hiyo. Kwa haya yote hii miongozo miwili iliyoombwa kwa vile Serikali iko hapa wataweza kuyatolea maelezo, lakini huo ndio mwongozo wangu wa kikanuni kwa hayo.

Mheshimiwa John Heche, umeomba mwongozo, kanuni ulizozitaja zinasimama peke yake, ulipaswa tu wewe mwenyewe unipeleke huko na mimi kama ilivyoandikwa kanuni hiyo nipime kama suala hilo linawezesha kusimamisha shughuli iliyombele yetu kama ulivyoomba. Ndiyo maana nilikuwa nakupeleka polepole, ukifika uko unasema mpaka Spika aone kwamba suala hilo kweli linahitaji njia hiyo na nasema kwa sasa suala hilo halihitaji. Nakubali

utaratibu wako kuzingatiwa lakini niliamulie kwamba sijaridhika kwamba tunahitaji kwenda kusimamisha shughuli zinazoendelea ili kujadili suala hilo. (Makofii)

Nimemaliza hilo, nina tangazo, Waheshimiwa Wabunge kwenye mashine zetu za usalama kuna Waheshimiwa Wabunge wamebadilishana funguo. Kuna ufunguo hapa sjui mwagine amechukua wa gari yake lakini najua leo hatoweza kuiendesha mpaka achukue hii. Tutawakabidhi pale maaskari mwende mkapatiwe. Huo ndio mwongozo wangu kwa hayo tuliyoyasema. Katibu!

**NDG.CHARLES MLOKA -KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha  
wa 2016/2017 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

(Majadiliano yanaendelea)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuna orodha yetu tangu jana tunaanza na Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda, atafuatwa na Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda na Mheshimiwa Aweso ajiandae.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara asubuhi ya leo. Wizara ya Maliasili na Utalii ni mionganini mwa Wizara mtambuka inapokuja mahusiano yake na wakulima, inapofika mahusiano yake na wafugaji. Nchi yetu ina ukubwa wa takribani kilomita za mraba 947,300. Kati ya hizo ardhi ambayo tunaweza kutumia kwa ajili ya kufuga, kulima, kujenga na shughuli nyingine za miundombinu ya kijamii ni takribani kilomita za mraba 885,800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilomita za mraba 61,500 ni kwa ajili ya water bodies, kwa ajili ya bahari, mito na maziwa. Kwa maneno mengine shughuli zote tunazotumia kwa ajili ya ustawi wa maisha yetu, tunategemea kilomita za mraba 885,800 ambazo wakulima wanazihitaji hizo hizo, wafugaji wanazihitaji hizo na hifadhi wanahitaji hizo hizo. Ukifuatilia hotuba ya Mheshimiwa Waziri unakuja kugundua asilimia 33 ya hizo kilomita za mraba nilizozitaja ndiyo mbuga na hifadhi za misitu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tunaendelea kuongezeka kwa idadi kila siku na ng'ombe wanazidi kuzaliana na kuongezeka kila siku. Katika hiyo 885,800 kilomita za mraba, kuna ukame unaikuta hilo hilo eneo, kuna mafuriko, lakini kuna shughuli nyingine za volcano kwa mfano kule Oldoinyo

Lengai ikipiga volcano pale huwezi kulima, huwezi kufuga. Kwa hiyo, ardhi bado inaendelea kupungua. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana hapa watu wamesema wafugaji wanahitaji malisho na hizi sababu nilizozitaja ndizo zinazowafanya wahamehame. Tumesahau kwamba na wakulima nao wanahamahama kutafuta chakula, kutafuta sehemu nzuri ya kulima kwa hoja hizo hizo kama za wafugaji. Tukisema leo tuangalie tu mgogoro kati ya wakulima na wafugaji kwenye sehemu ya malisho ya wanyama, tukienda kutazama mgogoro kati ya hifadhi na wakulima kwenye yale maeneo ya buffer zone kama maeneo ya Mto Kilombero, eneo lina rutuba nzuri wakulima wanakuja eneo la hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ukienda upande wa selous kule wakulima wamekata miti wanaingia eneo la hifadhi. Ukija Kilosa, Mikumi *the same*, kila sehemu utakuta mkulima anaongezeka kutafuta maeneo ya kilimo kwa sababu eneo analolima kwanza rutuba nayo inapungua, ikipungua rutuba aina yetu ya kilimo kwa sababu siyo kilimo cha kisasa tunakutana na matatizo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye upande wa mifugo, takwimu zinatuonesha tuna zaidi ya ng'ombe milioni 25 na hawa ng'ombe wanazaliana kila mwaka kwa zaidi ya milioni moja. Baada ya miaka 10 tutakuwa na ng'ombe milioni 35. Nashangaa humu ndani tunasema tuna wafugaji, mniwie radhi humu ndani tuna wachungaji hatuna wafugaji. Huwezi ukajiita mfugaji unahama pori moja unakwenda pori lingine na huwezi ukajiita mkulima, hatuna wakulima, tuna wabangaizaji wanaotafua maeneo kwa ajili ya kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri kitu kimoja, juzi nilisema hizi Wizara nne, tano zikae pamoja kwa ajili ya kupanga vizuri, tukisema leo tutenge maeneo kwa ajili ya ufugaji, ng'ombe wanazidi kuongezeka, ardhi bado ni ndogo na aina yetu ya ufugaji tunaona kabisa hatuwezi kuja ku-solve hili tatizo. Baada ya miaka 10 tuna ng'ombe milioni 35 tutawatengea maeneo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaondoa kule Ihefu tumewapeleka Lindi, yale maeneo Lindi yaliyopangwa kwa ajili ya wafugaji leo watu wanalima ufuta. Kwa tatizo lile lile wakulima wana matatizo, wafugaji wana matatizo. Sasa hili haliwezi likajibowi kwa Waziri kuja kutuambia hili tatizo atalimaliza. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tujadiliane hivi, lakini baada ya bajeti mimi niiombe Serikali, ikae Wizara ya Ardhi, Wizara ya Kilimo, Maliasili na Utalii na Wizara ya Mazingira. Lazima haya tuangalie, tunakwenda tunamsahau wa mazingira huyo, ukame ukija, tunamsahau wa mazingira huyo, mafuriko yakija na haya maeneo yanayotengwa yanatengwa kwa hoja za ikolojia. Tukisema tulime kote, tufuge kote, mwisho wa siku mvua tutakosa, nchi nzima itakuwa

jangwa. Kwa hiyo, hoja siyo hoja ya hisia, siyo hoja ya kusema mimi ni mkulima nataka wakulima wangu wakae vizuri, mimi ni mfugaji nataka ng'ombe wangu akue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku tutalima wote, tutafuga wote, tutashindwa sehemu ya kufuga, ardhi itageuka jangwa na hata tunaohama hama wakulima kutafuta maeneo mazuri ya hifadhi yeye udongo wa rutuba kwa ajili ya kupata mahindi mazuri, kwa ajili ya kupata maharage mazuri, ufuta, itafika muda haya maeneo mvua haitafika, na hiyo mito tunayotegemea kumwagilia nayo mvua haitakuwepo, maji hayatakuwepo, samaki hawatakuwepo. Kwa hiyo, sekta moja ikikorofisha itapelekea sekta nyingine kuharibikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kwa nia njema kabisa, tutajadili kila kona kuhusu Maliasili na Utalii kwenye eneo la migogoro ya wafugaji, kwenye maeneo ya matumizi bora ya ardhi, lakini hatutafika mwishoni kama hakutakuwa na mpango mkakati wenyе sura mbili. Kwanza mpango wa dharura, uitwe *transformation strategy*, kuwatoa wakulima wanaohama hama wawe centralized katika kilimo cha kisasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuwaondoa wachungaji wanaohama kuchunga chunga wawe centralized, wafuge ng'ombe wao vizuri wazaliane na wawe na tija. tukienda hapo tutafika mbele kwa haraka na ardhi yetu tutaitunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kosa moja tunalifanya, tunapoongelea vyanzo vya mapato na nguvu kazi ya Taifa letu tunatazama wakulima, tunatazama wafanyakazi tunasahau kuwatazama wafugaji kama sekta rasmi ambayo ipangiwe mipango kama tunavyopanga mipango kwenye maeneo ya kilimo. Tunamwangalia mkulima, yaani mfugaji anakwenda kwenda tu, ndiyo kwa maana leo yuko Lindi, keshokutwa anatoka, hatuwezi kwenda kwa staili hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali, wafugaji sasa kwa sababu sio wafugaji, tuwa-transform kwenda kuwa wafugaji, wawekwe kwenye utaratibu mzuri, tija tutaipata. Hatuwezi leo kusema tuna ng'ombe milioni 25, halafu pato hatulioni. Baada ya miaka 10 tutakuwa milioni 35 halafu wao wanazunguka tu nchini, haiwezekani hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kwa nia njema kabisa hizi Wizara nne zikae pamoja, zije na mkakati mkubwa, hii migogoro haitakuwepo na wala tusitoe hapa maneno ya kuwafurahisha wakulima, kuwafurahisha wafanyakazi ili migogoro itulie, haitatulia. Ardhi ni ndogo sana, msijidanganye mnatoka hapa mpaka Dumila mnaona yale si mapori, yale ndiyo kwa ajili ya kuleta *vertilization*

ni AC ile ya kuleta hali ya hewa nzuri. Sasa siku mki-clear ile miti, cha moto mtakiona. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, atafuatiwa na Mheshimiwa Aweso na Mheshimiwa Janet Mbene ajiandae.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Wizara hii, lakini kabla sijaanza hivyo naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa neema, ameniwezesha leo kwa afya njema kusimama mbele yako na kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali yangu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Dkt. John Pombe Magufuli kwa mwanzo mzuri aliouanza. Tunaionba Tanzania na Watanzania wengine wote bila kujali vyama, tumuunge mkono kiongozi huyu, ana dhamira ya kweli na tukimuunga mkono tutafika mbali. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu nitajikita zaidi kwenye sekta ndogo ya wanyamapor na migogoro inayoendelea baina ya mapori haya tengevu au mapori ya akiba na vijiji ambavyo vinapakana. Wenzangu wameongea sana, nitaongea kwa vielelezo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtakumbuka mwaka 2009 wakati tunarejea Sheria ya Wanyamapor, Bunge hili lilitoa maelekezo kwa Serikali na yalikuwa mawili, kwamba, kwa kuwa sheria zamani ilikuwa inaruhusu matumizi ya binadamu katika mapori haya ya akiba, mapori tengevu, lakini sheria ile baada ya kurejewa hairuhusu tena. Kwa hiyo, ilikuwa la maangalizo mawili, Serikali ilipewa kazi wakaifanye, lakini mpaka leo bado linasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza waangalie umuhimu wa uendelezaji wa mapori tengevu hayo na mapori ya akiba. La pili, urekebishaji wa mipaka, lakini naweza kusema na wote tunashuhudia mpaka leo Serikali hawajafanya. Naomba nimwombe ndugu yangu, Profesa Kaka yangu, yeye amebobea kwenye mambo haya na hapa kama upele umepata mkunaji, hembu athubutu kufanya haya mawili. Kwa kuwa mazingira haya wananchi tunalalamika, Serikali wanashindwa kuchukua hatua, nitatoa mfano kwanye pori tengevu la Kilombero. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 baada ya kusitiza kusukuma sana ndiyo kidogo walijaribu kuweka mipaka, kurejea ile mipaka ya pori tengevu baada ya marekebisho ya ile Sheria ya Wanyamapor 2009, lakini walichofanya

wamemega ardhi ya vijiji na ndiyo maana mgogoro kule bado unaendelea. Maeneo ya Vijiji vya Igawa, Kiwale, Lupemenda na vijiji vingine eneo lile wamekuja kurekebisha ile mipaka wamemega ardhi yao, wananchi wale wanapotumia ardhi yao kiuhalali, ndiyo migogoro kila siku inaendelea na wananchi wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama haitoshi, badala ya kurekebisha mipaka mrudishe ardhi ile sasa kwa Serikali ya vijiji eneo lile mkatengeneza kitu kinaitwa *buffer zone*. Buffer zone kwenye eneo lile la bonde la Mto Kilombero kwenye Wilaya zile mbili; Malinyi na Ulanga ina range inatoka kilomita moja, maeneo mengine mpaka kilomita 12. Ukubwa wote huo wanaita buffer zone, matokeo yake sasa mmeingiza vijiji 18 na vitongoji karibu 22, vijiji na vitongoji hivyo vimesajiliwa, watu wanaishi kihalali, kuna shule za msingi, kuna mashamba, wananchi wanaishi kule kihalali, lakini wanaishi kila siku kwa hofu. Hawana amani, wanashindwa kuijendeleza kwa sababu hawajui hatima yao ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Kijiji cha Kiswago, kuna Kitongoji cha Salamiti, kitongoji kile kinashindwa kuendeleza shule ya msingi, watoto inabidi watoke kule kilomita 18, mtoto huyu wa shule ya msingi miaka saba aende mpaka shule ya msingi Kiswago kwenda na kurudi kilomita 36 kwa siku. Matatizo yote haya ni kwa sababu bado wameng'ang'ania, bado hawataki kutoa uamuzi ili maeneo ambayo wametenga kama *buffer zone* watayarejesha kwenye ardhi ya kijiji ili wananchi waendeleze pale kwa maendeleo mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema na mara ya mwisho na mpaka Bunge liliopita watani zangu majirani walikuwa wananiita mzee wa buffer zone na nitaendelea kwa sababu Serikali bado kila wakiambiwa hawasikii. Mara ya mwisho kuuliza swali hapa Bungeni 2015 mwezi wa Nne, niliuliza swali hapa nikitaka majibu ya Serikali kuhusu suala la buffer zone ndani ya pori tengevu la Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Serikali walisema Serikali tayari kupitia Waziri Mkuu, wakati huo Mheshimiwa Mizengo Pinda alitoa agizo kwamba Wizara hizi tatu, Wizara ya Maliasili, Wizara ya Mazingira, Wizara ya Ardhi na TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Mkoa Morogoro, wakae pamoja na walisema tayari wameshakaa na wataalam wameshapendekeza na taarifa njema kwamba tayari hata tafiti za TAWIRI zimeelekeza maeneo yale ya buffer zone maeneo mengi siyo rafiki tena kwa wanyama wanatakiwa wayarudishe kwa matumizi ya binadamu, matumizi ya wananchi kwa ajili ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ilikuwa 2015 mwezi wa Nne, wamesema tayari wataalam wameshakaa wamependekeza. Namwomba Mheshimiwa Waziri Profesa, leo atakapohitimisha hapa, wananchi wa Malinyi, wananchi wa Ulanga wanataka wasikie nini hatima ya hii buffer zone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake wanaishi kule kwenye buffer zone kila siku wanawasumbua, hiyo mifugo kila siku wanawapiga faini, wengine wamefika hatua mpaka wamekata tamaa, wakienda Lindi wanafukuzwa, wakienda maeneo mengine wanafukuzwa, hawa Watanzania wana haki ndani ya Katiba na sheria zinawalinda, mpaka lini wataendelea kuwanyanyasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ndiyo inayosema nawashauri tena, habari njema Sheria ile ile ya 2009 ya Wanyamapori, ukiangalia kifungu cha 21 imempa mamlaka Waziri, wakati huo kabla hawajafanya maamuzi yao, lakini eneo lile la buffer zone Waziri ana mamlaka ya kutoa matumizi ya eneo lile. Sasa namwomba Profesa leo anapohitimisha atuambie kwa kutumia mamlaka aliyokuwa nayo, ni lini sasa hiyo buffer zone ndani ya pori tengefu la Kilombero inarejeshwa kwa wananchi kwa ajili ya maendelezo ya kilimo na mifugo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naona nisichanganye mada, nataka nimalizie hapo lakini naomba unipe nafasi wakati tunapopitisha bajeti hii nataka nishike shilingi ya kaka yangu. Kama hatakuwa na kauli thabitii juu ya suala hili la kuondoa migogoro kati ya Pori Tengefu la Kilombero na wananchi wanaoishi vijiji jirani na pori hilo, basi nitakuwa tayari ndugu yangu hata kama hatutaelewana siku nyingine leo nitatoa shilingi yake na naomba nitendewe hiyo haki, nataka nikamate mshahara wa Waziri leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mponda. Tunaendelea na Mheshimiwa Juma Aweso atafuatiwa na Mheshimiwa Mbene.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha leo kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri Profesa Maghembe kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Wizara hii, kwa kweli anaitendea haki. Waswahili wanasema mzigo mzito mpe Mnyamwezi, naamini Wizara hii Mnyamwezi ni Mheshimiwa Profesa Maghembe na kazi anaifanya. Pamoja na changamoto kubwa anazokabiliana nazo, namwambia songa mbele bahari kubwa ndiyo ivukwayo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina maneno mengi sana ila kubwa nataka nijikite katika suala zima la mambo kale. Tanzania ni mionganini mwa nchi zenyehazina kubwa ya mali kale. Baadhi ya mali kale zilizopo ni pamoja na majengo ya zamani ambayo yalijengwa na matumbawe katika Miji ya Pwani ikiwemo Pangani, Bagamoyo, Kilwa na Kilindi lakini Serikali haijewekeza katika utalii wa mali kale hizi. Serikali inapoteza mapato mengi kwa kutowekeza kwenye utalii huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe katika bajeti hii itenye fedha za kutosha kuhakikisha kwamba inakarabati majengo yale ili yawe katika hadhi na kuongeza utalii katika mali kale na kuongeza pato la Taifa. Hii iende sambamba na kuajiri watumishi wanaohusiana na mambo ya kale ili kuhakikisha kwamba tunaongeza pato la Taifa katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya maliasili na utalii ni muhimu na mhimili wa maendeleo katika Taifa letu, lakini mchango wake siyo mkubwa pamoja na fursa zilizopo. Nchi yetu imejaaliwa kuwa na vivutio mbalimbali kama vya wanyamaporii na hifadhi mbalimbali, lakini mchango wake umekuwa ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali itenye fedha na kuhakikisha kwamba inakuwa na mpango mkakati wa kuvitangaza vivutio hivi ili viende kuchangia pato la Taifa. Biashara ya utalii inategemea matangazo. Tunapovitangaza vivutio hivi kwa kasi kubwa, ndiyo tunapoongeza watalii kuja kuvitembelea na kuchangia pato la Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yangu ya Pangani nataka nizungumzie mbuga ya Saadani. Mbuga ya Saadani ni mionganini mwa mbuga pekee Afrika ambayo imepakana na bahari. Mbuga hii inapata changamoto kubwa ya miundombinu mibovu ya barabara. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, ni muda muafaka sasa acae na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kuhakikisha kwamba wanaiangalia barabara hii ya Tanga - Pangani - Saadani na kuhakikisha inajengwa kwa kiwango cha lami ili kuweza kuwavutia watalii kutoka Kanda ya Kaskazini, Zanzibar pamoja na nchi jirani ya Kenya kuja katika Wilaya ya Pangani na kuinua sekta hii ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi sana ya kusema ila kikubwa tu nimwombe Mheshimiwa Waziri aendelee kufanya kazi na kuweza kuwatumikia Watanzania na sisi kama viongozi vijana tunaendelea kumuunga mkono kuhakikisha kwamba anafikia azma iliyowekwa katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aweso kwa kuokoa muda. Mheshimiwa Janet Mbene.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Pia namshukuru Mungu kwa kutuamsha salama na kutufikisha hapa. Nami naomba nichangie mambo machache juu ya hii hotuba ya Mheshimiwa Profesa Maghembe. Nataka kuwapongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa hotuba nzuri iliyosheheni masuala mbalimbali ya maendeleo ya utalii na uhifadhi katika nchi yetu. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusikitika juu ya bajeti ya Wizara hii. Wizara hii ni kati ya Wizara ambazo zinachangia pato kubwa sana kwa nchi yetu na ina fursa kubwa sana ya kuchangia pato letu la Taifa, lakini ni Wizara ambayo vilevile haitendewi haki inapokuja kwenye bajeti. Bajeti yake haiendani na uwezo wa Wizara hii kuiletea nchi yetu mapato. Wizara hii haitengewi bajeti ya kutosha kwa utangazaji, tumeona mifano mingi ya nchi jirani na nchi nyingine duniani kiasi ambacho wanatenga kwa ajili ya utangazaji peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna vivutio vingi sana na tunapenda kujikumbusha kila mara, lakini vivutio hivyo tunavijua sisi tulimo humu ndani, walioko nje ambao wanatakiwa kuja kuvifaidi hawavitambui. Kwa hiyo, ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha kuwa matangazo yanapewa bajeti na profile ya kutosha ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha watalii wanavutiwa kuja. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia utalii wa ndani. Bado utalii wa ndani haujapewa kipaumbele au haujazingatiwa. Sisi Watanzania vile vite tunaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa sana utalii wa ndani. Kama hiyo haitoshi, Maafisa Maliasili walioko katika wilaya hawazitendei haki fursa za utalii zilizoko katika wilaya zetu. Karibu wilaya zote zina nafasi na fursa za vivutio vya utalii, lakini inaonekana yanazingatiwa maeneo makubwa makubwa tu ya Kaskazini, hifadhi za wanyama lakini hatuangalii utalii wa aina nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija katika Mkao wangu wa Songwe peke yake kuna vivutio vingi sana vya utalii. Kuna vijito au chemichemi za maji ya moto, hicho ni kivutio cha kutosha. Tuna kimondo Mbozi ni kivutio cha kutosha. Zamani tulikuwa tunasikia kinatajwatajwa sasa hivi hata kutajwa hakitajwi tena. Mikoa yetu sisi ni ya milima na mabonde ambayo ni mizuri sana kwa utalii wa kijiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watalii wengi wanapenda kupanda milima, trekking na camp sites. Watalii wengi wanapenda sana kuja kuangalia mazingira yetu jinsi tunavyoishi. Kwa hiyo, hivi vyote ni vivutio ambavyo vingepaswa kuendelezwa ili vilette kwanza ajira kwa wananchi walioko pale

lakini vilevile vituletee mapato kwa ajili ya nchi yetu na kupanua wigo wa utalii ambao unapatikana kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika vilevile kuwa katika mradi au mpango wa *BRN* utalii haupo wakati tunajua kabisa kuwa ni chanzo kikubwa cha mapato. Napenda Serikali ituambie huo mpango wa *BRN* kwa nini umeacha utalii nje na kuacha kuushughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la miundombinu ya utalii, kuna matatizo makubwa ya miundombinu ya utalii kwa mfano barabara, hoteli katika maeneo mbalimbali ambayo watalii wanatakiwa kufikia hata katika Mlima Kilimanjaro. Tumesikia na wale waliopanda mlima ule wameona, vle vibanda vinavyotumika kufikia wageni havifai, sasa hivi vinatakiwa viboreshw kwa kiasi kikubwa, kuna masuala ya vyoo na sehemu za kupumzika zote hazifai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mlima Kilimanjaro ni kivutio kikubwa dunia nzima na wageni wanaokuja pale ni wengi sana kwa nini isitengwe fedha kutokana na Mlima Kilimanjaro peke yake kwa ajili ya kuboresha ile miundombinu ya kutumika kwenda kupanda? Vilevile Watanzania wengi wahamasishwe na wawezeshwe kwenda kupanda Mlima Kilimanjaro, mlima uko kwenye nchi yao lakini wao wenyewe hawajaupanda. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia vilevile ufugaji wa nyuki na uhifadhi wa mazingira. Tanzania ni nchi ya pili Afrika kwa kuzalisha asali lakini hata kiwango ambacho asali hiyo inazalishwa bado ni kidogo sana. Tuna uwezo wa kuzalisha asali nyingi sana Tanzania, lakini Maafisa Maliasili wetu wala hili hawalizingatii. Wanakimbizana na kuuza magogo tu na kukata miti tu, jamani sasa hivi warudi kuzingatia mambo ya utalii katika maeneo yetu, lakini vilevile ufugaji wa nyuki na upandaji wa miti. Hii ndiyo njia pekee ambayo kwanza itatuletea uhifadhi lakini vilevile itatuwezesha kufuga nyuki wengi na kupata pato kubwa na kwa vijana wetu ufugaji wa nyuki ni ajira nzuri sana. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kurudi kwenye suala la Bodi ya Utalii. Pamoja na malalamiko kuwa haipati fedha ya kutosha lakini bado na yenewe haitumii ubunifu wa kutosha. Kuna mambo mengine bodi inaweza kufanya bila kutegemea fedha nyingi. Nchi yetu mara nyingi inashiriki kwenye maonesho nchi za nje, ya kibiashara, mikutano mikubwa ya Kimataifa na maonesho ya mambo mbalimbali, hizi ni fursa zinazoweza kutumika vilevile katika kutangaza utalii wetu. Tuna fursa vilevile za sisi wenyewe kukusanya watu nje ya nchi, wafanyabiashara au watalii wenyewe, ma-agent wa utalii kuja katika maonesho hayo ili tuoneshe nini tunacho ili waweze kuvutiwa. Hili suala naona bado halijatiliwa mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mheshimiwa jana alisema kuwa ni wavivu, mimi naweza nikakubaliana naye, kwa sababu uvivu ni pamoja na kutokuwa mbunifu. Kama umepewa majukumu lazima uyatendee haki majukumu yako kwa kuhakikisha unajituma kwa kiasi kikubwa ili nchi yako ikafaidike. Hatuwezi kuendelea kuimba nyimbo za kuwa sisi tuna vivutio vingi wakati vivutio hivyo hatuviendeze wala havituletei faida yoyote. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea ningependa kutoa pendekezo kuhusiana na miundombinu ya hoteli. Tunasema kuwa sisi tuna upungufu mkubwa wa vitanda ndiyo maana watalii hawaii kwa wingi. Nataka kutoa pendekezo ambalo naomba lifikiriwe kuwa, mifano imeonekana kwa nchi nyingine kwa mfano Zambia, walitoa msamaha wa kodi na ushuru kwa wale wanaokuja kuwekeza kwenye hoteli za nyota tatu mpaka tano kwa kipindi cha miaka miwili wakati wanajenga na baada ya kumaliza ujenzi wakati wa kuanza ku-operate zile hoteli ndiyo wakaanza kulipishwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi sana walijitokeza kujenga hoteli katika sehemu mbalimbali za utalii na sasa hivi Zambia wanapata watalii wengi. Hebu na sisi tulitafakari hilo, tulifanyie mahesabu tuone, je, itatugharimu kiasi gani kwa muda wa miaka miwili, mitatu kuachia wawekezaji wajenge kwa misamaha maalum, baada ya hapo tuanze kuwatoza kodi inayostahili na tutahakikisha kuwa tunapata watalii wa kutosha. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa hoteli zilizopo ziboreshw, watenda kazi wafundishwe jinsi ya kuhudumia wageni ili tuweze kuwa na ubora unaohitajika kwa sababu tunalalamika sana kuwa wanakuja wageni kuja kufanya kazi katika hoteli zetu lakini ni kwa sababu wafanyakazi wetu labda hawajapata ujuzi wa kutosha jinsi ya kuhudumia watalii na kutoa huduma ambazo zinaffaa kuvutia watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii, lakini naomba yote ambayo tumeyatoa hapa yakazingatiwe. Ahsante. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa kutuokolea na muda pia. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Dkt. Kikwembe atafuatwa na Mheshimiwa Hamidu Bobali, dakika tano kwa Mheshimiwa Bobali.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kuwashukuru waandaaji, maana yake kuandaa hizi taarifa nayo ni shughuli. Kwa hiyo, wameweza kutuandalia vitu ambavyo na sisi tumeweza kuviperuzi na sasa tunaweza tukatoa michango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kavuu kwa uvumilivu wao na ushirikiano wao wanaonipatia mimi Mbunge wao wa Jimbo la Kavuu. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na hotuba, naomba niwaombe wafugaji wangu wa Kata ya Ikuba, Kijiji cha Kikulwe na Ikulwe (Maji Moto), wawe na uvumilivu wa kuhamisha mifugo yao vizuri pindi watakapooneshwa maeneo ya kupeleka mifugo hiyo. Niiombe Serikali kupitia tangazo lake la kuwaambia watoke mita 500 kwenye vyanzo vya maji, niliomba kuchangia katika Wizara ya Kilimo na Mifugo, nikawaambia waende wakatengeneze malambo, ni ahadi ya llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakatengeneze malambo kule ili wafugaji wale wa Kata ya Ikuba wasiweze kwenda kwenye ule mto wanaowaambia waondoke mita 500 na wanawafukuza bila kuwapa mbadala wa maeneo ya kwenda. Wizara na Serikali wanasema wametenga maeneo Katavi, sasa wanawaondoa hawajawapeleka kule, leo wakikataa kutoka kule watasema wanaleta vurugu, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawatawaonesha maeneo ya kwenda kuweka mifugo yao maana yake ni nini? Sasa hivi wakulima wanavuna, maana yake watatoka pale walipo wanaenda kuongeza shughuli na vita nyiningine na wakulima. Wamenitatulia tatizo lile lakini sasa wameongeza tatizo lingine jana. Leo hii ninavyoongea hapa wakulima na wafugaji kule ni shughuli kubwa, ni vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Profesa Maghembe akitoka hapo saa saba kapige simu kule uwaeleze waache vurugu zile. Mkuu wa Mkoa na Serikali ya Mkoa imetoa tamko kule kuwa-disturb wafugaji lakini wakulima hawajatoa mazao yao shambani, kwa hiyo leo wanataka kuleta fujo juu ya fujo, jambo ambalo sitalikubali. Tumesema hapa, tunataka kutatua matatizo na si kuongeza matatizo. Haya ni matatizo ambayo yanatokana na mbuga ya Katavi pamoja na hiki kijiji ninachokisema Kata ya Ikuba pamoja na Kata ya Chamalendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo mita 500 mkulima wa kawaida, mfugaji wa kawaida anazipimaje? Waende wakaweke alama, wakachimbe malambo waache kwenda kwenye ule mto, hakuna maji, kila siku hapa ni kilio na tunapiga kelele hapa Wabunge wote wanazungumzia tatizo hili la maji. Sasa kama hawana maji wakanyweshe wapi mifugo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakiingia pale kunywesha askari wa TANAPA wanawaswaga wale ng'ombe kuwapeleka ndani ya mbuga na kuwaua. Jambo ambalo wanawasababishia umaskini wafugaji na wakulima hawa na sisi

lengo letu tunasema watu hawa waende kwenye uchumi wa kima cha kat. Tunafikaje kule kama leo sisi wenyewe tunakuwa ndani ya sheria zetu tunakinzana namna ya kuzitekeleza. Naomba waka-harmonize hizo sheria zao na waangalie ni namna gani wanatekeleza hayo majukumu na kwa wakati gani na kama eneo lile limetengwa wawapeleke wale wafugaji kule. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika suala lingine na naomba Mheshimiwa Waziri anielewe ni suala la utalii. Kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Lucy Owenya jana amechangia vizuri sana kwenye suala zima la utalii, hakuwa bias na upande wao. Utalii imeonekana sasa ni Kaskazini tu, jamani kila siku nasema Mbuga ya Katavi ina wanyama wakubwa kuliko wanyama wote Tanzania. Anayebisha hapa leo aende lakini haitangazwi hata kidogo. Tuna twiga mazeruzeru kule, hakuna mbuga yoyote utawapata, tuna viboko wakubwa hakuna popote utawapata Tanzania nzima. Kwa nini hawatangazi mbuga zingine tumekazana tu na Serengeti, Ngorongoro, Manyara, sana sana tukisema tunakuja kusema hii hapa ya Iringa, kwa nini hatuvuki kwenye mbunga nyingine? Tunapoteza mapato kwa ajili tu ya utangazaji. Naomba hilo suala waliangalie. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye suala la wahanga katika Operesheni Tokomeza Ujangili. Katika Bunge lililopita Bunge lilitoa maazimio hapa mambo gani yakafanyiwe kazi, mojawapo ikiwa ni pamoja na kuwalipa wahanga ambao kwa namna moja au nyingine hawakuwa majangili bali walikuwa katika utekelezaji wao wa majukumu mbalimbali wakiwemo Watendaji wa Kata na Vijiji na baadhi ya Waheshimiwa Madiwani. Tuliwahi kusema hapa, wapo waliopigwa mpaka kupoteza viungo vyao na tulitoa maazimio wakasema watawalipa fidia. Nataka kujua fidia hiyo imekwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri asiniambie ndiyo kwanza anaingia ofisini, ofisi ipo na shughuli ziko mezani, ukifika ni kuperuzi tu na kuendelea na utaratibu wa kazi. Kwa hiyo, tunaomba hili nalo alitolee ufanuzi ili wahanga hawa ambao wengine waliweza hata kupoteza watoto wao bila sababu za msingi kutokana na kazi kufanyika bila kufanya utafiti wa kutosha. Kwa hiyo, watu wengi waliumizwa kwa namna moja ama nyingine na tulitoa maamuzi hapa na maazimio kwamba wapatiwe fidia. Kwa hiyo, tunaomba wale wote walioingia katika zoezi hilo bila wao wenyewe kuwa majangili wapatiwe fidia zao na Serikali itupe hapa majibu kwamba wanafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye suala langu la Ikuba na Chamalendi, tafadhali sana Mheshimiwa Waziri mpaka saa nane mchana naomba awe amekwishaongea na Serikali ya Mkoa waangalie wale wafugaji wanawapeleka wapi. Sitaki niende kule nikute watu wamechapwa fimbo, watu wameuawa na kwetu kule unajua wakianza kupigana, ni mapanga na fimbo,

hatutaki tusababishe vita kati ya wakulima na wafugaji. Tumeoana na tumeingiliana katika familia, hatutaki sasa tuanze kuwa na demarcation kati ya mkulima na mfugaji. Sisi wote ni wamoja, tuna namna tunavyoishi kule, mkianza kuleta vurugu zile mkulima hatakubali mwingine aingize ng'ombe mle wala mwenye ng'ombe hatakubali ng'ombe wake wauawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachelea kusema majipu yapo ndani ya TANAPA, maaskari wale wa mbugani wana mipango fulani. Haiwezekani askari anaajiriwa ndani ya mwezi mmoja ni milionea, ndani ya miezi miwili siyo mwenzio, lazima kuna namna inayofanyika kule, naomba wafanye utafiti. Haiwezekani hata kidogo mtu mmoja kapigiwa ng'ombe 80, ng'ombe 70, ng'ombe 200 kwa kosa lipi? Sheria haisemi hivyo, sheria inasema hata kama wale ng'ombe wamewakamata basi walipishwe faini. Kama faini zao wanaona ndogo walete sheria hapa tufanye marekebisho, tuone tunafanya nini kupata mapato na kuongeza uchumi katika Halmashauri zetu lakini kuwaonea wafugaji, kuwaonea wakulima kwa kweli ni kosa la jinai. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante muda wako ndiyo huo Mheshimiwa umekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Hamidu Bobali.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Ni zamu yangu.

**MWENYEKITI:** Hapana, Mheshimiwa Bobali.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Choice ni yetu Mheshimiwa Mwenyekiti na jina langu liko mwanzo.

**MWENYEKITI:** Please.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Hajakuwa tayari yeye tumemuweka jioni ndiyo maana tukampa dakika tano.

**MWENYEKITI:** Don't command me! Mheshimiwa Bobali sasa siyo dakika tano kwa maelewano yenu wewe ni dakika kumi sasa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza, niombe tu Mheshimiwa Waziri anisikilize kwa makini kwenye suala hili ambalo nataka nilizungumze sasa hivi. Niunge mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye kipengele cha mabaki ya mjusi ambayo yapo Ujeruman. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo hapa, kuna mabaki ya mjusi ambayo yalichukuliwa katika eneo la Tendenguru, Jimbo la Mchinga ambako mimi ndiyo Mbunge wao, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi kupelekwa Ujerumani. Dinosaur huyu ndiyo mjusi mkubwa kuwahi kuishi katika dunia hii tuliyonayo, anatengeneza historia kubwa kwa nchi yetu. Mungu hakufanya makosa mjusi huyu kupatikana katika ardhi ya Tanzania, unfortunately alichukuliwa akapelekwa Ujerumani. Hivi sasa ninavyowaambia mabaki yake yapo pale Ujerumani, watalii maelfu kwa maelfu wanakwenda kuangalia pale Serikali ya Ujerumani inapata pesa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kifupi nilichokuwa Mbunge wa Jimbo la Mchinga nimekwenda Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambako nilielekezwa kwamba wao ndiyo wanalishughulikia suala hilo. Mheshimiwa Waziri jioni nitamletea barua niliyojibiwa na Katibu wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, majibu yake yanositisha Mheshimiwa Waziri. Hapa kwa sababu Mnadhimu alikuwa amesema kwamba nichangie jioni ningekuwa nayo hapa lakini jioni nitaileta. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya kusikitisha na ambayo sikutarajia Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ananijibu kwamba mpaka sasa Serikali inafanya calculation kujua huyu mjusi anaingiza kiasi gani kwa mwaka, *this is very shameful*. Mwaka 1907 alipochukuliwa, Tanzania imepata uhuru mwaka 1961 mpaka hivi sasa hatujui mjusi huyu anaingiza kiasi gani Ujerumani, *this is very shameful*. Ananijibu kwamba Wizara inaendelea kuhakikisha inafanya calculation kujua kwa mwaka inapata shilingi ngapi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira mengine ya kusikitisha wiki mbili mbele wanantumia tena barua nyingine ya majibu wakijibu barua yangu hiyo moja, imepata barua mbili za majibu kwamba sasa Serikali ya Tanzania imeshirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo ndiyo Wizara hii kwamba waanzishe ushirikiano na mahusiano ya utunzaji wa mambo ya kale. Hii ina maana kwamba mahusiano yatatengenezwa kati ya Ujerumani na Tanzania ili kuhakikisha kwamba Tanzania inanufaika kutokana na mjusi yule. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la aibu. Alikuwepo Mbunge wa Jimbo la Mchinga Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, alizungumza sana juu ya suala la mjusi mpaka amemaliza kipindi chake hakuna majibu. Haya mama Fatma Mikidadi akapewa jina kabisa kwamba mama mjusi, Mbunge wa Viti Maalum amezungumza mpaka mkambatiza jina la mama mjusi, chwee majibu hakuna. Bi. Riziki Lulida miaka kumi huu sasa mwaka wa 11 anazungumzia suala hilo la mjusi majibu hakuna. Mimi Mbunge wa Jimbo la Mchinga leo

nazungumza suala la mjesi na nitatoka hivi miaka mitano chwee majibu hakuna. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Waziri jambo moja, kama kuna suala ambalo lilinipa Ubunge na mkimuuila Mbunge niliyemtoa Mtanda atawaambia wananchi hawataki kusikia juu ya suala lolote kuhusu mjesi, wananchi wa Jimbo la Mchinga hawataki CCM kwa sababu ya suala la mjesi, nawaambia kabisa. Mheshimiwa Magufuli Rais wetu wakati yupo kwenye kampeni alivyofika Mchinga aliwekewa mabango *bring back our dinosaur*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Magufuli kwenye mkutano pale Nangalu, waliokuwa wanatembea na mgombea wa Urais watawaambia, Mheshimiwa Nape angekuwepo angesema hapa, alisema pale Nangalu kwamba najua tunapoteza fedha za mjesi huyu hatutaweza kumrejesha lakini nitahakikisha kwamba fedha za mjesi zinarudi katika Serikali ya Tanzania na kuletwta Halmashauri ya Wilaya ya Lindi kuja kutatua kero ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa mgombea wa Urais ambaye sasa ndiye Rais kwa hii ahadi yake aliyowaahidi wana Mchinga wanaisemaje? Ahadi aliyowaahidi Watanzania kwamba pesa za mjesi zitapatikana inakuwaje? Inakuwaje sisi Tanzania hatuthamini mali zetu kwa nini? Kwani Mungu mwenyewe alivyoamua huyu mjesi apatikane Tanzania unadhani alifanya makosa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ya hoja suala la mjesi alizungumzie. Namwambia kabisa Waziri asipozungumza juu ya suala hili nakamata mshahara wake, tunahitaji majibu ya kutosha juu ya masuala ya mjesi. Kwanza atakuwa anatunasua sisi kutohama na aibu, wenzetu watu wa Kenya wakitangaza Mlima Kilimanjaro, mnalalamika leo watu wa Kenya wala hawasemi kwamba mjesi anatoka kwao wamekubali kwamba mjesi anatoka Tanzania, anatoka huko huko kwetu lakini wao kuchukua kwamba huyu ni wa kwetu hawataki, tatizo nini? Kama kuna mtu anapata maslahi ndiyo anatukwamisha wamtaje kwamba labda kuna mtu anapata maslahi juu ya hili ili watu tuju. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu suala la ndovu kuvamia kwenye Jimbo langu la Mchinga. Kwanza Mheshimiwa Waziri nimpongeze sana mzee wangu ametusaidia vya kutosha, Serikali yake imehakikisha kwamba kila ndovu wanapovamia mashamba ya wakulima wangu wanakuja kuwafukuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Mchinga wastaarabu sana, ndovu wanatembea kwenye vijiji vyangu vile yaani kama mbuzi tu na wanakotoka mbali. Kutoka Selou kuja Mchinga ni zaidi ya kilometra 180, wanakuja wanakaa kule siku 20 - 30 lakini hakuna tembo amepigwa au

amebugudhiwa. Wananchi wa kule wastaarabu, sisi watu wa Pwani wakifika tunawaachia mashamba tunakimbia tunawaambia kuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ustaarabu unafika mwisho mtu anachoka, nakuomba sana ili huu unyongeunyonge tulionao ukasema hawa watu wa Mchingga ni wanyonge wanyonge hawapigi tembo, sisi tunawatunza, tunathamini maliasili zetu lakini sasa inaonekana inakuwa shida. Leo kuna zaidi ya ekari 183 za chakula za wananchi wa Jimbo la Mchingga zimeliwa na tembo mpaka sasa hakuna chochote kinachoendelea, hata watu kwenda kufanya tathmini hawaendi, wale wananchi wakichukua hasira baadaye wakaamua kuwapiga watawalaamu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amenisaidia sana kila walipokuwa wanakuja alikuwa anapeleka askari kwa hili namshukuru na kumpongeza lakini isiishie pale. Yale mashamba ekari 183 za wananchi wale ambazo wamelima kipindi chote cha miezi sita (6), akinamama maskini wale, watu maskini wale, mtu amelima shamba lake la mihogo lote limeliwa na tembo, leo wanakuja kuniuliza Mheshimiwa Mbunge unatusaidiaje? Siyo mimi ni ninyi Serikali mnawasaidiaje wananchi wa Jimbo la Mchingga kutokana na chakula chao kuliwa? Naomba ifanyike tathmini haraka ili wananchi wa Jimbo la Mchingga walipwe fidia kutokana na mazao yaliyoliwa na tembo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mnadhimu kwamba ilikuwa nichangie jioni, lakini nakushukuru hayo ndiyo maamuzi ya Kiti. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa mchango wako. Tunaendelea, nihame kidogo huku kwenu nirudi huku, Mheshimiwa Innocent Bashungwa atafuatiwa na Mheshimiwa Elias John Kwandikwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii nyeti na muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Maghembe na Naibu Waziri, Mheshimiwa Injinia Ramo kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mdau mkubwa na naamini kwamba maendeleo ya watu na utunzaji wa mazingira ni vitu viwili ambavyo vinaendana (*environmental conservation can co-exist with social economic development*). Kwa hali inayoendelea katika Pori la Hifadhi la Kimisi nimeanza kuwa na mashaka kwamba tusipojipanga vizuri kama nchi itafika mahali nchi yetu itageuka kuwa jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikiwa mtoto Pori la Akiba la Kimisi tulikuwa tuna wanyamapori wengi, kulikuwa kuna twiga, zebra, tembo na wanyama wengi lakini sasa hivi limejaa ng'ombe kutoka nchi za jirani. Nimeangalia kwenye sheria za nchi yetu, nimeangalia kwenye Mpango wa Taifa wa Ardhi wa 2013 - 2033 sijaona sehemu yoyote inayosema kwamba mapori ya akiba yatumiwe na ndugu zetu wa nchi za jirani kufuga ng'ombe wao na wakati wananchi wetu wana shida ya malisho bora na maeneo ya kulima. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa upande wa Karagwe, Kata ya Rugu, Nyakasimbi, Nyakakika, Nyakabanga na Bweranyange wananchi wangu wana shida sana na maeneo ya malisho bora na maeneo ya kulima lakini wanapakana na Pori la Akiba la Kimisi ambalo inasemekana kuna ng'ombe wengi sana kutoka nchi za jirani. Naiomba Serikali iliangularie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama kiongozi siwezi kuingia mle kwenye pori hata wananchi wangu wanashindwa kuingia na kwa kuwa wananchi wanafahamu kwamba haya mapori matumizi yake hayafuati sheria za nchi za mapori ya akiba, wengine wanashawishika kuingia mle kwa sababu hawako tayari kuona ng'ombe wao wanakufa kwa kukosa malisho na wakati kuna wafugaji kutoka nchi jirani wapo kwenye lile pori. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali iandae Tume iende mle ichunguze status ya Kimisi irudi kwenye Pori la Akiba. Mimi na Madiwani wangu tutafuata utaratibu pale itakapobidi kama ni kuomba Serikali itenye maeneo kwa ajili ya wakulima na wafugaji basi tufuate utaratibu wa bottom up kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. Watu wanatoka nchi jirani wanakuja kufugia kwenye mapori ya akiba na hiki ndiyo chanzo cha migogoro. Nazungumzia kwa Kimisi, lakini naamini pengine picha ya Kimisi inafanana na mapori ya akiba mengine. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali baada ya ku-clear Kimisi ikawa katika hali ambayo inafuata utawala wa sheria, turudi kule zamani ambapo lile pori la akiba lilikuwa ni pori ambalo tunaweza tukafanya utalii. Wenzetu nchi ya jirani ya Rwanda wana ardhi chache lakini wanaitumia vizuri. Kwa mfano, pale Kimisi natamani sana Serikali ituletee twiga, zebra na tembo pawe conserved tuweze kufanya utalili kama majirani zetu Rwanda wanavyofanya. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili niombe Serikali kwa sababu wakati wa kutenga Kimisi Serikali haikuhusisha vijiji vya jirani kunyoosha mipaka iende pale Kimisi katika hizi kata ambazo nimezitaja tuangularie upya ile mipaka na tuweke mipaka ya kudumu. Mimi kama Mbunge wa Karagwe naamini kabisa kwamba wananchi wa Karagwe tunaweza tukawa tuna conservation ya pori ambalo

linatuletea mapato ya kitalii na wakati huo huo tukapata malisho bora na sehemu za kulima. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuiomba Serikali, sasa haya ni mambo ya Kitaifa kidogo, kuna asilimia 25 ya mapato kutoka mapori ya akiba yanatakiwa kwenda kwenye Halmashauri kusaidia vijiji ambayo viro jirani na mapori ya akiba, lakini kwenye Halmashauri ya Karagwe hii hela hatujawahi kuiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri Mheshimiwa Profesa Maghembe atakaposimama kujibu hoja nisikie msimamo wa Serikali kwenye Kimisi na pia nisikie msimamo wa Serikali kuhusu asilimia 25 ambayo inatakiwa kuja kwenye Halmashauri ya Karagwe kutoka kwenye mapato ambayo yamepatikana kutoka kwenye mapori ya akiba. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la utalii kwenye nchi yetu umekuwa ni wimbo sasa tunasema nchi yetu ina-potential ya utalii inaweza ikatuingizia fedha za kigeni zaidi lakini sioni mikakati ambayo inanipa matumaini kwamba sasa sekta ya utalii itakua na kuweza kuchangia pato la Taifa. Napenda kuishauri Serikali, Wizara ya Maliasili na Utalii wasifanye kazi kwenye silos, washirikiane na Wizara nyingine kwa mfano kama kuna maeneo ambayo ni ya kipaumbele kwenye uwekezaji wa utalii, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ishirikiane na Wizara ya Maliasili kuhakikisha hayo maeneo yanapata miundombinu ili tuweze kuvutia uwekezaji kwenye maeneo hayo ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kwenye ranking imekuwa nchi ya 130 na wakati kwenye vivutio duniani ni ya pili. Hii inaonesha kwamba hatujajipanga na tukijipanga sekta ya utalii inaweza ikatusaidia kukuza uchumi wa nchi na kutengeneza ajira. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la mambo ya kale na hii ni sehemu ambayo tukijipanga vizuri inaweza ikatusaidia kuongeza pato na ajira kwa wananchi wetu. Karagwe kwenye historia na sisi tumo. Kama mnakumbuka Speke na Grant walipita Karagwe wakati wanaangalia jinsi ya kwenda Uganda. Kwa mfano sehemu ambapo Chifu Rumanyika alipokuwa anakaa tunaiomba Wizara ya Maliasili na Utalii itusaidie. Nimeshaongea na wana diaspora kutoka Karagwe wapo tayari kushirikiana lakini tunahitaji msaada wa Serikali kutuwekea miundombinu ya pale na tukae tuangalie ni namna gani tunaweza tukasaidia kuhifadhi malikale kwa Karagwe na sehemu nyingine za nchi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kidogo kwenye Kata ya Bweranyange, hizi ni Wilaya ambazo ziko mipakani na nchi za jirani na ni vizuri tukahakikisha tunatunza ulinzi na usalama wa mipaka yetu. Kule kwenye Kata

ya Bweranyange kuna kambi ndogo ya jeshi wananchi wangu wanani pigia simu wanalamika kwamba wamefika mahali wanaogopa kuoa wanawake wazuri kwa sababu wanahofia eti watanyang'anya na wanajeshi. Mimi siamini kwamba hali iko hivi lakini...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Elias John Kwandikwa atafuatiwa na Mheshimiwa Paresto na Mheshimiwa Bulaya ajiandae.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kuunga mkono hoja. Pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa namna ambavyo ameanza kwa kuonesha juhudhi ya kuweza kuhakikisha kwamba rasilimali hii muhimu inakuwa katika hali ambayo inalineemesha Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Ushetu kwa sababu tumekuwa na matatizo makubwa sana, lakini wamekuwa wavumilivu lakini pia wamekuwa sehemu ya kutoa ushirikiano ili kuweza kutatua matatizo ya migogoro ambayo ipo kwenye mipaka. Sisi katika Jimbo letu la Ushetu tumepakana na Hifadhi ya Kigosi Moyowosi lakini pia tuna hifadhi za misitu nyingi kwenye Kata za Ulowa, Ubagwe, Ulewe, Nyankende, Idahina na Igomanoni. Kote huko tunapakana na misitu lakini wananchi hawa wamekuwa na utayari wa kushirikiana ili tuhakikishe kwamba uhifadhi unaendelea lakini pia mifugo yetu inapata sehemu ya malisho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakubaliana kwamba sekta hii ya maliasili na utalii imetoa mchango mkubwa sana kwenye Taifa letu. Utashuhudia kwamba kuna ajira imepatikana maeneo mbalimbali ya moja kwa moja na ile ambayo ni *indirect*. Pia imechangia kama wachangiaji wengine walivyosema katika pato la Taifa, fedha za kigeni tumezipata lakini mchango mkubwa umekwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Jambo lingine pia uhifadhi wetu umeipa heshima nchi yetu, niipongeze sana Wizara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini utaona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumza pia kwamba uko mchango mkubwa kwenye nishati. Asilimia 90 ya nishati imetokana na rasilimali zetu hasa hasa za kwenye misitu. Pia kumekuwa na 75% kwa mujibu wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri imetupa faida ya kupata vifaa vya ujenzi. Kwa hiyo, utaona kabisa sekta hii ni muhimu lakini ni lazima kuhakikisha kwamba kunakuwa na uhifadhi lakini pia kutokuwa na migogoro ambayo inatusumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alivyoanza kutoa hotuba yake aliturejesha kwenye Ibara ya 27 ya Katiba lakini napenda nimshauri Mheshimiwa Waziri ajaribu kuiangalia Ibara ya 24 kwa madhumuni ya kuziangalia sheria zetu. Hizi sheria zetu ambazo zinatoa fursa ya uhifadhi wa misitu yetu zinahitajika ziletwe katika Bunge lako kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho. Kwa sababu ukiangalia Ibara ya 24, naomba kwa ruksa yako niisome kwa haraka, inazungumza juu ya haki ya kumiliki mali, inasema kwamba:-

*"(1) Kila mtu anayo haki ya kumiliki mali, na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria.*

*(2) Bila kuathiri masharti ya Ibara ndogo ya (1), ni marufuku kwa mtu ye yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisha au madhumuni mengineyo bila idhini ya sheria ambayo inaweka masharti ya kutoa fidia inayostahili". (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo yetu tumekuwa na utaifishaji wa mifugo, sasa nashauri sheria hizi zije hapa tuzitazame. Sheria hizi zimepitwa na muda kwa sababu ukiangalia hata zile sheria ambazo zinatoa uhifadhi katika maeneo kama ya TANAPA ziko faini ndogo sana. Nilikuwa nafikiria kwamba tufanye marekebisho lakini pia itupe nafasi sisi wananchi, kama Mheshimiwa Waziri alivyozungumza katika hii Ibara ya pili, anapozungumza juu ya uhifadhi, nani ahifadhi na hizi rasilimali ni za nani, ni zetu sisi sote. Kwa hiyo, lazima tushiriki pia kuhifadhi na kulinda hizi rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri afanye mapitio ili tu tupate sheria ambazo na sisi wananchi kwa kupitia vikundi vyetu kama wakati mwingine nilivyoshauri hapa tuweze kutoa nafasi kwa wananchi kupitia vikundi vyetu na uongozi wa mila kuweza kupeana faini kidogo kidogo za kila siku ili kuhakikisha kwamba uhifadhi unakwenda vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kuangalia katika migogoro hii ambayo imekuwepo, chanzo chake ni nini? Ni ukweli Mheshimiwa Waziri akubaliane na mimi kwamba siku za nyuma tumekuwa na utaratibu kwamba wale wahifadhi walikuwa kwanza hawatoshi lakini pia wamekuwa wakitumika katika kuhifadhi

watu ambao walikuwa wanawachukua kwa muda ambao sasa kutokana na kutokuwa na nidhamu tulichochea sana wananchi wetu kuingiza mifugo katika hifadhi. Matokeo yake ilizoeleka kama ni jambo la kawaida kwa mwananchi kupeleka mifugo yake katika hizi hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo kadhaa napenda kushauri. La kwanza Mheshimiwa Waziri lazima tuwe na dhamira ya kweli kwa upande wa Serikali na kwa upande wa wananchi na Waheshimiwa Wabunge ya kutatua hii migogoro, lazima tudhamirie kuliondoa hili suala. Tukidhamiria tutapata nafasi ya kurejesha yale mahusiano ambayo yalianza kupotea ili tushirikiane kwa pamoja kuona kwamba uelewa wa uhifashi unapanuka lakini pia tunashiriki kuweza kuhifadhi maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko pengo la uelewa ambalo nimwombe Mheshimiwa Waziri na timu yake wajipange vizuri ili tuendelee kuwaelimisha wananchi kwa kuweka vile vikundi ambavyo vimetajwa na sheria kwa ajili ya kushiriki katika uhifadhi, kwa pamoja tatizo hili tutaweza kuliondoa. Pia bajeti ya Mheshimiwa Waziri haitoshi ili kuhakikisha mafunzo yanatolewa na vikundi vinasaidiwa ili tuweze kusonga mbele. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la wafanyakazi hawa kwa ajili ya doria hawatoshi. Mheshimiwa Waziri litazame suala hili ili tupate watu wenye weledi ili tuweze kwenda vizuri. Pia liko jambo ambalo nafikiria kwamba lazima tuwe na sheria ndondogo kwa upande wetu wa uhifadhi ili tuweze kusaidia kama walivyofanya wenzetu upande wa TANAPA na maeneo ya kwetu iwe hivyo ili tuweze kupiga hatua vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuangalia taarifa hizi za bajeti katika kipindi hiki cha miaka miwili, mitatu, utaona uharibifu kwa mwaka ni hekta 372,000 lakini kwa mwaka tunapanda miti 95,000 na tunasema ikifikia 2030 tutakuwa angalau tumeweza kuwa na misitu ya kutosha, haiwezekani kwa sababu uharibifu huu ni mkubwa kuliko namna ambavyo tunaweza kufanya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kuangalia għarama za kupanda miti, miche ya miti ina bei kubwa sana Mheshimiwa Waziri aangalie eneo hili kwani wananchi wetu wakipata miche ya miti watasaidia kupanda miti mingi ili tuweze kurejesha huu uharibifu. Kwa hiyo, ukiangalia uwiano wa uharibifu na namna ambavyo tunarejeshea misitu utaona kabisa haiwezekani kuhakikisha kwamba kweli hii maliasili inabaki vizuri. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi tumeyazungumza kwenye mifugo, lakini timesahau kuna eneo lingine ambalo pia linaharibu misitu yetu. Utaona kabisa kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba mkaa

tani milioni 1.7 inaingia mjini, asilimia 50 inaingia Dar es Salaam, inatoka maeneo ya pembezoni kuja mjini. Eneo hii ni muhimu sana tuliangalie vinginevyo tutaona kwamba labda mifugo ndiyo inaharibu misitu hii, lakini bado nishati ni sehemu kubwa ya uharibu wa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri aje na mkakati mzuri wa kuhakikisha kwamba tunaweza kushikiriana na upande mwininge wa nishati mbadala ili kuhakikisha kwamba hii *retention* ya misitu inakwenda vizuri. Suala la uhifadhi shirikishi ni muhimu sana, lazima tushirikiane na wananchi ili kuhakikisha kwamba misitu yetu inakaa vizuri. Twende sambamba na Wizara zingine kuhakikisha wananchi wetu tunawajengea kipato cha kutosha ili ule ushawishi wa kuharibu na kutumia rasilimali zetu uweze kupungua ili misitu yetu iweze kwenda vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze juu ya utafiti na sensa ya wanyamapori. Nimejaribu kuangalia ripoti mbalimbali naona kwamba kulikuwa kuna *sample* tu ya sensa kwa kuangalia namna ambavyo wanyama wamepungua, kama tembo wamepungua sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako tunaendelea.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso atafuatiwa na Mheshimiwa Bulaya na Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Mchango wangu wa kwanza utajikita katika suala zima la misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kushuhudia misitu yetu ikizidi kutoweka kwa kasi kubwa sana na hatujaona mikakati ya dhati ya Serikali kuhakikisha kunakuwa na misitu endelevu. Kuna takwimu ambazo zinaonesha *national annual deforestation* ni kati ya 0.8% mpaka 1.1%. Kwa kiwango kikubwa misitu hii inatoweka kwa shughuli mbalimbali ikiwemo shughuli za kilimo, uvunaji wa miti, moto na pia biashara kubwa ya mkaa. Ni vizuri Serikali ikatambua misitu hii leo tunaipoteza miaka 20, 30 ijayo nchi hii inaenda kuwa jangwa na hatujaona mkakati wa dhati kabisa wa Serikali kuhakikisha tunakuwa na misitu endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba tuna hiyo TFS ambapo jukumu lake kubwa ni kuhakikisha inasimamia na kutunza hiyo misitu ya asili. Hata hivyo, hii TFS imejikita katika kukusanya mapato zaidi bila kuwa na mipango endelevu ya misitu hii. Mheshimiwa Mbunge mmoja jana alichangia hapa akahoji hata mapato yenyewe yanakusanywaje na haya mapato yanayokusanywa kweli yana uhalisia? Ukichukua mfano, kuna tafiti zimefanywa, kwa Mkoa wa Tabora peke yake kwa mwaka wanazalisha magunia ya mkaa 2,244,050 wanapata shilingi bilioni karibu 21 kwa mwaka kwa shughuli za mkaa peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa za TFS wao wanasema makusanyo ya mkaa tu kwa mwaka ni shilingi bilioni saba, lakini Mkoa tu wa Tabora ni bilioni 21, kitaifa wanasema ni shilingi bilioni saba. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri anapaswa ku-deal na hawa watu wa TFS, kuna tatizo hapa. Kuna watafiti wamefanya utafiti wanaonesha hizi takwimu mkoja mmoja wanaingiza fedha nyingi, lakini Kitaifa TFS wanasema ni shilingi bilioni saba tu. Wizara inatakiwa kuhakikisha wanaitazama vizuri hiyo TFS kwa sababu wao nadhani ama ni rushwa ama kuna watendaji ambao si sahihi wanakwamisha shughuli hizi za kukusanya mapato. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niishauri Serikali kwamba pia wasiitazame TFS katika kuhakikisha inawaletea mapato tu au kutoa vibali vyta misitu na vitu kama hivyo. Ni muhimu TFS ikatekeleza majukumu yake kama dhamira ya uanzishwaji wa TFS ilivyokuwa katika taratibu zake za uanzishwaji. Ni muhimu sana Serikali mkatazama hawa TFS wanapotoa leseni, watoe leseni lakini hao wanaopewa leseni walete mpango mbadala au mkakati mbadala wa kuendeleza misitu yetu ili tuweze kuondokana na kutoweka kwa misitu kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la migogoro ya mifugo inayoingia hifadhini. Waheshimiwa Wabunge sisi kama viongozi pia wakati mwingine ni lazima tuangalie kauli zetu zisije zikalibomoa Taifa. Ni kweli kwamba tunawahitaji wafugaji, ni kweli tunawahitaji wakulima, ni kweli kwamba tunahitaji hifadhi au misitu. Ni muhimu tukafahamu kuwa mifugo inaongezeka na mahitaji ya kilimo kwa maana ya wakulima wanaendelea kuhitaji ardhi lakini ardhi ni ile ile tu haiongezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sana Serikali wakakaa na Wizara zote ambazo zinaingiliana katika masuala haya ya mifugo, kilimo na wa maliasili kuhakikisha wanaweka mipango madhubuti ya kuhakikisha wafugaji wanapata maeneo yao, wanatengewa kabisa, hifadhi nayo inakuwa na maeneo yasiingiliwe na wafugaji, vivyo hivyo kwa wakulima pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kusema pia wakati mwingine unaruhusu moja kwa moja mifugo inaingia hifadhini lakini kama hawa watu wangetengewa maeneo yao hakika tusingekuwa na hii migogoro ambayo inaendelea. Serikali lazima ipime, ukipima kati ya suala la maliasili na utalii na kati ya sekta ya mifugo utaona kwa takwimu kwa sasa kwamba maliasili inaiingizia Serikali pato zaidi kuliko mifugo. Inawezekana pia mifugo ingeweza kuliingizia Taifa pato zaidi kuliko maliasili lakini kama wangekuwa na ufugaji wa kisasa, wakapangia maeneo yao, wasiingiliane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana Serikali wakayapima haya, wakahakikisha migogoro hii ya wakulima na wafugaji inakwisha. Niwasihii Waheshimiwa viongozi wenzangu Wabunge, ni muhimu sana tukachunga kauli zetu, tungalie tunawahitaji watu wote. Tunawahitaji wakulima, tunawahitaji wafugaji, tunahitaji pia na misitu yetu na uhifadhi kwa ujumla. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la utalii. Wizara imetoa takwimu hapa kwamba kwa mwaka nchi yetu inaingiza watalii karibu 1,200,000 na kuna Mheshimiwa Mbunge wa Arusha jana alichangia vizuri sana akafanya comparison na nchi nyingine ambazo zinakuwa na idadi kubwa ya watalii. Nchi yetu mtalii kuja hapa anakumbana na tozo kibao. Anaanzia kwanza kwenye viza, akienda kama ni Ngorongoro getini kuna fees, akilala kwenye hoteli kitanda kina fees, kila mahali Mzungu huyu au mtani huyu anatozwa tozo na hizi tozo zimekuwa ni fixed mwaka mzima na watalii ni wale wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishauri Serikali kwa nini msiwe na promotion package kwa kipindi fulani ili muongeze idadi ya watalii halafu baadaye mkifika kwenye pick fulani mtaendelea na hizi tozo zenu ambazo ziko fixed ili tuhakikishe tunaongeza idadi ya watalii. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni muhimu sana pia wakahakikisha wanakuza utalii wa ndani. Kuna baadhi ya maeneo, mimi natoka Wilaya ya Karatu, Wilaya ya Karatu ina hoteli za kitalii 54, wako Watanzania ambao hawajui. Mtanzania yuko Dar es Salaam anafikiria kwenda kupumzika South Africa lakini kumbe angekuja kupumzika Karatu kuna hoteli nzuri, zile ambazo wanazifuata nje ya nchi pia ziko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, una hoteli nzuri sana ambazo wageni wengi wanapenda kulala pale halafu wanakwenda kutembea Ngorongoro. Wilaya kama hizi ambazo ziko pembezoni mwa Hifadhi ya Ngorongoro ambayo ni sehemu ya lango la kuingilia Ngorongoro tayari kuna hizi hoteli za wawekezaji na wazawa pia wamejitatidi kujenga hoteli za standard mbalimbali, unakuta kuna hoteli ya mpaka kulala siku moja ni karibu dola 700, hoteli yenye standard na quality ya juu kuliko labda hizo mnazofuata South Africa na kwingine, ziko Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu pia Wizara wakaangalia Wilaya kama hizi ambazo tayari kuna hoteli kama hizi wakazitangaza, wakafanya utalii wa ndani pia wakawa na *target* ya kukuza utalii wa ndani na si tu kuangalia *target* ya kukuza utalii wa wageni kutoka nje. Kwa hiyo, ni muhimu sana wakalitazama hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kuhusu TANAPA. TANAPA ina jukumu la msingi la kusimamia hifadhi za Taifa, uhifadhi wa wanyamapori na shughuli za utalii. Leo TANAPA mapato yake yote yanapelekwa kwenya pool moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini hawa baadaye wakitaka kutekeleza shughuli zao maana yake waje tena waombe huko, kwa maana ya Hazina au Mfuko Mkuu wa Serikali waweze kwenda kutekeleza majukumu yale. Mfano, leo pale Ziwa Manyara liko chini ya hifadhi ya TANAPA linapotea kwa sababu limejaa tope hakuna kinachofanyika. TANAPA wanakusanya fedha badala nyingine zirudi kwenda kutekeleza zile shughuli zinapelekwa Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wanaipa TANAPA kazi ya kutengeneza madawati nchi nzima halafu Waheshimiwa Wabunge wanapongeza wakati TANAPA ina kazi ya kudhibiti ujangili, ina kazi ya kudhibiti na kuhakikisha kunakuwa na uhifadhi endelevu, ina kazi ya kuhakikisha mfano Ziwa Manyara linaendelea kuwepo? Mheshimiwa Waziri baada ya miaka 10 au 20 Ziwa Manyara linapotea kwa sababu limejaa tope maji yale yanakuwepo tu msimu wa masika baada ya muda ni tope linajaa pale. Kwa hiyo, ni muhimu sana Wizara wakaangalia shughuli za TANAPA zisiweze kusimama. Haiwezekani wao wanakusanya fedha wanawapelekea halafu mwisho wa siku yale majukumu yao ambayo wanapaswa kuyafanya hawawezi kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bulaya atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi na Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba ajandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipompongeza dada yangu Mheshimiwa Esther Matiko kwa hotuba yake nzuri ambayo inaonesha wanawake tunaweza, hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwambia Mheshimiwa Maghembe kwamba tutakayoyachangia hapa ndiyo atatudhihirishia ule msemo wa Kinana kumwita ni mzigo au lumbesa ni kweli au atudhihirishie hapa yeye ni mwepesi kama *tissue*.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema hayo...

### KUHUSU UTARATIBU

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa keti.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya sitini na...

**MWENYEKITI:** Ngoja, ngoja. Mheshimiwa huwezi kuanza kuongea kabla sijakuruhusu, sema sasa utaratibu, niambie kifungu. (Makofi)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu Kanuni ya 68(1) lakini Kanuni ya 64(1)(g). Maneno yaliyosemwa na Mheshimiwa Mbunge anayechangia ni maneno kwa kweli ya kudhalilisha siyo maneno mazuri. Huwezi kumfananisha Mbunge kwamba atafananishwa na tissue. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana mdogo wangu Mheshimiwa Ester ana uwezo wa kujenga hoja vizuri sana. Nimsaidie tu asivunje Kanuni hiyo ya 64 atumie maneno ambayo yanaweza ku-deliver massage yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Kwa hiyo, kusema mzigo ni sahihi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya sijakuruhusu kuongea, hebu keti, hebu twende vizuri. Kanuni ya 64 ni katazo, amesema ametumia neno tissue, tissue ni karatasi nyepesi lakini katika muktadha ambao umeutumia kwa jinsi nilivyosikia umesema Waziri ajithhibitish kama yeye siyo mzigo kama alivyosema fulani leo au yeye ni kitu chepesi. Unafahamu kwa nafasi hizi, pamoja na kwamba lazima tuwe na vifua vipana, huyu ni Waziri wa Nchi ya Tanzania, wewe ni Mbunge, nakuagiza tu hebu futa haya maneno 'nyepesi' twende mbele.

**MBUNGE FULANI:** Huyu ni baba yake mzazi kabisa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namaanisha ‘wepesi’. Sasa aseme Kinana kutumia ‘mzigo’ sawa, sisi tukisema ‘tissue’ kwa maana ya wepesi, aseme siyo mzigo. Nimevunja Kanuni ipi hapo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya sasa unabishana na Kiti? Mheshimiwa Bulaya useme tu kama unakaidi maneno ya kufuta au... (Makof)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Nimemaanisha ‘wepesi’.

**MBUNGE FULANI:** Futa maneno.

**MWENYEKITI:** Futa maneno tu hayo ‘wepesi’ twende mbele.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Nifute nini Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Aah basi, mimi nitamwita mtu mwingine kuchangia.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya Waziri kutupangia Wabunge tuseme nini siyo nzuri. (Makof)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya keti kitako, keti tu.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mimi nimekuagiza futa neno ‘wepesi’ twende mbele.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Nasema hivi, kama ‘tissue’ linakwaza namaanisha ‘wepesi’ basi ‘tissue’ litoke ‘wepesi’ libaki pale pale. Atuambie kama yeye ni mzigo au mwepesi. (Makof)

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kujua, nilipomaliza uchaguzi nilienda Ngorongoro, sikwenda South Africa kama wanavyoenda wengine, kuna mbuyu pale una eneo kama sebule, majangili walitengeneza ndani ya hifadhi ya Tarangire. Nataka kujua, tangu Wizara yake imegundua nchi yetu imepoteza tembo wangapi? Yaani majangili wanaenda

kwenye mbuga, wanatengeneza mbuyu unakuwa kama sebule na askari wapo halafu tunaambiwa baadaye ndiyo waligundua. Tunataka kujua waliohusika na eneo hilo walichukuliwa hatua gani? Hilo ni jambo la msingi. Akitujibu hayo, nitajua yeze mwepesi au mzigo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine limeongelewa kwenye Kambi ya Upinzani kuhusiana na kampuni iliyopewa kuwinda, Waziri ametoa barua tena wakati Waziri aliyejusika aliinyima. Miogoni mwa waliokuwa Wajumbe kwenye Tume ya Uwindaji jana alipokuwa akichangia Mheshimiwa Nsanzugwanko alisema watu wale walikuwa hawaifuati taratibu na inasemekana walishaua mpaka na simba. Sasa ni sababu zipo ambazo Wizara hiyohiyo moja ina maamuzi mawili tofauti kwenye hiyo kampuni inayolalamikiwa haifuati taratibu, huyu ananyima kibali, huyu anakuja kurudisha, kuna kitu gani? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kimezunguka hapo? Yaani huyo mtu anachezea tu sharubu za Wizara anavyotaka. Tunaposema haya, tunayaongea kwa sababu hatuhitaji Serikali ichezewe na hao mapapa. Haiwezekani Wizara hiyohiyo moja mnakuwa na maamuzi mawili kwenye kampuni moja yaani mnapingana na Tume yenu ya Wanyamaporii? Kweli, atujibu mzigo au mwepesi? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukichangia humu ndani kuhusiana na mambo ya wakulima na wafugaji. Jimboni kwangu nina hifadhi, wakulima na wafugaji, yote nayahitaji. Kama kiongozi, siwezi nikaja hapa nikasema nahitaji uhifadhi halafu eti najitoa wazimu nasema nawachukia wafugaji, sitakuwa natenda haki. Wala sisemi kwamba napenda wafugaji halafu niseme sihitaji uhifadhi, sitakuwa nalitendea haki Taifa langu. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili hili hawezi akalimaliza kwa kauli, hawezi kulimaliza peke yako, lazima Wizara zote tatu zikae na tukubali kwamba fulikosea, hatukuwa na mpango bora wa matumizi ya ardhi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa alisema kukiri kukosea siyo shida, ni mwanzo wa kuijpanga upya. Taifa letu lilikuwa halijajipanga kwa future kwenye matumizi bora ya ardhi. Leo hii ukiwa unatoka Hong Kong ukapanda treni unaenda Guangzhou utaona upande huu ni mashamba ya kilimo na upande huu kuna mashamba ya mifugo, hakuna mwingiliano pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua hatujapanga matumizi bora ya ardhi na hawa wafugaji bado hatujawafatutia soko la kutosha. Tujiulize leo tuna viwanda vingapi? Tunalamika wengi, tuna mkakati gani wa kuhakikisha wanafuga mifugo ya kisasa na wanapata soko ndani ya nchi yao kuliko kuja hapa kama viongozi tunapasuka humu ndani, hivi tukitoka nje tunaweza kulisaidia Taifa letu? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ya msingi lazima Mheshimiwa Waziri wa Maliasili akae na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Waziri wa Ardhi ili kuona ni namna gani tunaweza tukalitatua tatizo hili lakini kwa Wabunge kutupiana mpira humu ndani hatuwezi kufika na tusicheze na vita ya ardhi, ni mbaya sana. Mheshimiwa Waziri, hili ni jambo nyeti, jambo linalohusu Taifa letu, kama tumeshindwa kugombana katika uchaguzi, hatuhitaji ardhi yetu ije itugombanishe. Lazima tutengeneze mazingira mazuri ya vizazi vyetu siyo kuja kugombana humu ndani ya Bunge. Sisi ni viongozi, lazima busara itutawale katika kutatua migogoro hii, siyo kwa kauli tu ondokeni, mnakowapeleka kuna malambo au mazingira yakoje? Hilo ni jambo la msingi sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la tozo kwenye hoteli, nilikuwa Mjumbe wa Kamati, naomba jambo hili Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa muktadha wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther amezungumzia hapa kwamba kuna shilingi bilioni tatu zinapotea lakini tangu kesi ilipokuwa mahakamani Serikali imepoteza zaidi ya shilingi bilioni nane. Leo Wizara hii inashindwa kukazia hukumu wakati Jaji amekuwa mzalendo kwa Taifa lake, kuna nini hapa au hawa watu wenye hoteli bado na wenyewe wanaichezea Serikali wanavyotaka? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kusitiza, duniani kote hakuna utaratibu wa *double entry*, utaratibu ni *single entry*. Mheshimiwa Waziri, mtalii anaingia akitoka lazima aliipe tena, tunaona katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nije Jimboni. Nilizungumzia suala la wananchi wangu kuhusu tatizo la mamba, Naibu Waziri akajibu amekwenda kupeleka swali langu katika Halmashauri ya Wilaya, mimi niko ya Mji ndiyo maana alipewa yale majibu. Mimi mwenyewe ofisi yangu ya Mbunge nimehudumia zaidi ya wananchi wanne Mheshimiwa Maghembe, kuna tatizo hili na nashukuru Mheshimiwa Waziri alikiri kwamba ataenda kulifuatilia. Peleka tu watu wa kuvua hatujaomba pesa ili wananchi waondokane na tatizo hili la mamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, wananchi wangu hawataki kuomba chakula. Wanalima lakini tembo wanakuja kuharibu mazao ya wananchi. Hawa nao wameingia kwenye hifadhi? Mheshimiwa Maghembe, please wananchi wa Mara wanaona haya kuomba, tunalima! (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu wa Nyatwali, Tamahu, Serengeti, Kunzugu, Mihale, Bukole, Mihale nilienda na Mheshimiwa Jenista ameona mwenyewe shamba lilivyoharibiwa. Mkasema mtapeleka magari kule hawafanyi patrol, juzi tembo wamekula heka 20, please, tafuteni ufumbuzi wa

kudumu. Watu hawafanyi *patrol* tuone ni namna gani hawa wananchi wataondokana na tatizo la kuliwa mazao yao. Namwomba sana Mheshimiwa Maghembe ashughulikie suala hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, wananchi wangu wa Kijiji cha Serengeti, Tamahu, Nyatwari wanataka kujua hatma yao maana wanatishiwatishiwa kuhama. Hawajapewa fidia, hawajashirikishwa na kuna maendeleo kule kuna shule, zahanati na kuna kila kitu. Haiwezekani mtu akaamka tu akawambia leo mnahama bila kuwashirikisha wananchi. Kuna wazee pale wa miaka mingi lazima haya mambo yaye wazi. Wanahama mnawapeleka wapi, kwa fidia ipi, mbona hamjawashirikisha? Hayo ni mambo ambayo nataka anipatie majibu ili nimpime yeye ni mzito au mwepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi na Mheshimiwa Zainab Katimba ajiandae.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda tu nimshauri Mheshimiwa Waziri ili anapokuja wakati mwingine kwa sababu hii ni bajeti yake ya kwanza ajaribu sana kuangalia yale masuala ambayo ni *controversial* ili yaweze kuingia kwenye taarifa tusiwe na kuhoji wala kushauri kwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nijikite katika masuala machache sana kutokana na muda wenye kwa mfupi. La kwanza ni katika sekta hii ya utalii ambapo Serikali inapata pato la Taifa asilimia 17.5, ile GDP. Hii ingeweza kuongezeka zaidi lakini inategemea na matatizo ambayo wanayo wale *tour operators* wetu ambao wako nchi za nje kwa maana ya kwamba ile *package* wanayochaji pesa za nje zinabaki kule Serikali inapata kiduchu, inaambulia patupu. Naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa atuletee mikakati ambayo itakuwa ina tija ili Serikali iweze kupata pesa nydingi zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, hapa Waheshimiwa wengi wanazungumzia suala la concession fee, ni kweli hili jambo Serikali imekuwa ikipoteza fedha nydingi sana na kama tunavyoelewa TANAPA ni shirika kubwa sana na linafanya kazi nzuri sana. Pamoja na hayo, ninachoelewa ni kwamba TANAPA wameshatoa mapendekezo yao kwa ajili ya kuongezea pato Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, lazima tujiulize Waheshimiwa wengi wamesema concession fee imechukwa muda mrefu hivyo, TANAPA mpaka leo hii, zaidi ya miaka miwili na nusu haina Bodi, masuala mengine hata hili suala la concession fee haliwezi kufanyika bila Bodi ku-approve. Kwa hiyo, pamoja na kwamba suala la Bodi pia Mwenyekiti lazima ateuliwe na Rais, ni jukumu la Mheshimiwa Waziri kama mwenye dhamana kuhakikisha kwamba ana-push TANAPA iweze kuwa na Bodi ili masuala mengine kama haya ya concession fee yaweze kwenda mbele. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo katika Shirika hili la TANAPA, Wabunge wengi hapa ndani wamelipongeza. Ni kweli linafanya kazi vizuri, wote ni mashahidi tunajua kabisa kwamba katika programu yao ya CSR, mikoa 16, wilaya zaidi ya 55 zinazopakana na hifadhi wamechangia madawati shilingi bilioni moja, hii ni kazi nzuri. Kama vile haitoshi bado TANAPA ni mojawapo ya mashirika machache ambayo yanachangia gawio kubwa sana kwa Serikali. Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika suala zima la misitu. Waheshimiwa wengi hapa wamechangia, utoaji vibali vya uvunaji ni jipu. Ni jipu kwa sababu hili limekuwa ni tatizo kubwa sana, huko hakujakaa vizuri kabisa, wananchi wanlanguliwa vibali vya uvunaji, vinatolewa kwa kujuana, wanauziana wale wale, vibali hewa. Mheshimiwa Waziri asipokaa vizuri hapa tunamtolea shilingi maana sisi wengine tunatoka katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Kwa hiyo, tunataka mkakati wa kina katika suala zima la utoaji wa vibali vya uvunaji na mbinu mbadala tunataka iwepo na yenyewe atuletee majibu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema pesa nyingi zinapotea katika sekta hii ya utalii tunamaanisha. Pale Ngorongoro, pamoja na mengineyo, suala zima lile la *smart card* kwenye gate fees ni tatizo. Naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa atueleze pia suala la *smart card* kwenye gate fees likoje? Maana vilevile pale kuna utata, pesa nyingi sana inapotea, hili jambo ni very serious na lishughulikiwe mara moja. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije katika migogoro hii ya wakulima, wafugaji pamoja na hifadhi. Kwenye Bunge lililopita nilikuwa katika ile Kamati ya Operesheni Tokomeza Ujangili. Kwa hiyo, ninaposema hivi nina uhakika tulijiona nini katika suala zima la migogoro ya hifadhi, wakulima na wafugaji. Nawashukuru sana Waheshimiwa wengi ambao wamechangia hapa uhifadhi una maana yake, uhifadhi una umuhimu wake katika katika Taifa letu, wakulima wana umuhimu wake na wafugaji wana umuhimu wake, nini kifanyike hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote hapa tumetokana na uhifadhi, tumetokana na wakulima, tumetokana na wafugaji, lakini kila mtu akisimama akaanza kufagilia yale mambo ya kwake hatutafika hata huo uhifadhi pia utakufa. Kwa hiyo, nini kifanyike hapa, Waziri wa Maliasili awasiliane na Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Sheria, Wizara ya Ardhi pamoja na watalaam na watendaji wao, wakae chini, sheria ni msumeno, watuletee masuala ambayo yataleta tija, sheria itumike. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna wenzangu wengine hapa wameuliza kuhusu Operesheni Tokomeza Ujangili, Bunge lililopita sote ni mashahidi. Baada ya sisi kusoma ile taarifa yetu hapa, Mawaziri wanen walistep down. Mheshimiwa Rais akaunda Tume ya Majaji mpaka leo hii hatujapata taarifa ili tuweze kujuu haki ilitendekaje ama namna gani? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu ni mchache, naomba niunge mkono hoja. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nichangie katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kumteua Profesa Jumanne Maghembe kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Tunamtambua Mheshimiwa Maghembe yeye ni profesa, ni mtalaam na tuna imani naye sana kwamba atawenza kuingoza vizuri Wizara hii. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake wote wanatosha na wanafaa kuiendesha Wizara hii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine ni Walimu tumetoka mashulenii, tunafundisha watoto nidhamu na nini wafanye au ni wakati gani wazungumze na mazungumzo hayo yatolewe kwa wakati gani? Tunakwazika, tunachanganyikiwa tunapoona zinatolewa sentensi nyingine hazieleweki ndani ya Bunge. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nirudi kwenye hoja yangu. Wabunge wenzangu wamechangia mengi sana, lakini naomba nichangie katika eneo la misitu. Serikali ilikuwa na nia njema sana ya kuhifadhi maeneo ya ardhi yetu kwa kuweka misitu kwa akiba ya baadaye lakini pia katika kusaidia kuboresha mazingira lakini kila panapokuwa na jambo jema halikosi kuwa na ubaya ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hizi hifadhi kwa mfano sisi tunaotoka maeneo ya Mbagala kuna hifadhi ya Mwandege, hifadhi hii haiendelezwi, haina usafi, matokeo yake imekuwa ni makazi ya majambazi. Majambazi yanakuja yanaua watu Mbagala, Temeke, Vituka huko yanakimbilia kwenda kujificha katika msitu huu wa Mwandege. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima nitoe pongezi za wazi kwa Kamanda wangu wa Polisi wa Mkoa wa Dar es Salaam, Kamanda Siro, amekuwa akifanya operesheni na katika operesheni yake idadi kubwa ya majambazi, majangili, magaidi, yamekamatwa katika msitu huu wa Mwandege uliopo Mkuranga. Hili sasa limekuwa tatizo badala ya raha. Kweli tuna nia njema ya kuhifadhi msitu ule lakini kwa hali ilivyofikia sasa hivi msitu ule ni tatizo kwa wakazi wa Dar es Salaam hususan wakazi wa maeneo ya Mbagala. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuna changamoto nyingi sana katika maeneo haya lakini niiombe Serikali sasa hivi Mkoa wa Dar es Salaam una matatizo makubwa ya ardhi lakini pia kuna msongamano wa magari usiokwisha katika maeneo ya Mbagala. Niiombe kabisa Serikali kwa nia njema kwa nini wasipunguze eneo la msitu huu wakatengeneza kituo kikubwa cha mabasi kuondoa ule msongamano uliko pale Mbagala Rangitatu? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo hivi huu msitu mwisho wake ni nini? Msitu huo umekuwa ukiingiliwa na wakazi kwenye maeneo yote ya pembezoni lakini wakati watu wale wanajenga nyumba Serikali inawaangalia, kesho na keshokutwa Serikali inakuja kuwavunja zile nyumba, hawaoni kwamba wanawaonea wale wananchi? Dar es Salaam imejaa, maeneo ya ujenzi yamekuwa machache watu wanaanza kumega kidogokidogo pemberi mwa msitu ule, Serikali inawaona, Maafisa Misitu wapo hakuna wanachowaambia. Sasa mimi kama Mbunge ole wenu mkawaambie wale watu waje wavunje nyumba zao. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie gharama za tozo za misitu. Katika maeneo ya Mkuranga kwenye kituo cha Mkuranga ukitaka kupitisha kitanda kimoja gharama yake unalipia Sh.120,000/=, kitanda hicho kiwe cha zamani, kiwe kipyä au kabati liwe la zamani au liwe jipyä. Sasa Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani maeneo ya Mkuranga umeungana, mtu anaweza kuhama kwenye nyumba Mkuranga akahamia Mbagala Temeke, akahama Mwandege akahamia Kongowe. Sasa hizi gharama wakati mtu anahamahama atakuwa anatozwa Sh.120,000/= kila anapohama kutoka huku kwenda kule, hii kweli ni sawa, huu siyo uonevu? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie hiyo sheria inavyosema kwamba watu wanapotoa kitanda au mazao yoyote ya misitu kutoka huku kwenda huku kulipa gharama kubwa. Kitanda cha futi tatu hapa Dodoma

kinauzwa Sh.180,000/= wewe unalipiwa ushuru Sh.120,000/= hivi jamani hii ni kweli! Niombe kabisa Serikali iangalie eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwenye manunuzi ya mkaa, unakuja pale Mkuranga ukitoka Rufiji unakuta kuna barrier kibao, mbona wenzetu huku Dodoma hakuna barrier za aina ile? Kwa nini kule kumekuwa barriers hizo kila sehemu unatozwa tozo mpaka unachanganyikiwa. Niombe hilo nalo liangaliwe. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niingie kwenye eneo la utalii. Nitazungumzia utalii wa mambokale au wa maeneo ya kihistoria. Kuna maeneo ya kihistoria yanapotea, maeneo kama Bagamoyo, Kaole, Kunduchi, Isimila, Olduvai Gorge, Mapango ya Amboni, Mikindani, Kilwa Kisiwani, Songomnara, yote hayo ni maeneo ya kihistoria ambayo kama yataboreshwa yangeweza kutuletea mapato makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya hayawekewi bajeti nzuri ya kuyaendeleza matokeo yake yanamasbaratika, urithi ule wa kihistoria unamasbaratika. Kwa hiyo, niombe Serikali iweke bajeti ya maeneo hayo. Pia maeneo haya hayana *information* yoyote, hujui hiki kiko wapi wala kile kiko wapi. Kwa hiyo, niombe Serikali iyatolee maelezo maeneo haya lakini pia iyatangaze. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye nchi za wenzetu, kwa mfano unakwenda India, unakuta ushawishi mkubwa, wewe kama mgeni unaambiwa nenda Taj Mahal, huelewi, mara nyingine unafuata tu mkumbo lakini sisi mbona tumekuwa kimya! Mtalii anakuja hapa, hakuna maelezo yoyote, hakuna *promotion* yoyote, unaingia kwenye ndege mpaka unafika Dar es Salaam hata huambiwi kwenye ndege Dar es Salaam utakumbana na kitu gani cha kitalii au ukaone maeneo gani ya kitalii, hili kwa kweli ni tatizo. Niombe sasa Serikali yetu ibadilike, itangaze vyanzo vyake vya utalii vizuri ili wageni wanapoingia wavitambue na waende wakavitembelee. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Mkoa wangu wa Dar es Salaam kuwa mji wa kihistoria. Hakuna ambaye hafahamu kwamba Dar es Salaam ndiyo mji mkuu kuliko mikoa yote ya Tanzania lakini wapi Dar es Salaam imewekwa, wapi Dar es Salaam imepangwa kiutalii, tujue Dar es Salaam hii inakwendaje au tunamshawishije mtu wa kutoka nje akiingia Dar es Salaam aweze kutambua kwamba anaingia kwenye mji mkuu, mji bora, mji ambaa una mambo yote muhimu, hata uhuru wa nchi hii bendera yake ilipandishwa katika Mkoa wa Dar es Salaam, Uwanja wa Taifa. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali, najua mpango huu ulizungumzwa hapa lakini ukaishia, je, imepanga mkakati gani wa kuitangaza Dar es Salaam sasa? Tunataka Dar es Salaam uwe mji wa kitalii na utangazike na watu walioko nje wautambue. Ndiyo wenyewe uwanja mkubwa wa Kimataifa, Serikali imejenga ule uwanja, uwanja ule ni wa nini, wa kushusha na kupandisha tu, ni lazima ulete soko la watalii. Kwa hiyo, niiombe Serikali ipange mpango mkakati wa kuitangaza Dar es Salaam kama mji wa kitalii. (Makofij)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na kama nilivyo sema mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Zainab Katimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Norman King na Mheshimiwa Ulega ajiandae. Mheshimiwa Zainab Katimba hayupo basi tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wenzangu walivyochangia, nimpongeze Profesa Maghembe na wenzake kwa kazi nzito waliyonayo. Mmoja alisema mzigo mzito mpe Mnyamwezi nadhani kwa mzigo huu hata Mnyamwezi anaweza akashindwa kuubeba. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimemsikiliza sana Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Profesa Maghembe nikafikiri sikumsikia vizuri. Nikaisoma hotuba yake nikaridhika kwamba nilichosikia jana ndicho kilichoandikwa. Nimesikitika sana kuona katika kitabu chake chote ameacha hifadhi pekee ya maua kwenye Bara letu la Afrika lakini ukisoma kitabu chake, utalii Tanzania unapungua. Yeye hasemi chochote kabisa kuhusu habari ya kuendeleza Hifadhi ya Kitulo iliyoko Makete, hasemi chochote kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Makete wa Kata za Mfumbi, Mlondwe, Matamba, Kinyika, Ikuwo, Kigala, Ipelele pamoja na Kitulo yenyewe, wamehamishwa ili kupisha hifadhi hii muhimu. Sasa miaka inakwenda Wizara haifanyi chochote na bahati mbaya sana kwenye hotuba ya Waziri hasemi chochote kabisa juu ya mkakati wake wa kuendeleza Hifadhi ya Kitulo. Nimesikitika sana na nasikitika sana, kwa vyovvye vile sitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi utalii katika nchi yetu unachangia kiasi kikubwa sana cha Pato la Taifa lakini mkakati wa Wizara ni nini kuongeza watalii? Hasemi chochote juu ya kuboresha Hifadhi ya Kitulo, hasemi chochote juu ya kuboresha miundombinu ili angalau sasa watalii waone Makete kwenye Hifadhi ya Kitulo ni sehemu ya kukimbilia. Sikutaka kushawishika kwamba Mheshimiwa Profesa Maghembe yeye anaziona hifadhi zilizoko Kaskazini tu, sikutaka kufika huko, lakini naanza kushawishika. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana, ni lazima Waziri aje na majibu ni jinsi gani anafanya kwenye bajeti hii kuwafanya wananchi wa Makete ambao wanaitunza hifadhi hii, wamehama kuacha maeneo yao wasilime ili kuheshimu Pato la Taifa, basi wagawane Watanzania wote, maana wangelima wao mapato yale ni ya kwao. Wamepisha ili sasa hifadhi hii iwe mali ya Watanzania wote. Waziri atoe majibu hapa anaifanyia nini hifadhi hii ili kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba Ngorongoro na Serengeti zimetajwa lakini Waziri anafahamu moja ya sifa zilizopelekea Hifadhi zetu za Ngorongoro, Serengeti na Manyara kuongeza watalii ni baada ya kuboresha miundombinu hasa barabara ya kutoka Arusha kuelekea Manyara na Monduli pia kuelekea kwenye lango la Ngorongoro, Kitulo mnafanyaje? Ni wazi ni lazima barabara ya kutoka Chimala – Matamba – Kitulo - Makete ijengwe kwa kiwango cha lami ili kuimarisha utalii kwenye hifadhi hii, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tufikiri *heuristically* kwa sababu ni kweli utalii ni *leisure*, utalii ni burudani, siyo mateso. Hakuna mtalii atakayekwenda Kitulo kama miundombinu mingine haionyesi kuwasaidia wao. Sambamba na hilo, ndiyo maana nilimfuata Mheshimiwa Profesa Maghembe nikasisitiza umuhimu wa TANAPA kuweka hoteli au kutengeneza mazingira ya kuweka hoteli za kitalii eneo la Matamba ili kuboresha au kuongeza Pato la Taifa, kwenye hotuba yake, kimya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kidogo kuhusu mwingiliano wa mipaka kati ya mifugo pamoja na hifadhi zetu. Kwa suala hili ni lazima Serikali ijipange, bahati nzuri mimi natoka wilaya ambayo ina wachungaji wa ng'ombe, ina wafugaji wa ng'ombe, ina wakulima na pia ina hifadhi. Narudia, ina wachungaji, ina wafugaji na ina wakulima lakini hifadhi pia inayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani dhana hapa, pia weledi kidogo unatofautiana kwenye kufasili kwa usahihi juu ya wachungaji wa ng'ombe. Duniani kote inajulikana, ukisema unafanya kuchunga, wachungaji wote wanafuata malisho, nchi zetu hizi ni za *ki-tropic*, kwa hiyo mvua ina kiangazi na masika. Wakati wa kiangazi lazima mchungaji, siyo mfugaji, mchungaji atahama na mifugo yake kufuata malisho, lazima ugomvi na wakulima utakuwepo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana naunga mkono hoja iliyotolewa na Mbunge wa Mbinga Mjini, Mheshimiwa Sixtus kwamba Wizara lazima wakae, *and on this you must be strict*. Hamuweze ku-compromise na Wabunge kwa sababu *its impossible*, kama anatoka eneo ambalo watu wanachunga nitatetea wananchi wangu na ndiyo sifa kwangu. Ninyi lazima mje na ukweli

kwamba pamoja na kwamba unatetea wachungaji wako lakini dunia ya sasa ni ya kufuga siyo ya kuchunga, lazima tuelewane hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara husika ishirikiane na Wizara nyingine kutengeneza mkakati amba ni endelevu. Ni lazima tutafika mahali tutachagua, tunataka hifadhi au tunataka ng'ombe wa kuchungwa. Kama tunataka wa kufuga, yes you can set aside a piece of land kwa ajili ya kuchunga lakini huwezi kutengeneza eneo kwa ajili ya kuswaga ng'ombe, haiwezekani, kiangazi kitaingia lazima watatafuta malisho. Sisi amba tumetumika sehemu mbalimbali kwenye eneo ambalo ni la wafugaji zikiwemo Wilaya za Hai, Siha, Mbeya, Songea na Makete kwenyewe tunajua, uko mtihani mkubwa wa ku-harness kati ya ufahamu wa kuchunga na kufuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize hoja yangu kwa kusema, ndiyo maana nilisema Mwalimu Nyerere na Mzee Karume wamezikwa kaburini lakini wana hekima kuliko sisi, wao waliweka shamba la mifugo Kitulo ili wachungaji wakajifunze kufuga Kitulo. Bahati mbaya Serikali haisemi chochote kuhusu hili. Ni muhimu sana shamba lile lifufuliwe ili wachungaji, waswagaji wa ng'ombe wajue kwamba zama za sasa ni kufuga siyo kuchunga siyo kuswaga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ifufue shamba la mifugo la Kitulo lililopo Makete pamoja na hifadhi ile ili liwe shamba darasa kwa mikoa yote Tanzania. Tutapona na tutaondoa migongano kati ya wafugaji na wakulima, vinginevyo haiwezekani, narudia, vinginevyo haiwezekani. Ukitaka kutibu hili ni lazima ukumbuke shamba darasa ni shamba la mifugo kule Makete, lakini Hifadhi ya Kitulo ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize, nakusudia kushika shilingi kama Waziri, Mheshimiwa Profesa Maghembe hatakuja na majibu ya kwa nini katika mpango wake Hifadhi ya Kitulo ameiacha kirahisirahisi tu, ameiacha tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Ulega atafuatiwa na Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza na Mheshimiwa Yahaya Massare ajiandae.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nikushukuru kwa nafasi hii niliyoipata ya kuchangia bajeti ya Wizara yetu hii ya Maliasili na Utalii. Pia naomba niendelee kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Maghembe na kaka yangu Naibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Ramo Makani. Nataka tu niwaambie kwamba wafanye kazi na wala wasitishike na haya manenomaneno mengine ya kuwavunja moyo na sisi tunaelewa juu ya weledi na uwezo wao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine hata mimi naanza kushawishika kuunga mkono wale wanaofikiria kwamba kabla hatujaingia kwenye jengo hili tuwe tunapimwa pale kama tumevuta hata *marijuana* hivi. Katika hali ya kawaida, kijana hata kama umepigiwa kura na kuaminiwa na wananchi ukaenda kumtukana mzee wa namna ile na kumuita majina ya hovyo, lazima utakuwa una tatizo kidogo katika akili yako, siyo wa kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imedhihiri hata jana, yupo mwenzetu mmoja hapa wa kutoka katika chama ninachotoka mimi amezungumza mambo ya ajabu sana hapa. Unaweza ukaona ni kwa namna gani watu hawaelewi ni nani katika nyumba hii ameingia bila ya chama kilichomleta hapa. Wote kwa umoja wetu, iwe wa upinzani, iwe wa chama kinachotawala, sisi tumezaliwa na vyama vyetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima sisi kama viongozi tujue wajibu wetu na hii michezo haitaki hasira. Wala usidhani kwamba wewe ukiwa na hasira sana ndiyo hoja yako itafanikiwa, la hasha! Wakati mwingine unajielekeza tu katika kukata udugu. Nataka nikuhakikishie sisi kule kwetu tunasema mkataa udugu kala hasara huyo! (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme juu ya misitu na Mheshimiwa mama Mariam Kisangi amesema vizuri hapa juu ya msitu, mkaa na vitu vya namna hiyo. Nafahamu kwamba mkaa, kwanza naomba ni-declare interest, mimi ni mwana mazingira na profession yangu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni Shahada ya Sayansi ya Mazingira. Nina weledi mzuri na mkubwa sana juu ya masuala ya mazingira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Dar es Salaam nyumbani kwetu na Mkuranga yake watu wanaendelea kutumia nishati ya mkaa na Serikali tunajua kwamba inapiga vita matumizi ya mkaa. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba nguvu tunayoitumia katika kupiga vita matumizi ya nishati hii ya mkaa, tutumie nguvu hiyohiyo katika kuhakikisha tunawatafutia nishati mbadala wananchi hawa. Watu wanapata shida sana, watu hawaelewi wafanyaje, tunawaambia watumie gesi, hata elimu yenye ya matumizi ya gesi inafahamika? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya gesi hayakuanza leo, watu walio wengi, hata wasomi wenyewe wanaogopa kutumia majiko ya gesi maana yameua watu wengi sana katika nchi hii. Wewe mwenyewe unafahamu mwaka mmoja, mwishoni mwa miaka ya tisini, hoteli ya Kibodi ya Dar es Salaam katikati ya mji iliungua moto kwa sababu ya jiko la gesi. Sasa tufanye jitihada ya kutoa elimu, kabla ya kusema kwamba watu hawa wasitumie mkaa,

tumefanya jitihada gani ya kuwaelimisha, tumefanya jitihada gani ya kupoletka nishati mbadala? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti imezungumzwa hapa kodi ya vitanda nami naunga mkono hoja ya kodi hii ya vitanda ni lazima itazamwe, lasivyo yanaendelea kuwa ni yale yale ya kutokuwasidia watu hawa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa Msitu wa Mwandege pale Mkuranga, kile kimekuwa ni kichaka cha majangili. Mkuranga yenyewe imetajwa kama ni eneo ambalo si salama sana. Wewe mwenyewe unafahamu kwamba walikamatwa pale watu zaidi ya 50 na bunduki, wamezificha. Haukupita muda mrefu Benki yetu ya NMB pale Mkuranga ikavamiwa na majambazi. Hatujakaa muda mrefu Benki ya Access pale Mbagala Rangitatu ikavamiwa na majambazi. Hawa wote wanakimbilia kwenye msitu huo huo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kumwambia Mheshimiwa Waziri, kama tunashindwa kwa kuwa hatuna pesa za kutosha za kuutunza msitu ule Dar es Salaam imejaa, ni kweli. Eneo lile ni kubwa sana linachukua vijiji zaidi ya vinne Mwandege yenyewe, vikindu, Mlamleni Luzando na kwingineko. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitenge eneo lile dogo tupate eneo la kutosha pale tujenge kituo cha kisasa, watu wanaotoka Mikoa ya Kusini hawana haja ya kwenda na mabasi yao mpaka Ubungo mpaka Dar es Salaam. Waishie pale Mkuranga waingie kwenye shuttles waende Dar es Salaam hii itatusaidia tutapata pesa tutafanya msitu ule kuwa ni botanical garden. Badala ya kuuweka tu vile kuwa ni kichaka cha majangiri. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niseme juu ya ng'ombe na hasa hao wanaoingia katika maeneo ya hifadhi. Juu ya wakulima na juu ya ng'ombe imeshazungumzwa sana. Naomba niseme wazi hapo kwetu sisi ng'ombe ni kitu kipyä, hapa nasema jambo jipyä kabisa. Kwanza zamani tulikuwa tunamwita mdudu, leo tumeletewa ng'ombe wengi sana na ugomvi ni mwangi sana pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyosemwa na wenzangu ni lazima tutafute suluhisho la kudumu la jambo hili, wakulima wetu hawamjui ng'ombe na wala hawana haja ya kumjua. Eee!

Mheshimiwa Mwenyekiti, issue ya misitu tena katika mazingira naomba nimwambie jambo moja Mheshimiwa Waziri kwamba hili jambo liwe ni two way traffic. Mpaka hivi sasa sisi tunatumia nguvu nyingi sana juu ya kulinda hifadhi zetu lakini bado hatujajifunza. Nilipokuwa Mkuu wa Wilaya kule Kilwa ninao

mfano mzuri sana wa Kijiji cha Nanjilinji, tulikuwa na jambo kule la hifadhi ya misitu ya jamii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Nanjilinji kimefanikiwa sana katika uhifadhi wa jamii wa misitu yake. Leo mtu akikuona umeshika fito hawezi kukuelewa, lazima atakuchukulia hatua yeye mwenyewe pasipo kwenda na askari wa games wala jambo la namna gani. Kwa hivyo, hebu tuiangalie sera yetu vizuri hapa, namna ambavyo tunaweza tukawashirikisha jamii tukawasakiya ili wao wenyewe wawe walini wa rasilimali hizi badala ya kutumia maguvu mengi sana ambayo wakati mwingine wala hayana tija na yanatupoteza pesa zetu nyingi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji nawahakikishia watani zangu Wasukuma na wengineo watoe mifugo ile; kule South Africa, Limpopo kwenye hifadhi ile maarufu kabisa ya Great Kruger pametokea tatizo. Ng'ombe wote wamepata matatizo ya magonjwa ya miguu na midomo na ule ugonjwa sasa umeshaanza kutokea kwa wanadamu na umeshaingia mpaka Zimbabwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya jitiada hao ng'ombe watakufa na watu nao watakufa na mazingira yetu yataharibika. Kwa hivyo, ni lazima watu kukubaliana na jambo hili, ni kinyume cha utaratibu kabisa kufanya jambo la namna hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalize na utalii. Nafasi ya Tanzania katika utalii ni nzuri, tunahitaji kufanya jitihada zaidi ili kuhakikisha kwamba utalii wetu uweze kuwa na faida hasa ya kuondoa umaskini. Juzi hapa China tarehe 21 umemalizika Mkutano wa World Tourism Organization, ulifanyikia Beijing pale, moja ya jambo kubwa kabisa lililokubaliwa katika mkutano ule ni kuhakikisha kwamba utalii uondoe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea...

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Massare,

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza bwana.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Haya.

**MWENYEKITI:** Na Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Wizara hii ni Wizara Mtambuka, ni Wizara nyeti, ni Wizara inayolitangaza Taifa, ni Wizara inayotangaza fahari za Taifa, ni Wizara ambayo ina umuhimu wake. Najua wachangiaji waliotangulia wamechangia mambo mengi na nitasisitiza katika mambo kadha wa kadha. Nianze tu kwa kujikita kwenye bajeti yenyewe, nikimpongeza Waziri Mwenye dhamana kwa hotuba nzuri aliyoitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii kulingana na umuhimu wa Wizara hii naweza nikasema kwamba upo upungufu hususan katika bajeti ile ya maendeleo kulinganisha na changamoto ambazo zinakabili Wizara hii. Ningemba na ningeshauri kwamba kiasi kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo kiongezwe ili kuweza kukabiliana na changamoto ambazo Wizara hii inakabiliana nazo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwanza kwenye upande wa utalii. Waliotangulia pia wamesema juu ya promotion katika sehemu hii ya utalii. Naweza nikasema kwamba promotion bado haijafanyika kwa kiasi cha kutosha, hasa promotion kwa utalii wa ndani. Ukijaribu kuangalia Watanzania walio wengi leo ambao angalau wana ufahamu, zaidi ya milioni 30 hawajui fahari, hawajui rasilimali za utalii ambazo tunazo sisi Watanzania. Kwa maana ya kwamba ni wengi ambao hawapati access kuingia kwenye vile vivutio vya utalii. kwa hiyo tunayo kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba tuna-promote utalii wa ndani ili kuweza kuongeza pato katika sekta hii ya utalii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado pia tunavyo vyanzo vingi ambavyo hatujavitumia vizuri ili kuweza kuongeza utalii. Vyanzo hivyo ni pamoja na fukwe ambazo tunazo katika bahari kuu, ukianzia Tanga, Dar es Salaam ukashuka mpaka Mtwara zipo fukwe nzuri ambazo tungezitumia vizuri zingeweza kuongeza utalii na kuongeza pato la Taifa. Kwa mfano, ukienda Maputo Msumbiji unaweza kuona jinsi ambavyo wamejaribu kutumia fukwe zao na zinaingiza pato kubwa la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia bado yapo maeneo ya asili ambayo hatujayatumia vizuri. Ukienda kwa mfano, Iringa kwenye zile palace za Ki-chief kwa Chief Mkwawa, leo inatumika kama kituo cha utalii. Kuna aliye-raise hoja ya mjesi mrefu duniani ambaye alitoka Tanzania na akapelekwa Ujerumanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niwakumbushe Watanzania pia kwamba katika harakati kama mnakumbuka wakati ule wa Vita vya Maji Maji hata Chief Mwenyewe Mkwawa mnakumbuka kwamba baada ya kuuawa kichwa chake kilichukuliwa kikapelekwa Ujeruman. Lakini tarehe 9 Julai, 1954, Kichwa chake kilirudishwa Tanzania na kikawekwa mahali maalum kama makumbusho kwenye palace ya Chief Mkwawa pale Iringa Kalenga. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali kupitia Wizara hii, kichwa cha Chief Songea ambacho nacho pia kilipelekwa Ujeruman ni wakati sasa wa kupaza sauti na kukirudisha, ili kusudi kiwekwe kwenye museum na hatimaye kiweze kuwa kituo cha utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna miundombinu pia ambayo haitoshelezi, haikidhi hususani katika maeneo ya utalii kwenye Wizara hii. Kwenye kitabu cha bajeti wameeleza juu ya kuongeza vifaa kwa ajili ya (patrol) ya doria kupambana na majangili. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kutokana na miundombinu kutokuwa rafiki wakati mwingine kufika kwenye maeneo ya utalii ni ngumu; niombe pia waweze kuongeza ndege kwa ajili ya shughuli yenewe ya utalii, kwa sababu mahali pengine barabara hazipitiki, huwezi kwenda kwa magari. Kwa hiyo, wajaribu kuongeza pia ndege kwa ajili ya shughuli hizo za kitalii. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi Jimboni kwangu, kwa sababu muda siyo rafiki. Jimbo la Ngara ni Jimbo ambalo lina takribani game reserve mbili. Kuna Game Reserve ya Burigi yenze hekta 13500 na kuna Game Reserve ya Kimisi ambayo ina takribani hekta 35,000. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba katika hifadhi hizi Jimbo langu la Ngara na Halmashauri yangu ya Ngara hainufaiki na chochote. Burigi Game reserve iliingizwa kwenye gazeti la Serikali tangu mwaka 1959, lakini mpaka leo ile tozo ambayo inatakiwa kurudishwa Halmashauri ya asilimia 25 kutokana na shughuli za uwindaji zinazofanyika haijawahi kutumwa hata siku moja. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Game Reserve ya Kimisi vivyo hivyo imekuwa gazetted tangu mwaka 2005, mpaka leo haijawahi kutolewa hata senti tano. Mbaya zaidi Kimisi Game Reserve sasa imekuwa ni kama kichaka cha majangili, wanaonufaika katika Kimisi Game Reserve ni wageni kabisa tofauti na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka wa hii Kimisi Game Reserve unaanza Rusumo boda unashuka kwenda Karagwe jirani kwa ndugu yangu Innocent Bashungwa. Kuna Kijiji cha Kashasha kule ni mpakani na Rwanda, upande wa Rwanda ni wananchi wanaishi pale. Game reserve yao ya Kagera iko ndani na

ndiyo game ambayo wanaitegemea sana kwa upande wa Rwanda kwa ajili ya kuingiza kipato kama utalii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa Tanzania unapovuka mto tu unaanza na pori na kule kuna wanyama, kule kuna ardhi nzuri kwa ajili ya kilimo, kuna maziwa kama Ziwa Ngoma ambalo ziwa lile nafikiri halijawahi kufanyiwa utaratibu wa uvuvi au wa uwindaji mzuri. Kuna viboko wanaibiwa mle, tena wanaibiwa na watu kutoka Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kambi moja ya Wanyamapor iko Rusumo pale lakini nashindwa kuelewa wanafanya nini? Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri pamoja na changamoto iliyoko ya mifugo iliyoko mle ndani, lakini niseme kwamba changamoto ni usalama wa maeneo yale na mipaka yetu ile. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kama ambavyo upande wa Rwanda wamefanya kutengeneza kama Buffer Zone ambayo wananchi wanakaa wanaendesha shughuli za kilimo, basi na upande huu mwagine kwa ajili ya kuimarisha usalama, tuweze kuangalia namna gani tunaweza kuitumia ardhi ile kwa ufasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ngara ni Jimbo ambalo lina vivutio vingi vya kitalii. Tuna maporomoko ya Mto Rusumo, mto unaotenganisha Rwanda na Tanzania. Maporomoko yale ni maporomoko ambayo tukiyatumia vizuri ni kivutio kizuri sana cha kitalii. Bahati nzuri eneo lile ni eneo ambalo sasa lina miradi mikubwa. Kuna mradi wa umeme unaozalishwa pale, kuna daraja kubwa la Kimataifa ambalo limefunguliwa juzi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, kuna maeneo ambayo tukiyatumia tunaweza tukainua pato hususani katika sekta hii ya utalii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna vilima vinaitwa vilima vitatu. Hivi vilima vitatu vinaunganisha nchi tatu ambazo ni washirika wa Afrika Mashariki, Tanzania, Rwanda na Burundi. Vilima vile ni kituo kizuri kinachoweza kuwa kituo cha kitalii kama Wizara hii inaweza ikawekeza katika eneo lile. Pia bado tuna pango ambalo lilikuwa linatumika kama root ya kupitishia watumwa wakati wa utumwa. Pango ambalo ni *underground*, unatembea kilomita tano uko ndani ya pango. Lile limegeuka kuwa ni pango kwa ajili ya maficho ya majambazi. Hili likiandaliwa vizuri, likatunzwa vizuri ni eneo ambalo linaweza likawa ni zuri sana kwa ajili ya kivutio cha utalii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo kadha wa kadha ambayo ningeweza kushauri. Kama nilivyotangulia kusema kwamba, Wizara hii ina changamoto nydingi, ikiwa ni pamoja na changamoto ya ujangili, naomba Serikali sasa ifanye mipango mikakati ya dhati kwa ajili ya kuhakikisha kwamba

inadhibiti hali hii ya ujangili, pia migogoro inayojitokeza ya wakulima na wafugaji. Pamoja na kwamba tumeshauri kuwa Wizara zote ambazo zinaingiliana ziweze kukaa pamoja na kuweka mipango ya pamoja, naomba ufanyike utafiti wa kuona ni namna gani ambavyo ardhi hizi, misitu hii, reserve hizi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofii)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Massare atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Niungane na wenzangu kupongeza uteuzi wa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe katika nafasi hii nyeti na ngumu kidogo ya Uwaziri pamoja na Naibu Waziri. Niwapongeze kwa kuteuliwa lakini niwapongeze kwa kazi yenu nzuri mlizozionyesha toka mmeteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mionganini mwa Wabunge ambaao majimbo yao yanapakana na mapori ya akiba. Napakana na pori la Rungwa Game Reserve na Muheesi, liko katika Halmashauri yangu mpya ya Itigi lakini Jimbo la Manyoni Magharibi. Ni mionganini mwa wanufaika wazuri sana na mapori haya na mchango wao mkubwa umekuwa ukisaidia vijiji vyetu katika maendeleo mbalimbali kutokana na mgawanyo ule unaotokana na asilimia ile ambayo inapelekwa katika vijiji na pia katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki cha madawati na sisi ni mionganini mwa watu ambaao tumenufaika kwa pesa zile lakini hatujajua tu hizi zilizotolewa na Wizara ni kiasi gani tutapata. Sasa si vibaya Mheshimiwa Waziri akatuonesha Halmashauri yangu ya Itigi imepatiwa nini kwa sababu nasi tunapakana na Game Reserve hizi za Rungwa na Muheesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matukio na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa kazi za kila siku za Wizara hii hususani katika vijiji vinavyopakana na hifadhi hizi. Kumekuwa na tatizo ambalo sijui ni la watumishi, sijui ndiyo sera ya Wizara, lakini dhana yangu nadhani ni kwamba baadhi ya watumishi wanapelekea sasa Wizara hii iendelee kulaumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la watumishi hawa ambao wamekuwa wanajihuisha sana na rushwa ndio wanaofanya leo Mawaziri toka mwaka 2010 waliopita katika Wizara hii wamekuwa na hesabu kubwa na wengine wakiwa wanatoka kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi hawa wameendelea kuwepo pale na watumishi wa juu sana ni watumishi wa kati kati wakiwemo Maafisa hawa wa Wanyamapor tuseme Maaskari wa Ma-game hao wanachukua pesa kidogo wanawaweka watu katika hifadhi wanaposhindana ndipo migogoro inapokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu miaka miwili iliyopita kulitokea tatizo kama hili, walishindana na kijana mmoja katika Kitongoji cha Matumaini katika Kijiji cha Kintanula, yule Bwana aliuwawa kwa kutofautiana tu lakini hadi leo hamna taarifa nzuri iliyotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi majuzi tu hata mwezi bado katika Kijiji cha Mwamageme Maaskari wa reserve walimuua kijana mmoja. Walikwenda kijijini akawasaidie kwenda nao porini kutafuta majangili kwa sababu wanakuwa na knowledge ya kujua ni nani na nani wanaojishughulisha; walipofika yule kijana mmoja walimuua wao wakasema kauawa na majangili. Lakini wale watatu wengine ambao walikwenda nao walikuja kuonekana baadaye. Bahati mbaya au nzuri shauri hii tumeliachia vyombo vya usalama vishughulike nalo pamoja na Diwani wa Mwamageme ambaye alifichwa juu ya tukio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na-declare interest, mimi ni mdau katika uvunaji wa mazao ya misitu katika nchi hii lakini pia nashughulika na usafirishaji wa mazao haya ya misitu nje, sasa nihamie katika sekta ambayo naijua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna jambo hili la recovery rate ya mbao ambayo ni asilimia 30. Recovery hii iliwekwa wakati ule mashine zilipokuwa za kizamani, misumeno ilikuwa na milimita zaidi ya tano, sita; sasa hivi taaluma imeongezeka, teknolojia imepanda bado tuna-recovery rate ya asilimia 30 ambayo inapelekea kuchonganisha wadau wavunaji wa mazao ya misitu pamoja na Maafisa ambao wanakagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka porini kupata 70 percent ni sawa, recovery ya asilimia 60 ya slipper ni sawa, kunakuja shida hapa tunapokuja katika recovery ya asilimia 30 ya mbao. Ukitumia mashine nzuri recovery ni kubwa sasa unapoonyesha kiwango kikubwa basi inakuwa tatizo linahamia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Wizara ichukue juhud za makusudi kabisa kuitia Taasisi zake za FIT lakini na Taasisi zingine ikiwepo TAFORI kufanya tafiti za sasa recover rate iliyo nzuri kwa mbao ni ipi ili kuondoa

mgogoro huu ambao unatengeneza rushwa kwa sababu wale wakaguzi wanatumia fursa hii ya wavunaji wengi wasiojua hesabu za kutafuta *volume* hii ya cubic meter kuwasulubu kwa kutumia Sheria namba 14 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji mbovu wa baadhi ya maafisa hawa ambao tumesema katika Wanyamapori lakini huku upande wa misitu ndio umekithiri sana. Kamati ya TFS tangu imeundwa imekua ni taasisi iliyofanya kazi vizuri sana kuanzia juu mpaka katikati; lakini kule chini bado ni kuzuri, hapa katikati ndiyo kuna shida kama nilivyokwisha kusema. Kuna Maafisa ambao wanafanya kazi kwa kutegemea sana kupata kipato nije ya mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ndio wanaopelekea leo Mawaziri wengi wanasulubiwa. Hapa katikati Mheshimiwa tunavyovizua ambavyo ukaguzi wake haueleweki, ni vigumu sana kukagua mzigo ukiwa ndani ya gari, lakini kuna *checkpoint* ya mwisho, Mbezi pale ambayo nayo wanakagua, bandarini ambapo mizigo ya *export* inapelekwa nayo ina ukaguzi; kuna Maafisa zaidi ya saba pale, lakini hawaaminiani, hakuna Afisa mmoja anayekuwa na maamuzi mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe Wizara hii, ni wakati umefika wa kufanya kama walivyofanya TRA. TRA wao walikuwa wanakimbizana hivi hivi na wadau wao, lakini mwisho wa siku walipoamua kuwa waaminifu, wakweli kwamba wewe unatakiwa kulipia kodi ya asilimia ya pesa hizi, basi watu wote walipe asilimia hizo. Yule mwingine anayekuwa ana-verify kwamba wewe ulistahili kulipa hiki. Na kama hukustahili kulipa anafanya maamuzi ya papo kwa hapo na ni maamuzi ambayo yana tija na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwenye TFS watumishi wao wamekuwa na shida. Kuna mionganini mwao Mheshimiwa Waziri nilishampa na taarifa na anajua, jinsi wanavyotumia udhaifu huu wa watu hawa ambao hawajui kutengeneza *volume* hii ya cubic meter, wanavyosulubiwa na Maafisa hawa. Anatumia kutokujua kwa yule mtu anam-sue mara mbili na anam-compensate mara nne zaidi ambacho hawakupaswa kukilipia. Sasa shida ni pale anapokutana na watu kidogo wanaojua ndipo linakuwa tatizo. Tuliwaambia huyu mtu amekuwa akitajwa mara nyingi, amekuwa akizungumzwa na watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri sasa asiingie katika mtego ambao wamekuwa wakiingia Mawaziri wengi, wa kukumbatia watu na taasisi za rushwa zilishawakamata, lakini kwa sababu ushahidi wa moja kwa moja unakuwa ni mgumu kumtia hatiani mtu wa namna ile, ni vizuri akaondoka katika lile eneo ambalo nadhani kwamba atatengeneza mazingira ya kupata rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka nizungumzie leo kinachoendelea katika Bandari ya Dar es Salaam. Inapofika mwezi wa Saba, Wizara hii huwa inatoa kitu kinachoitwa approval, yaani nikibali cha mtu kusafirisha mazao ya misitu nje ya nchi. Kile kibali kinampelekea mtu aingie mikataba na mabenki na wadau mbalimbali....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nimpongeze Waziri kwa kazi nzuri na hasa kwa hatua yake ya kuwatimua baadhi ya watumishi wasio waaminifu katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Nampongeza sana Waziri kwa hili na namwomba aendelee kwa sababu bado wezi wapo wengi na ndiyo maana kwa kiasi kikubwa fedha nyingi zinazopatikana za utalii zinaishia mikononi mwao. Nampongeza sana kwa hili. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Niwapongeze baadhi ya Wabunge na hasa wale ambao kwa namna moja au nyingine wametambua jitihada, uhifadhi wa mazingira unaofanywa na baadhi ya makabila ambayo yanaishi katika hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu turudi nyuma kidogo. Nimefurahishwa na baadhi ya michango na baadhi ya michango mingine kwa kweli inaniweka katika wakati mgumu. Ni kweli, wanasema kitanda usichokilalia huwezi kujua kunguni wake; najua kunguni wake, kwa sababu hata mimi pia nimesomeshwa na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo kati ya wafugaji na wakulima linahitaji busara, kwa sababu kila mmoja anavutia upande wake. Wengine wanasema kwamba wafugaji ni waharibifu na ndiyo chanzo cha uharibifu wa mazingira. Katika kumbukumbu zangu, Mkoa wa Morogoro ni mionganini mwa mikoa ambayo ilikuwa inatiririsha maji kwa kipindi chote cha mwaka mzima, lakini leo hii hata mkoa huu kwa kiasi kikubwa hayo maji ambayo siku za nyuma

Mwanamuziki Salum ambaye alikuwa ni mzaliwa wa Morogoro aliimba kwamba Mji wa Morogoro unatiririsha maji safi, lakini leo si kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ni kutokana na uharibifu wa mazingira uliofanywa na wakulima katika vyanzo vya milima; je, hapa wafugaji wanaingia pipi? Kwa sababu wafugaji ndiyo wanaohesabika kwamba ni waharibifu wakubwa wa mazingira; ndiyo maana nikasema hili jambo linahitaji busara. Humu ndani kila mmoja atavutia upande wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wetu wasipokaa, wakaandaa mipango ambayo itawawezesha wafugaji waweze kufuga kwa amani na utulivu, wakulima waweze kulima pasipo usumbufu wowote ili pasiwepo na malalamiko ya watu mifugo yao kuuawa, kusiwepo na malalamiko ya wananchi nyumba zao kuchomwa moto, tutapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tu tulishuhudia ukatili uliofanywa kwa baadhi ya mifugo kule Morogoro. Kwa maana hiyo, kama busara isipotumika, narudia tena kama busara isipotumika, wataalam wetu wakakaa, mipango hii ikapangwa kuhakikisha kwamba kila mmoja ana fuga katika eneo ambalo Serikali imeweka mipaka, inatambua lile eneo na linatambuliwa eneo hili ni kwa ajili ya wakulima, hii migogoro itaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wanasema ng'ombe ni wadudu, lakini utashangaa ndiyo hao hao wanakula nyama. Ikitika Jumamosi Waheshimiwa wengi tunakimbilia mnadani, tunakwenda kula nyama hivi kama wafugaji wasinge fuga tungekula wapi hizo nyama? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vyema tukatambua kwamba kila mmoja ana nafasi yake katika nchi hii na hata hao wanaohama kutoka sehemu moja kwenda nyingine hakuna anayependa; hebu fikiria kutoka Mwanza mtu mpaka anakwenda Lindi mwendo huo ni wa siku ngapi? ni kutokana na kutokuwepo na mipango ambayo inawafanya hawa watoke sehemu moja kwenda eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo narudia tena busara itumike ili tuweke mipango ya kuhakikisha kwamba kila Mtanzania ana haki ya kuishi katika nchi yake, popote pale anapoweza, ili mradi tu kwamba sheria hazivunjwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, zipo sheria za tangu mwaka 1959; pamoja na kwamba ipo Sheria ya 2009 au 2010 lakini je, hii sheria ya tangu enzi za ukoloni ni lini sheria hii italetwa ili ifanyiwe marekebisho? Kwa kufanya hivyo tutapunguza kwa kiasi kikubwa migogoro, tutawaacha watu wanaoishi katika jamii ile, hasa ya wafugaji ambao ni Wamasai, wataishi lakini pia wakitunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri pia Serikali, kuhakikisha kwamba katika haya mapori tengefu, yapo maeneo mengine ambayo tuwaachie wafugaji, kwa maana kwamba, kama kweli yakitengwa na kuhakikisha kwamba wafugaji na wao wanafuga; kwa sababu tangu tunazaliwa wananchi, babu zetu, mama zetu, baba zetu, walikuwa wakiishi huko. Kwa hiyo, tuangalie ni maeneo gani ambayo ni mapori tengefu, tutawatengea wananchi wetu ili waweze kuishi na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije katika suala la utalii. Katika suala la utalii nimwombe Mheshimiwa Waziri, hebu aiangalie Bodi ya Utalii, sioni kama kuna kazi wanafanya, kwa sababu tuliwatarajia hawa waweze kutangaza kwa kiasi kikubwa utalii wetu, lakini mpaka leo kitu gani kinachofanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende katika Jiji la Dar es Salaam, hivi mtalii anaposhuka katika Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam kuna kituo gani pale anakwenda kupata maelezo kuona kwamba Tanzania kuna utalii huu? Hakuna! Akitoka katika uwanja wa ndege anapoingia barabarani anakaribishwa na mabango ya simu yanatusaidia nini sisi Watanzania? Kwa nini tusitumie haya mabango kuhakikisha kwamba ni njia mojawapo ya kutangaza utalii wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jiji la Dar es Salaam, wengi na ndiyo maana kila siku wanazidi katika hili jiji la Dar es Salaam. Hivi katika sheria za mipango miji na hasa kwa sababu utalii si lazima twende mbugani tu, hata baadhi ya majengo yakihifadhiwa vyema ni utalii. Leo hii katika majengo ya Posta ambayo yalijengwa kabla hata hatujazaliwa, yanabomolewa yanajengwa mengine, kwa nini tusitenge eneo ambalo haya majengo yakahifadhiwa ili kiwe ni kituo cha utalii tuje tuone haya majengo ya miaka nenda miaka rudi yasaidie hata vizazi vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi suala la utalii lina mapana sana na naumia sana ninapoona nchi ya Kenya inatumia advantage ya sisi kulegalega, vivutio vilivyoko Tanzania wanavitangaza wao. Ndiyo maana siku za karibuni, tulimwona Mkenya amesimama kabisa anasema bonde la Olduvai Gorge lipo nchini Kenya, Serikali imejibu nini? Itumie nafasi hiyo wakati mwininge kuhakikisha kwamba wanaeleza, huo utalii upo Tanzania; lakini Serikali imekaa kimya. Huu ni utalii wa kwetu; ni vitu vya kwetu ambavyo tunajivunia. Mlima Kilimanjaro, mara ngapi wameutangaza, kwa kujivunia kwamba njoo Kenya uone Mlima Kilimanjaro, lakini ukweli ni kwamba Mlima huu upo Tanzania tunajipanga vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, mtalii anapotoka katika hifadhi tumejipanga vipi kuhakikisha kwamba anapata maeneo mengine ya kwenda kutembelea? Kwa mfano, Mbuga ya Kruger nchini Afrika ya Kusini, Mtalii akitoka pale atakwenda katika Mji wa Soweto. Kule atawezu kushuhudia, wakati

mwingine hata mauaji ya watoto yaliyofanyika mwaka 1976; ni vivutio pia wanakwenda kule kuangalia na kujifunza historia. Historia ya Nelson Mandela, katika vitu vingine tofauti tofauti, pesa zinaendelea kubaki, je, sisi tumejipanga vipi? Mtalii anapotoka Ngorongoro, anapotoka kupanda Mlima wa Kilimanjaro anapotoka huku Gombe, anakwenda wapi? Utamaduni wetu ni upi?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kawaida nilikuwa nihamie kwenye Kambi hii ya Upinzani, lakini nina matangazo na mwongozo kidogo. Niseme wazi mpaka sasa hivi waliochangia upande wa Chama cha Mapinduzi, ni 14, upande wa chama cha CHADEMA wamechangia wawili, upande wa chama cha CUF ni mmoja na ndiyo maana mtiririko uliokuwa unafuata wawili mchana watakuwa wa CHADEMA, mmoja upande wa CUF Mheshimiwa Ally Saleh, *Then tutakuja upande wa CCM halafu wawili CHADEMA na mmoja CUF.* Sasa majina ya vyama yako mbele ya meza hapa, kwa hiyo hakuna kuchakachua hapa.

Kwa haki tu niseme watakaoanza mchana ni Mheshimiwa Joseph Haule na Mheshimiwa Joshua Nassari, halafu atafuatiwa CUF, Mheshimiwa Ally Saleh. Halafu sasa ndipo tutaenda upande wa CCM Mheshimiwa Saul H. Amon, Mheshimiwa Daniel Mtuka, Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mheshimiwa Zainab Katimba kama atarejea humu ndani, Mheshimiwa Vicky Kamata Likwelile na Mheshimiwa Desderius Mipata. Halafu tutaenda Waheshimiwa wengine, John Heche, Mheshimiwa Joseph Selasini na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

Waheshimiwa Wabunge, katika ile miongozo ambayo nilisema siyo miongozo, ilikuwa ishuke katika utaratibu wa kawaida wa kanuni. Niigize Serikali kwa upande wa Wizara ya Elimu, kwa sababu aliyoyasema Mheshimiwa Suzan Lyimo, yanagusa Wizara ya Elimu na kesho ndiyo hoja yao. Nadhani tuitendee haki Serikali, tumtake Waziri wa Elimu anapohitimisha hoja yake, ambayo ni ya siku mbili, kesho na kesho kutwa, alisemee hili ili tupate majibu yaliyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa upande wa Magereza; kwa askari wetu wa Magereza ambao Mheshimiwa Matiko alilisema. Serikali na yenyewe kwa wakati ambao utaona unafaa lakini ndani ya wiki hii watoe maelezo kuhusiana na stahiki ya hawa Maaskari wetu wa magereza.

Baada ya maelekezo hayo, kuna taarifa moja, Kiongozi wa Yanga Bungeni, Mratibu, Mheshimiwa Kikwete Ridhiwan anawataka wafuatao mkutane kwenye kantini ya Bunge, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Mheshimiwa Anthony Mavunde, Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mheshimiwa Issa Mangungu, Mheshimiwa Juma Ngwali, Mheshimiwa Seif Gulamali na Mheshimiwa Gashaza, mwende pale mkawaulize sasa. (Makofij)

## MWONGOZO WA SPIKA

### **MWONGOZO KUHUSU KAULI ZILIZOTOLEWA NA MHESHIMIWA ESTHER ALEXANDER MAHAWE**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge la mwongozo. Mwongozo wa Spika kuhusu suala liliombewa mwongozo na Mheshimiwa Cecilia Paresso kuhusu kauli zilizotolewa na Mheshimiwa Esther Mahawe.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 18 Mei, mwaka huu, katika Kikao cha jioni nadhani, Mheshimiwa Cecilia Paresso aliomba mwongozo chini ya Kanuni ya 68(7). Akieleza kuwa masharti ya Kanuni ya 64(1)(g) yalikiukwa na Mheshimiwa Esther Mahawe. Kwani wakati anachangia Mheshimiwa Mahawe alitoa maneno ya kudhalilisha watu wengine, kwa kusema kwamba wananchi wa Mbulu kipindi kilichopita walichagua debe la gunzi na sasa hivi wamechagua debe la mahindi.

Baada ya kuomba mwongozo huo kiti kilielekeza kuwa majibu ya mwongozo huo yatatolewa baadaye.

Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya ufanuzi wa suala hili naomba kunukuu Masharti ya Kanuni ya 64(1) (g), ya kanuni za kudumu, kwa sababu ya muda nitaliruka hilo maana tunazifahamu, mlion na kanuni (g) inasemataka hatutatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kurejea pia baadhi ya maneno yaliyosemwa na Mheshimiwa Mahawe na kunukuliwa na Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge kama ifuatavyo, nanukuu: "Wananchi wa Mbulu kipindi kilichopita walichagua debe la gunzi na sasa hivi wamechagua debe la mahindi." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kurejea Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge; kiti kimeridhika kuwa maneno wananchi wa Mbulu kipindi kilichopita walichagua debe la gunzi na sasa hivi wamechagua debe la mahindi yamekiuka masharti ya kanuni ya 64(1) (g) kama ilivyorejewa hapo juu. (Makofij)

Hivyo, kama ambavyo iliwahi kuamuliwa katika mwongozo wa Mheshimiwa Cecilia Paresso Mbunge, unaofanana na huu, kuhusu maneno yaliyotolewa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Musongozi Mbunge na kwa kuzingatiwa masharti ya kanuni tajwa; naelekeza maneno hayo yafutwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, naomba pia nirudie kuwakumbusha na kuwasihii kuzingatia kanuni zetu tulizojiwekea sisi wenyewe, hususani kanuni za majadiliano ili kupunguza miongozo inayotokana na ukiukwaji wa kanuni hizo. Aidha, kuanzia sasa kitii hakitasita kuchukua hatua kali kwa yeoyote atakayekiuka masharti ya kanuni hizi.

Waheshimiwa Wabunge huu ndiyo mwongozo wangu kuhusu jambo hilo na umetolewa leo tarehe 25 Mei, 2016.

Mheshimiwa Heche, mimi nafuata orodha yenu; lakini silazimishwi kufuatilia kama kasuku, hayo yaliyoko, kama kuchangia utachangia tu, ndiyo maana nimesema jina lako lipo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge *lilahirishwa mpaka saa 10.00 Jioni*)

(Saa 10.00 Jioni Bunge *lilrudia*)

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa Azzan Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kuna orodha hapa nafikiri imeshaitwa, tunaanza na Mheshimiwa Joseph Haule.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika bajeti hii ya Maliasili na Utalii maana ukizungumzia Jimbo la Mikumi moja kwa moja unazungumzia masuala haya muhimu ya utalii na maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa masikitiko makubwa niongelee jinsi ambavyo wananchi wa Mikumi wamekuwa wakilia kutokana na jinsi ambavyo wanabanwa na migogoro mbalimbali ambayo inasababishwa na kuongezwa mara kwa mara kwa mipaka ya hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana wananchi wa Jimbo la Mikumi waliokuwa wakiishi katika maeneo ya Kipogoga pamoja na Mgoda walihamishwa mwaka 1963 na kupelekwa kwenye Vijiji vipyta vya Vikweme,

Rwembe maeneo ya Tindiga na sehemu nyingine. Hiyo ilisaidia kuifanya hifadhi ya Mikumi iweze kuanza mwaka 1963, lakini sasa hivi mipaka hiyo imeonekana kuwa inaongezwa na sasa hivi wananchi wamefuatwa kwenye vijiji, kwa mfano Kijiji cha Vikweme wanaambiwa tena waondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Vikweme wamekuwa na kilio cha muda mrefu sana ambapo upande mmoja wanakabwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania na sasa hivi wameambiwa wahame maeneo yale kwa sababu ni ya Jeshi, lakini upande wa pili Hifadhi ya Mikumi inasema ni eneo lao, mnataka wananchi hao wa Mikumi waende maeneo gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wazee ninaozungumza wamehamishwa mwaka 63 ni pamoja na akina mzee Leonard Haule ambaye tulimzika mwaka 1981, ambaye ni babu yangu. Wazee mwenzake akina mzee Mbegani mpaka leo wamekuwa wakitaabika na wakiililia Serikali kwamba mnataka waende wapi wakati wenyewe ndiyo watu wa Mikumi wazawa walikuwa pale?.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro mingi kutokana na hifadhi kuongeza mipaka katika maeneo mengine kama ya Uledi, Ng'ombe ambapo inaonekana kuna heka karibu 200 za wakazi wa Lugawilo ambao hifadhi pia imesema huu mpaka ni mpya. Wananchi wa huku wamekuwa wakilia kwa muda mrefu wakiitaka Serikali iweze kurudisha ule mpaka wa zamani wa mwaka 1957 uliokuwa ukiwawezesha kupata ardhi ya kulima na kujenga nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi kama wa Vikwema, Kitete Msindazi, maeneo ya Mululu, maeneo ya Msange pamoja na maeneo ya Lumango wameonekana kuwa wanataabika kwa sababu wamekuwa na ugomvi wa mara kwa mara na watu wa hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna suala la buffer zone. Eneo la Buffer Zone limekuwa likiongezeka kila siku. Eneo hili wananchi hawatakiwi kuingia kabisa. Mama zetu wamekuwa wakipigwa kwa sababu ya kuingia kuokota kuni kwenye maeneo haya. Ndugu zetu wamekuwa wanataabika na sasa tumesema kuwa Mikumi mpya ya Profesa J. tunataka haya mambo yakome na tuweze kukaa chini na wananchi ili tuweze kusuluuhisha. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia masuala ya hifadhi tunazungumzia ujirani mwema. Hapo zamani sisi tulipokuwa tunakua tulikuwa tunaingia kwenye mbuga ya wanyama ya Mikumi kwenda kuona wanyama, lakini pia tukicheza michezo pamoja na Maaskari wa Wanyamapori na vitu vingine kama hivyo. Pia walikuwa wakitusaidia kujenga zahanati, shule na wanafunzi walikuwa wakibadilishana uwezo. Sasa hivi kumekuwa na uadui

mkubwa kati ya watu wanaokaa katika vijiji vinavyopakana na hifadhi na wahifadhi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiongelea suala la ujirani mwema kwa sababu tunasema wananchi kama watathaminiwa watapewa thamani wanaostahili na fidia lakini pia watashirikishwa kwenye mambo mbalimbali, hii itawasaidia sana kulinda rasilimali zetu na wanyama wetu. Kwa hiyo, tunataka tuisisitze suala la ujirani mwema ili tuweze kuwatumia wananchi kuweza kulinda wanyama wetu na rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa style hii mnayosema kila siku kuna ujangili, wananchi wanawachukia tembo, wanawachukia askari wa wanyamapori na ndiyo wamewaweka kama maadui, kwa hiyo hata wakiona majangili wanaingia hawawezi kuwapa ripoti ndugu zangu wa Serikali. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli mnataka tulinde rasilimali zetu, tuwape nafasi hiyo wananchi wa Tanzania tuwaoneshe umoja na ushirikiano, tuwaoneshe jinsi ya kucheza michezo ya pamoja; na kama inahitajika tuwape elimu ili wajue kitu gani cha kufanya na kipi sio cha kufanya, lakini sasa hivi ndugu zetu wanaokaa kwenye vijiji vinavyopakana na mbuga wameonekana kuwa wanateswa. Niwaambie tu Mikumi kuna watu wengine tumezika nguo kwa sababu hata maiti zao hatujaweza kuzipata kwa sababu wamepigwa risasi ndani ya hifadhi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kutokana na hilo tunataka tuisisitze Serikali kama kweli mnataka tulinde rasilimali za Mikumi tupunguze uadui huu kati wa wananchi wanaoishi kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi na watu wa hifadhi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tuzungumzie pia masuala ya tembo. Wanyama hawa sasa hivi imekuwa kama *fashion* kila mtu anayekaa karibu na hifadhi anazungumzia masuala ya tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa juzi, karibu wiki mbili katika kijiji kilicho katikati ya Kilosa na Mvomero kinachoitwa Mangae mtu mmoja ameuawa na tembo. Sasa ndugu zangu Serikali kila anapokufa mtu ndipo mnataka mje? Kila siku tunalia, tunapaza sauti ndugu wanakufa lakini hakuna linalochukuliwa lolote. Tunataka tuwaambie tunawapenda tembo, tunapenda ralisilimali zetu, tunaomba mtusikilize na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zetu wanalima mashamba makubwa ya mpunga, watu wanatumia hela nyingi, lakini tembo wanakula zile mali. Wananchi wanapata tabu, sasa hivi kuna mafuriko huko Mikumi, watu wana

njaa, wanajitahidi kulima lakini tembo wanakula, Serikali imekaa kimya. Kuna Kata inaitwa Kilangali kila siku wimbo ni kuhusu tembo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, tunaomba watuangalie kwa jicho pevu, itafika kipindi hawa wananchi watachoka na tutaamua kufanya jambo litakalokuwa baya, watatuongeza kwenye magereza yao. (Makofii)

Mheshimimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kinatakiwa kusema ni kwamba, tunaangalia sana utaratibu wa kuwatunza tembo wetu lakini pia kuna suala la mamba, ambapo katika mto Mwega kwenye Kata ya Maloyo, mamba wameonekana kujeruhi sana ndugu zetu na watu wengine wamekufa. Kitu cha kustaajabisha ni kwamba, Halmashauri ya Kilosa imenunua bunduki mbili kwa ajili ya kuongezea nguvu kwenye maliasili, lakini cha ajabu ni kwamba mpaka leo wameshindwa kupata vibali kutoka mkoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atumie nafasi hii. Halmashauri ya Kilosa imenunua bunduki, lakini vibali vinaonekana kupigwa chenga. Sasa tusije tukawafanya wananchi na sisi tukawaambia watumie mbinu mbadala ili kuweza kukabiliana na wanyama hao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa pale Mikumi tozo lote limeonekana kuwa linakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, wananchi wa Mikumi wamekuwa lonely, pesa ya pale haiwahu, ni kama wamekaa kisiwani hata mbuga imekuwa kama sio mali yao tena. Tunataka wananchi wa Mikumi wasikie ownership, waone ile mbuga kama ni ya kwao, tuwashirikishe wakae pale wajione kwamba ile mbuga ni ya kwetu na sisi ni watanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi kila kitu kinatolewa kinapelekwa Dar es Salaam, Mikumi hakuna kitu. Waheshimiwa Wabunge mnapita sana Mikumi pale mnaangalia wanyama mnapiga selfie, lakini mnashindwa kujua hata mnawasaidiaje wananchi wa Mikumi ambaa mbuga ipo pale. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Serikali iliangularie kwa jicho pevu mnawaachaje watu wa Mikumi? Maana imekuwa kama kisiwa, tunakuwa maskini wakati tumebarikiwa kuwa na mbuga nzuri ya wanyama ndugu zangu. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali tunataka tutengeneze kijiji cha makumbusho. Kama Zanzibar wameweza kuwa na mji mkongwe, watu wakishafanya utalii pale wanakaa tunacheza ngoma tunakula misosi, tunakula vyakula vya asili na kuza vitu vyetu ambavyo vitakuwa pale Mikumi. Kwa hiyo tunataka tutengeneze kijiji cha makumbusho pale Mikumi wazungu na ninyi mkitoka mbugani kuzunguka mnaweza kuzunguka Mikumi ili ku- boost uchumi wa watu wa mikumi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Wizara wanatuacha kama kisiwa, hakuna shughuli yoyote ya utalii inayoendelea Mikumi. Tena nimesikia wametenga bilioni moja ambazo zimeenda kwenye vijiji vinavyohusika na mbuga, kwa Mikumi sijasikia, mimi ndiye Mbunge lakini sijasikia hayo madawati sijui walimpa nani au hiyo michango imekuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipouliza kuhusu giving back kwenye society kuchangia vitu vingine wamesema sasa hivi hawataki kujadili kuhusu majengo, hospitali na vitu vingine bali wanataka sasa hivi kuweka hela inayozunguka zunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine. Kuna ile Mikumi Lodge ambayo ilikuwa pale Mikumi, ndiyo iliyokuwa tegemeo la watu wa Mikumi kwenda kutalii, lakini sasa hivi ile hoteli ilibinafsishwa tukasikia imechomwa moto. Nataka Waziri akirudi hapa aje atuambie nini mustakbali wa ile Mikumi Lodge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye barabara inayopita Mikumi ya kilomita 50, takwimu zinaonesha mnyama mmoja anagongwa kila siku, wanyama 956 wanagongwa kwa miaka mitano, tangu 2011 mpaka 2015 wamegongwa wanyama 956. Nataka Serikali ije na majibu ituambie wanataka kufanya jambo gani kuhusu kukomboa hawa wanyama wa Kitanzania na ina mpango gani na hawa wanyama ambao wanagongwa kila siku na wanawaona na takwimu wanazo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza na hayo, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Saul Henry Amon, ajiandae Mheshimiwa Mtuka. Waheshimiwa orodha ninayo Nassari umo, nawapanga ili baadaye na wewe upate kuchangamka naona hujachangamka, haya Mheshimiwa Nassari changamka sasa.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Kwa kuanza, sincerely kabisa nimpongeze sana Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Hifadhi la Taifa pamoja na timu yake kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. Pamoja na changamoto ndogo ndogo ambazo bado zipo, lakini nyingi tunajua zinasababishwa na financial constraints na tukizingatia kwamba makusanyo yote yanayokusanywa na TANAPA yanakwenda kwanza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, kwa kweli nimpongeze na ni matumaini yangu kwamba, yale madogo madogo ambayo bado hayajafanyiwa kazi na yenyewe yatafanyiwa kazi kadiri muda unavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwazungumzia ma-guides ambao ndiyo wanafanya kazi za kuwa na watalii tangu wanapoingia nchini mpaka wanapoondoka. Makampuni ya utalii yanatengeneza fedha kupitia biashara ya utalii, lakini ukiangalia mtu ambaye ana-deal na utalii tangu mtalii anapotua *airport* mpaka siku ya mwisho anaporuka ni guide, lakini ukiangalia maisha yao, ukiangalia namna gani ambavyo wanakuwa *mistreated*, kwa kweli inasikitisha sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie fursa hii kumwomba ndugu yangu Profesa Jumanne Maghembe pamoja na Mhandisi Ramo Makani kwamba sasa waielekeze Wizara au hao Maafisa ambao wapo kwenye Wizara yao waangalie ni namna gani ya kukaa chini na vyama vya hawa waongoza utalii kwa maana ya guides ili wazungumze nao na waangalie changamoto ambazo wamekuwa nazo na waangalie ni kwa namna gani wanakuwa *mistreated* na kampuni na ni namna gani ambavyo kampuni zinaamua tu *ku-hire and fire* leo ama kesho. Vile vile guides wengi wamekuwa hawapati ajira za kudumu kwenye kampuni zao, bado wanafanya kazi kama vibarua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiachilia mbali hawa guides vile vile wapo watu ambao wanaitwa *porters* ambao wanabeba mizigo na kusindikiza wageni kupanda mlimani. Siku za nyuma Serikali iliagiza kwamba kila porter ambaye anakwenda na mgeni mlimani kwa siku moja alipwe fedha ambazo siyo chini ya dola 10 za Kimarekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka tunavyozungumza leo hii bado wapandisha wageni mlimani wapo ambao mpaka leo hii wanalipwa sh. 6,000/= mpaka sh. 5,000/= kwa siku; na kazi wanayoifanya ni kubwa kupindukia kwa sababu wakati mwingine watalii wanaugua wakiwa njiani na wengine wanazidiwa wakiwa wanapanda mlima. Pia hawa watu kazi yao si tu kubeba mizigo peke yake kuna wakati mwingine unakuta mpaka kuwabeba watalii wakati wakizidiwa wanapougu huko njiani na wanaofanya ile kazi ni *porters*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawahi kuona *porters* wakisafirisha watalii ambao wamejiharishia kwa sababu ya hali mbaya ya hewa, kuzidiwa wakiwa mlimani, lakini ukiangalia pesa wanayolipwa mtu analipwa sh. 6,000/- kwa siku na anapanda mlima kwenye *high altitude*. Kwa kweli inasikitisha. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atoe maelekezo upya kwamba wanaopandisha wageni mlimani wanapaswa kulipwa shilingi ngapi na kampuni ambazo haziwapi ile dola 10 ambayo Wizara ilielekeza tujue wanachukuliwa hatua gani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo, niongelee suala moja ambalo limezungumzwa pia kwenye hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu kampuni inayoitwa *Green Mile Safari Limited*. Kampuni hii na naamini kwamba

ofisi ya umma (*The Public office*) is an institution. Anapoamua Waziri mmoja kumnyanganya mtu leseni kwa sababu amekosa sifa za uwindaji na ushahidi upo wa nyaraka, picha za video na picha za mnato, halafu mwaka mmoja au miwili baadaye anakuja Waziri anamrudishia tena mtu yule yule leseni ya kurudi kuendelea kuwinda kwenye kitalu. Halafu unamnyang'anya kampuni nyingine kama wanavyonyang'anywa hao *Winget Window safaris*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tufahamu, hivi ni kwamba maamuzi yaliyofanyika miaka miwili iliyopita hayakuwa maamuzi sahihi? Hizi zile picha za video na picha za mnato ambazo zilionyesha namna gani hawa watu walikuwa wanawinda jike wadogo ambao hawaruhusiwi kuwindwa kwa mujibu wa taratibu leo hii wamekuwa watakatifu tena?. Ndiyo maana inasemwa mtaani kwamba kampuni hii ilikuwa ina backup kutoka State House.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sina uhakika lakini mtanifanya niamini hivyo kwa sababu kama imenyanganya leseni kwa kutokufuata taratibu halafu leo hii mnairudishia bila kufuata taratibu tena, tunapata mashaka kidogo. Mheshimiwa Maghembe tusije tukapata wasiwasi na yeye na utendaji wake wa ofisi, naomba alizungumze wakati anahitimisha, vinginevyo tutafanya vile ambavyo huwa tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine niongelee kuhusu TFS. Sisi kule Meru kwa mfano lipo shamba la miti na wanaotunza mashamba yale ni wananchi wa vijiji vinavyozunguka, kama Vijiji vya Kilinga, Mulala, Songolo, Sakila na vijiji vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa juzi baada ya kuvuna miti; wakati TFS wanapanda miti mingine wananchi huwa wanapewa zile plot wanalima huku wanatunza miti. Lakini badala yake tumeona kwa miaka ya hapo nyuma na hususan mwaka 2014; kwamba badala ya kuwapa wananchi ambao wanazunguka yale mashamba, wanapewa watu wengine kutoka nje, wanapewa watu kutoka Jeshi la Polisi, anapewa OCD wa Wilaya ili waki-backfire awasadie kuzuia wananchi. Sasa tunaomba tu kujua hivi nini maana ya dhana ya ujirani mwema? Hivi hawa wananchi siku moja akaamka tu mwananchi kichaa akachukua dawa akaenda akapiga ile miti si itakufa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba hawa watu wa TFS wahakikishe wanaboresha mahusiano na vijiji vinavyozunguka na mojawapo ya namna ya kuboresha mahusiano ni ikiwepo kuhakikisha wanaopata zile plots za kulima ni wa vijiji vinavyozunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni habari ya hoteli za kitalii na masuala ya service levy kwenye Halmashauri zetu. Kwa mfano tu kwa Halmashauri yangu ya Meru peke yake, kwa takwimu za mwaka mmoja wa fedha peke yake, nitasoma baadhi ya hoteli tu hapa. Hoteli ya Dik Dik peke yake tumeshindwa kupata mapato kwa mwaka mmoja shilingi milioni tisa na laki tisa. Hoteli ya Kigongoni shilingi milioni mbili laki nane; hoteli ya Arumeru River Lodge shilingi milioni tatu na laki nne; hoteli ya Hatari Lodge shilingi milioni kumi na laki moja; hoteli ya Mountain Village shilingi milioni thelathini na laki tisa; kampuni ya Macho Porini Tours zaidi ya shilingi milioni mbili na laki tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijumlisha kwa mwaka mmoja wa fedha kwa haya makampuni sita niliyoyataja hapa peke yake Halmashauri tume-loose zaidi ya shilingi milioni 59. Sasa milioni 59 kwa hoteli sita peke yake kwa Halmashauri moja maana yake *it's a lot of money* kwa miaka mitano ambazo zingeweza kusaidia wananchi wetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tungeomba kujua ni kwa namna gani hawa watu wanakwepa? Wengine wanajisajili kwenye EPZ ili waweze kupata grace ya kodi? Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri hili nalo akija alizungumzie ili tusije tuka-suffocate Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho na muhimu sana, ni *Operation Tokomeza*. Nilikuwepo kwenye Bunge lilitopita na tulizungumza kuhusu habari ya *Operation Tokomeza* na Bunge hili lilelekeza Serikali kwamba ifanye nini na maazimio tuliyapitisha hapa ndani ya Bunge lako Tukufu. Badala yake leo hii ni miaka miwili ama mitatu baadaye bado maazimio ya Bunge hayajatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani tuisahau kwenye *Operation Tokomeza* tunao wananchi ambao wamepoteza maisha, ambao walilazimishwa mpaka kufanya mapenzi na miti, tunao watu ambao walilazimishwa kufanya mapenzi mbele ya watoto wao wakiwa wanaona, tunao watu ambao walinyanganywa ya mbaa mpaka leo wameingizwa kwenye umaskini, tunataka kujua fidia zao ni lini? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maazimio ambayo yaliazimiwa ndani ya Bunge hili Tukufu ni lini yanakwenda kutekelezwa. Kwa sababu tunajua kuna baadhi ya watu wamesafishwa lakini mimi ninao wananchi mpaka leo wanaripoti polisi, ninao wananchi mpaka leo wamenyang'anywa silaha zao halali ambazo wamemilikishwa kihalali zipo polisi mpaka leo hawajarudishiwa. Tunao watu ambao wameingizwa kwenye umaskini baada ya *Operation Tokomeza* na kwa kweli hatujui ni kwa namna gani wanakwenda kufidiwa, hatujui ni kwa namna gani tunaenda kugusa ile trauma ambayo waliipata kuitia *Operation Tokomeza*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni hii ha bari ya ufugaji, uhifadhi pamoja na ukulima. Ndugu zangu katika hili niseme wazi kwamba, viongozi lazima tuangalie tusije tukaligawa Taifa vipande vipande. La pili, vile vile niulize hivi ni lini ng'ombe wamewahi kula miti, hivi ni lini ng'ombe wamewahi kuchoma mkaa, kwa sababu leo hii tunasema kwamba wafugaji tuwaondoe kabisa kama vile hawapo kwenye ramani ya hili Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba baadhi yetu tumekuwa Wabunge, tumekuwa Mawaziri, tunesoma kwa sababu ya ng'ombe. Naomba nioneshwe leo hii nani Waziri hapa ambaye amewahi kusoma kwa sababu ya utalii peke yake? Ni mwananchi gani Mtanzania ambaye anaguswa moja kwa moja na *impact* ya utalii kwenye nchi ukilinganisha na *impact* ya ufugaji kwenye Taifa letu? (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakosea viongozi na baada ya hapo tunakwenda kuwatesa wananchi. Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, nilimsikia kauli yake aliyoisema, anapaswa kuwaomba radhi Watanzania na hususani wafugaji wa Taifa hili. Narudia akitaka abaki salama kwenye kitu chake na nilifikiri pengine angekuwa Waziri wa kwanza kuja kutumbuliwa kwa ile kauli, kwa bahati mbaya Kitwanga ametangulia, nimwombe anapaswa kuwaomba radhi Watanzania baada ya hapo akaw chini na Waziri wa Ardhi na Waziri wa Mifugo wazungumze waangalie ni kwa namna gani tunaweza ku-strike a balance. Tunahitaji mifugo, tunahitaji conservation at the same time tunawahitaji wakulima. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hawezi tu kuwafanya wafugaji ni kama vile ni jamii ambayo imekuwa neglected, ni watu ambao wamekuwa vulnerable kwa miaka mingi, at the same time na yeye Minister anasimama anaanza kusema kama vile kwanza hatufugi, hatuhitaji ng'ombe kwenye nchi, hatuhitaji nyama wakati nimemwona leo akila nyama canteen. Sasa nashindwa kuelewa, hawa ng'ombe anaowakataa mbona leo aliquwa anawala kwa nini asingekula msitu pale canteen leo, kwa nini asingekula nyama ya simba pale canteen! (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana tunapokuwa viongozi tuangalie namna ya kuliunganisha Taifa na siyo kuligawa Taifa, tunawahitaji wafugaji, tunahitaji uhifadhi, tunawahitaji wakulima ili Taifa liweze kusonga mbele...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Alberto.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa mara ya kwanza nimeitwa jina ninalolipenda la Albeto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ya kuzungumzia na kwanza nitaanza na mjusi, Wajumbe wengi humu wamepiga kelele juu ya mjusi kwamba, kwa nini harejeshwi Tanzania! Mimi ni katika wale ambao wanaunga mkono arejeshwe, lakini najiuliza kama tuko tayari kumpokea na tunaweza kumtunza; lakini kumrudisha tunaweza. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kuna *international precedents* nyingi zimetokea za mali ambazo zimechukuliwa katika nchi na zikarudishwa. Mfano wa karibuni kabisa ni wa Ethiopia, kuna mnara unaitwa Obelisk, umri wake ni karibu miaka 1700 na una urefu wa mita kama 24, ulikuwepo Italia kwa miaka 68. Baadaye Ethiopia wameweza kuurudisha na upo nchini kwao na ni sehemu ya utalii wao. Sasa inategemea kama Serikali tunaweza ku-negotiate tukaweza kumrudisha. Hata hivyo, kabla ya hapo ningependa sana futengeze mazingira ili mjusi huyo asije akaozea kwetu. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la utalii nitalizungumza kwa undani kidogo kwa sababu ni area ambayo nailewa vizuri zaidi. Kwanza, ningetaka kusema kwamba, tuna haja ya kushambulia *emerging markets, emerging markets, markets* mpya hizi za China, Urusi, India, Arabia, ni sehemu ambazo zinatengeneza pesa sana na hata ukilinganisha namna ambavyo wanatengeneza mamilionea per day wao wako mbele. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni namna gani utatumia kuwavutia kuja kwetu? Nitatoa mfano mdogo wa namna ambavyo kama tutaweza kufaidika na *emerging markets*, mfano nitakaotoa ni wa Mauritius. China katika mwaka 2011 walipeleka watalii 15,000 Mauritius. Mwaka uliofuata walipeleka watalii 22,000, mwaka mwingine walipeleka watalii 14,000 na mwaka 2014 wakapeleka watalii 63,000 na ushee. Mwaka 2011 India walipeleka watalii 53,000, ikawa 55,000, ikawa 57,000, ikawa 61,000 na naamini tukisema hivi sasa *rate* yao itakuwa imepanda. Kwa hivyo, namshauri Mheshimiwa Waziri kwenye Wizara yake ajaribu kwenye *emerging markets*, hilo la kwanza. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni suala la *re-branding* Tanzania. Tanzania tumepitia process mpya kubwa na ndiyo maana hata tukaona kuna haja ya kufanya katiba mpya kwa sababu kama nchi tumepitia mambo mengi lazima tujitambulishé upya kama Tanzania. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *branding* ambayo tunayo hivi sasa ndiyo ambayo kwa miaka yote imetupa watalii milioni, labda 1,200,000. Hii *branding* nataka ifanywe upya tujitambulishé tuna vitu gani vyaa kuuza, vinapatikana wapi, vinapatikana vipi, *rates* zetu ziko vipi. Kwa mfano, tumetumia *brand* ya

Tanzania, land of Kilimanjaro and Zanzibar kwa miaka yote hiyo, tumepeata watalii 1,100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashindwa kupata watalii zaidi kwa sababu sisi hatutaki kujilinganisha na wengine, sisi tuna vivutio vingi, Mauritius wana vivutio vichache kuliko sisi lakini wao wanatupita, wao tayari 2014 walikuwa wana watalii 1,200,000. Ni kisiwa cha watu 1,500,000 lakini wamepata watalii 1,200,000. Kwa hivyo kuna haja ya ku-re-brand. Lakini hiyo re- branding tusiifanye sisi tuwape watu, mashirika makubwa wanaoweza kufanya re-branding ili tuweze kupata faida. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo hiyo na sasa nataka nizungumzie habari ya *re-discovering our potentials*. Watu wengi wamezungumza hapa, kuna watu wamezungumza kwamba, inaonekana kama kuna upendeleo au ndiyo *culture* tuliyoachiwa, kwamba utalii ni kaskazini. Lakini kuna *southern circuit* ambayo inaweza ikatusaidia sana. Pia kuna sehemu nyingine za pembezoni, kwa mfano Mara, Arusha wameungana na Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumejipanga vipi sisi utalii wetu kuungana na Uganda, tumejipanga vipi utalii wetu kuungana na Mozambique, kuungana na sehemu nyingine ambazo tunapakana nazo. Nitatoa mfano wa Kagera, kagera tuko na Uganda. Lazima tuwe na package ambayo inamfanya mtu akienda Uganda baadaye akija Kagera ashawishike. Juzi nilifunuliwa macho na Profesa Tibaijuka hapa aliposema kuna ziwa linaitwa Ziwa Burigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiambiwa chochote dakika ile ile nakwenda kwenye internet. Pale pale nikaenda kwenye *internet* nikaona *how beautiful that place is*. Ni mahali ambapo mtu yeyote angeweza kwenda. Tuna game reserve ya Burigi lakini tuna ziwa, lakini hakuna hata kibanda cha mtalii kufika. Pale kwa nilivyosoma na nimetamani, nimemwambia mama Mwigaje hapa nataka niende nikaone, ile picha niliyopata Ziwa Burigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tunaweza tukamshawishi mtalii kutoka Uganda akaja pale, hali kadhalika *southern circuit*. Kuna fursa nyingi beach sun mpya za Mtwara na Lindi, mnazitumiaje kama sehemu ya *southern circuit*. Kwa hiyo, tubadilike katika hilo.

Mheshimwa Mwenyekiti, halafu nataka kuzungumzia juu ya *advertising*. Nchi kama Malaysia, Indonesia, zimepiga hatua kubwa sana katika utalii, lakini bado wanatangaza *costing millions to them*. Tangazo lao linapendeza, unalipenda, unalisikiliza. Kwa hivyo lazima tuchukue *international firms* siyo tunapeleka tangazo kwenye Sunderland ambalo linawekwa tu hivi. Tangazo lazima liwe *strategic*, idadi ya watu wangapi, tunafaidika vipi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika nukta hii hii nataka nizungumzie Walking billboard. Tuna Mbwana Samata anacheza mpira Belgium, kwa nini kama Taifa au kama Wizara tusiingie naye mkataba akifunga goli akiinua jezi tu visit Tanzania, ambayo inaonekana dunia nzima na sio Belgium tu, lakini hatutumii potential tulizonazo. Kwa hivyo, ningependa hili tulitazame. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sports tourism. Nilizungumza na Mheshimiwa Nape juu ya namna ya sisi kujipanga kama Taifa. Nchi hii hakuna international tournament ya golf, hakuna international tournament ya Tennis, hakuna international tournament ya cycling. Nchi kubwa lakini haijajipanga vyovoyote vile kimichezo. Kwa hivyo, ningependa kwamba, eneo hilo pia tulitengeneze ili tuweze kuzitumia vizuri tufaidike. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka nizungumzie role mpya ya Mabalozi. Mabalozi wote lazima waelekezwe kwamba, hivi sasa tutengeneze tourism diplomacy kuwe na package, watayarishwe, wawekewe na malengo namna ambavyo wanaweza kukuza utalii wetu; lakini isaidie kwamba, watengenezewe package ili tuweze kufaidika ndani ya nchi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nataka nizungumzie suala la kutengeneza mnaso wa community kubwa ya wageni wanaishi maeneo ya East Africa. Mzungu au expert yejote ambaye yuko East Africa unamtoza visa sawasawa na ambaye amekuja leo kutoka Marekani. Tuwe na package maalum ya expertise kutoka Rwanda, Kenya, Uganda, tuwe na package maalum washawishike kuja kwetu. Mtu mmoja alisema lazima tuweke rates za kuvutia ili watu waje, baadaye tuweze kubadilisha lakini lazima tu-change katika strategy hizi na kwamba, tunatoza kodi nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni very expensive destination, tuisjisifu kwa watu wanaokuja, tungeweza kupata watu zaidi kama tutajitengeneza vizuri zaidi. Sisi ni losers, hatuna haja ya kushindana na Kenya, hatuna haja ya kushindana na Uganda, tuweke rates ambazo zinatufaidisha sisi na ndiyo maana tutawashinda. Ndiyo maana kukitokea matatizo Kenya sisi tunafaidika. Kwa hiyo, tusingojee mpaka Kenya wapigane sisi tufaidike. Pia tunaweza tukaweka rates ndogo ili tuvutie watalii zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ningependa kuzungumzia habari ya standards. Tunakwenda nchi za wenzetu, tuna hotel higher lakini unaona kwamba, bado tuko nyuma, service mbovu. Ningependa tuhakikishe kwamba, tunakuza sekta kwa kuwa hata na masomo ya degree na tuweze ... (Makof)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Alberto. Mheshimiwa Saul Henry Amon ajiandae Mheshimiwa Mtuka.

**MHE. SAUL H. AMON:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu. Vilevile niwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Rungwe kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, sina mengi lakini vilevile siko mbali na Profesa Norman alichokizungumza, kwamba, utalii na hata mzungumzaji aliyejita ameongea hicho hicho, utalii umeangaliwa sehemu moja, hilo ndilo langu la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu misitu. Pamoja na kwamba kuna historia na jiografia ya misitu iliyopo na inayovunwa lakini naona ni Mufindi, Mufindi, Mufindi wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msitu pale Mbeya ulikuwepo siku zote, siku hizi naona ni jangwa. Msitu wa Kawetele, toka ulivyovunwa sijui mwaka gani lakini mpaka leo hii Kawetele hakuna miti, Kawetele ni jangwa, hatujui kwa nini wanafanya hivi na kwa nini Maliasili na Utalii wameamua kufanya hivyo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina sababu ya kujuliza, tunashangaa hata Mbeya, Iringa tuna matatizo ya madawati, lakini hiyo miti ingeweza kusaidia madawati kwa ajili ya thamani ya ofisi zetu na shule zetu. Mimi kwa Mheshimiwa Waziri nina ombi kwamba, ningependa kuona mapema iwezekanavyo Kawetele inarudishwa kama ilivyokuwa zamani. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna watu wanaoshambulia misitu ambayo imewekwa kama hifadhi. Rungwe na misitu mingine ya asili bado haihifadhiwi inavyotakiwa, sijajua ni wapi ambako mnaangalia, ni nchi nzima au kuna kipande ambacho mmeamua kukiangalia. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia utalii, tunapozungumza maliasili, ni lazima tuzungumzie nchi yote kwa ujumla; kwa sababu pamoja na kwamba, ina faida kwa ajili ya kupata fedha, lakini vilevile kuna faida kwa ajili ya mazingira yanayoharibika na kupotea bure kwa sababu tu wahusika hawafuatilii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali haiwezi itupe wananchi wa Mbeya tupande ile miti tuweze kuitumia ile ardhi; kwa sababu Mbeya kuna watu wengi. Ukiangalia Mbeya misitu mingi imepandwa na wananchi na bado inavunwa vizuri na wananarudishia iweje Serikali ambayo inapata faida, kwa

sababu ile ni kama biashara ya Serikali. Chukueni faida yenu lakini rudisheni mtaji pale pale, kwamba wakati wa kuvuna vilevile irudishwe. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye Sekta ya Utalii. Mchangiaji hoja aliyejita ameongea habari ya kwamba, kuna service mbovu, lakini hiyo yote ni kwa sababu ya kutokuwa na utamaduni. Hatuna chuo ambacho ni thabitii kwa ajili ya kufundisha watu watakaohudumia hoteli zetu ili kuwe na kiwango cha Kimataifa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana tunacho chuo lakini hakitoi na tumebakia kugombana na kusema hawa hawafai. Angalia wenzetu wanaotoka nje standard zao wanavyofanya, ni kwa sababu wamewekeza kwenye vyuo vya utalii. Huko wanapata ma-manager wazuri, wapishi wazuri, wahudumu wazuri. Sisi hivyo vyuo viko wapi? Kweli mtu atoke Mwanza, aje ajifunze Dar es Salaam peke yake ni kweli? Mtu atoke Mbeya aende Dar es Salaam kujifunza habari ya chuo. Vyuo vilivyopo havikidhi haja ambayo inaweza ikatoa *international services*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo bado kwenye utalii. Utalii hautangazwi Nyanda za Juu Kusini na kusini mwa Tanzania na maeneo mengine, watu mmejikita maeneo ya kaskazini peke yake. Mheshimiwa Waziri aende Malawi, akaone utalii unavyofanya kazi kwenye Ziwa Nyasa. Sisi hapa tuna Ziwa Nyasa na tuna fukwe ambazo ni nzuri, ambazo hazichafuki, hazina takataka, lakini hatuzitangazi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono asilimia mia moja mchangiaji aliyejita kwa uchangiaji wake, ametoa mchango wa kizalendo. Naomba Wizara na vitengo vyake, viweze kutangaza utalii uliopo. Kwa mfano, Nyanda za Juu Kusini wameongea habari ya barabara kwenda kwenye mbuga za wanyama, vilevile tunaongea habari ya barabara kwenda Mlima Rungwe, hakuna barabara watu waende wakatembelee Mlima Rungwe. Hatuna barabara kwenda kwenye fukwe nzuri za Nyasa, kuna Ziwa Ngozi ambalo haliingizi maji wala halitoi maji, hamna anayetangaza. Tuna Ziwa Kisiba, kuna ziwa zuri sana ambalo halichafuki, halitoi maji na wala haliingizi maji lakini hatulitangazi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wangu ninavyojua ni kwamba, hii Wizara inafanya biashara, tunaweza kufikiria kwamba, inafanya biashara kwa kulipa Serikali mapato ya bilioni 10 au15, lakini si biashara ambayo watu tungejiwekeza zaidi kwenye hayo maeneo kama ingekuwa zaidi ya hapo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu nyingi sana ambazo ningeweza kuchangia, lakini kufikia hapo haya yalikuwa ni mawazo yangu na kwamba, tuchukulie umuhimu wa hali ya juu kutangaza vitega uchumi vyote, vivutio vyote ambavyo viro maeneo yote ya Tanzania bila kujali ni wapi, watu waende kote. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimempa Mheshimiwa Waziri mfano wa kwenda Malawi akaangalie, wanatoka watu sehemu mbalimbali lakini fukwe tulizonazo sisi ni nzuri zaidi kuliko zilizoko Malawi. Haya ni yangu machache kwa leo. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtuka.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekii, nikushukuru kwa nafasi hii, na mimi niweze kutoa mchango kwenye Wizara hii ya maliasili na utalii. Niende moja kwa moja kwenye eneo la migogoro kati ya hifadhi na wananchi, lakini migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini chanzo cha migogoro hii? Iko mingi lakini mimi nimeona viko vyanzo vinne. Sababu ya kwanza ni ongezeko ya watu na mifugo wakati ardhi haiongezeki. Ni kweli wakati wa uhuru tulikuwa watu milioni tisa sasa hivi tunakwenda kwenye 50. Mifugo ilikuwa michache lakini sasa hivi mifugo ni mingi, lakini ardhi iko palepale. Pale kwangu Manyoni sasa hivi tumeongezeka sana lakini pia watu wanaohamia. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ya migogoro hii, ni uharibifu wa mazingira, tunakata miti sana. Kwa mfano, kwangu pale Manyoni upande wa Mikoa ya Magharibi wamekata miti sana, mazingira yameharibika, sasa wanakuja wanaseoge Mkao wa Singida-Tabora wanavamia huko kuja mpaka Chunya na Mbeya. Watu wanakata miti watu wanachoma mikaa. Kaskazini huku, kuna shida pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho ni chanzo cha mgogoro cha nne kwamba, baada ya mwaka 2009 sheria ilibadilishwa mipaka ya hizi hifadhi ikafinywa ikala maeneo makubwa sana, Umashaini huku, Ugogoni huku, imekula sana Usukumani huku. Watu wanahama kutoka Umashaini, watu wanahama kutoka Usukumani magharibi wanakuja kuvamia Morogoro, Rukwa na maeneo mengine; huu ni mgogoro wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikia mchangiaji mmoja jana anachangia kwa nguvu sana kwamba sisi hatukuwahi kuona ng'ombe wengi wa namna hiyo. Sasa hivi tunaona malaki ya ng'ombe ni vitu vigeni kwetu lazima huo ni mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha mwisho nilichokiona mimi ni uvamizi wa mifugo kutoka majirani zetu, Rwanda, Kenya, wanaingia kwenye misitu, wanawasukuma wenyeji huku tunaanza kugombana nao, hicho ni chanzo pia cha migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini sasa kifanyike? naiomba Serikali yangu ambayo ni sikivu ya Chama cha Mapinduzi irejeshe mipaka ya zamani kwenye hifadhi. Zamani ile mipaka Mungu ameiweka ni ya asili, Wanyama wanakaa kule Binadamu anakaa huku tusilazimishe kuongeza mbuga zile, tusilazimishe kuongeza misitu wakati sisi tunaongezeka, mifugo inaongezeka. Naomba sheria hii ibadilishwe, mipaka hii irejeshwe ile ya zamani, eneo hili litatupa ardhi kubwa sana migogoro hii itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia nyininge ya kupunguza migogoro ni wakati sasa wa kutekeleza ule mpango wa matumizi bora ya ardhi. Tutenge sasa matumizi bora ya ardhi. Kilimo tuwatengee eneo lao, wafugaji maeneo yao, makazi maeneo yake, viwanda maeneo yake, madini maeneo yake. Hebu tupange hii. Tuipime nchi tuweke mipaka ambayo iko *clear*, ugomvi huu utapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho kitasaidia, kuna *dormant Ranches*. Ranch ambazo hazitumiki, tuangalie uwezekano wa kubadilisha matumizi. Kuna maeneo ya hifadhi pia ambayo hayana tija, tuyabadijishe matumizi pia. Tugawe kwa wakulima, tugawe kwa wafugaji, itatuongezea ardhi na pia migogoro hii itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine. Sisi wakulima na wafugaji, mimi ni mkulima pia na ni mfugaji. Namwomba hata Mzee Mtuka anisikilize kwenye jambo hili. Wafugaji tuwe tayari kupunguza idadi ya mifugo. Tupunguze idadi ya mifugo tumeongezeka na mifugo imeongezeka. Ardhi haiongezeki, sehemu za kuchungia hazongezeki, tuwe tayari kupunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ilisimamie hili, zile Wizara nne zile zisimamie, zikae na wakulima, zikae na wafugaji, waseme wao kiwango cha mwisho cha mfugaji kuwa na mifugo ni kiasi gani? Kama ni ng'ombe mia moja tukubaliane iwekwe kwenye sheria, tukubaliane hilo. Haiwezekani mtu ana ng'ombe 2,000 mwagine 5,000 haiwezekani ardhi haipo. Wafugaji wenzangu natoa wito, tukubaliane kiwango rasmi ambacho kila mfugaji ataishia kufuga. Huwezi kufuga tu yaani ng'ombe unaotaka, haiwezekani, hili pia liwekwe kwenye sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti lakini kingine, baada ya kugawa yale maeneo, upande wa wafugaji nashauri sana wawekewe miundombinu. Hebu Serikali itusaidie, leteni hata yale magreda na vile vijiko vyta Jeshi. Chimbeni mabwawa

kule kwenye maeneo ya wafugaji ambayo yametengwa, chimba hata mabwawa maji yajae huko, weka majosho, weka majengo ambayo Wataalam wa Mifugo watakuwepo kule ili kuwa-control hawa wafugaji wasiweze kuhamza hama. Ukiweka miundombinu hii, wafugaji hawatahama. Naliomba sana hilo, Serikali isaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihami hapo, nizungumzie kidogo vivutio vya utalii. Sisi Manyoni kule tuna kivutio kipyaa ambacho tunataka tukitilie nguvu na tunaomba Serikali ituunge mkono. Ukiiwaka Tanzania kwenye ramani, ukai-set kwenye mitambo ile, ukatafuta kile kitovu cha nchi kinatua Manyoni, kuna sehemu inaitwa Kisingisa. Hebu naomba mtusaidie Serikali eneo lile.

*(Hapa kengele iilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tweve, ajiandae Zainab Katimba na Mheshimiwa Vicky Likwelile.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia siku ya leo. Kwa kuwa hoja iliyoleta na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 inagusa maslahi mapana ya wananchi wa Mkoa wa Iringa hususani wanawake ambaa wameniwezesha kufika hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mionganini mwa Wabunge wanaowakilisha wananchi wa Mkoa wa Iringa. Sasa ndani ya huu Mkoa wa Iringa tunahifadhi kubwa ya Msitu wa Taifa wa Sao hill. Kwa muda huu niliopewa nina jambo moja kubwa ambalo nitalizungumzia, ni suala zima la TFS na utaratibu mzima wa utoaji wa hivi vibali vya kuvuna msitu wa Sao hill. Hili limekuwa ni tatizo kubwa sana. System nzima ya utoaji wa hivi vibali haieleweki. Vibali hivi vimekuwa vinawanufaisha wachache. Watanzania ambaa ni wazawa, wavunaji wadogo wadogo, kundi la akinamama, vijana na walemau hawapewi kipaumbele. Hawa wazawa ndiyo waloliwa msitu huu, hawa ndiyo wameweza kuutunza huu msitu mpaka umefikia hapo ulipo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka Serikali inatoa cubic meter 600,000 kwa Watanzania waweze kuvuna msitu huu. Hapa ndipo nina tatizo napo na ndipo panaposikitisha. Watanzania hawa ambaa ni wazawa hawanufaiki na huu mgao, ni wawekezaji ambaa wanapewa kipaumbele kuweza kunufaika na huu msitu. Nitatoa mfano mmoja, tuna hawa Wawekezaji ambaa wamepewa kuendesha Kiwanda cha Mgololo, wanajiita RAI-Group. Hawa ndio wamekuwa beneficiary wakubwa wa huu mgao wa vibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii 600,000 inayotolewa na Serikali RAI-Group wanapewa cubic meter 250,000 na kinachosikitisha zaidi, hawa RAI-Group wanalipa nusu ya bei ambayo wanatakiwa kulipia vibali hivi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibali kimoja, Mtanzania, Mwanairinga, Mwanamufindi analipa sh. 28,000/=, RAI-Group wanalipa sh. 14,000/= tu. Sasa ukipiga mahesabu kutoka kwenye hizo cubic meter 250,000 wanazopewa, ukizidisha mara hiyo Sh. 14,000/= maana yake wanalipa bilioni 3.5 kwa mwaka. Sasa wangeweza kulipa hiyo Sh. 28,000/= ambayo Mtanzania wa kawaida analipa, Serikali ingeingiza bilioni saba kwa mwaka. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo, ni vigezo gani wanatumia kuwapunguzia bei hawa RAI-Group na ni vigezo gani wanafanya hawa Watanzania waendelee kulipa hii Sh. 28,000/=? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa nipewe maelezo ni kwa sababu gani hawa RAI-Group wanapewa kipaumbele? Wanapewa hizi cubic meter 250,000 wakati hawa Watanzania wa kawaida Wanairinga hawawezi kunufaika na msitu huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa nipewe ufanuzi wa ukusanyaji wa kodi kutoka kwa hawa wawekezaji wa hiki Kiwanda cha Mgololo. Cha kusikitisha zaidi hawa RAI-Group wanapasua haya magogo, wanatengeneza hizi raw materials wanapeleka Kenya, wanaenda ku-process makaratasi ndipo waturudishie sisi hapa kununua wakati haya makaratasi yangekuwa processed hapa Tanzania, tungetengeneza ajira kwa vijana wetu. Kwa hiyo, naomba majibu yanayonitosheleza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa RAI-Group walishakuwa na Kiwanda Malawi, wamefukuzwa wamekuja hapa, sasa sisi tunawa-protect, moja tuwape vibali vingi, mbili bei ya chini, hii kweli inahuzunisha, inatukatisha tamaa sisi Wanairinga, inatukatisha tamaa sisi Wanamufindi, naomba tulifanyie kazi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, hawa RAI-Group wapande misitu yao na kama bado wataendelea kupanda msitu huu wa sao *hill* basi walipe bei moja sawa na Watanzania. Hata kama wakilipa bei hiyo moja lazima hivi vibali vipunguzwe, viende kwenye makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua asilimia kubwa ya wanawake na vijana sasa hivi wako kwenye hivi vikundi vya ujasiriamali. Tatizo la hivi vikundi ni maskini, havina pesa, hakuna miradi endelevu ambayo ingeweza kuwasaidia wao kuendelea kupambana na hizi changamoto zao za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri angewawezesha hawa vijana, angewawezesha hawa akinamama katika Wilaya zote, Iringa Mjini, Iringa Vijiini, Kilolo na Mufindi waweze kutumia hivi vibali angekuwa; moja, amewainua kiuchumi; pili, hivi ndivyo vitakavyokuwa vikundi darasa vya kuwashawishi watu wengine waendelee kupanda miti kwa sababu watakuwa wameona matunda na *benefits* ambazo zinatokana na upandaji na upasuaji wa miti hii. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa RAI-Group tunawapa vibali vikubwa. Hawajihusishi na mambo yoyote ya kijamii, barabara mbovu, madawati watoto wanakaa chini, kuna manufaa gani ya kuendelea kuwashikilia watu hawa wakati pale Mufindi tuna wavunaji wazuri wana viwanda, wamekuwa msaada mkubwa kuchangia madawati, kuchangia hospitali, hebu tuwape kipaumbele watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri *please, doesn't get me wrong*. Najua ndiyo umepata kuongoza Wizara hii, so prove to me kuwa unakasirishwa na jambo hili, tuwapiganie Watanzania wetu waweze ku-enjoy matunda ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *after all* Mheshimiwa Waziri tunasema tunataka Tanzania iende katika uchumi wa kat, Wizara hii ina nafasi kubwa ya kuwainua hawa wananchi, tuwawezeshe, tuwape kipaumbele hii ita-trickle down sasa tukiendelea kuwashikilia hawa RAI-Group tunawapa vibali cubic meter 250,000, hawa wengine hawanufaiki tutafikaje huko, lazima tuwaonjeshe matunda ya nchi yao. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti sasa kwa kumalizia namwomba Mheshimiwa Waziri, najua yeye ni msikivu, *he is competent*. Naomba tufike Mufindi, hawa wavunaji wanajua matatizo ya hivi vibali, wanajua solution ya kuweza kutatua hili tatizo... (Makofij)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zainab, jiandae Mheshimiwa Vicky Likwelile. Mheshimiwa Zainab Katimba yumo? Mheshimiwa Likwelile, ajiandae Mheshimiwa Heche na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Nami nianze kwa kuunga hoja mkono na kumpongeza sana Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hifadhi zetu kuna madini mengi sana na ili Mtanzania aweze kuyachimba lazima apate kibali kutoka kwa Wakala wa

Misitu. Akishakipata kile kibali anatakiwa kulipia ada milioni moja kwa mwaka na kama ana hekta kumi ina maana atalipa milioni kumi. Vilevile anatakiwa kulipia leseni 800,000 kila mwaka. Wakati huo huo anatakiwa kulipa asilimia nne kama *loyalty*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maombi ya wachimbaji wadogo wa Geita wamenituma nimweleze Waziri kwamba wanaomba sana kwamba hili haliwasaidii wachimbaji wadogo wadogo kwa sababu ada ile ni kubwa, lakini pia wanachangia maendeleo siyo kitu kibaya, kwa kuwa wanachangia maendeleo basi wafikiriwe kupunguziwa. Hilo ni ombi maalum kutoka kwa wachimbaji wadogo wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumzie kidogo hili jambo ambalo limezungumziwa sana na Wabunge wenzangu linalohusu wafugaji. Mimi pia ni mfugaji na nimetoka sehemu ya wafugaji. Naungana mkono na wale wenzangu wanaosema kweli kuna umuhimu wa kuwashawishi wafugaji wetu kuona kama inawezekana wakapunguza hii mifugo ambayo pengine imekuwa mingi kama ambavyo mnasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini natofautiana na wenzangu kwa namna wanayosema mifugo hii ipunguzwe. Isipunguzwe kwa kuwaumiza hawa wafugaji lakini ipunguzwe kwa kuwanufaisha, huo upunguzaji uwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kaka yangu Dotto aliongea na mimi nilipata uchungu sana. Inaumiza kuona mfugaji anauliwa mifugo yake ng'ombe sitini, ishirini, thelathini, yaani hiyo ni *torturing* ya aina gani? Yaani jiweke tu kwenye viatu vya huyo mfugaji maumivu aliyo yapata, achilia mbali hasara kwamsababu mtu anapofuga kitu tayari anammapenzi nacho. Mimi ni mfugaji nina mbwa kama wanne nyumbani kwangu. Hivi juzi kuna mbwa mmoja, amekufa katika mazingira ambayo mimi sikuya elewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hao mbwa nilikuwa nampenda sana yule mbwa, amekufa sikuelewa amekufaje, mpaka hivi ninavyozungumza ameniuma na ni mbwa tu mmoja, hebu fikiria hawa ng'ombe sitini ana maumivu kiasi gani? Yapo mengi ya kuwasaidia wafugaji wetu wakafuga katika hali nzuri na wakanufaika na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri akae vizuri na Waziri wa Mifugo, wakae vizuri na Waziri wa Ardhi, wakae vizuri pia na Waziri wa Viwanda waje na Mkakati Maalum wa kuwasaidia hawa wafugaji ili wasije wakajiona kwamba kumbe kufuga katika nchi hii ya Tanzania ni mateso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa Serikali ikishirikiana na hawa wafugaji ambao wana mifugo mingi na wana pesa nyingi, wanaweza wakawasaidia hata wakaenda kujifunza kwa wenzetu Netherland wanafugaje! Ufugaji wao utakuwa ufugaji wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nilikuwa najaribu ku-google kidogo asubuhi, nijaribu kuona wenzetu walifanyaje. Netherland wanafuga na ufugaji wao una tija, sitaki kujilinganisha nao kwa sababu wenzetu wako mbali sana, lakini bado tunaweza tukajifunza kutoka kwao. Serikali ikawasaidia hawa wafugaji, ikachukua labda kila mkoa ambao una wafugaji wengi wakachukuliwa kumi au kumi na tano ama ishirini wakaenda kule Netherland wakaenda kujifunza, kuna teknolojia nzuri kabisa ambayo wakirudi nayo hawa wafugaji watakubali wenyewe kwa kusema kwamba tunapunguza mifugo na sisi tunafuga kisasa na ufugaji wetu uweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanayo teknolojia nzuri sana ambayo siwezi kuizungumza hapa, nimejifunza mimi leo hii, lakini naamini Mheshimiwa Waziri akifanyia kazi, akashirikiana na hawa wafugaji; kwanza wana pesa wanaweza hata wao wenyewe wakajilipia ndege na hoteli kule wakaenda kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile vijana wetu wanaosoma vyuo vikuu, wanaosomea mambo ya kilimo, tuwapeleke nje wakasome. Hili jambo hatuwezi tukaliondoa haraka sana bali taratibu, kama kweli tunataka ufugaji upungue, watu wasifuge ng'ombe elfu thelathini, wasifuge ng'ombe wengi kiasi hicho, tuisiwakatili ghafla sasa kwamba mnaanza kufuga ng'ombe watano, mwisho kumi, hapana. Taratibu, taratibu kwa kuanza na *mind set* zao, tuwaelimishe kwanza kwa kuwapa hiyo exposure, waende wakajifunze, warudi na vijana wetu wanaosoma pia watatusaidia kuhakikisha kwamba ufugaji wetu unakuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilivyosema Mheshimiwa Waziri akae na Wizara hizo kwa maana ya Wizara ya Ardh, Wizara ya Viwanda bado naona kuna umuhimu wa kutengewa maeneo. Watengewe maeneo maalum ili waweze kulisha mifugo yao wakati tukiendelea huko kwenye teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kidogo kuhusu suala la utalii, nilipokuwa naangalia hiki kitabu ukurasa wa 15 nimeona jinsi ambavyo, (sintasoma) lakini nimeona jinsi ambavyo utalii umeweza kuchangia pato la Taifa kwa kiasi kikubwa, nawapongeza sana. Ninaamini bado kuna vitu vya ziada vya kufanya ili utalii huu uweze kutuletea pato kubwa sana kwenye Taifa letu na kukuza uchumi wa nchi yetu. Kwa mfano, tukiamua kumleta Jay Z na familia yake hapa, tukamleta David Beckham na Victoria Beckham hapa, tukakubaliana nao kabisa kwamba hiyo tour yao iwe broadcasted na vyombo

vyote vikubwa vikaimulika Tanzania kwa siku zote watakazo kaa hapa, Serikali mkakubali kabisa kuwa-host, wakawa kila mahali wanapoenda vyombo vyote viimulike Tanzania, ninaamini watajua Mlima Kilimanjaro uko Tanzania maana sasa hivi tunalalmika tu, ooh, Kenya wanasema Mlima Kilimanjaro uko kwao, ili tuijoneshe dunia kwamba mlima Kilimanjaro uko Tanzania tukubali kuingia gharama kama hizo, tuwalete watu maarufu duniani, watembelee Mlima Kilimanjaro, vyombo vyote vikubwa vya habari vimulike nchi yetu, kila mahali wanakoenda wamulikwe, itaonekana kumbe Mlima Kilimanjaro uko Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyayo amba yule binti wa Kenya alikurupuka akasema sijui Olduvai Gorge iko Kenya tutawa-prove wrong kwamba kumbe haiko Kenya iko Tanzania kwa kuwaleta watu mashuhuri wakatembelea hayo maeneo. Waende Rubondo, Rubondo - Geita kuna hifadhi zetu nzuri sana pale, lakini haijulikani. Wakija watu kama hao wakatembelea hata hivi vivutio vyetu ambavyo havijulikani itakuwa mojawapo ya kuvitangaza na watalii wengi watakuja na mwisho wa siku tutapata pesa nzuri sana. (Makofl)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema Tanzania hii ndiyo nchi pekee tunatoa Tanzanite, ninasikitika sana kuona kwamba hatujitangazi kwamba hata hii Tanzanite inatoka kwetu. Hao hao akina Jay Z wakija hapa wakaenda kwenye duka moja hapo Arusha itajulikana kumbe Tanzanite inatoka Tanzania. Camilla alikuja hapa na Prince Charles wakenda pale *Cultural Heritage* wakanunua Tanzanite nyingi, lakini hakuna mtu aliyejua kwamba wamekuja lakini kama tungekuwa tuliongea nao, tukafanya utaratibu, wakaonekana wakiwa kwenye lile duka walilonunua zile Tanzanite tayari tungekuwa tumeonesha dunia kwamba Tanzanite iko kwetu na tayari tungevutia watu wengi kuja kutalii hapa nchini kwetu. (Makofl)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa utalii unaweza ukawa chanzo kikubwa sana cha mapato kuliko hapa huu ukurasa wa 15 unavyosema. Naamini tunaweza kufanya vizuri zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nimpongeze Waziri na nimirikie kila la kheri nikiamini kwamba atayazingatia hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Heche, ajiandae Mheshimiwa Selasini na ajiandae Mheshimiwa Ryoba Chacha.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili ni chombo cha wananchi na nataka niseme Bunge hili lingefanya kazi yake kama chombo cha wananchi na siyo vikao vya vyama, hii bajeti ya Mheshimiwa Maghembe ilikuwa haipiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alikwenda kwenye tv anasema wafugaji wanatembea nyuma ya mikia ya ng'ombe. Waziri anasema ng'ombe hawana faida, kwanza faida yao Pato la Taifa wanachangia asilimia nne tu! Kwamba utalii sijui unachangia asilimia 22. Sasa unajuliza hivi leo tungekuwa tumeondoa ng'ombe wote katika nchi hii, kama sukari tu imetushinda kuagiza, nyama ninyi mngeweza kuagiza watu wakala nyama? Sukari peke yake imetushinda. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kitu kwenye ng'ombe ni pesa, maziwa, kwato, kila kitu! unachotupa pale labda ni sauti tu peke yake. Kila kitu kwenye ng'ombe ni pesa. Tumeshindwa wenyewe kusimamia ng'ombe hawa, leo watu wanasimama kwenye Bunge la Watanzania wanasema ng'ombe wanaharibu mazingira, kwamba mifugo inaharibu mazingira. Ni utafiti wa wapi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Dar es Salaam watu wanatumia mkaa, nchi nzima ni mikaa. Watu wanakata miti kwa ajili ya mikaa, watu wanatumia nishati, tumeshindwa kupelekea watu nishati tunasema mifugo inaharibu mazingira. Hata mkiua ng'ombe wote nchi hii halafu mkaacha watu wakaendela kutumia mkaa, nchi hii itakuwa jangwa. Pelekeeni watu nishati Dar es Salaam, pelekeeni watu nishati rahisi Arusha na Mwanza, Majiji matatu peke yake mki-control watu wasitumie mkaa kesho yake nchi hii itakuwa kijani tupu. Leo mnakuja kusema ng'ombe anaharibu mazingira, ng'ombe anakata mtii? Hiyo haikubaliki. (Kicheko/Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Maghembe ukumbuke kwenye Bunge la Katiba aliwaita wafugaji nyumbani kwake akawanunulia chakula anawashawishi wapigie Katiba kura, leo unawaita kwamba wanaharibu, unasema ng'ombe anaambukiza magonjwa, hauli nyama ya ng'ombe wewe? Utakula pundamilia kila siku kweli? Hilo ni vyema likaeleweka. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijiji vimeingia kwenye migogoro na TANAPA na mbuga kwa sababu watu wa mbuga wana extend mipaka yao. Vijiji vya Nyanungu, Kegonga, vijiji vya Masanga, hivi vijiji mpaka mwaka 1963 vilikuwepo na vina GN! Baada ya mwaka 1963 mipaka ya mbuga imekuwa extended, ni migogoro kila siku watu wanauawa.

Mheshimiwa Waziri ninaomba Kata tatu hizo nilizozitaja, Kata ya Kwhancha, Kata ya Nyanungu, Kata ya Masanga - Gorong, I mean uende pale ukatatue ile mipaka, vile vijiji vilikuwa nje ya mbuga na mipaka ya TANAPA ndiyo imekuwa extended kufuata mwananchi na mnawahamisha hamna sehemu wanayochungia ndiyo maana inaleta migogoro. Kwa hiyo, hilo nilitaka niliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo leo tungekuwa tuna Bunge la Wananchi tusingepitisha bajeti hii ni Operesheni Tokomeza. Nina picha hapa, naomba karatasi moja ije mezani kwako na nyingine iende kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013 watu waliuawa, watu walichomewa nyumba zao, mifugo ilipigwa risasi, ng'ombe anauawa, ng'ombe anaua tembo. Mbuzi waliuawa, watu wakabaki wanalala nje, Bunge likaja likajadili hapa, mkasema watu walipwe fidia. Kuna watu waliuawa kinyama, panga linachomwa moto mtu anaambiwa akanyage kwenye panga, akikanyaga akitoa mguu nyama inabaki pale, watu walipigwa misumari. Bunge likaja likajadili hapa, hakuna kitu chochote mpaka sasa kilichozungumzwa kwenye bajeti hii ya Serikali kwamba hawa watu wanakwenda kulipwa vipi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali wanapokuja ku-wind up hapa watuambie hoja ya operesheni tokomeza, ambayo ilitokomeza watu wetu, watu maskini! Madiwani, Wenyeviti wa vijiji na mpaka leo majangili wakubwa hawajaguswa na operesheni hii. Hawakuguswa na hawajaguswa. Ninyi wote ni mashahidi mnakumbuka hapa, Al Jazeera walitangaza na BBC kwamba Rais wa China alipokuja Tanzania aliondoka na meno ya tembo. Hamkuwahi kukanusha. Wachina kila siku ndiyo wanakamatwa kwa sababu Serikali yetu inakwenda kupiga magoti kwa Wachina kila siku hamtaki kushughulika na Wachina. mnakuja kushughulika na watu wanyonge! watu maskini. Leo mnasema utalii, utalii huu, mimi sikatai kwamba utalii uwepo na unachangia kwenye Pato la Taifa lakini utalii unagusa mwananchi wa kawaida kule chini kweli kwa maisha yake? Mpaka pesa hizi zije kwenu, mje mzishushe ziende kwa wananchi, mzunguko wenu, mnaweza kweli? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu akiwa na matatizo atauza ng'ombe wake, atatibu mke wake, atasomesha mtoto wake, atafanya maendeleo yake binafsi kwa pesa zake. Lakini pesa ambazo zinaingia Serikalini hatukatai, tunahitaji pesa hizi zije Serikalini, lakini ni lini mtazishusha ziende kwenye maendeleo ya mtu mmoja mmoja kule kijijini? Ng'ombe ana mfungamano au mifugo ina mfungamano na maisha ya watu moja kwa moja ya kila siku. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba anapokuja ku-wind up hapa Waziri atuambie, hatukatai wafugaji watengewe maeneo, wapate maeneo yao ya kulisha, lakini leo tusije hapa tunawapaka rangi kana kwamba wafugaji hawafuati sheria, wafugaji siyo watu wazuri, wafugaji wanahonga Mahakama, yaani kila anayesimama hapa, kuna watu wanafikiri ng'ombe ni mdudu lakini nyama ya ng'ombe wanataka kula. Wamesimama huku wanazungumza mpaka wanatetemeka, wanasema tupigwe risasi. Tupigwe risasi kwenye nchi yetu? Tuna kosa gani sisi? Sisi ndiyo tunawaletea nyama mnakula kila siku hapa

kantini nawaona pale mnabugia nyama, supu, makongoro sijui nini, yanatoka kwenye ng'ombe hayo na maziwa, usipoletewa chai ya maziwa unalalamika, unafikiri maziwa ya mbwa hayo? Hayo ni maziwa ya ng'ombe ni lazima yatoke kwenye ng'ombe. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba watu wasizungumze hapa kudhalilisha watu wengine na wakazungumza kana kwamba hii nchi ni ya kwao peke yao. Hatukatai tunahitaji wakulima walime, tunahitaji na wafugaji tupewe nafasi ya kufuga katika nchi yetu.

Ninaomba sana Mheshimiwa Maghembe unapokuja hapa utuambie hawa watu waliouawa kwa mfano kule kwangu waliuawa Peter Maseya alipigwa vibaya sana na akauawa na familia yake mpaka sasa iko *traumatized*. Aliuawa Nicholas Wegesa Moserega, Mheshimiwa Waziri uje hapa utuambie nyumba zilizochomwa moto, ng'ombe waliouawa kwenye Kata zile tatu zaidi ya ng'ombe 184, uje utuambie majibu yake ni nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais aliunda Tume ya Majaji kwenda kuchunguza na mnachukua vitu hivi kwasababu mmeshawaona Watanzania ni wasahafulifu, mnachukua mnavitunza, mnaunda Tume, hamtoi majibu mnakalia yale majibu. Tunataka hayo majibu tuambiwe ni nini *findings* za hayo majibu na ni kwa vipi tunakwenda kuondoa matatizo yaliyojitekeza. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Selasini anaafuata na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha ajiandae.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, na kwa kweli hii ni nafasi ambayo nilikuwa naisubiri kwa hamu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nzungumzie mambo mawili ambayo yanaendelea katika Jimbo langu. Mwaka 2011 nilisimama katika Bunge hili nikasema Jimbo la Rombo halina hifadhi ya wanyama, nilisema hivyo kwa sababu tembo kutoka Kenya, Mbuga ya Tsavo pamoja na Amboseli walileta maafa makubwa sana katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu vijiji 20, Kata ya Holili, kijiji cha Kidondoni Kata ya Chana, kijiji cha Ngoyoni, kijiji cha Ngareni, Shimbi Kati, Kiraeni, Msaranga, Mahorosha, Leto, Urauri na Rongai, mazao ya wananchi yaliliwa na tembo, wananchi waliuawa na wengine wakapata vilema vya kudumu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fidia yaliipelekwa Wizarani kuanzia mwaka 2012 hadi leo hakuna majibu, hakuna chochote. Ninaionba sana Wizara ishughulikie jambo hili kwa sababu ni kero na wananchi wamejenga chuki kubwa kati yao na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliahidi kutujengea vituo vya kudhibiti wanyama pori. Iliahidi kutujengea vituo vitatu, kimoja Ngoyoni, kituo cha pili Mahorosha na kituo cha tatu Kikelelwa, hadi sasa ni kituo kimoja tu kimejengwa. Naomba Wizara ifanye jithada za kuhakikisha kwamba vituo vingine viwili vimekamilishwa na ninapenda nimsikie Waziri wakati anafanya majumuisho ili kero hii iishe moja kwa moja kwa wananchi wa Rombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine ambayo ningependa kuizungumza ni uvamizi wa nyani kutoka mlima Kilimanjaro. Kijiografia, Mlima Kilimanjaro wote uko katika Jimbo la Rombo, pamoja na kwamba mlima huu unahudumiwa na Halmashauri zote ambazo zinazunguka ule mlima. Mlima Kilimanjaro ukiungua ni wananchi wa Rombo wanawagwa kwenda kuzima moto mlimani. Wapo waliovunjika, wapo waliokuwa vilema kwa sababu ya kwenda kuzima moto, wanachoambulia ni nusu mkate kwa kila anaekwenda kuzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lucy Owenya amezungumza hapa imefika wakati Mheshimiwa Maghembe, wananchi wa Rombo na Halmashauri zinazozunguka Mlima Kilimanjaro tunataka mrabaha kama wenzetu wa madini wanavyopata. Vinginevyo tumedhamiria safari hii mlima ukiungua hatuzimi, mje mzime wenyewe. Kwa sababu mlima unaingizia TANAPA zaidi ya shilingi bilioni 60 kwa mwaka, lakini hakuna ambacho Halmashauri hizi hususan watu wangu wa Rombo wanakipata zaidi ya vilema ambavyo vinatokana na maporomoko wakati wanaenda kuzima moto mlimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kama vile haitoshi mlikuwa mmetupa *half mile* kwa ajili ya akina mama kwenda kukata kuni pamoja na majani mkijua kabisa kwamba Jimbo la Rombo ardhı yetu ni ndogo na kwa sababu hiyo hatuna maeneo ya kuswaga wanyama wetu, wanyama wetu tunawaweka ndani.

Kwa hiyo, eneo lile mlitupa, tulikuwa tunapata majani pamoja na kuni, sasa taabu tunayoipata ni kwamba wananchi ambao wanaishi karibu na eneo hili, vijiji vya Masho, Maharo, Mokara, Ubaa, Mashuba, Kirwa, Katangara, Lesoroma wanapata shida mbili; shida ya kwanza ni kwamba kila wanapolima nyani wanatoka mlimani wanakula mahindi yao yote na mwaka huu wameshindwa kulima kwasababu ya shida ya nyani, KINAPA hawataki kutuwezesha ili kupambana na wale nyani. Shida ya pili ni akina mama ambao wanakwenda kwenye ile *half mile* kwa ajili ya majani na kuni kinachowapata ni

kwamba wanatandikwa viboko, wengine wanabakwa, wengine wananyang'anya vifaa vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme mwaka jana askari wa KINAPA waliwakamata akina mama wafuatao, Ndugu Selfina Mtengesi Luka wa Kitongoji cha Mori, Ndugu Fabiola Joseph, Ndugu Rose Luka, Ndugu Witness John, Ndugu Rafia Makongoro wa Kitongoji cha Kimongoni, wakawalaza chini na kuwatandika viboko. Ninaimbilia Serikali tabia hii ya askari wenu kupiga wananchi hovyo hovyo, mnawakomaza na mnaleta matatizo katika nchi kwa sababu itafika mahali watasema hapana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba wakati wa kufanya mjumuisho aibu hii ambayo imetokea Rombo ya akina mama ambao hawajawahi hata kupigwa na waume zao wanaambiwa walale chini, watandikwe viboko vya makalio katika Serikali hii ambayo tunasema ni Serikali yenye amani na utulivu, uniambie ni hatua gani zitakazochukuliwa, kwa sababu ikiendelea hivi itafika mahali sisi tutasema hapana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiondoka kwenye masuala yanyohusu Jimbo langu, ni kwamba tunazungumza habari ya utalii lakini kuna mambo mengi sana katika nchi yetu ambayo tungeweza tukayatumia yakatuletea uchumi mzuri tu. Kamati ya Bajeti chini ya Mheshimiwa Chenge mwaka jana nakumbuka tulienda Dubai kwa ajili ya semina wakatucheka, wakatuambia mnahangaika na vitu chungu nzima, utalii peke yake ungefanya Tanzania ikawa kitu cha ajabu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza habari ya Serengeti, habari ya Mlima Kilimanjaro na kadhalika, mbona kuna vitu vingi vinapotea? Mimi nashangaa watu wanakuja kutalii Bungeni hapa, nashangaa. Kila Halmashauri TANAPA ingeweza ikaamua kujenga makumbusho katika kila Halmashauri watu wakaenda kujifunza habari ya vita ya Maji Maji, watu wakaenda kujifunza kwa mfano pale Kilwa pana handaki linakwenda mpaka Mombasa, linafukiwa tu. Pale Rombo kuna Kata inaitwa Keni, kuna handaki Machifu walichimba zamani linatoka Keni linaenda mpaka Wilayani, yanafukiwa tu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa walivyotumia wazee wetu akina Mirambo, akina Mkwawa, akina Mangi Mareale, vinapotea mnaona tu, hakuna mtu anayejali ajenge makumbusho avihifadhi viweze...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba niseme mambo machache na ninaomba Mheshimiwa Waziri unisikilize kwa makini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza mwaka jana kuna vijana wamepotea katika Jimbo langu la Serengeti, walikamatwa porini vijana zaidi ya 20, mpaka leo ninavyoongea ndugu zao wamewatafuta hawajulikani waliko. Inasemekana wameuawa na askari wa wanyama pori, unapokuja hapa niambie wako wapi? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Mheshimiwa Waziri unakumbuka walikuja hapa Wajumbe wa WMA mwaka huu, walikuja Madiwani, walikuja Wenyeviti wa Serikali za Vijiji, walikuja na baadhi ya watendaji kwa ajili ya tatizo la *single entry!* Sasa tulikutana na wewe ukasema Kamati imekataa. Inawezekana Kamati imeamua, imechukua maamuzi haya kwa sababu haijafika Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mapori ya akiba ya Ikorongo na Grumet Game Reserve pamoja na WMA ya Ikona, jiografia ya kwake ni tofauti kabisa na WMA ambazo ziko maeneo mengine.

Mimi ninakuomba Mheshimiwa Waziri tusaidiane wote na Kamati iende ikakutane na Wajumbe wa Ikona WMA, otherwise you want to kill WMA! Na WMA ikifa pale maana yake mapori ya akiba yale yote yataangamia. Maana kama yataangamia maana yake hakuna ajira. Vijana wataanza kuwinda, no conservation will proceed there. Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri fanya juu chini, Kamati yako itembelee Serengeti ili ikajiridhishe nini kilio cha watu wa pale Serengeti, lakini kama mkikaa hapa mezani mkaamua, kule mtua yale mapori na hakuna kitakachoendelea. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, Serengeti National Park imeanzishwa kwa mujibu wa sheria na imekuwa Gazzeted kwenye Gazeti la Serikali tangu mwaka 1968 kwenye GN Na. 235; ukisoma ile GN iko clear, inataja mipaka ya Hifadhi ya Serengeti National Park. Kilichotokea Wizara yako imeendelea ku-extend mipaka kila kunapoitwa leo. Tangu GN itangazwe wame-extend mipaka zaidi ya mitano, wamechukua maeneo ya wananchi. Sasa sielewi nini maana ya GN? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama GN imetangaza mipaka, leo Wizara yako ina-violate, inachukua maeneo ya wananchi na bahati nzuri beacon zilipo zote tunazifahamu sisi watu wa Serengeti na Mheshimiwa Waziri ukitaka tutakuonesha. Naomba kitu kimoja, unapokuja naomba uniambie uko tayari wewe na Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Lukuvi, kwenda kuhakiki mipaka ambayo

ilitangazwa kwenye GN mwaka 1968? Ninataka hayo majibu wakati unapokuja kujumuisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni tembo na simba. Nimepiga kelele sana kwenye maswali na imefikia sehemu ninaitwa tembo. Iko hivi, hakuna watu wanaopata shida kama wananchi wa Serengeti dhidi ya tembo na simba. Tembo siku hizi anatembea tu kama binadamu wa kawaida, mnagongana naye kama binadamu wa kawaida, hakuna mtu anayechukua hatua dhidi ya tembo na simba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja simba wamevamia kijiji cha Park Nyigoti, sasa wananchi siku hizi walishaelewa ili askari waje hawasemi simba amekamata mnyama, wanapiga simu wanasema tumeuwa simba hapa, dakika tano haziishi wameshafika. Kwa hiyo maana yake ni nini! Tembo, simba ni wa thamani kuliko binadamu. (Kicheko)

Sasa Mheshimiwa Waziri nataka pia unapokuja hapa utuambie katika Sheria ya Wanyamapori mko tayari ku-review, kuileta hapa Bungeni tuipitie upya vile viwango vya kifuta machozi na kifuta jasho? Maana tunajua hamtoi fidia. Mnatoa kifuta machozi na kifuta jasho ambavyo kimsingi haviendani na wakati tulionao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tembo wamekula mashamba ekari tano unampa mtu shilingi 100,000 *for what?* Shilingi 100,000 kwa eka tano shilingi 100,000 inatosha hata kwa mbegu? Mtu akiuawa mnampa shilingi 1,000,000 hata hiyo shilingi 1,000,000 ataomba miaka 10 ndiyo mnampa. Wewe ni shahidi unafahamu, hamjawahi kulipa. Pale Serengeti watu wameuawa wengi sana na tembo, sijawahi kuona mtu amelipwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimeona wameleta wanalipa laki moja moja kwa baadhi ya watu, wengine wote walioathirika hakuna.

Sasa naomba unapokuja ku-wind up uniambie ni lini utaleta ile sheria tuipitie, kifuta machozi, kifuta jasho ili kiendane na wakati tulionao? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu barabara. Mimi sijawahi kuona, ninasikia sijatembea sana, lakini nasikia kuna Mbuga inaitwa Kruger iko Afrika ya Kusini, ukitembea kwenye ile mbuga na wanasema ndiyo mbuga inayoingiza watalii wengi na ndiyo mbuga inaingiza mapato mengi, lakini ukienda kwenye mbuga ile kuna lami. Wale ambaao mmefika mtakuwa mashahidi, lakini kwenye Mbuga yetu ya Serengeti, hiyo hakuna! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Serengeti ukianzia Tarime, watalii wengi wanatokea Tarime, Sirari. Barabara ile watalii wanalamika kila leo ingawa ninyi

mnapuuza lakini watalii wanalamika. Wanahitaji kutembelea Serengeti, lakini kutokana na barabara mbovu zilizopo wanaogopa.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, ghamama ambayo mnaitumia kila siku ku-maintain barabara za hifadhini ni afadhali mngeangalia zile barabara za msingi, zile ambazo zinatumwa na magari mkaziwekea lami, hizo nyingine za kawaida kwa sababu hazina magari mazito, mnaweza kuzi-maintain kwa kutumia kifusi na kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ukija kwenye Mbuga ya Wanyama ya Serengeti National Park kuna hoteli lukuki, zaidi ya hoteli 100 ziko mle. Kuna camp nyingi lakini hayalipi service levy wamekimbia mahakamani yet Serikali mko hapa, hamzisaidii Halmashauri zetu kupata mapato! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapochukulia Halmashauri kama Wilaya ya Serengeti kwa muda mrefu hatunufaiki na utalii. Inafikia sehemu watu wanakata tamaa. Sasa hakuna wananchi wenye nidhamu kama wananchi wa Serengeti kwenye conservation. Huwa wanakuja pundamilia (zebra), tunawarudisha, tunawapigia simu wanakuja wanawachukua. Wananchi wana nidhamu kweli, lakini itafikia sehemu tutachoka. Hebu tusaidie Mheshimiwa Maghembe tupate service levy! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, mkatunyang'anya na bed fee, gate fee unajua ya kwamba Serengeti mizigo tunayoipata, vitu vya madukani tunavyovipata tunatoa Arusha, lakini mnawa-charge wafanyabiashara wa Serengeti kwenye mageti ya Ikomma Gate, wapi huko kwenda Ngorongoro wanachajiwa (charge) ghamama kubwa! Vitu Serengeti ni bei ya juu kweli kweli. Mfuko wa saruji ninavyoongea sasa hivi ni shilingi 23,000 nadhani ndio inaongoza... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Chacha. Mheshimiwa Kuchauka, ajiandae Mheshimiwa Mipata na Mheshimiwa Bashe ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii ya Maliasili. Wizara ya Maliasili ni Wizara ambayo nilikuwa naisubiri kwa hamu sana kwa sababu asilimia 60 ya Wilaya ya Liwale ni Mbuga ya Selous. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina wasiwasi na weledi, ufahamu na nia ya Mheshimiwa Waziri. Tunalo tatizo kama Watanzania, tunazo fursa nyingi sana Watanzania, lakini maisha yetu fursa hizi hazijawahi kutusaidia. Hivi najaribu kujiuliza nini tatizo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufahamu wangu mdogo tatizo la Watanzania ni kwamba tumepeoteza uzalendo wa nchi yetu, tumetawaliwa na ubinafsi. Hii ndiyo sababu kubwa inayotufanya tushindwe kufikia malengo yetu pamoja na kuwa na rasilimali za kutosha katika nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye vivutio vya utalii hasa malikale. Hapa tunalo tatizo la Watanzania kupoteza historia ya nchi yetu. Tunashindwa kutambua vivutio vilivyopo kwenye nchi yetu ni kwa sababu watu tumepeoteza historia ya nchi yetu, hatujui historia ya nchi yetu, tumepeoteza hata jiografia ya nchi yetu. Natoa wito kwa Waziri wa Elimu aimarishe somo la historia na jiografia pengine vizazi vijavyo vitawenza kukumbuka haya ninayoyasema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuisahau Liwale kama utaikumbuka vita ya Majimaji. Lipo boma pale la Mjerumani linaitwa Boma la Mdachi, boma lile pale mpaka leo ziko picha za wahanga wa vita ya Majimaji, ziko sanamu za wahanga wa vita ya Majimaji. Nani analikumbuka Boma la Liwale leo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Liwale tunao mlima ule tunauita Mlima Lukundi, uko Lilombe, mlima ambaa ulikuwa na volcano iliyolala, nani anaijua hii? Tumepeoteza historia. Naomba turudi kwenye historia, tutawenza tu kuzikumbuka hizi rasilimali zetu kama tutakwenda na historia ya nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hifadhi ya Selous, asilimia 60 ya Wilaya ya Liwale imezungukwa na Mbuga ya Selous katika vijiji vya Mpigamiti, Barikiwa, Ndapata, Kimambi na Tukuyungu, lakini kuwepo kwetu Selous hakujatusaidia chochote. Nimezunguka katika vijiji hivi nilivivotaja hatuna alama yoyote kuonesha kwamba sisi tuko karibu na Selous. Hatuna hoteli, hatuna barabara, hatuna miundombinu yoyote wala hatuna kiwanja cha ndege. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie kwa Kusini nzima kwa upande wa utalii tumeiacha nyuma. Lindi hakuna hoteli, Mtwara hakuna hoteli. Mtwara ndiko kuna uwanja wa ndege, lakini siyo ule wa Kimataifa kama ambavyo viwanja vingine viro. Sasa tunategemea ile rasilimali ya Kusini, ule utalii wa Kusini ni nani atakuja kuukumbuka? Kama Mjerumani anaijua Kusini kwa nini Watanzania tusijue? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji wa Liwale kuna kumbukumbu ya Mikukuyumbu, pale ndipo ambapo mmisionari wa kwanza kuja Pwani ya Afrika Mashariki waliuwawa pale. Mpaka leo Wafaransa wanakuja Liwale, wanakuja Mikukuyumbu kuzuru pale, lakini Watanzania hatuna habari hiyo, tumepeoteza historia yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu askari wa wanyamapor, mimi nina wasiwasi na askari wa wanyamapor, aidha kwa sababu ya kutokutunzwa vizuri wanafanya haya mambo makusudi kuwachonganisha Serikali na wananchi. Kwa sababu vitendo wanavyovifanya askari wa wanyamapor havilingani na ubinadamu. Mimi nasema hivyo kwa ushahidi, ninayo picha hapa, huyu ni Mwenyekiti wa Kitongoji wa Kijiji cha Kichonda, hana mkono wa kulia, amekatwa mkono mnamo tarehe 08 Septemba, 2015 tukiwa kwenye kampeni na kesi yake imefutwa tarehe 08 Februari, 2016. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi hii kisa chake ni nini, huyu amekatwa mkono akiwa nyumbani kwake. Askari wa wanyamapor wametoka porini wamemfukuza mtu na pikipiki wamesema ameingia pale kijiji wanataka kwenda ku-search. Wanakivamia kile kijiji kufanya searching nyumba kwa nyumba. Mwenyekiti wa Kitongoji akatoka akawauliza, ninyi mmekujaje hapa? Mbona hamna kibali cha polisi? Mbona hamjasindikizwa na polisi? Mbona hamjaja ofisini? Imekuwaje muwaingilie watu? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni kosa lake lililomfanya akose mkono na file la kesi yote ninalo hapa. Hii kesi imefutwa na Wakili wa Serikali. Wakili wa Serikali anasema silaha zile zilikuwa ni zaidi ya moja, kwa hiyo, haijulikani katika zile silaha ni ipi iliyomjeruhi huyu mkono, yule mshtakiwa ameshindwa kumtia hatiani kuona kwamba je, ni bunduki yake au bunduki nyingine? Ndiyo kesi ikafutwa hapo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hawa askari wa wanyamapor wana ajenda ya siri na Serikali yenu, inawezekana hamuwahudumii vizuri, wanafanya mambo kuwachonganisha ndiyo maana watu wengine wote hapa watasema, utampaje adhabu mtu afanye mapenzi na mti ina uhusiano gani? Tunaomba hawa askari waangaliwe. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upande wa TFS. Jamani TFS ni taasisi ya Serikali, lakini hii tuiangalie, hawa TFS kwa jinsi nilivyowaona wao kazi yao ni moja tu, kufanya udalali wa mbao na mali za misitu, hawana kazi nyingine wanayoifanya. Ukiwaliza mna mikakati gani ya kuendeleza misitu, hawajui chochote. Wao kazi yao ni kugonga mbao, kugonga mali za misitu, basi wamemaliza. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala hili la kitanda. Tunaomba hili suala la kitanda mliangalie. Kwa nini Kusini leo hii tumetengeneza vijana wajajiri, wana viwanda vyao vidogo vidogo vya mbao, lakini havina soko. Ukinunua kitii Liwale, ukinunua kitii Kusini huwezi kukisafirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatujui kwamba zile mbao zote wanazotengeneza furniture ni za wizi, maana haiwezekani? Watu wanakwenda mpaka kwenye majumba, kwenye paa. TFS wanafuata mbao kwenye paa zinashushwa. Sasa mbao zimefikaje kule? Hili ni suala ambalo tunatakiwa tuliangalie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mgogoro kwa upande wa Liwale. Mgogoro ule umetengenezwa kati ya Hifadhi ya Selous pamoja na Kijiji cha Kikulyungu, huu mgogoro ni wa muda mrefu sana. Tatizo lake ni kwamba huu mgogoro wakati walikuja kutengeneza barabara wakasema tutengeneze barabara ili tuweze kufanya patrol, lakini badala yake leo wanasema ule ndiyo mpaka wa Selous. Hata GN hawana, lakini ukienda kuwaliza hakuna wanachofanya zaidi ya kupiga watu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuambie hiki Kijiji cha Kikulyungu leo askari hakuna anayekanyaga, hivi vijiji nimevitaja hapo zaidi ya vitano, ina maana vijiji vyote hivi vikifunga njia Selous askari wa wanyamapori hawaingii. Tutafikia huko iwapo huu mgogoro hautaweza kutatuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi sasa kwenye wanyamapori, tembo, simba pamoja na nguruwe. Kule kwetu ukisikia njaa Liwale imeletwa na nguruwe, ukisikia njaa Liwale imeletwa na tembo, simba kule Liwale ni kama mbwa au kama paka wako wengi sana, tunaomba mje mtusaidie. Tunapokwenda pale kituoni kuomba msaada tunapovamiwa na simba wanatuambia usafiri hawana. Hawana askari wakutosha, watu wetu wanateseka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kabla sijaja Bungeni nilikwenda kwa Mhifadhi wa Kanda anaitwa Salum, nikamwambia Salum kinachokubakiza hapa ni uvumilivu tu wa hawa watu, siku watakapokataa huna kazi hapa. Haiwezekani watu wanauwawa, haiwezekani watu mazao yao yanaliwa wewe unakuja hapa unaleta nahau. Nikamwambia Salum tafadhali, siku nitakayokuja kusema nimechoka, huna salama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mtusaidie, Mikoa ya Kusini mtuwekee hata Chuo kimoja cha Misitu. (Makofi)

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi. Niungane na wenzangu kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri na naiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo kadhaa ya kuchangia, kwanza ni migogoro ya vijiji vinavyozunguka kando kando ya hifadhi. Nkasi tuna Hifadhi ya Rwamfi Game Reserve, hifadhi hii ilikuwa mali ya Halmashauri, Halmashauri

waliamu baada ya kuzidiwa kwamba hawawezi kuitunza wakaipa Serikali, lakini kulikuwa na vijiji kadhaa ambavyo vina migogoro na mipaka ambavyo ni Kasapa, King'ombe, Mlambo, Mundwe, Namasi, Kata, China na Mlalambo. Vijiji hivi vinaambiwa kwamba viko ndani ya hifadhi, lakini vimekuwepo kabla hata ya hifadhi. Tunaomba sheria ziangaliwe upya ili waweze kurekebishiwa mipaka wapate maeneo mazuri ya kulima kwa sababu watu wameongezeka na kwa uhakika wanahitaji namna ya kuendeleza maisha yao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka kuzungumza ni suala la uhifadhi, namna ya kuendeleza maeneo ya utalii. Ninyi wenzetu mnaangalia huku tu, jaribuni kuangalia katika mikoa ya pembezoni na Rukwa ni mojawapo. Ukienda kwenye Ziwa Tanganyika kuna ufukwe mzuri sana, ufukwe ambaao ni wa ajabu, una kingo za aina aina, mawe yaliyojipanga vizuri, visiwa vizuri lakini hakuna watu wanaowekeza. Nimeona tu kampuni moja kule Kipili kwa Mheshimiwa Keissy ndiyo amewekeza kutoka Arusha, lakini ni maeneo mazuri sana na hayatangaziki kwa sababu Wizara hamfanyi hivyo, barabara zenyewe zinazoteremka katika maeneo haya hazitoi hata motisha kwa mtu kwenda kufika. Kwa hiyo, mtusaidie kuangalia maeneo haya yakitumiwa vizuri yanaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu Namanyere kuna eneo linatoa maji moto linaweza likatumika vizuri kwa utalii. Ukienda njia ya Wampembe kuna mahali kuna maporomoko mazuri sana, Halmashauri wameweza kutembelea pale. Ukienda Jimbo la Kalambo kwa Mheshimiwa Kandege kuna eneo linaitwa *Kalambo falls*, yale maporomoko ni mazuri sana. Wenzetu wa Zambia wamekuwa aggressive wamejenga barabara nzuri wamefika pale wanafikia kirahisi, mwisho watu wanaamini labda *Kalambo falls* iko Zambia lakini sisi tumeshindwa kujenga barabara tu kusongeza pale na kuweza kuitangaza vizuri. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo ngome ya Bismark pale Kasanga bado haijatangazwa vizuri na mambo mengine mengi tunaweza tukayaangalia kwa upya, vilevile lugha yetu ya Kiswahili, humu Bungeni tunaiharibu lugha, tungezungumza vizuri lugha ya Kiswahili ingekuwa kivutio duniani hapa na Bunge lingetoa nafasi ya kuitangaza vizuri zaidi. Tukija humu sasa tunavuruga vuruga tunazungumza Kiswahili siyo Kiswahili tunachanganya na Kingereza basi tunakuwa tunaharibu, bado tungekuwa na utalii mzuri tu katika hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Utalii lazima iwe dhana pana iangaliwe katika mitazamo mbalimbali, wakati Halmashauri tunajenga miradi mbalimbali tuangalie maeneo ambayo tunayapa vipaumbele. Tuwe na timu ambayo inashauri hata uwekezaji binafsi kwa mfano, kule Nkasi, Kipili, kuna watu wenyewe wanaamu kujenga nyumba za wageni. Je, mnachukua

initiative zozote kuwashauri ili wajenge waje na kitu kinachofanana na jengo ambalo mtalii anaweza kufikia?(Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wantumia mitaji sawasawa tu inalingana na mataji wowote ambao mtu anaweza akajenga lakini wanakosa utaalam na ushauri wa kitaalam ambao uwekezaji ule ungeweza kufanywa na mtu binafsi lakini ukaleta vivutio au mahali pa kulaza kwa watu ambao wanatutembelea katika maeneo hayo. Kadhalika katika miradi mingine yOyote tungekuwa na dhana pana katika suala zima la utalii, tusiangularie katika eneo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la tatu na la mwisho ni huu mogogoro ambao ninaita mgogoro lazima tusiukwepe, mgogoro baina ya wahifadhi, wafugaji na wakulima. Mgogoro huu watu wengi wanauzungumza na tunauzungumza hapa katika mitazamo miwili, mitazamo yote iko sahihi. Kuna wanaosema wafugaji wanafanya makosa, wanatuharibia sijui ardhi, wengine wanaosema maliasili wanafanya makosa. Serikali lazima myapokee haya, sisi tumechaguliwa na wakulima, wapo waliochaguliwa na wafugaji, lakini haya yote matatizo tumeona athari zake kutokana na Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata ripoti hapa, tumeangalia madhara ambayo huwezi kuyavumilia. Sasa kama Serikali na jambo hili lazima lije hapa Bungeni lipatiwe muafaka, hiki chombo hakiwezi kukwepa kulizungumza hili jambo, lazima liishe na tuzungumze hapa na msikwepe wajibu, watu wetu wana kufa, watu wetu wanaumia. Vilevile mazingira yanaharibika, mito sasa haitiririshi maji kwa sababu ya ufugaji wa hovyo, kwa nini msije na suluhisho mbona mambo mengine mnasuluhisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii naiamini kwa kujenga mikakati ambayo imeshindikana, kwa mfano nimeona katika Serikali hii tumeanza kukusanya mapato mengi kitu ambacho kilikuwa ni tatizo kubwa sana, katika Serikali hii nimeona ufisadi unaanza kupungua, nidhamu kazini imeanza kurejea hili litawashinda. Kaeni muone namna mtakavyoweza kuja na mawazo ambayo yatatusaidia kuondoa tatizo hili. Haiwezekani tatizo likawa linaumiza watu wetu, linaumiza wafugaji, linaumiza wakulima na Serikali isije na suluhisho, mimi siamini katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushindwa kutoa suluhisho katika hili ni kushindwa kutekeleza wajibu wako Mheshimiwa Waziri, ninasema wazi kwamba ni lazima ukae na Wizara zilizo na mahusiano na Wizara yako ili jambo hili ambalo limekuwa kero kwa watu wote liweze kupatia suluhu, hatuwezi kuendelea katika mazingira hayo. Lazima mje na utaratibu, ndugu zangu ni kweli kule Rukwa tulianzisha Azimio la Mto Wisa, tunamkumbuka Mkoo wetu wa Mkoo alikuwa anaitwa Jaka Mwambi, namkumbuka mpaka leo. Mkoo wa Mkoo aliweza ku-manage kuweka wakulima na wafugaji wakakaa pamoja bila

ugomvi wowote na wakahitajiana wote, kilichotakiwa kufanyika ni wale wafugaji waliokuwa wanafuga bila kuelewa wafanye nini mifugo yao, wakapata elimu wakaanza kuwekeza, kusomesha watoto, kujenga nyumba nzuri, kuwekeza katika maeneo mbalimbali na hivyo kuvuna mifugo ile ambayo ilikuwa inazidi.

Kwa hiyo, bado hilo linaweza likafanyika, baada ya kuondoka yule Mkuu wa Mkoa, mifugo imefurika kule Rukwa, Mheshimiwa Keissy hapa alizungumza vizuri sana, imezidi uwezo wa ardhi yetu kubeba, lakini kama Serikali wala hatujaona tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili tumeliona tangu wakati wa enzi ya Serikali ya Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne tulilizungumza sana na kwa wakati fulani nilisikia Rais anasema lazima litafutiwe ufumbuzi. Awamu hii ya Tano kama tutakosa kupata ufumbuzi tutashindwa kuelewa na wananchi watakimbilia wapi? Wataendelea kuuawa? Mtaendelea kuridhika tu watu wanauawa? Kama kweli utakuwa unaendesha Wizara na watu wanazidi kuuawa na hatua zozote hazijachukuliwa sioni kama ni vizuri. Ni vizuri hata kusema nimeshindwa ukaondoka kwenye nafasi, kwa sababu haiwezekani kabisa watu wanauawa tukatoa, lazima tutoe suluhisho na nafasi hiyo lazima ukae ujenge hoja ya msingi, wewe ndiyo sasa tumekupa dawati la mbele la kusuluhsisha hili. Wizara yako na wengine wote Serikalini lazima mliangalie hili hatuna namna ya kufanya, hatuwezi kumwambia mkulima ndiye aje hapa aseme, hapana ni lazima tuseme na chombo cha kusemea ni sisi hapa. Hatuwezi kukaa katika makundi mawili tunashindana hapana ni kukaa mezani na kutafuta suluhu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, naomba suala hili liwe na mwisho wake inawezekana mkiamua, kama hamjaamua haiwezekani. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Bashe, ajiandae Mheshimiwa Dau.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema jambo moja, tulipopata Uhuru mwaka 1961 tulisema na tuli-declare wazi kwamba nchi yetu ni nchi ya wafanyakazi na wakulima. Hii ndiyo ilikuwa kauli na ndiyo iliyotengeneza direction ya nchi yetu, wafanyakazi wakawa na vyama vya wafanyakazi, wakulima wakawa na ushirika na Serikali ikaweka nguvu katika kutunga sheria, kutengeneza sera ambazo zingeweza kuwajengea mazingira bora wakulima na wafanyakazi wa nchi hii. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 1990 tukafanya *liberalization* tukatambua kundi la tatu katika nchi yetu, kundi la wafanyabiashara tukawapa heshima kubwa na kuwaita wawekezaji, tukawatengenezea sera, tukawatengenezea sheria ili kuwajengea mazingira ya wao kufanya biashara. Mpaka leo kama nchi hatujawahi kuwa na *deliberate move* ya kuweza kuli-accommodate kundi kubwa linaloitwa la wafugaji. Huko nyuma tumekuwa tukisema kwamba nchi hii ni yetu sote, sungura mdogo tutagawana wote. Nataka niseme leo, Mwalimu Nyerere aliwahi kuongea mwaka 1975 na wafanyakazi, akiwaambia wafanyakazi utii ukizidi unakuwa uoga, na siku zote uoga huzaa unafiki na unafiki huzaa kujipendekeza na hivyo kuzaa mauti. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu aliendelea kuwaambia wafanyakazi, kama ninyi watumishi wa umma kwa wingi wenu mmeshindwa kupiga kura ya kuwaondoa viongozi dhalimu ni bora mfe. Na mimi nasema sisi kama CCM kwa wingi wetu tunashindwa kuishauri Serikali kwa ukweli hatuna sababu ya kubaki kuwa madarakani. Nayasema haya kwa moyo mweupe, nikiwa mwanachama wa chama chetu. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi. Hili ni jukumu letu Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutafuta suluhisho la migogoro ya wakulima na wafugaji na hili siyo jukumu la Waziri peke yake ni jukumu letu sote kama chama na kama Serikali. Hili siyo jukumu la Mheshimiwa Maghembe, hili ni jukumu la Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Kilimo, Waziri wa Ardhi, Waziri wa Katiba na Sheria ili tuweze kutengeneza mazingira bora kwa ajili ya wananchi wetu. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuambie leo hii kaka yangu Mheshimiwa Kakunda yule pale, katika Wilaya ya Sikunge over 70 percent ni hifadhi, hawa wananchi wakulima na wafugaji wanaenda wapi? Mkao wa Tabora Pori la Ipala linaanza Nzega linaenda Uyui, linaenda Tabora Manispaa, linaenda Sikunge, hakuna maeneo. Wakulima wetu na wafugaji wetu wanakwenda wapi? Lazima ufile wakati na ningemuomba Waziri wakati unakuja kufanya *wind up* hapa useme *clearly* kwamba tarehe 15 mfugaji hatotolewa porini bila kumuandalia maeneo. Maana yake mkimtoa porini mnaenda kumchonganisha na ndugu yake mkulima waanze kuumizana, hili ni jambo la kwanza. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndugu zangu, dhambi hii na Bunge liiagize Serikali, Bunge la Oktoba wanapokuja hapa kama Serikali waje wametoa *affirmative action* juu ya tatizo la wafugaji na wakulima. Nataka niwape mfano, mwaka 2006 wafugaji waliondolewa lhefu wakapelekwa tena Mheshimiwa Abdallah Ulega alikuwa DC yule pale, mnampaleka mfugaji eneo la kijiji hamjamwekea miundombinu. Bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Mwigulu

hana fedha ya kuchimba hata mabwawa mawili na tumeipitisha hapa, tunataka kwenda kusaidia matatizo ya wafugaji na wakulima hatuwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuiombe Serikali ije na *affirmative action* na *solution* ya jambo hili ili tuondoke kwenye mgogoro huu iwe ni leo, ni kesho, kwa kizazi cha watoto wetu na wajukuu zetu huko mbele. Inawezekana hatupendi kuyasikia, lakin ndiyo ukweli wa jambo hili. (Makofij)

Mheshimiwa mwenyekiti, jambo la pili, siongelei wafugaji na wakulima tena. Jambo la pili leo maliasili ukitazama takwimu zilizotolewa na *World Travel Tourism Council on Economic Impact in Tanzania* ya mwaka 2015, inasema maliasili yaani utalii ume-create ajira mwaka 2014 watu 1,300,000. Wana-project mwaka 2025 watu watakaokuwa wameajiriwa katika sekta hii *direct or indirect* ni 1.6 million, *growth* ya 2.7 percent. Lakini *investment* lile kapu la uwekezaji kutoka nje na ndani kwa mwaka 2014 uwekezaji uliyofanywa katika sekta ya utalii ni triliioni 1.8. Wana-project mwaka 2025 utakuwa 3.7 amba ni 9.8 growth ya 0.3 percent.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Ally Saleh kaka yangu kaongea mambo ya msingi sana. Tunasema tuangalie *emerging economics* kwa ajili ya uwekezaji, kwa ajili ya *ku-attract* watalii, swali la *kujiuliza ripoti za dunia* zinasema uchumi wa dunia kuna *slow growth*. Nimeisoma hotuba ya Mheshimiwa Profesa, hakuna *plan* iliyo-accommodate kuwepo kwa kushuka kwa uchumi wa dunia kwa 0.0 percent namna gani utaathiri Utalii wetu wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kitabu alichokiandika kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango, anakiri *Southern part and Western part of this country tourism* haiwezi kukua kwa sababu ya *infrastructure* mbovu. Tunafanya nini kama Serikali? Mbali na hapo *hunting* (uwindaji) na Serikali ilipitisha katika Bunge lililopita kuwasaidia *locals* wawekeze katika uwindaji, kati ya vitalu 160 walivyopewa wawindaji, vitalu 50 vimerudishwa Serikalini kwa sababu gharama ya leseni, ushuru ni kubwa mno. *One of expensive destination* duniani ni Tanzania, eneo lingine hata *landing rate* za kutua kwenye viwanja vyetu vya ndege ni kubwa watalii wanatua Kenya ndiyo wanakuja Tanzania. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningiomba Serikali iende ikafanye review upya, itazame upya sekta hii ya utalii kwa kuangalia variables zote za dunia, waje na mpango amba kama watahitaji idhini ya Bunge tuwasaidie, bila ya hivyo *growth* kwenye sekta ya utalii ukiitazama kwa miaka mitano ijayo mpaka kumi ni 2.5 percent peke yake. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbaraka Dau, hayupo, Mheshimiwa Ester Mmasi

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Dau yupo.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo.

**MWENYEKITI:** Haya endelea.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Waziri nianze kwa kuunga mkono hoja yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili suala la utalii ni suala ambalo lipo *interconnected*, tunazungumzia utalii ambaao uko *under utilized*. Utalii ili uwe utalii, utalii ili uweze kufanya kazi sawasawa ni lazima sekta nyingine saidizi ziweze kusukuma twenda sambamba, kwa mfano, suala la miundombinu kuanzia barabara na maeneo mengine ya usafiri, hata huduma za viwanja vya ndege. Matatizo yetu ya usafiri na utalii yanaanza pale *airport* ya Dar es Salaam na Kilimanjaro. Mtalii anakuja anakutana na mazingira ambayo ni very *unfriendly*, hawesi kupata huduma nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtalii anakaa anasubiri wale wanaochukua visa on arrival anakaa masaa matatu, mwininge anakaa kwenye foleni pale *airport* yenyewe, kuna joto, *air condition* hazifanyi kazi anaanza ku-experience matatizo akiwa pale kiwanja cha ndege. Sasa tunapozungumzia kukuza utalii tuangalie na aspect kama hizi tuhakikishe kwamba vituo vyetu vya *airport* na maeneo mengine ambayo watalii wanakuja wanaanza ku-experience mambo mazuri, pamoja na vitanda kule kwenye hoteli zetu ziwe za kutosha na miundombinu mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii dhana ya utalii tumejikita zaidi kuangalia mbuga pamoja na Mlima Kilimanjaro na vivutio kama hivyo. Lakini dhana ya utalii ni pana zaidi ya Mlima wa Kilimanjaro na mbuga. Kwa mfano, mimi natokea kisiwani Mafia, Kisiwa cha Mafia ni kisiwa tajiri sana kwa utalii, lakini mazingira ili uingie Mafia ni magumu kweli kuanzia usafiri kwa maana usafiri wa bahari na usafiri wa ndege. Lakini kubwa zaidi ni namna gani Serikali inatangaza utalii katika maeneo mbalimbali ya vivutio hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafia tuna samaki anaitwa a *whale shark* au kwa jina lingine la Kiswahili anaitwa *Potwe*, samaki huyu ana tabia kama za *dolphin*, ni samaki *friendly* anaweza akaogelea na watalii, hana matatizo. Lakini dunia nzima samaki huyu anapatikana Australia na Mafia tu. Ni wangapi mionganoni mwa Watanzania tunalijua hilo kwa utalii wa ndani peke yake

ikilinganishwa na utalii wa nje? Kwa hiyo tunahitaji kwanza kutangaza na kuwekeza katika miundombinu ili vitu hivi vinapokuwa connected pamoja, basi utalii wetu utasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafia kuna vivutio mbalimbali kama scuba diving, sport fishing na utalii wa kwenda kuangalia papa Potwe, lakini bado Serikali haijatia mkazo kuweza kutusaidia kutangaza utalii huu. Kikubwa zaidi Mheshimiwa Waziri pale kisiwani Mafia hatuna hata Afisa wa Utalii utawezaje kukuza utalii kwenye destination muhimu kama ya Mafia bila ya kuwa na Afisa wa Utalii wa Wilaya? Tumelizungumza hili sana, tumeandika barua lakini mpaka leo hatujapata Afisa wa Utalii.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante muda wako ulikuwa ni dakika tano tu.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi sana kwa Wizara kwa hotuba nzuri sana. Pamoja na mambo mengine, naiomba Wizara iangalie na isaidie wananchi wa Bukombe kwa mambo kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo kubwa la Wilaya ya Bukombe ni la hifadhi ya Kigosi Muyowosi. Nashauri Wizara iwe na mpango wa kuwashirikisha wananchi katika uhifadhi na kuweka mahusiano mazuri kati ya wananchi na wahifadhi

Kwa kuwa eneo kubwa la Wilaya ya Bukombe ni hifadhi, naiomba Wizara na kuishauri iweke Ofisi ya Maliasili Wilayani Bukombe. Kwa sasa wananchi wanafuata huduma Wilayani Kahama ambako ni mbali kwa kilometra 96. Nawatakia kazi njema Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa naomba kuchangia mawazo yangu baada ya kupitia kitabu cha hotuba ya Wizara ya Maliasili na utalii. Nimesikitishwa sana kuona hotuba yenye kurasa zisizopungua 120 kutoelezea vizuri mipango na mikakati ya sekta ya utalii Zanzibar. Sote tunajua contribution ya Zanzibar kwenye sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Wizara yako inajitihada za makusudi katika kuhakikisha utalii wa Zanzibar unainuka na unatambulika zaidi duniani, ila kiukweli wazawa hawafaidiki ipasavyo. Inasikitisha kuona hata mpishi wa hoteli ni foreigner, sitaki kuamini kwamba wazawa hawana elimu ya kutosha ku-operate hoteli na sehemu nyingi za kitalii. Ni kwa nini Wizara isichukue juhudzi za kuboresha mitaala katika vyuo vyetu vya utalii vilivyo ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata maelezo mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wakati wa ku-wind-up nakusudia kushika mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Mchango wangu upo kwenye suala zima la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lushoto kuna vivutio vingi vya kitalii lakini vivutio vile havichangii Pato lolote la Taifa letu kwa sababu utalii ule unafanywa kienyeji. Hivyo basi niombe Serikali ifungue chuo cha kitalii Lushoto ili vijana wetu wapate elimu ya utalii ili wasiendelee kufanya kazi ile kienyeji na kuisababishia Serikali kukosa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishauri Serikali, yale maeneo yote yenye vivutio yatengenezwe ili watu wasiingie kiholela, ikiwezekana kuwe na vizuizi. Niombe Serikali yangu Tukufu iwaangalie hawa watu wanaovuna mti mmoja mmoja, waweze kuchana mbao zao kwa kutumia chainsaw kwani wakulima hawa hawana uwezo wa kununua mashine za kuchana mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo walikuwa wanatumia misumeno ya mikono ambayo hakuna watu wanaoitumia kwa sasa maana walikuwa wanatumia wazee na wazee wengi wameshakufa na waliobaki wamezeeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii pia imepelekea baadhi ya watu ambaa hawana nia nzuri hasa polisi wanawakamata sana watu wanaokata mti kwa chainsaw, na askari hawa wameacha kufanya kazi zao nyingine, kazi yao kusikiliza maeneo yanayolia chainsaw ili wakakamate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la asilimia 20 kumekuwa na tabia ya Maafisa Misitu kuchukua asilimia hizo hata kama mtu anavuna mti wake kwa matumizi yake binafsi. Niombe Serikali yangu iwape Wabunge zile sheria za misitu ili Wabunge tukawaelimishe wakulima wetu wa mti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi yaliyozungukwa na misitu mameneja hawatoi mgao kwa vijiji vilivyozunguka msitu pamoja na vikundi vya kina mama wajane, vijana pamoja na vikundi vya kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu, hasa katika Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mungu amlinde na kumzidishia umri pamoja na kumpa afya nzuri.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri wazozifanya. Aidha, nawapongeza watendaji wa Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya bajeti. Pamoja na pongezi hizi nashauri yafuatayo:-

- (i) Wakati umefika wa kuboresha utalii kwa Mikoa ya Kusini (Mtwara na Lindi) kwa kuwekeza fedha za kutosha kwenye miundombinu itakayowezesha watalii kufika maeneo hayo.
- (ii) Mbuga za wanyama na hifadhi zingine zitangazwe kwa uwiano sawa badala ya kutangaza zile za Arusha na Mara.
- (iii) Wilayani Newala kuna Shimo la Mungu na lina maajabu ya aina yake. Naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri waende wakajionee ili waweze kuchukua hatua ya kuweza kukiendeleza kivutio hiki.
- (iv) Mto Ruvuma una pwani yenyе kilometa 156 ambazo zinatafaa kwa ufugaji wa mamba kwa ajili ya vivutio, tutumie beach hii ipasavyo.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja ilioletwa mbele yetu. Aidha, baada ya kuunga mkono hoja naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine ikiwa ni mara yangu ya nne kuongelea suala zima la maporomoko ya Kalambo pamoja na Hifadhi ya Msitu wa Kalambo kuwa chini ya TANAPA nimekuwa nikileta ombi hili na nitaendelea kurudia nikiamini ipo siku Serikali itanielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maporomoko ya Kalambo yako mpakani mwa nchi ya Tanzania na Zambia. Pamoja na maanguko ya maji kuwa mazuri sana upande wa Tanzania kuliko upande wa Zambia lakini kwa upande wa Zambia wameyatangaza maporomoko haya kwamba ni maporomoko ya pili Afrika baada ya yale ya Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linashindikana kutohaka na uwezo mdogo wa Halmashauri ya Kalambo kwa maana ya uwezo mdogo wa kifedha na weledi katika tasnia ya utalii. Hivi ninavyoongea tembo wanaokadiriwa 17 mpaka 25 wapo ndani ya msitu wa Kalambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara kwa mara nyingine maporomoko ya Kalambo na Msitu wa Hifadhi ya Kalambo viwe chini ya TANAPA ili wahifadhi na kutangaza vivutio hivi vya utalii.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naishauri Serikali, Sheria za Ardhi na Sheria za Uhifadhi, kwa maana ya mipaka inayohusiana na maeneo ya maliasili itazamwe upya kwa lengo la kuondoa migogoro na migongano kati ya wananchi na maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha wataalam wa ardhi, maliasili, kilimo na maji wakutane ili kuisaidia Serikali kumaliza migongano na migogoro ya ardhi kwa kufanya uchambuzi wa kina na hatimaye watoe mapendekezo kwa Serikali ili yaweze kupitiwa na kufanyiwa kazi, bila hivyo migogoro hii haitaondoka au haitakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifugo kuingizwa kwenye hifadhi na hifadhi kufanya malisho halikubaliki. Kuachia jambo hili liendelee litasababisha uharibifu mkubwa wa ardhi, mazingira, kuondoa uoto wa asili kutokana na ng'ombe kukanyaga hovyo. Misitu itakwisha kwani wafugaji ndio wanaokata miti na kuchoma moto kwa lengo la kutaka nyasi ziole upya kwa ajili ya malisho yao, maliasili itatoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la majangili, askari wa wanyamapori waendelee kupatiwa mafunzo na mbinu zitakazowawezesha kukabiliana na majangili. Aidha, vitendea kazi ni lazima vipatikane kwa askari hawa, bila kufanya hivyo kuhimili vishindo vya majangili itakuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuboresha miundombinu itakayowawezesha watalii kutembelea hifadhi kwa urahisi zaidi na kuingizia mapato ya Serikali kwa wingi.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wa Wizara hii nyeti kwa uchumi wa nchi yetu. Kwa kuzingatia unyeti wa Wizara hii naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni Makumbusho ya Taifa, kumekuwa na tatizo la muda mrefu kwa watumishi wa Makumbusho ya Taifa kutopandishwa vyeo. Hali hii inakatisha moyo sana kwa wafanyakazi wengi kuhamia taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya waajiriwa wapya wanapogundua Makumbusho hawatoi vipaumbele kwa wafanyakazi wake wanaamua kuacha kazi. Shirika la Makumbusho ya Taifa ni muhimu katika kuhifadhi mambo yanayoshamiriwa na jamii na ambayo yanapotea kwa kasi sana, lakini Wizara haiipi kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imetegemea zaidi kwa wanyamapori na tangu Waziri na Katibu Mkuu wateuliwe hakuna aliyefika Makumbusho. Nyumba

za Kijiji cha Makumbusho zinaanguka, hakuna pesa za kukarabati; kama haitoshi Makumbusho ya Posta kumbi mbili zimefungwa, ukumbi wa baiolojia na wa mila na desturi umefungwa kwa zaidi ya mwaka sasa.

Naomba suala hili lifanyiwe kazi na Makumbusho ya Taifa ipewe kipaumbele katika bajeti hii ili kuyapa uhai. Vilevile kuongeza motisha kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kimondo Wilayani Mbozi. Wilaya ya Mbozi Mkoani Songwe kuna kimondo ambacho kilianguka, kimekuwa kikitembelewa na Watanzania kutoka pande zote za nchi yetu na vilevile wasanii kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali iangalie namna nzuri ya kuboresha mazingira ya kile kimondo. Mazingira yale yakiboreshwa na vilevile kimondo kile kikipewa kipaumbele na Wizara katika kutangazwa kitaweza kujulikana Kimataifa na hivyo Taifa litaweza kujiingiza kipato huku wakazi wa Mbozi wakinufaika kiuchumi na kijamii na uwepo wa kivutio hicho katika Wilaya yao na Mkoa wa Songwe kiujumla.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii nikiamini kabisa kuwa kupitishwa kwa Bajeti ya Wizara hii kutaleta changamoto chanya katika kutangaza na kuinua sekta ya utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa sekta ya utalii katika nchi yetu ni mkubwa sana kwa kuwa ni chanzo kikubwa cha uingizaji wa fedha za kigeni kupitia watalii mbalimbali wanaoitembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu limejaaliwa kuwa na vivutio vya utalii kuanzia mbuga za wanyama (*national parks*) na mapori ya akiba (*game reserves*), utalii wa mali kale, fukwe mbalimbali zenyenye mandhari nzuri na zenyenye kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto lukuki hasa katika mapori ya akiba yakiwemo mapori ya akiba ya Kigosi Moyowosi ambavyo kimsingi yanazo changamoto nydingi hasa miundombinu ya barabara za viwanja vya ndege na huduma za hoteli za kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kujenga barabara za kudumu kuyaunganisha mapori yetu haya ya Kigosi na Moyowosi kuanzia Kata ya Iponya, Wilayani Mbogwe kuunganisha na makao makuu ya mapori huko Kifura katika Wilaya ya Kibondo Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ikifunguliwa na ikaimarishwa itasaidia sana shughuli za ulinzi wa wanyama pori kwani doria zitaweza kufanyika kwa urahisi hivyo kudhibiti uwindaji haramu hasa ujangili unaofanywa na waharibifu kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uwepo wa barabara za uhakika katika mapori haya kutasaidia doria zitakazosaidia kuyabaini makundi makubwa ya mifugo yaliyovamia mapori haya na kuharibu ikolojia ya mapori haya mazuri na tegemeo la Taifa katika ukuaji wa sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwepo wa Shirika la Ndege lenye ndege zake za uhakika zenyе kufanya safari zake katika Mataifa mbalimbali duniani kutasaidia kuvitangaza vivutio mbalimbali tulivyonavyo hapa nchini. Hii itaongeza idadi ya watalii wanaotembelea hapa nchini na kuvitembelea vivutio hivi na hivyo kuchangia pakubwa katika Pato la Taifa na pengine kusaidia kuwavutia wageni wawekezaji katika sekta hii kutoka katika mataifa ya nje tajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ni jukumu la Serikali na Bodi ya Utalii nchini kuhakikisha kuwa vivutio hivi vingi tulivyonavyo vinatangazwa duniani kote ili viweze kuwezesha watalii wengi zaidi kuja hapa nchini na kuchangia katika upanuzi wa ukuaji wa uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii kuchangia Bungeni kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili natoa hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu misitu. Nashauri uwepo mkakati kabambe wa kutunza misitu yetu. Itungwe sheria ya kuwabana wananchi waache kukata miti hovyo hovyo. Misitu inakatwa kwa matumizi mbalimbali kama nishati (mkaa), ujenzi na pia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya kata mti panda mti ipo, je, inafuatiliwa? Pia kila Halmashauri kupanda miche ya miti milioni 1.5 kwa mwaka, hivi ni kweli inafuatiliwa sawasawa kuona kuwa miche inayopandwa na ile inayostawi ni asilimia ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu asilimia 90 ya Watanzania wanatumia mkaa kama chanzo cha nishati (utafiti umefanyika). Nashauri kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini uangaliwe mkakati kabambe wa kupunguza kutumia mkaa kama chanzo cha nishati badala yake wananchi watumie nishati mbadala na nafuu. Tusipoangalia nchi yetu itakuwa jangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili vyanzo vya maji vitazidi kuharibika na maji yatakauka. Nashauri uwepo mpango kamili wa kunusuru misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majangili wamezidi kuua wanyama na hasa tembo katika hifadhi zetu na hasa Ruaha, Selous na hata Mikumi. Tembo wanaauawa, kilio cha tembo, tembo wachanga wanabaki yatima. Nashauri waajiriwe askari wa kutosha kusudi waweze kunusuru tatizo hili la majangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Waziri aweke mikakati kabambe ya kukomesha ujangili huu na hasa ujangili wa tembo. Serikali iangalie sana chanzo cha kuua tembo na kuchukua meno ya tembo hasa ni nini na ni akina nani wapo nyuma ya ujangili huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya uongozi wa Awamu ya Tano naomba jambo hili lifanyiwe kazi, atakayebainika yuko nyuma ya biashara hizi achukuliwe hatua kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii uzidi kutiliwa maanani ili nchi yetu ipate mapato zaidi. Nchi kama Israel uchumi wake unaendelea kuwa mzuri kwa sababu ya utalii, na baadhi ya nchi nyingine. Nchi yetu ni nzuri, inavyo vivutio vingi vya utalii kila kanda na kila mkoa. Ni kwa nini vivutio vya nchi yetu havitangazwi na hasa Kanda ya Kusini, Kanda ya Mashariki na Kanda ya Ziwa? Vyanzo vizidi kutangazwa kama utalii wa Kaskazini unavyotangazwa. Namna hii tutaweza kupata watalii wengi katika nchi yetu na pato la nchi kuititia utalii litazidi kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahotelii katika hifadhi zetu za wanyama zingine hazifanyi kazi, zimeachwa tu. Mheshimiwa Waziri kuna hoteli ambayo ilikuwa nzuri sana kwa muonekano na kwa huduma kwa watalii wa ndani na nje katika Hifadhi ya Wanyama Mikumi, lakini imeachwa kama gofu ndani ya hifadhi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri anieleze kuna mkakati gani wa kufufua na kuendeleza hoteli hii ambayo ilikuwa inatoa huduma nzuri kwa watalii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie migogoro inayotokea kati ya wafugaji na wakulima na hasa mifugo kutoka nchi jirani kuingia kwenye misitu inayozunguka Wilaya ya Karagwe. Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Wizara husika zingatieni matumizi bora ya ardhi. Migogoro si mizuri katika maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi. Pia nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kuwa Waziri Mkuu. Nimpongeze Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana na kuwa Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo kwa kunichagua mimi Mattar Ali Salum kuwa Mbunge wao, nawaahidi sitowaangusha.

Kuhusu kukabiliana na uamuzi wa kusababisha migogoro baina ya hifadhi zetu na watu wanaotumia kwa kulima au kufuga ndani ya hifadhi hizo, naiomba Wizara kukata mipaka na kugawa maeneo haya ili wakulima na wafugaji wapewe maeneo yao na kuweza kufanya shughuli bila ya kuingiliana na maeneo ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie upungufu wa watumishi na vitendea kazi ni mojawapo ya tatizo kubwa linalosababisha kuzorotesha kwa maendeleo ya utalii. Naomba Wizara ifanye kila linalowezekana kuongeza wafanyakazi na kuwaongezea uwezo watendaji wa Wizara kwa kuwapa vifaa vyta kazi ili kuweza kukabiliana na ongezeko la utalii. Pia kupata wafanyakazi ambao wanajua utalii kwa kuwa utalii ni moyo wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kupangua kwa watumishi na vifaa vyta kutendea kazi husababisha kushuka kwa idadi ya watalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvunaji wa mkaa unaathiri sana ubora wa misitu. Naomba Serikali kupambana na wavunaji mkaa ili kuondoa na kupunguza matumizi ya mkaa. Naomba Wizara kuendelea kushirikiana na Wizara nyingine juu ya uuzaji na ukataji wa mkaa na kuongeza juhudhi kuhakikisha wananchi wetu wanaacha kuchoma mkaa na kupunguza kwa sana matumizi ya kuni, mkaa na kuanza kutumia matumizi mbadala kama gesi na umeme. Pia Wizara iwashauri wananchi wetu wote kuanza matumizi haya. Naiomba Serikali iwashauri au kuwapa ushauri wananchi wetu kuacha matumizi ya mkaa ili kulinda misitu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ipunguze ghamra za gesi ili wananchi waweze kumiliki matumizi hayo wenywewe. Bei iliyopo hivi sasa ni kubwa sana kiasi kwamba hupelekea wananchi wetu kushindwa kutumia gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara itoe mafunzo makubwa kwa wananchi wa vijiji ili waache ukataji wa miti ya kuchoma mkaa. Pia waache kupika kwa kutumia kuni na mkaa na waweze kutumia gesi. Nashauri Serikali kuongeza idadi ya pesa kwa kuongeza matangazo kwa kuwa sasa matangazo hayatoshi. Utengenezaji wa matangazo ndiyo sababu kubwa ya kukua kwa utalii wa nchi yetu na itazidisha mapato ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutolewa kwa mafunzo maalum kwa watumishi wa sekta ya utalii kutasababisha kupanda hali ya uchumi na pia kutengeneza ubunifu wa maeneo mengine ili kuweza kutumika na sio kubakia na yaliyopo tu. Nashauri Serikali kuongeza maeneo mengine, hii ni mojawapo ya kukuza utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Zanzibar, namshukuru sana Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Jumanne Maghembe, pia naishukuru Wizara ya Utalii Zanzibar kwa kazi nzuri wanazozifanya, na sasa utalii umekua sana, watalii wanaongezeka kuja Zanzibar, na ni watalii wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utunzaji wa misitu na maliasili yetu ni jambo la msingi sana. Kila Mtanzania ana wajibu wa kutunza na kuhifadhi mazingira. Wafugaji wapo ambao wanafuata sheria za nchi za uhifadhi wa mazingira yetu na wapo ambao ni waharibifu wa mazingira. Kuna haja Serikali kusimamia sheria katika kuhakikisha ufugaji hauathiri mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wafugaji ambao hawafulati sheria za uhifadhi wasisababishe wafugaji wote wakaonekana ni adui mkubwa wa hifadhi ya nchi. Lazima pia tuijulize ni kwa nini wapo baadhi wanafuata sheria na wengine wanakiuka sheria? Je, Serikali yetu imetimiza wajibu wake katika kuwasaidia wafugaji wetu? Sheria za nchi zinaangalia vipi hifadhi zetu za mapori zilizotengwa miaka hiyo, idadi ya watu waliokuwepo miaka hiyo na mahitaji yao ya ardhi, ikiwepo mahitaji ya ardhi kwa ajili ya makazi, mahitaji ya ardhi na idadi ya mifugo yetu iliyopo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya kujangalia upya kisheria kuweza kupata ardhi kulingana na mahitaji ili kuepusha mauaji, mapigano na kugombea ardhi katika maeneo mbalimbali. Wafugaji wasibezwe na kuonekana wao ni tatizo kubwa katika kuharibu mazingira. Naomba niulize, je, wafugaji na wakata mkaa nani anaharibu mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwahukumu wafugaji kwa kigezo cha kwamba wao wandharibu mazingira. Tuwatengee maeneo kisheria, tuwamilikishe tuone kama kweli watakiuka utaratibu na wataharibu mazingira. Nakubali wapo wafugaji wanaingilia maeneo ya wakulima na kusababisha uharibifu. Narudia, haiwezi kuwa wafugaji wote wapo hivyo. Isituondoe katika kutetea wafugaji wetu kupatiwa haki zao na wajibu wetu wa kuwapatia mazingira bora ya ufugaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wangu katika Jimbo la Igalula, Kata ya Goweka Miyenze, Intende na Kigwa wanateseka sana na wanateswa na kusumbuliwa sana na askari wa maliasili, wakati mwингine ng'ombe wanakua nje ya reserve sisi tunaita *ujje*, wanaswaga mifugo hiyo na kuiingiza reserve na kuwakamata na kuwatoza fedha nydingi au kutaifisha mifugo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lote la Jimbo la Igalula halina eneo rasmi la wafugaji, lakini kuna mifugo mingi na pia wakulima wapo wengi lakini pia maeneo makubwa ya Jimbo yamo ndani ya hifadhi. Mgogoro wa eneo la kulimia, kufugia na makazi ni tatizo kubwa sana. Tunaomba wakulima wetu wapewe eneo la kufugia na kulimia ili kuondoa tatizo hili. Tulishaomba kumegewa eneo la kilometra nne katika eneo liliolahifadhiwa katika Kata ya Lutende na Miyenze ili wapewe wafugaji na wakulima ili kuondoa adha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwabeze wafugaji wetu, ndiyo wapiga kura wetu, leo tusiwadharau na kuwabeza. Watengenezewe mazingira rafiki ili wasiwe tatizo katika uharibifu wa mazingira. Tuangalie wakata mkaa na mbao kama waharibifu wakubwa wa mazingira na si wafugaji wetu ambao wana haki pia katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wafugaji wangu wa Kata za Lutende, Miyenze, Kigwa na Goweko wapewe maeneo na wamilikishwe ili wapate eneo la kufugia mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kama wafugaji wetu wataheshimiwa na kuthaminiwa na si kuonekana wahalifu na watu wabaya kwa mazingira.

**MHE. WILLIAM T. OLENASHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Naibu wake kwa kuwasilisha hotuba nzuri. Hotuba hii imetoa dira ya sekta katika mwaka ujao kwa ufasaha mkubwa. Kama Mbunge wa Ngorongoro, Jimbo ambalo zaidi ya asilimia 80 ni hifadhi za wanyama pori, naomba kuchangia hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kubadilisha Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (*Ngorongoro Conservation Area Act*), Sheria ya Ngorongoro imepitwa na wakati na ni sheria ya siku nyingi sana, ni sheria ya kikoloni. Sheria hii haiendani na mazingira ya sasa ya uhifadhi na inapingana na sheria za sekta nyingine kama ardhi, barabara, Serikali za Mitaa na kadhalika. Aidha, Sheria hii ya Ngorongoro haiendani na Sheria Kuu ya Uhifadhi (*Framework Legislation*), yaani Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009.

Vilevile sheria hii haitambui dhana ya kushirikisha wananchi katika uhifadhi (*community conservation*), dhana ambayo ni muhimu sana kwenye eno la matumizi mseto ya ardhi (*multiple land use*). Ni rai yangu kwa Wizara ichukue haraka hatua za kurekebisha sheria hii kwa kushirikiana na wadau muhimu hususan wenyeji wanaoishi ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vijiji kunufaika na uwekezaji Ngorongoro, vijiji vilivypo ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro havinufaiki moja kwa moja (*direct benefits*) kutokana na uwekezaji wa kitalii unaofanywa kwenye ardhi zao. Aidha, kwa utaratibu wa sasa wawekezaji hawalazimiki kuingia mkataba na vijiji badala yake wanaingia mkataba na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (*NCAA*). Kwa utaratibu huu ni vigumu wenyeji kupata ajira na fursa zingine zinazopatikana kwa kuingia mikataba na wawekezaji kama ilivyo kwa vijiji vingine Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa Wizara iainishe utaratibu wa kuviwezesha vijiji vya Hifadhi ya Ngorongoro kuweza kushirikishwa katika uwekezaji unaofanywa katika ardhi yao. Wizara iwalazimishe wawekezaji wanaotaka kujenga hoteli na kambi ya kitalii kupata ridhaa ya kimkataba kabla ya kuingia *lease* na mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mgogoro wa Pori tengefu la Loliondo, ningependa vilevile kuchangia kuhusu mgogoro wa muda mrefu uliopo ndani ya pori tengefu la Loliondo (*Loliondo Game Controlled Area*). Mgogoro huu kwa sehemu kubwa umechangiwa na muingiliano wa mamlaka ya usimamizi wa eneo husika kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Serikali za Viji. Wizara ina mamlaka kuhusu rasilimali za wanyamapori lakini vijiji vina mamlaka kuhusu ardhi. Wizara ya Maliasili imetoa kibali cha uwindaji kwa kampuni ya OBC tangu mwaka 1992 bila ridhaa ya vijiji. Mgogoro huu umedumu kwa zaidi ya miaka 20 na hauelekei kuisha bila hatua maalum za kisheria kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii itatekeleza matakwa ya Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009 inayomtaka Waziri kutenganisha mapori tengefu (*Game Controlled Areas*) na ardhi ya vijiji ili kuondoa migogoro isiyokuwa na maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la manyanyaso ya wananchi ndani ya pori tengefu la Loliondo, ningependa kuwasilisha kero inayowakumba wananchi wa Jimbo langu wanaoishi ndani ya pori tengefu la Loliondo. Askari na watendaji wa KDU wamekuwa na tabia ya kuwakamata na kuwanyanyasa wananchi pale wananchi wakikata miti kwa ajili ya ujenzi kwa kisingizio cha kuharibu mazingira. Wananchi wa kabile la kimaasai hawana tabia ya kukata miti hovyo au kuua wanyama na ndiyo maana eneo hilo lina wanyama na mazingira mazuri mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ardhi hii iko chini ya mamlaka za vijiji ambazo hazijakataza utumiaji wa ardhi kwa matumizi ya kujenga nyumba na maboma. Aidha, watendaji hao wamekuwa wakiwasumbua wananchi wasilime kwenye baadhi ya maeneo kwa kisingizio kuwa wanaharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa Wizara iwaonye watendaji wake waache tabia ya kuingilia mamlaka ya Serikali za Vijiji ambazo ndizo zinazohusika na mipango ya matumizi ya ardhi. Serikali za Vijiji kwenye pori tengefu la Loliondo ndilo zenye mamlaka ya matumizi ya ardhi. Ni vizuri Wizara ya Maliasili na Utalii ikishirikiana na Serikali za Mitaa (vijiji) pale inapohitaji kuchukua maamuzi kuhusu matumizi ya ardhi kwani ndizo zenye mamlaka kisheria.

Mheshimiwa Mmwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. LEONIDAS T. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kuchangia juu ya umuhimu wa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro kimekuwa chanzo kikuu cha utalii katika nchi yetu hivyo ni vizuri Serikali ikaamua kwa makusudi kuhakikisha mazingira yanayotunza Mlima Kilimanjaro ni mazuri. Yapo matatizo yafuatayo ambayo ni hatari kwa hifadhi ya mlima:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni tatizo la moto. Mara kwa mara hutokea moto katika Mlima Kilimanjaro, ni vyema Serikali ikadhibiti vyanzo vya moto na tabia zinazosababisha moto. Lakini pia ni vyema Serikali kufuatilia kwa makini juu ya tuhuma za watumishi na baadhi ya wafanyakazi wasio waaminifu kujihusisha na tuhuma za kusababisha moto kwa sababu zao binafsi za kujinufaisha kimaslahi.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, lipo tatizo kubwa la mifugo kuwapo ndani ya hifadhi na kuharibu sana mazingira na uoto wa asili wa Mlima Kilimanjaro ambao husababisha ukosefu wa mvua, pia katika vyanzo vya mito vinavyoanzia kandokando ya Mlima Kilimanjaro.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, lipo pia tatizo kubwa la ukataji wa magogo na upasuaji wa mbao katika misitu inayozunguka Mlima Kilimanjaro. Aidha, ukataji mkubwa wa magogo na upasuaji miti unatokana na matumizi makubwa ya chainsaw ambazo nyingi zilitoka Kenya mara baada ya udhibiti mkubwa wa upasuaji mbao na magogo uliofanywa ndani ya nchi ya Kenya.

Aidha, yapo mahitaji ya badhi ya viwanda vinavyohitaji magogo, mbao na kadhalika na matokeo yake wananchi wa kawaida wanachukua tender ya kusambaza/kutoa magogo na mbao ambayo wanalazimika kuingia katika misitu ya hifadhi. Naishauri Serikali kwa nguvu zinazostahili izue kwa nguvu zoezi hili la ukataji wa magogo na mbao katika maeneo ya Mlima Kilimanjaro ambapo inaharibu na kuuwavyanzo vya mito na chemchemi za maji.

(iv) Mheshikiwa Mwenyekiti, tatizo la kilimo pia ni moja kati ya vyanzo vikubwa vya uharibifu wa mazingira. Bado hatujawa na udhibiti mkubwa wa watu wanaolima na kuharibu mazingira katika vyanzo vya maji na maeneo ya ardhi oevu. Ni vyema Serikali ikajipanga vizuri na kusimamia Sheria za Kilimo zikiwepo zinazozuia kulima katika kingo za mito, vyanzo vya maji, na kadhalika. Sheria ya mita 60 ni muhimu izingatiwe.

(v) Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la nusu maili (*half mile*) ambalo ni buffer zone kwa ajili ya Mlima Kilimanjaro. Dhamira kubwa ya eneo hili la kuwa kinga ya Mlima Kilimanjaro imepotea kwa watu kuvamia eneo hili kwa kilimo, ujenzi na upandaji wa miti usio rafiki na mazingira ya Mlima Kilimanjaro. Ni vyema Serikali ikafanya maamuzi ya makusudi ya kulinda eneo hili kwa ajili ya hifadhi ya Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendelekezo yangu ya jumla:-

- (a) Juhudi za upandaji wa miti katika eneo lote linalozunguka Mlima Kilimanjaro, ni vyema Serikali ifanye juhudi ya hali ya juu ya suala hili.
- (b) Ufanyike udhibiti madhubuti katika kuzuia kilimo holela na hifadhi ya ardhi.
- (c) Udhibiti wa ukataji miti uwe wa kina na kuzisimamia sheria zote.
- (d) Udhibiti wa mifugo inayoingia msituni uwe wa nguvu zaidi na adhabu kali kwa wanaovunja sheria zichukuliwe.
- (e) Uaminifu na uadilifu na kufanya kazi kwa weledi ni muhimu kwa watumishi wa KINAPA na TANAPA kwa ujumla, Serikali ione namna ya kuimarisha na kuhakikisha weledi kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri maalum ni kuwa utalii wa Mlima Kilimanjaro ni muhimu na unakubalika sana duniani, lakini lazima tufikiri zaidi. Wapo ambao wangependa kuupanda Mlima Kilimanjaro, lakini wanashindwa kutohakana na sababu mbalimbali ikiwepo afya ya mtu, umri wa mtu, mapenzi ya kutembea/*interest*, uwezo wa kutembea kwa kupanda mlima kwa siku tano na kadhalika, ili watu wengi waweze kupanda na kuona Mlima Kilimanjaro. Upo uwezekano wa kutengeneza mnara/tower au reli/treni ya juu ya mlima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikaandaa mazingira haya kwa kuweka vitu vitakavyowawezesha watalii wengi wanaovutiwa na Mlima Kilimanjaro kuja kutalii kwa njia nyingine na si ya kuupanda mlima kwa kutembea; njia hii itawezesha kuongeza watalii wengi zaidi ya mara mbili ya watalii wanaokuja kupanda Mlima Kilimanjaro. Uzoefu wa China kutengeneza tower ndefu ungeweza kutumika kujenga tower katika maeneo yanayozunguka Mlima Kilimanjaro na watalii kuja kwenye tower na kutembelea mlima kwa kutumia tower hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Manispaa ya Songea ni kuuingiza Mji wa Songea katika sekta ya utalii ili kuweza kuufanya uwe mji wa utalii. Songea ina vivutio vingi vya utalii ambavyo inabidi viendelezwe na kutangazwa; mambo kama:-

- (i) Vita vya Majimaji, watu/mababu zetu walionyongwa katika mapambano na ukoloni wa Kijerumani.
- (ii) Kumbukumbu za mashujaa na mapambano ya Wajerumani na mababu zetu.
- (iii) Maeneo ya mapango na maporomoko ya maji.
- (iv) Mila na desturi za makabila mbalimbali ya Songea, vyakula, malazi, mavazi, zana za kazi, uwindaji, utunzanji wa chakula, ngoma, tamaduni za malezi bora na kadhalika.
- (v) Michezo ya jadi; mieleka, mashindano ya mila, ngoma za kivita, michezo ya kishujaa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ione uwezekano wa kutuma ujumbe Songea, tutakaokaa nao pamoja ili kupanga na kuchambua mambo yanayoweza kutangazwa na kuanza kazi ya kutangaza utalii wa Songea na kuanzisha utalii katika Mji wa Songea. Aidha, ni vizuri kwa Wizara kwa kushirikiana na Manispaa ya Songea kuanzisha Kituo cha Taarifa za Utalii (*Tourism Information Centre*) ili baada ya kuvibainisha vituo hivyo vya utalii na mambo ya utalii kuwe na kituo cha kupokelea na kutolea taarifa za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa ushirikiano kati ya Serikali Kuu na Manispaa ya Songea tuweze kuvitangaza vivutio hivyo kwa njia mbalimbali. Dhamira kuu ni kukuza utalii na kuupelekeea Mji wa Songea kuwa mji wa utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ya waendesa utalii wa ndani (*local investors*) kuhusu gharama kubwa ya leseni yashughulikiwe. Waendesa utalii wa ndani wanaoomba leseni TALA kwa uwekezaji wa ndani iwe dola za Kimarekani 500 badala ya dola 2,000. Hii itasababisha Serikali kupata mapato zaidi kwa vile mzunguko wa fedha utabaki ndani tofauti na sasa ambapo fedha nyingi zinabaki nje kutokana na kampuni nyingi za kitalii kumilikiwa kwa ubia na wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya waongoza watalii na wapagazi bado ni duni sana, mikataba yao ni mibovu na mazingira yao ya kufanyia kazi ni magumu. Serikali ni vyema isimamie Sheria ya mwaka 2008 iliyotangazwa katika GN mwaka 2008 ambapo pamoja na mambo mengine sheria hiyo itasimamia usajili wa waongoza watalii na kuwapatia leseni; ambapo mapato yataongezeka kwa Serikali kuwa na takwimu za waongoza watalii. Kuwe na waongoza watalii wanaokidhi vigezo na kuongezeka kwa watalii kwa kuwa huduma itakayotolewa itakuwa ina ubora na inakidhi viwango vyta utalii wa ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kukomesha wageni ambaa wanafanya kazi ya kuongoza watalii, Serikali inaelewa kwamba ni kinyume cha sheria kwa wageni kuongoza watalii. Aidha, kumekuwa na volunteers ambaa wanaingia nchini na kuingiza watalii kwa kuwalaza katika malazi bubu, hali hii huchangia kudumaza utendaji wa hoteli zetu katika Mji wa Moshi na Mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa kuboresha njia za kupandia Mlima Kilimanjaro, mfano ni njia ya Machame, ni vyema kukawa na namna bora ya KINAPA kutengeneza tent za kulia (*mess tent*) zinazofanana ili kutunza mazingira kuliko kuacha kila muendesa biashara ya utalii akajenga tent lake la kulia. Hivyo, nashauri njia ya Machame katika camp ya Machame Hut patengenezwe uniformity plan ya kujenga ma-tent yanayofanana na yenye kiwango kizuri kinachovutia kwa ajili ya wageni kupata chakula. Machame Hut iwe kama pilot na njia nyingine zitafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuongeza mapato kwa kuagiza TRA wawe na maafisa wao ambao watacaa kwenye lango la mlima kukagua tax clearance za wenye makampuni ya utalii ili kulinganisha taarifa za usajili wa makampuni hayo na uhalisia wa kodi wanazolipa. Tatizo kubwa lililopo ni kwamba makampuni yanakuwa na leseni lakini yanakuwa ni makampuni ya nje yanayotumia baadhi ya waongoza watalii kujificha katika hicho kivuli chao na hivyo kukwepa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa Mlima Kilimanjaro kwenda sambamba na hali ya uchumi ya wananchi wa Kilimanjaro, hususan wananchi wa Manispaa ya Moshi. Nashauri Serikali kuona jinsi ambavyo itakubali ombi la Manispaa ya Moshi kuwa Jiji kwa vile ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwa wananchi wa Moshi, jambo ambalo liliisababisha Manispaa ya Moshi kuanza mchakato wa kuhamasisha maeneo ya vijiji na kata jirani ili wakubali wazo la Manispaa ya Moshi kupanukia katika maeneo yao. Jambo la kusikitisha baada ya mchakato huo uliotumia fedha za ndani za Halmashauri, Serikali haijaleta majibu mazuri ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa Manispaa ya Moshi kuwa Jiji ni kuinua thamani ya mlima ambapo watalii wataiona Moshi kama Jiji la Mlima Kilimanjaro, hivyo kusaidia kuongeza idadi ya watalii wanaofika Moshi na Kilimanjaro kwa ujumla na hatimaye kuhamasisha watu kuwekeza kwenye miundombinu ya utalii na hivyo kukuza uchumi wa Mkoa wa Kilimanjaro ambao umeanguka kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa ndege wa Moshi ni lazima uboreshwe. Hoja kwamba Kilimanjaro kuna uwanja wa KIA haitendei haki utalii wa Mlima Kilimanjaro ambapo uwanja wa Moshi ungetumika vizuri ungeweza kupokea ndege ndogo kutoka Mbuga za Serengeti na mbuga nyingine za wanyama za Kanda ya Kaskazini. Aidha, uwanja wa ndege wa Moshi unaweza kupokea ndege ndogo moja kwa moja kutoka Kenya, vilevile unaweza kusaidia kupokea helkopta za uokoaji katika Mlima Kilimanjaro kwa wale watalii wanaopata shida za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii wa utamaduni unaweza kufanyika Moshi kwa kujenga Jumba la Makumbusho (Museum) ambalo litatunza historia ya watu wa Mkoa wa Kilimanjaro, hivyo kutumika kama eneo la kuvutia watalii kabla na baada ya kupanda Mlima Kilimanjaro.

Aidha, Msitu wa Rau katika Manispaa ya Moshi unaafaa kutumika kama eneo la kivutio cha watalii kwa vile lina aina za miti ambayo haipatikani maeneo mengi duniani. Hivyo, ni vizuri ikawa kama *recreational centre*.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wote chini ya Katibu Mkuu wa Wizara katika kipindi kifupi wameweza kufanya kazi ya kuwapa matumaini makubwa wananchi, ingawa matatizo ni mengi kwenye sekta ndani ya Wizara hii. Pamoja na yote tunapaswa kuwa na subira ya kujipanga na kuweka miundombinu ya mikakati ya kusafisha matatizo yaliyopo kwa kuyaweka katika kipaumbele ndani ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na hali halisi ya wananchi kuongezeka na ardhi/nchi ipo vilevile ni dhahiri haya mapori ya akiba 28 na mapori tengefu 42 yawezekana yamepotea au kupungukiwa sifa ya kuwa mapori ya akiba au mapori tengefu. Nashauri Serikali kufanya utafiti wa kukagua maeneo hayo na kupata idadi halisi ya uhalisia uliopo sasa na tupatiwe idadi na orodha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu tunaitumia wananchi katika shughuli mbalimbali na kuendelea kupungua kutokana na ukosefu wa nishati mbadala na kusababisha baadhi ya watumishi wa maliasili kuwa wasumbufu kwa wananchi wetu. Mazao ya misitu yamekuwa yanawanufaisha wachache na kukosesha mapato kwa Serikali. Ni vyema tukaweka mkakati wezeshi wa kupunguza usumbufu wa tozo zinazoingiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TANAPA inajitahidi katika kujenga mahusiano mazuri na wananchi wetu, nashauri badala ya makusanyo yote kupelekwa kwenye Mfuko Mkuu, ni vyema wakabakiwa na hata asilimia 30 ili kuboresha shughuli wazifanyazo kwa wananchi wanaozunguka maeneo yao ya huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii una mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa. Mkoa wa Rukwa una vivutio kadhaa, mfano, *Kalambo Falls*. Tunahitaji vivutio vипитишве na kutambuliwa na kufanyiwa matangazo, huku miundombinu ya kufikia kwenye eneo inafanyiwa kazi. Barabara ya kiwango cha lami (Matai – Kisumba – Mpombwe (Kapozwa) – Kalambo Falls) kwani eneo hilo linatumwa zaidi na utalii wa Zambia kuliko Tanzania wenye eneo kubwa linalovutia katika kuyaona maporomoko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kuona umuhimu wa kukuza utalii wa Nyanda za Juu Kusini (Rukwa), kubadilisha mwelekeo wa Mashariki na Kaskazini. Nchi hii pande zote kuna vivutio vya utalii. Naomba Waziri atuthibitishie vivutio vyetu vitatambuliwa lini ili watalii wafike na tuongeze Pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na kuunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nina maombi maalum kama ifuatavyo:-

- (i) Mgao wa madawati ufile Peramiho, kwa kuwa corridor hiyo inafika Muhukuru kutokea Tunduru kuvuka kuelekea Msumbiji;
- (ii) Suala la upatikanaji wa teknolojia maalum kwa kuwezesha uwepo wa system ya vyoo Mlima Kilimanjaro ni muhimu sana kwa sasa;
- (iii) Kwa kuwa sasa Serikali imeamua kukuza utalii kwenye sekta ya hoteli na huduma, ili kukuza ujuzi wahudumu wa sekta hiyo, kuna kila haja Wizara hii na Idara ya Kazi na Ajira zishirikiane kukuza ujuzi na kuondoa tatizo hilo haraka. Ofisi ya Waziri Mkuu imezindua mpango mkakati wa kukuza ajira; na
- (iv) Kwa kuwa kuna malalamiko makubwa ya sekta ya upagazi katika kupandisha mizigo ya utalii Mlima Kilimanjaro, naomba masuala ya viwango vya kazi na ajira vilivyopo kisheria vizingatiwe katika kusimamia sekta hiyo.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu ameijalia nchi hii kuwa na neema na mali nyingi yapasa kumshukuru. Maliasili ya wanyamapori inaingiza faida kubwa ya Pato la Taifa kwa kuvutia watalii wa nchi mbalimbali na Serikali imepata pato la asilimia 25 siyo kidogo. Tunajua kuwa TANAPA inafanya kazi kubwa katika kuchangia pato kubwa katika sekta ya utalii katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wakulima na wafugaji ni lazima Waziri wa Maliasili na Utalii akae na wenzake wa Wizara ya TAMISEMI, Kilimo, Mifugo na Halmashauri ili waende pamoja katika kutatua migogoro hii ili kuleta amani juu kwa wakulima na wafugaji na kuleta suluhisho la kudumu ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kihistoria yaliyomo katika nchi hii yaboreshweli tuzidi kuvutia watalii katika maeneo yetu kama vile Kilwa au kule Zanzibar sehemu ya Chwaka, Tumbe na maeneo mbalimbali ili tuzidi kuukuza utalii na kuzalisha kipato zaidi.

Kuhusu suala la mazingira hususani ukataji wa miti kwa ajili ya kutengeneza mkaa au kukata miti kwa biashara ya mbaobinatali vinatolewa kiholela. Kwa kufanya hivi hii misitu itakwisha na ukame utashamiri katika nchi hii. Kwa hiyo, ni lazima Serikali iwe makini na kile wanachokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huu, naomba kuwasilisha.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuongelea kuhusu Operesheni Tokomeza. Kwa kuwa kulikuwa na Azimio la Bunge kwa wananchi walioathirika na Operesheni Tokomeza ni muhimu sana Serikali ikahakikisha inalipa fidia kwa wakati kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu leseni ya biashara ya Nyara, kuna baadhi ya kampuni zilizopewa leseni hizo na baada ya muda leseni zikafutwa na tayari kampuni hizo zilishakuwa na nyara hizo na baada ya muda wahusika kukamatwa ilhali wakati wanatekeleza jukumu hilo walikuwa na leseni halali. Serikali itueleze kwa nini kumekuwa na mkanganyiko huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Wilaya ya Karatu inapakana na TANAPA (upande mmoja) na Hifadhi ya Ngorongoro (kwa upande mwengine). Wilaya imekuwa haina makubaliano ya kimkataba wa namna gani Wilaya hiyo inafaidika na utalii ili kujenga ujirani mwema. Misaada hiyo imekuwa inatolewa bila ya kuwa na uhakika wa kuipata (hisani). Ni kwa nini mamlaka hizi zisiingie makubaliano rasmi ya kimkataba ili Halmashauri iwe na uhakika kwa mwaka ni miradi ipi, kwa gharama ipi itatekelezwa na mamlaka hizo? Ni muhimu mambo haya yakawekwa wazi ili kujenga ujirani mwema.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa kujikita katika suala moja.

Kwanza, napenda kuanza kwa kuunga mkono hoja katika Wizara hii ngumu, hususani upande majangili namna yanavyoipa wakati mgumu sekta hii ya maliasili na utalii, kitu ambacho kinapelekea kukosekana kwa watalii na ukosefu wa mapato kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania leo tunazungumzia kukua kwa utalii kwa kuwa na watalii milioni mbili, wenzetu South Africa wanazungumzia watalii milioni 12. Hivyo basi, ni kwa Serikali yetu (Wizara) kuhakikisha inaboresha miundombinu ya maeneo yetu ya watalii. Kwa mfano, utalii wa Mlima Kilimanjaro miundombinu ya majitaka siyo mizuri kabisa hususan upande wa vyoo, vyoo ni vichafu. Mbaya zaidi vyoo ambavyo wanatumia wananchi/wafanyakazi wa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ndiyo hivyo hivyo vinatumia na wageni wetu (watalii). Hii si sawa kabisa na ni moja ya sababu ya kufukuza watalii katika chanzo hicho cha Mlima Kilimanjaro. Sote tunafahamu wazungu/wageni ni waungwana na wasafi sana ukilinganisha na Watanzania wa maeneo yale. Hivyo basi, niitake Wizara kuhakikisha inajenga

choo mahsus i kwa wageni wetu (watalii) na siyo kuwachanganya na wenyeji. Usafi ni sehemu ya kutangaza utalii wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhusiana na mjisni aliyepelekwa nchini Ujeruman. Wabunge walio wengi wanahitaji mjisni huyo kurudishwa nchini, mimi naomba nitofautiane nao kidogo katika maana ya kwamba kuna ghamama kubwa sana katika kumtunza, mjisni huyo aendelee kuwepo na kuingiza faida ya nchi. Kwanza ni mkubwa sana, hivyo anahitaji eneo kubwa sana, ni sawa na viwanja vinne vya mpira, lakini pia anahitaji muda wote kuwepo kwenye AC ili asiweze kuharibika/kuoza. Hivyo basi, kuliko kutaka arejeshwe sasa ilhali hatujajipanga, nipende kuishauri Serikali (Wizara) ni bora tuone utaratibu wa kuweza kupata *royalty* (mrahaba). Ni vyema Serikali yetu ya Tanzania ione utaratibu bora wa kuitaka Serikali ya Ujeruman kutupatia gawio linalotokana na utalii wa mjisni huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mchango wangu ni huo. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Profesa Maghembe (Waziri) pamoja na wasaidizi wake wote. Masikitiko yangu makubwa ni juu ya mambo mawili:-

(i) Kutoweka mikakati ya kuendeleza Hifadhi ya Maua ya Kitulo. Hifadhi ya Maua Kitulo ni muhimu sana, lazima uboreshaji wa miundombinu ya utalii ikiwa ni pamoja na barabara za lami kutoka Chimala – Matamba – Kitulo; Mbeya – Kitulo – Makete; Njombe – Makete – Kitulo. Pia kuweka hoteli ya kitalii Matamba na Makete ili kuongeza utalii.

(ii) Ugomvi wa wachunga ng'ombe na Hifadhi ya Taifa. Ni muhimu sana kutambua kuwa haiwezekani ukatenga eneo la kuchunga ng'ombe, unaweza kutenga eneo la kufuga tu. Watu wetu sisi ni wachungaji amba tabia yao kuu ni kufuata malisho. Nchi yetu ni ya kitropiki ina misimu ya hali ya hewa mikuu miwili yaani masika na kiangazi. Wakati wa masika migogoro ni michache kwa kuwa malisho ni mengi, wakati wa kiangazi migogoro ni mingi kwa kuwa wachungaji wataswaga ng'ombe kufuata malisho. Muhimu ni Wizara kuamua kisayansi, haiwezekani kutenga eneo la kuchunga ng'ombe, ni lazima wachungaji wafundishwe kufuga na hili ni muhimu kufanyika kupidia kufufua shamba la mifugo Kitulo.

(iii) Shamba la mifugo Kitulo. Shamba hili likifufuliwa litatumika kama eneo la kutoa mafunzo kwa vitendo juu ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama. Shamba hili lilianzishwa mwaka 1965 na Mwalimu Nyerere pamoja na Mzee Karume, walijua huwezi kutenga eneo la kuchungia ng'ombe, lazima twende

kwenye uchumi wa kufuga ng'ombe wa maziwa na nyama. Ng'ombe wa maziwa wana faida kubwa kwa binadamu kiuchumi na kiafya.

(iv) Sheria ziwekwe na zisimamiwe kwa ukali. Waheshimiwa Wabunge bila shaka baadhi wana ng'ombe wanaoswaga, hivyo hawawezi kuunga mkono hoja hii lakini sheria zisimamiwe kwa ukali. Mfano huruhusiwi kuswaga ng'ombe kutoka Wilaya moja kwenda nyingine bila kibali, sheria hizi zizingatiwe.

(v) *Trespass* kwenye hifadhi. Ni vizuri Wizara ifahamu kuwa watu wanaochunga ng'ombe kwenye buffer zone, baadhi yao ndiyo hubadilika na kuvuna pembe za ndovu. Kwenye hili, Wizara lazima isimamie hifadhi hizi kwa ukali. Nchi jirani ya Kenya, ukipeleka mfugo au binadamu kwenye hifadhi unapigwa risasi na wamefanya hivi kwa sababu ni vigumu kutofautisha jangili na mchunga ng'ombe kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ni muhimu sana kwa Taifa letu, si tu uchumi wa Taifa bali kikolojia. Hifadhi ni msaada mkubwa wa kuhifadhi ikolojia ya mvua. Kama tukiruhusu uvamizi wa hifadhi, nchi yetu itakuwa jangwa. Serikali isimamie sheria kwa ukali, no compromise.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kwa kifupi nichangie hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji miti hovyo ni chanzo kikubwa sana kinachochangia mabadiliko ya hali ya hewa ikiwa ni pamoja na nchi yetu kuelekea kuwa jangwa. Uchomaji wa mikaa hovyo nao pia unachangia sana mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na uharibifu mkubwa sana juu wa vyanzo vya maji kutokana na matumzi mabaya ya ardhi. Kwa nini:-

(a) Halmashauri zetu zinaruhusu wananchi kujenga ndani ya vyanzo vya maji, sheria ifuate mkondo wake.

(b) Uchimbaji wa mchanga na kokoto navyo vinachangia uharibifu wa vyanzo vya maji, sheria ifuate mkondo wake.

(c) Shughuli za kilimo ndani ya vyanzo vya maji nalo ni tatizo kubwa, sheria ifuate mkondo wake.

(d) Shughuli za ufugaji ndani ya vyanzo vya maji zidhibitiwe ili vyanzo vyetu visiendelee kuharibiwa.

(e) Tusiruhusu nchi jirani kuingiza mifugo katika nchi yetu, ni hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono michango ya TANAPA kwa jamii na nawapongeza kwa dhati na niombe taasisi au mawakala wengine wa Serikali kama TANAPA watoe mchango kwa jamii kama TANAPA wanavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya hali ya hewa. Hili ni janga la kidunia, tukiwa kama nchi ambayo ina misitu na maliasili nydingi yafaa tuendelee *ku-maintain* misitu, uoto wa asili, vyanzo vya maji, tusichanganye mifugo na wanyamapori kama ambavyo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakichangia kwamba maeneo ya hifadhi nao wachunge ng'ombe. Napinga vikali jambo hilo, tena nasisitiza sana kuwa sheria itumike ili waamue kupunguza mifugo na wakipunguza mifugo watafuga kwa tija badala ya sasa ng'ombe kibao lakini ukiwatazama ng'ombe hao wana uzito sawa na bata. Ni wazi kuwa ng'ombe huyu hatamsaidia mfugaji, ni kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa kiwanda cha Baraghashi – Sao Hill. Hiki kiwanda kinapata gawio la misitu 60% bado wanapata bei punguzo. Jambo la kusikitisha ni kwamba kiwanda hiki kinazalisha karatasi ngumu, anasema *finishing* anakwenda kufanya Kenya, jambo ambalo sio kweli, anachokifanya huyu mwekezaji ni kukwepa kodi ya Serikali. Nashauri afuatiliwe kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Misitu Tanzania (*TFS*) wafanye kazi yao badala ya kujiingiza kwenye biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja na naomba mchango wangu uingie kwenye *Hansard*.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Tunduru kuna hifadhi kadhaa za misitu ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Selous iliyopo Jimbo la Tunduru Kaskazini pamoja na Hifadhi ya Misitu ya Mwambesi, Muheesi na kadhalika. Mwaka huu tembo wamekuwa wakipita katika hifadhi hizo na kuzagaa katika vijiji mbalimbali kama Mtina, Angalia, Mchesi, Kazamoyo na Kalulu na kuharibu mazao ya wananchi na wanadai malipo ya uharibifu huo wa tembo bila mafanikio. Kumekuwa na malalamiko mengi ya wakulima ambayo hayajafanyiwa kazi na Idara ya Wanyamapori, wanyama hao wanasumbua sana hivyo kuna uhitaji mkubwa wa watumishi wa Idara ya Wanyamapori ili kusaidia kufukuza wanyama hao waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Tunduru Kusini kumekuwa na kero kubwa ya fisi kuua watu. Mpaka sasa watu wawili wameuawa na fisi na watu wawili wameuawa na mamba katika Mto Ruvuma na wawili wamejeruhiwa lakini utaratibu wa kulipwa fidia unachukua muda mrefu. Mpaka sasa wahanga hao hawajalipwa, mbaya zaidi majibu wanayopewa yanawakatisha tamaa. Ni vyema utaratibu wa kuwalipa wahanga hawa wa wanyamaporu ukafanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TFS* inashirikiana na Watendaji wa Vijiji kukata miti/magogo bila kufuata utaratibu wa kisheria na wanashirikiana na wafanyabiashara kukata miti hovyo bila kufuata utaratibu. Kwa mfano, katika Kijiji cha Semeni na Muungano, mfanyabiashara mmoja amekata magogo bila ridhaa ya mikutano mikuu ya vijiji hivyo na hata ushuru wa vijiji hivyo haujalipwa na kuna mgogoro mkubwa unafukuta na wanataka viongozi wa Halmashauri wa Kijiji na Mtendaji kupelekwa mahakamani. Hivyo, *TFS* inamaliza misitu ya Tunduru kwa kuruhusu magogo na mbao kukatwa hovyo bila kufuata utaratibu wa kisheria na sasa wanakata magogo Kijiji cha Machemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya hifadhi za misitu na wakulima. Ni vyema mipaka ya hifadhi hizo ikaangaliwa upya ili kutoa maeneo kwa wakulima kutokana na ongezeko la watu mfano Muhesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa hifadhi na wanyamaporu kutumia nguvu kubwa kuwanyanya watu kwa kuwapiga, kuharibu mazao yao, kuwanyang'anya vitu vyao bila makosa. Ni vyema wakatumia ustaarabu katika kuwaelimisha wakulima badala ya kutumia nguvu. Ni vyema sheria ikatumika zaidi badala ya nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Operesheni Tokomeza. Jambo hili limekuwa mradi wa watu kwani kila mwaka wanaokamatwa ni watu walewale, wanateswa, wanapigwa, wanatoa rushwa ili waachiwe bila kupelekwa mahakamani. Ni vyema basi watuhumiwa wote wapelekwe mahakamani wakachukuliwe hatua badala ya kila mwaka wanakamatwa, wanateswa, wanawekwa ndani, wanatoa rushwa, wanaachiwa bila kuwapeleka mahakamani. Jambo hili linasababisha wananchi kuichukia Serikali yao bila sababu. Inaonekana kuwa umekuwa mradi wa watu fulani badala ya kufuata utaratibu. Ni vyema utaratibu wa kisheria ukafuatwa na haki za binadamu zikazingatiwa zaidi. Hakuna anayependa uharibifu unaofanywa, bila kuwachukulia hatua makundi mengine yanajitokeza, ila wakifungwa watu wataogopa kujishirikisha na biashara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kutenga maeneo ya hifadhi ni vyema elimu na mikutano ikafanyika katika vijiji husika ili kuondoa migongano na migogoro ya kutoelewa manufaa ya misitu. Naamini wananchi wakipewa elimu

migogoro hii itapungua kwa kiasi kikubwa na hifadhi zisaidie vijiji vinavyopakana ili kutoa imani na nguvu ya watu wa maeneo hayo kulinda hifadhi hizo. Hifadhi zikisaidia vijiji jirani vijiji vingine vitahamasika katika kuanzisha hifadhi zao ili kupata manufaa wanayopata wenzao.

**MHE. RICHARD P. MBODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri na watendaji wa Wizara kwa maandalizi na kuwasilisha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Taifa ya Katavi katika Mkoa wa Katavi upande wa Kaskazini inapakana na Kijiji cha Sitalike lakini kwa mujibu wa mipaka sehemu ya kijiji ipo eneo la hifadhi. Hivyo, tunaomba mpaka urudishwe nyuma mpaka ng'ambo ya Mto Katuma kwa kuwa wananchi hapo wanaishi tangu miaka ya 1990.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TANAPA inahitaji kuwa na ujirani mwema yaani tunaomba sehemu ya Mto Katuma iruhusiwe wananchi kuvuna samaki angalau eneo lenye urefu wa kilometa tano ili kuwezesha wananchi kupata vitoweo na pia kuondoa ugomvi. Hivi karibuni vijana watatu walikamatwa eneo la mto na walipigwa sana na kuumizwa ambapo hali zao siyo nzuri. Jambo hili lilipelekea wananchi kutaka kuchukua hatua zinazopelekea kuvunja amani kati ya watumishi na wafugaji. Kwa mantiki hiyo, tunaitaka Serikali itoe tamko la watumishi wa TANAPA kufuata taratibu, kanuni na sheria katika utendaji wao ili kuondoa hali ya kuvunja amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu promosheni ya hifadhi, kwa muda mrefu sana Serikali imekuwa ikitangaza sana baadhi ya hifadhi maarufu na kubwa hapa nchini bila kuhusisha pia hifadhi ambazo zinahitaji kutangazwa sana. Mfano mzuri ndege zetu zinabeba majina ya hifadhi kubwa. Tunahitaji Mbuga ya Katavi kuboreshwa na kutangazwa ili kupata watalii kwa kuwa uwanja wa ndege upo. Vilevile miundombinu na huduma nyingine ziboreshewe zaidi kama zilivyo sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujangili, Serikali imekuwa na juhudu kubwa zaidi kupambana na ujangili lakini uhalifu huo bado unaendelea. Tunahitaji Serikali iboreshe mbini za kukabiliana na wahalifu. Watumishi wa TANAPA wameonekana kuhusika, hivyo utaratibu wa kuwahamisha utumike na kuwafuatilia mienendo yao. Pia Serikali lazima ifuatilie taarifa zinazotolewa na vyombo vingine vya usalama. Vilevile maeneo yanayozunguka Hifadhi za Taifa yawe yanachunguzwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya misitu na pori la akiba. Nchi yetu imekuwa na ongezeko la watu kila mwaka, vilevile nchi yetu ilipokea wakimbizi kutoka jirani za Burundi, Rwanda na Congo DRC hivyo kuhitaji maeneo. Vilevile baadhi ya maeneo ya nchi yamekuwa na ufinyu wa maeneo yenye rutuba na

nyasi za kulisha mifugo na wafugaji na wakulima kuhamia maeneo mengine. Athari zilizotokea ni uvamizi wa maeneo ya hifadhi za misitu na mapori ya akiba. Vilevile migogoro imekuwa mingi. Pia tatizo la zana za kilimo imepelekeea watu kutafuta maeneo mapya ya kulima. Athari imekuwa wananchi kuchomeana nyumba na kufyeka mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na athari hizo tunaishauri Serikali iongeze kusimamia sheria husika kuanzia ngazi ya kijiji mpaka Taifa kwa kuwa rushwa imekuwa tatizo. Pili, ufugaji bora kwa kulima nyasi zinazokaa muda mrefu. Serikali ipange matumizi bora ya ardhii kwa kutoa fedha za kupima maeneo. Serikali ipunguze maeneo ya hifadhi ambayo tayari yamevamiwa muda mrefu, zaidi ya miaka 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vitalu vya uwindaji, kwa kupitia utaratibu wa sheria, wahitaji au kampuni zinaomba na kupata leseni za uwindaji kwa mfumo wa vitalu lakini tatizo lililopo ni taarifa kamili za mapato na uvunaji unaofanywa na kampuni zenye leseni. Hivyo, kuna umuhimu wa Serikali kuangalia upya mfumo wa vitalu kwa takwimu za kifedha na idadi ya wanyama. Vilevile vitalu vifanyiwe uchunguzi katika kudhibiti ujangili wa nyara za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo za misitu; Wizara imekuwa na tozo mbalimbali za mazao ya misitu lakini tozo kwenye mbao ni kubwa. Vilevile wachimbaji wadogo wa madini wanatozwa ada kubwa kwa hekta moja shilingi 1,400,000 ambayo haiendani na ukubwa na uharibifu. Hivyo tunaomba Serikali tozo ziendane na miti inayokatwa katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Memorandum of Understanding, Serikali ya Tanzania mwaka 2015 ilisaini mkataba kudhibiti biashara ya magendo kati ya Tanzania na Kenya na kuokoa fedha nyingi. Hivyo tunaomba Serikali iangalie upya MoU na nchi nyingine pia hata za mbali ili kuokoa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusiana na Makadirio na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaaliwa kwa wingi wa vivutio vya utalii ulimwenguni, vivutio ambavyo kwa bahati mbaya hatujavitumia ipasavyo kutuwezesha kuwa na fursa kubwa ya kiushindani katika sekta ya utalii. Wakati ambapo taarifa mbalimbali zimekuwa zikiisifu Tanzania kwa uwepo wa vivutio hivi, ikizidiwa tu na nchi kama Brazil, kama Taifa tumekuwa na changamoto kubwa ya udhaifu katika mikakati yetu ya kuvitangaza vivutio tulivyonyavyo. Ni

ukweli uliowazi kuwa endapo vivutio hivi vingetangazwa na kutumika vizuri, mchango wa sekta ya utalii katika uchumi wa nchi yetu ungekuwa mkubwa zaidi kuliko ilivyo sasa. Ni lazima tuwe na mkakati mahsus wa kutangaza vivutio tulivyonyavyo na mkakati huo lazima utengewe fedha za kutosha zitakazowezesha kutumika kwa mashirika makubwa ya utangazaji duniani kutangaza vivutio tulivyonyavyo na fursa za uwekezaji katika sekta hii zilizopo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kusuasua kwa ukuaji wa Dodoma kunasemakana kwa kiasi fulani kunachangiwa na mji huu kukosa bahari na maziwa ambayo husababisha utalii. Kwa kiasi cha maji tunachoona kinapotea kwa wingi kila msimu wa mvua unapofika hapa Dodoma, nani anasema hatuwezi kuanzisha *state of the art artificial lake* kama walivyofanya Malaysia kwenye mji wao mpya? Nani anasema hatuwezi kuwa na zoo ya kisasa kwenye viunga vya Dodoma? Nani anasema hatuwezi kuanzisha utalii wa zao la zabibu hasa ikizingatiwa kwama Dodoma inasifika kuwa sehemu pekee ulimwenguni ambapo uzalishaji wa zabibu unafanyika kwa misimu miwili katika mwaka? Au nani anasema hatuwezi kunufaika kwa kuanzisha utalii wa tamaduni za Wagogo na nyumba zao za tembe? Hii ni mifano michache tu ya fursa za uwekezaji na vyanzo vipyga vya sekta yetu ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri inaonesha kuwa idadi ya watalii walitembelea nchini imeshuka kidogo ikilinganishwa na mwaka uliopita. Hali hii inashabihiana na taarifa zilizomo kwenye ripoti ya *World Tourism Organisation* inayoonesha kumekuwa na kushuka kwa idadi ya watalii walitembelea Bara la Afrika wakati hali kwa Mabara mengine kama Amerika, Asia na Ulaya ni tofauti kwani Mabara hayo yameshuhudia ongezeko la idadi ya watalii katika maeneo yao. Funzo tunalopata hapa ni kuwa lazima tuwekeze katika ubora wa vivutio tulivyonyavyo na huduma tunazotoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kama Taifa lazima tuhakikishe kiwango tulichofikia cha idadi ya watalii wanaotembelea nchi kinalindwa kisishuke na wakati huo huo kuja na mikakati mpya ya kuongeza idadi ya watalii wanaokuja nchini. Ripoti ya *World Tourism Organisation* inaonyesha kuwa kwa mwaka 2015 safari za kiatalii zinazofanywa na Wachina zimeongezeka kufikia safari milioni 120, ukuaji ambao umeizidi Marekani na mataifa mengine ya Ulaya. Ukuaji huu wa safari za kiatalii zinazofanywa na Wachina unamaanisha kuwa kwa kila safari kumi za kiatalii zilizofanyika ulimwenguni, safari moja ilihuisha raia wa China. Ukuaji huu wa safari za kiatalii zinazofanywa na Wachina ni fursa muhimu sana kwetu katika kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea Tanzania. Nashauri Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje kuchukua hatua za haraka kuweka mikakati ya pamoja itakayotuwezesha kulikamata soko hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa wadau muhimu katika sekta ya utalii nchini wamelalamikia mfumo mbovu wa utoaji leseni kwa kampuni za wazawa na masharti magumu ya uanzishaji kampuni za kusafirisha watalii ikilinganishwa na zile za kigeni. Lazima tuondokane na urasimu usio wa lazima ili kuwezesha Watanzania wengi zaidi kuwekeza katika sekta ya utalii. Ileleweke kuwa urasimu katika utoaji wa leseni na masharti magumu kuhusiana na viwango vikubwa vyta mitaji si tu unazuia uanzishwaji wa makampuni ya utalii bali pia unadumaza ukuaji wa huduma zinazotolewa na sekta nyingine za uchumi kama uzalishaji wa chakula, usafiri, hoteli, wapagazi na watu wengine wanaotegemewa kutoa huduma kwa watalii wawe wa ndani au nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa mbalimbali zinaifananisha Tanzania na nchi kama Australia kwa kuwa na mfumo mbovu wa utoaji leseni, mfumo ambao hautoi mwanya kwa ukuaji wa sekta ya utalii. Aidha, utafiti wa IFC unabainisha kuwepo kwa urasimu mkubwa katika udhibiti wa leseni za utalii na upatikanaji wa mtaji hali ambayo inasababisha ugumu kwa wanaotaka kuingia katika sekta ya utalii hususani wazawa. Kwa kuwa kama Taifa tunakubaliana kimsingi kuwa sekta binafsi ni injini ya kukuza uchumi wa nchi yetu, lazima tuhakikishe tunatoa fursa pana kwa wazawa hususan wale wenye mitaji midogo ili nao waweze kushiriki katika kuwekeza. Lazima tuwaondolee vikwazo vinavyowanyima haki ya kujituma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii ina nafasi kubwa ya kuendelea kuwa mhimili muhimu wa kukuza uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, kufanikiwa kwa hili kunategemea sana kufanyika mambo kadhaa muhimu kama vile kuongeza jitihada katika kutangaza vivutio vyta utalii vilivyopo katika kila kona ya nchi yetu, kuboresha miundombinu muhimu, kuboresha taaluma ya utalii ili kuwa na watu wenye elimu na taaluma stahiki na hali kadhalika kuondoa urasimu katika maeneo mbalimbali yahusuyo sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na jitihada hizo ni muhimu vilevile kuelekeza nguvu zetu katika kukuza utalii wa ndani. Kuna umuhimu sasa wa kuja na mkakati mabsusi wa kukuza utalii wa ndani. Lazima mkakati huo uweke bayana jinsi ambavyo tutaweza kutumia makundi yenye ushawishi hapa nchini kama Wabunge, wasanii na hata timu zetu za mpira wa miguu kwenye ligi kuu kushiriki kwenye kuanzisha utamaduni wa utalii wa ndani hapa nchini. Jambo hili ni muhimu kutokana na ukweli kuwa utalii wa ndani ni uti wa mgongo katika ukuzaji wa sekta ya utalii katika nchi yoyote ile. Ni kutokana na ukweli huu hatuna budi kama Taifa kuelekeza nguvu zetu katika kujenga utamaduni wa wananchi kutembelea vivutio vilivyopo nchini na kuwa na mikakati ya kuhamasisha wanafunzi na vijana kwa ujumla kutembelea mbuga zetu na maeneo ya vivutio katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwe na mkakati kabambe wa kuongeza jitihada zetu katika kutangaza vivutio tulivyonyavyo ikibidi suala la utalii wa ndani liwe sehemu ya mitaala yetu ya kufundishia katika shule zetu, tufanye hivyo. Aidha, wakati umefika wa kuanzisha wiki maalum ya uzinduzi wa utalii wa ndani kila msimu wa utalii unapoanza nchini. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa jitihada zetu za kukuza na kutangaza utalii zinalenga makundi mbalimali ya watu nchini kwa kuzingatia umri, jinsia na uwezo wa kipato ili kumuwezesha kila Mtanzania kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ninalotaka kulizungumzia ni eneo la migogoro ya ardhi iliyopo katika Wilaya yangu ya Mkinga, migogoro ambayo kimsingi inaigusa Wizara hii. Migogoro hii imechukua muda mrefu kupatiwa ufumbuzi licha ya jitihada kubwa zilizofanyika kuishauri Serikali kuipatia ufumbuzi. Jambo hili limekuwa chanzo cha manung'uniko makubwa na wananchi kupoteza imani kwa Serikali yao. Migogoro hii ni kama ifuatavyo hapa chini:-

(i) Mgogoro wa wananchi wa Segoma na TFS. Msitu wa Segoma wenye ekari 2,311 upo ndani ya shamba la Sigi Segoma lenye ukubwa wa ekari 2,829. Shamba hili lilimilikishwa kwa Shirika la Uchumi la Wilaya ya Muheza (SHUWIMU) kwa hati Na. 7675 ya tarehe 01 Aprili, 1990 ya miaka 33. Kutokana na kukosa mtaji na kuzorota kwa SHUWIMU, hati hii ilibadilishwa umiliki kuwa Muheza District Council kuanzia tarehe 16 Februari, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1992 SHUWIMU kwa kukosa mtaji na utaaliam iliingia ubia na M/S Sigi Agricultural Co. Ltd. na SHUWIMU ilipovunjwa shamba lilimiliwa na Muheza District Council ambayo ilifuta ubia uliokuwepo na kuingia ubia na SWIFTCOM ya Tanga. Hii ilisababisha M/S Sigi Agricultural Co. Ltd. kufungua kesi Na. 18 ya 1996 kupinga kufutwa kwa ubia wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 hukumu ya kesi hii ilitolewa na Halmashauri ya Muheza kupewa ushindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ilianzhishwa kwa kumegwa toka Muheza. Katika zoezi la kugawana mali, shamba hili lilikuwa sehemu ya mali zilizogawiwa kwa Halmashauri ya Mkinga. Hivyo basi, kufuatia kutolewa kwa hukumu iliyohusisha shamba hili, Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga kwa ufadhili wa Tanzania Forest Conservation Group (TFCG) ilifanya ukaguzi wa uhalisia wa shamba kwa wakati huo na kutoa taarifa katika kikao kilichofanyika tarehe 08 Oktoba, 2012 kikihuisha viongozi wa kijiji cha Segoma, Kata, wataalam wa Halmashauri, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – Kanda ya Kaskazini na wataalam wa Mkoa. Kikao kilitoka na mapendekezo kuwa kwa kuwa kijiji cha Segoma kina tatizo kubwa la uhaba wa ardhi, ekari 518 za shamba zigawanywe kwa wananchi kwa shughuli za kilimo na makazi na ekari 2,311 zitengwe kuwa eneo la hifadhi ya msitu. Mnamo tarehe 05 Disemba,

2012 kikao cha Baraza la Madiwani kama wamiliki halali wa rasilimali hii kiliridhia mapendekezo haya na kuagiza ekari 518 zigawiwe kwa wananchi wa kijiji cha Segoma kwa shughuli za makazi na kilimo na ekari 2,311 zimilikishwe kwa kijiji cha Segoma kuwa msitu wa kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Meneja wa Kanda wa Wakala wa Huduma za Misitu aliomba kuonana na uongozi wa Halmashauri kwa majadiliano juu ya kijiji kumilikishwa msitu. Taarifa ya ombi hilo ilipofikishwa kweneye kikao cha Baraza cha tarehe 16 – 17 Julai, 2014, Baraza liliagiza kuwa wataalam wa ardhi na misitu wa Wilaya watekeleze Azimio la Baraza la tarehe 05 Disemba, 2012 bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Menejimenti kutekeleza agizo hilo, tarehe 28 Novemba, 2014 kwa mshangao mkubwa Halmashauri ilipokea barua kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ikiamuru kusitishwa kugawa ardhi kwa wananchi kwa ajili ya kilimo na makazi na halikadhalika kukabidhi msitu kuwa wa kijiji cha Segoma. Jambo hili limeleta taharuki kubwa kwa wananchi kiasi kwamba walikuja Dodoma wakati wa vikao vya bajeti kuwasilisha malalamiko yao. Aidha, wakati wa kuhitimisha mjadala wa bajeti nillazimika kuomba ufanuzi kuhusiana na jambo hili na Naibu Waziri alikiri kuwa wananchi wa Segoma wanayo haki ya kupatiwa ardhi tajwa na kwamba atatembelea Mkinga ili kulipatia ufumbuzi jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiendelea kusubiri utekelezwaji wa ahadi ya Naibu Waziri kutembelea Mkinga kuja kuapatia ufumbuzi mgogoro huu, Halmashauri ilipokea barua toka kwa Katibu Tawala wa Mkoa yeny Kumb. Na. BF 174/314/02/35 ya tarehe 02 Disemba, 2015 ikiagiza eneo la ekari 518 likabidhiwe rasmi kwa kijiji na eneo la msitu lenye ukubwa wa ekari 2,311 kuwa chini ya usimamizi wa Wakala wa Huduma za Misitu hadi hapo uamuzi mwingine utakapotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi haya ya kuinyang'anya Halmashauri ya Mkinga rasilimali yake siyo tu kuwa ni ya uonevu mkubwa bali pia yanakinzana na Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 ambayo inabainisha wazi kuwa jamii inaweza kulinda, kuhifadhi, kusimamia na kutumia kiendelevu misitu katika ardhi ya kijiji ili kukidhi mahitaji yao ya kimaendeleo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa zaidi ya hekta milioni 21.7 sawa na asilimia 45.7 za misitu hapa nchini zinasimamiwa na Serikali za Vijiji zaidi ya 1,000. Aidha, hekta milioni 3.5 sawa na asilimia 7.3 za msitu nchini zinasimamiwa na watu binafsi au vikundi. Hivyo, Kijiji cha Segoma kukabidhiwa kusimamia msitu wao wa asili haitakuwa kioja wala mara ya kwanza kwa kijiji kumiliki msitu. Ni kwa msingi huu tungependa kuona busara iliyotumika kuruhusu

vijiji zaidi ya 1,000 hapa nchini kusimamia misitu yao ikitumika hata kwa msitu wa Segoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutohana na ukweli kuwa wananchi hawa ndio wameutunza msitu wa Segoma na kuwajibika kuhakikisha msitu unabaki salama pasipo kuombwa wala kukabidhiwa na Serikali. Inasikitisha kuona leo wananchi hawa wakiporwa rasilimali hii kwa mabavu, kejeli na udhalilishwaji kuwa wao ni wavamizi.

Halmashauri ya Mkinga na wanakijiji wa Segoma wanataka kunufaika na umiliki wa rasilimali yao kupitia mapato yatokanayo na mavuno ya msitu huu ili kuboresha huduma za kijamii na kuleta maendeleo ya kijiji.

(ii) *Kwamtili Estate* - shamba hili lina ukubwa wa hekta 1,150 na linamiliwa na *Kwamtili Estate Ltd.* yenye Certificate of Incorporation Na. 2649 iliyosajiliwa tarehe 09 Januari, 1961 ikiwa na wanahisa wafuatao:

S/N	JINA LA MWENYE HISA	ANAPOISHI	MAELEZO
1.	Dennis Martin Fielder	4 Market Square Tenbury, Wells Worcestershire - UK	Amerudi Uingereza
2.	National Agriculture & Food Corporation (NAFCO)	Box 903 DSM	Shirika limefutwa
3.	Handrik Tjails Scheen	C 1/30 Algamines Bank, Amsterdam, Netherland	Amefariki
4.	Louis Van Wagenburg	Laycisan Ag Vaghel, Holland	Amefariki
5.	Schoonmakers Bart Vanderburg	De Congabsen, 163 Schikhher, Holland	Amefariki
6.	Tracey Elan Allison	The Wilos Terrigton, Herefordshire, UK	Amefariki
7.	Juvent Magoggo	42 Block S, Mikanjuni Box 5855 Tanga	Anaishi Tanga
8.	W. J. Tamé Ltd	Box 118 Tanga	Amefariki
9.	Jacobus Cornelius Josephus Moris	Logtanburg Vaghel, Holland	Amefariki

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba hili lililopo katika eneo la Kwamtili, Kata ya Bosha, Wilaya ya Mkinga lilitumika kwa kilimo cha kibashara cha zao la kakau. Hata hivyo, kwa muda wa miaka takribani 26 sasa shughuli za kilimo cha zao la kakau zimesimama baada ya iliyokuwa Menejimenti ya Kampuni chini ya Ndugu Dennis Fielder kutelekeza shamba hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, baada ya shamba kutelekezwa, mmoja wa wanahisa Ndugu Juvent Magoggo amekuwa akifanya shughuli ndogo ndogo ikiwemo kuvuna miti ndani ya shamba hili kwa lengo la kupata fedha za kufanya uzalishaji mdogo mdogo na hali kadhalika kuruhusu wananchi wanaozunguka shamba hilo kulima mazao ambayo si ya kudumu. Hata hivyo, kwa sasa Ndugu Magoggo ameshindwa kuendelea kufanya shughuli hizo baada ya kunyimwa vibali vya kuvuna miti na kusafirisha magogo.

Kutokana na kuwepo kwa ombi la umiliki wa shamba hili, yamezuka makundi ya watu yanayodai kuwa na haki ya kumiliki shamba hili na hivyo kuwakodisha wananchi wanaozunguka shamba hili maeneo ya kulima kwa kuwalipisha sehemu ya mavuno yatokanayo na matumizi ya ardhi hiyo. Aidha, kumekuwa na wimbi la kujitokeza raia wa kigeni kwa kutumia kivuli cha aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa shamba na kulitelekeza Ndugu Dennis Fielder kufanya uharibifu wa mali za kampuni, ikiwemo upasuaji wa mbao na kuanzisha michakato ya kujimilikisha ardhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, wananchi wanainyooshea kidole Ofisi ya Wakala wa Hifadhi ya Misitu Wilaya ya Mkinga kutaka kujingiza katika kufanya udalali wa ardhi hii. Wananchi bado wana kumbukumbu nzuri ya jinsi watumishi hawa wa TFS Wilayani Mkinga walivyotumika kuwezesha mwekezaji wa Kiitaliano aliyejaribu kupatiwa ardhi ya Mkinga takribani hekta 25,000 kinyume na taratibu ili kulima *jatropher*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali hajjaweza kulipatia ufumbuzi tatizo lingine ambalo kimsingi limeanzishwa na TFS kutaka kupora ardhi ya wananchi katika shamba la Segoma, TFS hiyo hiyo inataka kuzalisha mgogoro mwingine wa kupora ardhi nyingine katika Wilaya ya Mkinga. Hatupo tayari kuona hili likitokea hasa ikizingatiwa kuwa Kwamtili inakabiliwa na tatizo kubwa la ardhi. Tunaiomba Serikali kutumia busara kuacha jambo hili na kuirejesha ardhi hii kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kwamtili na Kata ya Bosha kwa ujumla wamebaki katika umaskini wa kutupwa baada ya shughuli za kilimo cha kakau katika shamba la Kwamtili ambacho ndicho kilitoa ajira kwao kusitishwa. Nusura pekee kwa wananchi hawa ni kupatiwa maeneo katika shamba hili ili kwa kutumia utaratibu wa wakulima wadogo waweze kufanya shughuli ya kilimo na hivyo kujikimu kimaisha. Naiomba Serikali ifanye uamuzi wa kufuta hati ya shamba la Kwamtili na kisha kuligawa kwa wananchi kwa ajili ya kilimo na sehemu nyingine kutengwa kuwa hifadhi ya msitu wa kijiji.

(iii) Mgogoro wa Kijiji cha Mkota na Hifadhi ya Taifa Mkomazi; wananchi wa Kitongoji cha Kimuuni katika Kijiji cha Mkota, Kata ya Mwakijembe wamekuwa wakiishi katika eneo hilo kabla ya uhuru. Kitongoji hiki kina takribani kaya 170 na wakazi wapato 530. Wananchi hawa kwa muda wote wamekuwa msaada mkubwa kwa ulinzi na rasilimali za nchi yetu hasa ikizingatiwa kuwa eneo hili linapakana na nchi jirani ya Kenya. Wananchi hawa wanalalamika kuwa eneo lao ambalo ni sehemu ya kijiji cha Mkota kwa mujibu wa ramani ya kijiji iliyosajiliwa, eneo lao limechukuliwa na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na pori tengefu la Umba na kwamba sasa wanatakiwa kuondoka kwenye eneo hilo licha ya kufanya uwekezaji mkubwa kwa kutumia nguvu zao kuchimba mabwawa makubwa ya kunywesha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu nimeufikisha Serikalini na nimelizungumzia jambo hili mara nyigi sana katika Bunge la Kumi lakini hadi sasa halijapatiwa ufumbuzi. Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka wakati akiwa Waziri wa Ardhi akiongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa alifanya ziara katika Wilaya ya Mkinga na kufanya mukutano wa hadhara katika kijiji hiki. Katika mukutano ule, Mheshimiwa Waziri aliwaahidi wananchi kuushughulikia mgogoro huu. Aidha, aliyekuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa akiandamana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa naye alifanya ziara katika eneo la mgogoro (Kimuuni) na kufanya mukutano wa hadhara ambapo alipokea ombi la wananchi kwa eneo hili kupewa hadhi ya kuwa *Wildlife Management Area (WMA)* na kuahidi Wizara kuanzisha mchakato wa kulitangaza eneo ili kuwa WMA. Tunaamini kuwa suluhisho la mgogoro huu ni Serikali kukamilisha mchakato huu ili wananchi waweze kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa sasa changamoto za muda mrefu za uwepo wa migogoro ya mipaka ya vijiji, umiliki wa ardhi na uwepo wa mashamba yaliyotelekezwa kwa muda mrefu katika Wilaya ya Mkinga yatapatiwa ufumbuzi. Namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja ya bajeti hii atueleze nini kauli ya Serikali kuhusiana na changamoto hizi na tunamuomba atoe kipaumbele cha kuitembelea Mkinga ili kuja kutatua migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja nikiamini kuwa Wizara itachukua hatua stahiki katika kutatua changamoto nilizoelezea na kuzielekeza taasisi zilizo chini yake kuacha kuwa chanzo cha migogoro na kuwanyima haki wananchi wetu.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto ya uchomaji wa misitu hovyo hasa kipindi cha miezi ya saba hadi kumi na moja. Tatizo hilo la uchomaji limekuwa kubwa sana na la kawaida katika Mkoa wa Njombe, katika maeneo ya Kifanya na maeneo mengine. Napenda kuishauri Serikali kusimamia sheria lakini pia wachukue hatua kali dhidi ya wananchi watakaobainika wanachoma moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na changamoto ya TANAPA kufyeka mahindi, ndizi, miwa katika kijiji cha Luduga, Wilaya ya Wanging'ombe. Nashauri Serikali itoe elimu kwa wananchi wa maeneo hayo kuhusu maeneo ya hifadhi na kuweka mipaka kati ya hifadhi na maeneo ya kulima wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wafanyakazi wa hifadhi wasinyanyase wananchi kwa kuwapiga na kuwapeleka kwenye vituo vyta polisi. Wawe na

uzalendo wa kujadiliana badala ya kutumia nguvu kwa kuwafyekea mazao yao na huo sio ubinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ahsante.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hotuba ya Wizara ya Utalii ambayo imesheheni mipango mizuri ya utalii nchini ili kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi halali na wawindaji nchini, kuhusiana na wavuvi ambao wapo katika maeneo yenye mito, maziwa, mabwawa na bahari, naomba hawa wavuvi leseni zao zichunguzwe upya maana kumekuwa na malalamiko mengi kwa wageni kuingia nchini kwa lengo la utalii na kumbe baadhi yao wanavuka mipaka ya kilichowapeleka katika maeneo ya utalii, hawana vibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matatizo mengi sana ya ujangili katika mbuga zetu. Serikali imejipangaje kuhusiana na kudhibiti hawa wawindaji halali wanaoingia kama watalii katika mbuga zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike, Serikali ichunguze ni namna gani ya kudhibiti hawa watalii na siyo kuwaacha peke yao mbugani. Wanafanya nini hasa maana tumeona ujangili mwengi umekuwa ukifanyika na wanaokamatwa wengi ni wageni. Hivyo, Serikali iongeze vitendea kazi kama magari kwa ajili ya kufanya *patrol* ndani ya mbuga zetu, kuwapa silaha zenye uwezo askari wa wanyamapor. Pia Serikali iboreshe maslahi ya askari wa wanyamapor ili wafanye kazi kwa moyo na kuwazuia kufanya biashara haramu (pembe za ndovu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwekezaji ndani na mbuga, kumekuwa na malalamiko mengi kwa baadhi ya mbuga kwamba wawekezaji hawa wanaajiri watu wengi ambao ni wageni kutoka nchi jirani na maeneo kama Pakstani, Wahindi na Wazungu. Je, Serikali haioni kwamba kwa kuendelea kuwapa uhuru hawa wawekezaji kuajiri wageni zaidi kuliko wazawa ambao wapo wenyе uwezo na elimu kuweza kuhudumia mfano hoteli zilizopo mbungani, customer services na madereva. Shughuli hizo wangeweza kufanya wazawa kwa wingi kuliko wageni wanaoletwa kuchukua fursa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbuga ya Katavi ichungwe zaidi. Je, ni jinsi gani wawekezaji hawa wanasaidia wakazi wa vijiji vya jirani kwa huduma kama maji, zahanati, barabara na madawati? Wawekezaji hawa wanaingiza vipato vikubwa hivyo wanapaswa pia kusaidia jamii inayowazunguka katika mbuga hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanja vya ndege, kutokana na uhaba, ukosefu wa vifaa vya kisasa kama kamera katika viwanja vya ndege inachangia kutoroshwa kwa rasilimali zetu mfano ndovu, vyura na kadhalika. Hivyo, Serikali ihakikishe inawezesha upatikanaji wa vitendea kazi bora kama kamera, mashine za ukaguzi, x-ray na screening machine. Nini kifanyike? Ulinzi uongezwe zaidi hasa katika viwanja vya ndege ambavyo viko ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia kwa waathirika wa Operesheni Tokomeza Serikali iangalie namna gani ya kufidia watu walioumizwa, kuibiwa na kupigwa. Mfano katika Mkoa wa Katavi, Wilaya ya Mpanda Vijiji, Kata za Isengule na Kapalambsenga, askari polisi walijeruhi watu ambao hata hawahusiki. Je, Serikali ina mpango gani wa kushughulikia suala hili?

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais kuikabidhi Wizara hii kwa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge ambaye ni mbobevu wa hifadhi za wanyamapori na misitu. Naamini tembo wa Selous Game Reserve sasa wamepata mlinzi na naahidi kwa eneo la Namtumbo nitamsaidia kwa uwezo wangu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba atusaidie wakazi wa Wilaya ya Namtumbo katika masuala yafuatayo:-

(i) Vijiji saba vya Jumuiya ya Mbarang'andu na vijiji vingine vinavyounda jumuiya mbili, nyingine za Kimbanda na Kusangura vinahitaji kuhuisha mipaka yao ya WMA ili kutoa fursa ya ardhi ya kilimo. Wananchi wameongezeka, wanahitaji maeneo zaidi ya kilimo kwa ajili ya kujikumu kimaisha. Muda wa kupitia upya mipaka hiyo ilikubalika miaka kumi na hadi sasa miaka imezidi bila kufanyika kwa makubaliano hayo ya kupitia upya mipaka hiyo ya WMA.

(ii) Watumishi wa Selous Game Reserve wameonekana wakiweka beacons ndani ya maeneo ya vijiji vya Mputa, Luhimbalilo, Luhangano, Mhangazi, Kitanda, Nangero, Mtumbatimaji na Nambecha na hivyo kutishia ama kuenea uvumi wa maeneo yao kuchukuliwa, yaani kupanua mipaka ya hifadhi na kuingilia WMA na mashamba ya wanavijiji bila taarifa yoyote kwao. Nitashukuru kama wananchi hao watahakikishiwa usalama wa maeneo yao.

(iii) Vijiji vinavyoizunguka Selous Game Reserve, Undendeule Forest Reserve na Lukwika Forest Reserve wala Halmashauri yetu ya Wilaya Namtumbo hainufaiki na uwepo wa hifadhi hizo. Namuomba Mheshimiwa Waziri atufikirie kama ilivyo kwa wenzenetu wanaozunguka hifadhi za Kaskazini.

(iv) Operesheni Tokomeza imewaacha baadhi ya wakazi wa Namtumbo bila silaha zao walizokuwa wakizimiliki kihalali kwa mujibu wa sheria na walielekezwa wakazikabidhi kwa uchunguzi na hadi leo hawajarudishiwa bila maelezo yoyote. Naomba Mheshimiwa Waziri silaha hizo warudishiwe waliokuwa wakizimiliki ili waendelee kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri kwa kutusikiliza na kutujali. Tafadhali Waziri chapa kazi ukimshirikisha Naibu wako Mheshimiwa *Engineer Ramo Makani*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilichangia kwa maandishi masuala manne yaliyojitekeza kwa nguvu kipindi cha Kampeni ya Uchaguzi Mkuu. Leo asubuhi Mkuu wa Wilaya ameniomba nikueleze yafuatayo ambayo kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama yanasurya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana hiyo alitembea Kijiji cha Likuyu Mandela ambacho asili yake ni waliokuwa wakimbizi kutoka Msumbiji na wamepata uraia wa Tanzania. Tembo wanaingia majumbani wanaipua hata mahindi yaliyoko jikoni. Mazao yao yamekuwa yakiliwa kila mwaka na maombi yao ya kulipwa fidia au kifuta jasho hayajashughulikiwa toka mwaka 2011. Wiki iliyopita mkazi mmoja ameuawa na tembo. Hiyo ni moja kati ya matukio ya karibuni ya madhara ya tembo ambao idadi yao imeongezeka sana baada ya ujangili kudhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hoja za wakazi hao wa kijiji cha Likuyu Mandela zipatiwe ufumbuzi. Aidha, kijiji hicho kisaidiwe chakula na itafutwe njia nzuri ya kuwazuia wanyamapori kutovuka mipaka ya hifadhi hata kwa kutumia uzio wa umeme kama inavyofanyika katika nchi za wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hoja hii iunganishwe na hoja zangu nyiningine nne za jana nilizochangia vilevile kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri na Naibu Waziri *Engineer Ramo Makani*, Katibu Mkuu na watumishi wote kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie uharibifu wa misitu kwa uvamizi wa wafugaji kwani kila wanapofika sehemu hukata miti yote. Kwa mfano, Kizengi, Bukene, Urambo, Bukumbi, Kitundo na kadhalika. Pia ukataji miti kwa kuchoma mkaa ni tatizo hivyo Serikali iangalie upya sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji nyuki, elimu itolewe kwa wajasiriamali ili wafuge kisasa kwa kutumia mizinga ya kisasa. Wajasiriamali hasa wanawake wakopeshwe mizinga ya kisasa kwa bei nafuu. Kuanzisha kiwanda cha kusindika asali kama ilivyokuwa zamani kwani Tabora ina historia ya kurina asali. Pia kiwanda hicho kinaweza kutumika kama Kanda ya Magharibi, Singida, Tabora, Kigoma na kadhalika kwa kusafirisha nje ya nchi pia kusindika nta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Nyuki tuombe chuo hicho kitambuliwe rasmi ili wanafunzi hao wanapohitimu mafunzo haya wapewe ajira kwani mpaka sasa ajira zao ni za kujitegemea, ni vyema sasa ajira hizo zilingane na vyuo vingine. Wanachuo hao wapewe vitendea kazi kama vile mizinga ya kisasa ili wakatoe elimu darasa maeneo mengine. Ukarabati wa chuo hicho niombe uendelee kwani maeneo mengi ni machakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya makumbusho; katika Mkoa wa Tabora katika Kata ya Kwhara kuna makumbusho ya kihistoria ya kumbukumbu za Dkt. Livingstone, Stanley, Said Ibin Batuta, waliokuwa watu maarufu kihistoria. Ni vyema eneo hilo pia likatangazwa kama utalii. Pia kuna majengo ya Ujerumanii ambayo yana historia, ni ya maajabu. Naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Katavi limepokea wafugaji wengi na mifugo yao na sasa maeneo hayatoshi kwa makazi, kilimo na malisho. Naomba eneo la hifadhi ya msitu wa Inyonga lipunguzwe na kuongezwa vijiji vya Mapili, Kamalampaka, Songambele, Imalauduki, Kafulu, Nzega, Kaulolo, Masigo, Nsemkwa na Ipwaga.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi ngumu lakini nzuri wanayoifanya. Mchango wangu utajielekeza kwenye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya hifadhi; kwa takwimu nilizonazo, Tanzania ina eneo la uhifadhi ambalo ni asilimia 38 ya eneo lote la nchi. Hili ni eneo kubwa sana na nchi yetu ni moja ya nchi iliyona eneo kubwa sana la uhifadhi duniani. Wakati wa uhuru nchi yetu ilikuwa na watu karibu milioni kumi tu, lakini hivi leo watu tunakaribia milioni 50. Eneo la makazi ya watu haliongezeki, watu wakiongezeka na shughuli zao za kiuchumi, kijamii nazo zinaongezeka na kwa sababu shughuli hizi zinafanyika kwenye ardhi, lazima maeneo ya uhifadhi yatalazimika kutumiwa na watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba Serikali iangalie upya maeneo ya uhifadhi kwa kuyapunguza ili yatumike kwa shughuli za watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapato ya utalii na idadi ya watalii; mapato yatokanayo na utalii bado ni madogo. Nakubaliana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba juhudhi kubwa zinafanyika ili kufikisha kipato kitokanacho na utalii hapo kilipo. Kama nchi yetu ni ya pili kwa kuwa na vivutio bora vyta utalii duniani baada ya Brazil, kwa nini mapato yetu kama nchi yakabaki kidogo namna hii? Mheshimiwa Waziri ni vyema akatoa maelezo juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mapato yetu ni kidogo kwa sababu idadi ya watalii wanaotembelea maeneo yetu ya utalii ni wachache. Ni kweli watalii wamekuwa wakiongezeka mwaka hadi mwaka, lakini ongezeko hili ni dogo kuwezesha kutupatia mapato makubwa ambayo yanatokana na utalii. Ninamtaka Mheshimiwa Waziri atueleze ana mkakati gani mpya wa kuongeza idadi ya watalii na hatimaye kutuongezea mapato kama nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la migogoro ya wafugaji na hifadhi; ipo migogoro kati ya wafugaji na Hifadhi za Taifa kwa sababu wafugaji wanapopata matatizo ya malisho na maji wanatafuta malisho na maji kwenye hifadhi. Nakubali huku ni kuvuruga sheria, lakini wafugaji hawa wanapovunja sheria kwa kuingiza mifugo yao kwenye hifadhi, Serikali nayo kwa kutumia wafanyakazi wake nao wavunje sheria kwa kuua ng'ombe ama mifugo yao? Nao pia wavunje sheria kwa kuchoma nyumba za wanavijiji, wafugaji amba wanaishi kando kando ya hifadhi? Wafanyakazi hao nao waombe rushwa kutoka kwa wafugaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Serikali i-balance, hapa sheria zifuatwe, lakini *with a human face*. Umejika wakati sasa maeneo ya wafugaji yatengwe na kuwekewa miundombinu muhimu inayohitajika ikiwepo utatuzi wa tatizo la malisho ya mifugo ya wafugaji. Serikali ikae kitako kwa kuhusisha Wizara zinazohusika ili kutatua migogoro hii na nchi ipate mabadiliko ambayo wananchi wanayahitaji. Wizara na Serikali ziache kufanyakazi kwenye silo, Serikali ni moja lazima ije na mkakati wa pamoja ili kuondoa udhia huu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi napenda nichangie kwa njia ya maandishi bajeti ya Wizara ya Maliasili kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uteuzi wake kwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri mwenye dhamana Wizara ya Maliasili na Utalii. Mimi binafsi naamini shule na weledi wa Profesa Maghembe katika Wizara

ya Maliasili na Utalii ni silaha nzuri katika ujenzi wa makuzi ya sekta ya maliasili na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na pongezi hizi pia ningependa nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uteuzi wake wa *Engineer Ramo Makani* katika ujenzi wa sekta ya utalii. Mimi napenda kusoma vitabu vya Peter Senge ambaye ameandika masuala mengi ya *management*, ambapo moja ya michango yake aliweza kuonesha mahusiano ya kada za Injinia na *best management practice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie kwa kujikita zaidi kwenye suala zima la mahusiano ya michezo na utalii. Moja kwa moja kwa uhusika wangu kwenye mbio za *marathon* zilizofanyika mapema mwezi Februari, 2016. Katika mbio hizo lipo jambo moja kuu la utangazaji wa maliasili kupitia michezo ambalo nilifikiri ni vyema tusilipuuzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *marathon* iliyofanyika mkoani Kilimanjaro ambapo Mheshimiwa Waziri wa Habari na Michezo alikuwa mgeni rasmi tuliona kwa pamoja namna ambavyo maliasili ya uoto wa Mlima Kilimanjaro unavyotumika na makampuni binafsi katika kujipatia vipato vya mtu mmoja mmoja. Katika *marathon* hii, napenda Bunge lako Tukufu litambue Ndugu John Harrison mzaliwa wa South Africa ambaye ndiye aliyeandaa mbio hizi za *marathon*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuonyesha masikitiko yangu makubwa katika maandalizi na uendeshaji wa mbio hizi za *marathon*. Mbio hizi zilizoshirikisha Mataifa ya nje, zaidi ya watu 30,000 na wazawa 70,000 hapakuwa na ushiriki wowote wa TANAPA, wala Tanzania Tourist Board. Tulichokiona pale ni Gapco, Tigo, TBL, Serengeti Breweries na kadhalika. Napenda pia Bunge lako Tukufu litambue theme iliyobeba mbio za *marathon* katika ku-promote Mlima Kilimanjaro ilikuwa; "Mbio zetu, Bia zetu." Hapa ninahojii hivi kwa nini isingelitokea walau tunakuwa na theme inayosema "Mbio zetu, Utalii wetu"? Hizi ndizo *t-shirt* tulizovaa katika kongamano hili zenye ujumbe wa "Mbio zetu, Bia yetu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu lilikuwa ni jambo la fedheha kuona Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana katika Wizara ya Habari anavalishwa *t-shirt* inayo promote Bia ya Kilimanjaro na siyo Mlima Kilimanjaro. Hii ni aibu kwa Wizara, aibu kwa Taifa na aibu kwa Mataifa yote yaliyoshiriki katika mbio hizi ambaao walifika takribani 30,000 katika mbio zile. Tulikuwa na watoto wadogo waliokimbia takribani 7,000, swali langu ni ujumbe gani tulioutoa kwa vijana hasa wadogo? Ni lini watafahamu umuhimu wa uwepo wa outo wa kivutio hiki muhimu katika Mkoa wa Kilimanjaro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hoja yangu ni moja, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imejipangaje kutangaza vivutio vya nchi yetu kupitia *olympic games* itakayofanyika mwezi Agosti, 2016 nchini Brazil? Nchi yetu na hususan Wizara ya Maliasili na Utalii itueleze imejipangaje kutumia fursa za michezo katika kutangaza maliasili yetu katika *olympic* ya mwezi Agosti, 2016? Tanzania ni sehemu ya delegates watakaohudhuria *olympic games*, ambapo katika event hii tunatarajia tutakuwa na zaidi ya viewers *three billion*. Kwangu hii ni sehemu muhimu katika kutangaza maliasili yetu. Ningependa kupitia majibu ya karatasi kutoka kwa Waziri, nini mpango wa Serikali katika kutangaza maliasili ya Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Bungeni tuna *half marathon* ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwahi ku-host event ya namna hii, Wabunge tumewahi kuwa sehemu ya ushiriki. Hapa nina hoja, je, Serikali kupitia Waziri mwenye dhamana, hatuoni umuhimu wa kutumia hata hizi *platform* za Ofisi ya Bunge katika ku-promote maliasili yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili nami napenda nimuombe Mheshimiwa Waziri kupitia ofisi yake aone na atambue umuhimu wa kutoa elimu ya kutosha kwa wafugaji, wakulima, na wadau wote katika sekta ya maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, personally napenda niseme kuwa suala ka *ecological system* lina two key players; uoto wa maliasili, binadamu na shughuli zake hapa namaanisha shughuli za kilimo na ufugaji lakini katika wahusika hawa wawili binadamu katika utashi wake ndiye amepewa uwezo wa kuleta *balance* kati ya uoto wa maliasili pamoja na wanyama na suala zima za kilimo sasa hapa nilitaka niseme nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi maingiliano ya uoto wa maliasili na wanyama pamoja na wakulima ni binadamu pekee mwenye uwezo wa kuhifadhi maliasili ya Tanzania kwa ujumla wake. Kilimanjaro leo vivutio vya maporomoko ya maji yaani *water falls* yametoweka, mito imekauka; Mto Karanga Kikafu pamoja na Bwawa la Nyumba ya Mungu yote yameonesha dalili za nje, nje za kutoweka katika uso wa Tanzania kama wakazi wa Kilimanjaro bado wataendelea kuchoma misitu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ni ushauri wangu kwa Wizara husika kutoa elimu ya kutosha ili uoto wa asili uendelee kuwepo kwa vizazi na vizazi. Nchi ya Rwanda imekuwa ni *role model* kwa Tanzania na East Africa katika suala zima la uhifadhi wa mazingira, hapa tuijulize nini wastani wa wanyama kwa mfugaji mmoja mmoja? Nafikiri katika jibu tutakalolipata tutaweza kupiga hatua kutokea hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hitimisho langu pia ningependa niiombe Serikali yangu iweze kukumbuka royalties kwa wananchi wangu wa Mkoa wa Kilimanjaro kutokana na *natural endowment* tuliyonayo kwa Mkoa wa Kilimanjaro. Nasisitiza kwamba vijana wa Kilimanjaro wamebaki kuwa watazamaji, wahitimu wa vyuo vikuu wamebaki kuwa wabeba mizigo ya wazungu wanaokuja kupanda Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimanjaro kama mikoa mingine nayo imekuwa ni sehemu ya wahanga katika suala zima la huduma za jamaii ilhali Mlima Kilimanjaro wenyewe na vivutio vyake vinachangia pato la sekta ya utalii kwa zaidi ya asilimia 34. Shule za Mkoa wa Kilimanjaro zina uhaba mkubwa wa matundu ya vyoo, katika shule za msingi na sekondari, hakuna madawati; zipo baadhi ya shule za msingi watoto wanakaa chini, vijana wengi wameingia kwenye mkumbo wa kuvuta bangi na dawa za kulevyia. Hii yote ni kutokana na hali ya kukata tamaa baada ya kukosa ajira na kubaki na ajira ya vibarua vya wazungu/watalii katika nchi yetu. Naomba kuwasilisha.

**MHE. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja. Aidha, niwapongeze sana Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na kuwa na changamoto nydingi, Mungu mweza wa yote awaties nguvu, mtende kazi bila kuchoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni tamaduni za makabila; niwaombe katika suala la utalii muangalie pia historia na tamaduni za makabila mbalimbali kwani chaweza kuwa kivutio kikubwa cha utalii, kupata historia na utamaduni wa makabila husika. Mfano Kituo cha Bujora na Kayenze Mkoa wa Mwanza, kwa Wanyamwezi Tabora (Mwinamila), tamaduni na historia za Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Iringa na Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Makumbusho ya Mkwawa - Iringa, kuna mengi ya kuvutia watalii, lakini pamesahaulika sana. Historia ya Mkwawa hakuna asiyeifahamu lakini kituo chake kimesahulika sana na pamechakaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia kwa waathirka wa kung'atwa na fisi; Jimboni kwangu katika Kata ya Sangabuye na Bugogwa zaidi ya watu nane waling'atwa na fisi na wawili hali zao zilikuwa mbaya sana. Halmashauri italeta madai ya wananchi wakidai fidia kwa madhara walipoyapata. Vilevile kwa habari nilizopewa, ninaomba walete ushahidi wao baadhi yao walipwe fidia siku za nyuma. Ninaomba mara watakapoleta madai yao yashughulikiwe mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wafugaji na wakulima; ni vyema kama ambavyo imesemwa mara nyingi na Wizara yetu imelizungumzia, tupange kukutana na Wizara zinazohusika ili tumalize kero hii, watu wawe wafugaji wasiosumbuliwa. Iwapo kuna haja ya kumega maeneo ambayo yamevamiwa na makazi ya watu, tupime uzito ili kuondoa kero na kelele za mara kwa mara. Lengo la Serikali ni kuondoa kero, lakini kuwafanya wananchi waheshimu sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu liwe endelevu ili watambue mipaka yao, zaidi sana wawe sehemu ya kulinda mazingira na hifadhi zetu.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda kuwa mdogo, ningependa kuongeza mchango wangu niliozungumza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwaombea wananchi 1,128 wa Derema wafikiriwe kuongezwa fidia, lakini bado hati ya shamba la Kibaranga tunapotegeMEA kuwahamishia haijapatikana, Waziri wa Ardhi anafahamu suala hili. Wizara ifikirie zaidi kuwaongezea vibali wanavijiji ambao wako karibu na shamba la Tiki. Wananchi hawa ambao ni vibarua wa shamba hilo la Derema wanalamika kwa kupewa vibali vichache mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ifikirie kuanzisha Chuo cha Hifadhi ya Asili ambacho hakuna hapa Afrika Mashariki na Kati. Muheza tutakuwa tayari kutoa eneo la chuo hicho. Ili kuongeza watalii nchini, pamoja na kununua ndege tatu ambazo hakikisha kati ya hizo zilenge nchi zenye watalii wengi, ni vizuri kuongeza au kuwatafuta *tour operators*, ambao wanaweza kufungua ofisi hizo kwa wingi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ifikirie kuboresha sehemu ya kituo cha Horombo ambacho ni njia ya kupanda Mlima Kilimanjaro. Iboreshe kukuza utalii wa ndani ili kuwawezesha wananchi kufika hapo kwa kuwa magari yanafika na wengi wanaweza kufika na kuona milima yote vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wanyamapor waendelee kupata mafunzo zaidi na waajiriwe wengi kukidhi mbuga zote.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuchangia Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya, nimpongeze Rais, Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri na pia kwa uteuzi wa viongozi wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Nimpongeze Waziri Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe na Naibu Waziri Mheshimiwa Engineer Ramo Makani na Katibu Mkuu - Meja Jenerali Gaudence S. Milanzi kwa kuongoza Wizara hii nyeti na maalum katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika baadhi ya maeneo na kushauri kutokana na maoni yangu na mengine ya kutoka kwa viongozi wa Wilaya na Mkoa wetu wa Manyara. Niombe Wizara ya Maliasili na Utalii isaidie Halmashauri zetu ambazo zina hoteli za kifahari na camp sites ambazo kisheria wanatakiwa kulipa ushuru wa huduma (*service levy*) asilimia 0.3 ya mapato yao hadi leo wamekataa na walienda mahakamani na kushindwa kesi, wamekata rufaa katika Mahakama ya Rufaa. Mapato mengi tunapoteza na hasa Halmashauri zetu zinazotegemea mapato hayo. Wizara inaweza kukaa na chama cha wenye Hoteli Tanzania (*HATS*) na kuleta suluhisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika WMA nydingi tunapokusanya mapato ya utalii, fedha hizo ambazo hugawanywa kwenda Taifa, Halmashauri na vijiji husika WMA huenda baada ya kukusanya katika WMA zetu na kupelekwa hadi Taifa, baada ya hapo hurudishwa chini tena. Tunaomba zile za Halmashauri na WMA zibadilishwe na gawio la Taifa ndiyo pekee liende.

Tatu, leo ni mwaka wa tatu, kifuta jasho na kifuta machozi wananchi wa Babati hawajalipwa pamoja na kufuatilia Wizarani mara kadhaa nikiwa na Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Halmashauri hadi leo shilingi milioni 12 tu kati ya hizo zimelipwa. Nashauri badala ya Wizara kuitia kitengo cha wanyamapori kulipa hizo gharama za kufuta machozi na vifuta jasho, hifadhi husika mfano, TANAPA, Ngorongoro Conservation Authority ndiyo walipe. Tubadilishe sheria yetu ili malipo haya yaende kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, naomba miradi ya kusaidia vijiji vinavyopakana na hifadhi zetu mfano, TANAPA, NCA, KINAPA ziwe zaidi ya kulenga mtu mmoja mmoja katika miradi ya kuwaongezea mapato. Wakiwa na uchumi mzuri basi wao wataweza miradi ya sasa kwa mfano, ujenzi wa madarasa, mabweni, zahanati na wataalam wamenufaika moja kwa moja, watu kuwa walini wazuri na watetezi wa hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, tunashauri matokeo ya Tume ya Kimahakama au Kijiji kufuatilia suala la mauaji ya Operesheni Tokomeza yatolewe mapema. Imani ya wananchi kuwa sheria itachukua mkondo wake na haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, tunaomba suala la vijiji vya Ayamango, Gedemas na Gidejabung, Wilayani Babati sasa vipatiwe ufumbuzi wa kudumu. Wananchi walipewa ardhi hiyo kisheria na baadaye kujikuta wako ndani ya Hifadhi ya Tarangire. Aidha, walipwe fidia ya ardhi, wapewe fedha ili wajitafutie ardhi wenyewe. Wapatiwe ardhi mbadala na kama haiwezekani wapewe hiyo ardhi yao waliyotumia miaka zaidi ya 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, eneo la Tarangire na vijiji vya Ayamango, Gedemas na Gedejabung wapewe wafugaji kwa malisho kwa mkataba maalum. Miundombinu ya joshu na malambo yawekwe, idadi maalum ya mifugo iruhusiwe hapo (*carrying capacity*) na wachunge kwa miezi sita, Januari hadi Juni na kutoka Julai hadi Disemba mifugo irudi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, eneo la kisheria la Burunge Game Controlled Area na zingine kama hizo zifanyiwe marekebisho yanayoendana na wakati. Leo hii kuna vijiji na mijji mingi kutoka Manyoni, Minjingu, Mdorie, Magugu, Mamire, Galapo, Kash hadi maeneo ya Kondoa yapo humo, kisheria imekaa vibaya na itaweza kuleta athari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, *Tanzania Forest Service Agency* inakusanya mapato mengi yanayotokana na maliasili ya misitu, magogo, mkaa, mbao, nta, asali na kadhalika. Kwa mwaka takribani bilioni 45 hadi bilioni 50, lakini hakuna fedha hata kidogo inayoenda kupanda miti na kurudishiwa pale palipovunwa. Nashauri asilimia 30 ya mapato hayo yaende kwenye Mfuko wa Taifa wa Mazingira ili itumike kupanda miti, kuboresha upatikanaji wa mbegu za miti mbalimbali na utoaji wa elimu kwa jamii. Taasisi ya Taifa ya Miti (*National Tree Centre*) pia wana hali mbaya kifedha hii michango itaweza kusaidia kueneza elimu na mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi, nashauri uwindaji wa kitalii upigwe marufuku kwa muda angalau miaka kumi ili wanyamaporu wetu waweze kurudi kama zamani. Nashauri hadi kwenye zana na vifaa vya ufugaji wa nyuki na kusindika asali iondolewe ili kukuza sekta hii na kupata viwango vizuri (*quality*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi na mbili, tozo mpya ya maliasili kwenye vinyago katika viwanja vya ndege iondolewe.

**MHE. ZAINABU MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ni sekta muhimu sana kwani inaleta pato kubwa kwa Taifa letu. Hivyo ni sekta ya kuthaminiwa sana na siyo ya kudharauliwa kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali ibadili utaratibu uliopo kwa utoaji wa leseni kwa wafanyabiashara wanaosafirisha watalii kwa kuondoa sharti la umiliki wa magari matano ndipo wapewe leseni ya kufanya biashara hiyo. Kiwango hiki kipunguzwe angalau yawe mawili au moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vivutio vingi tulivyonavyo vya watalii ni lazima pia kuwe na matangazo ambayo pia yatawavutia watalii, vinapotangazwa vivutio ndiyo watalii watakuja. Hivyo ni lazima tuwe na mpango madhubuti na bajeti ya kutosha ya kufanya matangazo ya vivutio vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia jambo lingine ni miundombinu imara husaidia na ni kivutio pia cha watalii kwani unapokuwa na miundombinu mizuri kunawafanya watalii wafike eneo hilo kwa urahisi bila ya machovu na kuweza kufurahia safari aliyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia viwanja vya ndege viimarishwe ili watalii waweze kufikia vivutio hivyo kwa wepesi zaidi. Jambo lingine ni malazi mazuri yenyenye mvuto na sehemu nzuri za kujenga hoteli hizo ambazo watalii zitawavutia. Ni vema Serikali kuzingatia pia maoni ya wananchi. Vilevile kuwa na kanuni zinazowabana watalii ambazo zingeleta madhara kwa wanajamii na kizazi chetu. Kwa mfano, kuwe na maadili ya kuzingatia kama vile uvaaji wa mavazi yasiwe yanakihirisha, yawe ya heshima. Kushirikisha watu au wananchi vilivyo kufuata silka na mila au tamaduni husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu watoto wetu ni wenye kuiga sana mambo, watoto wengine wameharibika na kuwa hawana maadili hasa sehemu nyingi za fukwe na zenye hoteli kubwa, maadili yameporomoka kwa kuona wanayofanya. Watoto wengi huacha shule ili tu wapate ajira ya kutembeza watalii maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Serikali iyaone haya na kuyafanyia kazi ipasavyo. Naomba kuwasilisha.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vivutio Wilaya ya Rungwe; Wilaya ya Rungwe ina vivutio vingi sana ikiwepo Ziwa Ngozi, Mlima Rungwe, Daraja la Mungu, Kijungu na vivutio vingine vingi sana. Tatizo Wizara haijasaidia kutengeneza miundombinu ya kuwezesha watu kuja kutembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Ngozi limeachwa chafu na kutoa tozo ndogo ambayo haiwezi kuleta maendeleo yoyote. Halmashauri zetu hazina pesa ya kuwezesha kutangaza vivutio hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misitu; Wilaya ya Rungwe tuna misitu ya kienyeji ambayo kiuchumi haina faida kwa wananchi wa kawaida. Vyura wa Kihansi tunaomba vyura hawa warudi Tanzania na nchi ya Marekani ilipe gharama kwa kukaa nao kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachina na meno ya tembo; kumekuwa na wimbi la Wachina hapa nchini wakikutwa na nyara za Serikali hasa meno ya tembo, swali langu Serikali inachuakua hatua gani ya kisheria kwa wananchi hawa, je, toka wameanza wamekamatwa wangapi na wamefungwa miaka mingapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upandaji miti na nyuki ninaomba Wizara chini ya kitengo cha upandaji miti kunisaidia miche ya kupanda kwa makundi ya vijana, katika Wilaya ya Rungwe na Mkoa wote wa Mbeya. Pia mgogoro wa wafugaji Wilayani Mbarali, je, Serikali itaumaliza lini?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mchango wangu nianze katika sekta ya utalii. Juhudi ya Serikali katika kutengeneza vivutio vya utalii bado siyo wa kuridhisha kwani kuna vivutio vingi bado hatujaweza kuvitambua na kuvitangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malikale, ukanda wa Kusini kuna vivutio vya malikale kama vile Boma la Mdachi (Wajerumani) lililojengwa miaka ya 1904 -1907 wakati wa vita vya Majimaji Mjini Liwale. Ndani ya boma hili kuna mabaki ya sanamu na michoro ya watumwa kwa ajili ya biashara ya utumwa.

Vilevile katika ukanda wa Liwale kuna milima ya Rondo yenyе misitu na vipepeo ambao hawapatikani popote duniani. Tunayo pia bwawa la Mlembe na Kiulumila. Haya ni mabwawa yenyе mamba na viboko wenye kuwasiliana na wazee wa mila zetu.

Kuhusu ulinzi wa misitu yetu siyo wa kuridhisha. Kuna Mamlaka ya Uvunaji wa Mali ya Misitu (TFS). Taasisi hii imekuwa kero kubwa kwa watu wanaokaa karibu na hifadhi zetu. Badala ya kuwa na wastawishaji wa misitu wamekuwa waharibifu wakubwa wa misitu yetu. TFS wanatuhumiwa kila mahali kuwa wao ndiyo waharibifu wakubwa wa misitu yetu. Kazi kubwa inayofanywa na watu hawa ni kugonga mihuri tu na kusafirisha mazao ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya mipaka, kumekuwa na migogoro mingi ya mipaka kati ya hifadhi zetu na wanavijiji. Hali hii huchangiwa sana na watendaji wa hifadhi kusogeza mipaka bila kushirikisha jamii husika. Mfano mgogoro wa kijiji cha Kikufungu Wilayani Liwale uliosababishwa na wahifadhi kuhamisha mpaka wa hifadhi bila kushirikisha jamii. Mgogoro huu una zaidi ya miaka kumi sasa. Hadi sasa zaidi ya watu wanne wamepoteza maisha na kuharibu kabisa mahusiano ya askari wa hifadhi na wanakijiji. Aidha, kijiji cha Ndapata wako watu wawili wamepoteza maisha kwa sababu ya mgogoro huu wa mipaka.

Kijiji cha Kichonda Mwenyekiti wa Kitongoji mwezi wa 8 mwaka 2015 amekatwa mikono na askari wa wanyamaporи hadi leo hakuna kesi wala fidia juu ya kadhia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Lindi sehemu kubwa ni sehemu ya Selous lakini kwa masikitiko makubwa Mkoa huu hauna manufaa yoyote na Selous. Mkoa wa Lindi hasa Wilaya ya Liwale hakuna hoteli ya kitalii Mkoa wa

Lindi pia kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Lindi hakijapanuliwa na kuwa na hadhi ya kuwezesha ndege kubwa kutua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Nangurukuru - Liwale ndiyo barabara ingewapeleka watalii kwenye hifadhi hiyo. Kanda ya Kusini haina Chuo cha Misitu Kanda nzima. Eneo kubwa la Hifadhi ya Selous ipo Mkoa wa Lindi Wilaya ya Liwale. Kuhusu ulinzi shirikishi, Serikali imeweza sana kwenye ulinzi wa silaha na mabavu kama njia pekee ya kulinda hifadhi zetu, jambo ambalo halina tija kubwa zaidi ya kuongeza uhasama baina ya wahifadhi na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika hili Serikali ijikite zaidi katika kutoa elimu juu ya ulinzi shirikishi sambamba na kuwaonyesha wananchi faida itokanayo na hifadhi zetu. Kwa mimi nadhani walinzi wa kwanza wawe wale watu wanaozungukwa na hifadhi husika badala ya kutumia silaha zaidi na kuendelea kuua watu na kuongeza uhasama. Mkoa wa Lindi hatujaona faida ya moja kwa moja inayotokana na hifadhi ya Selous zaidi ya kushuhudia mauaji.

Kuhusu uhaba wa watumishi na vitendea kazi, kwa Wilaya ya Liwale uhaba wa watumishi wa wanyamapori kumesababisha hasara kubwa sana kutokana na wanyama kuharibu mashamba ya wakulima. Ukienda kutoa taarifa watakujibu hawana gari au watumishi wa kwenda kuwasaidia watu hao wa vijiji vya Mpigamiti, Barikiwa, Kimambi, Kikulyungu na Ndapata wanakabiliwa na njaa mara kwa mara kutokana na mazao yao kuliwa au kuharibiwa na wanyama kama tembo na nguruwe. Nguruwe wamekuwa ni tishio kubwa sana kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la watu kuliwa na simba Wilayani Liwale ni kubwa sana hasa baada ya watu kunyang'anya silaha zao kwenye Operesheni Tokomeza. Wizara ifikirie namna bora ya kuanza kurudishiwa silaha watu wale ili zisaidie kuimarisha ulinzi vijijini hasa zile silaha ndogo. Naomba kuwasilisha.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya mipaka na shughuli za kibinadamu ndani ya hifadhi za wanyamapori, sababu za mifugo kuingia kwenye hifadhi husababishwa na viongozi na watumishi wa maliasili kwa kuwanyang'anya maeneo yao kuwa maeneo ya hifadhi bila kuwafidia maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzisha mapori tengefu, mapori ya akiba na ushoroba maeneo hayo yote ni vijiji vilivyopimwa kwa ajili ya wananchi wanaopakana na hifadhi. Bila kuwa na utaratibu unaoeleweka kwa Wizara ya Ardhi, Maliasili, Kilimo na Mifugo, TAMISEMI na Wizara ya Maji kamwe hamtapata suluhisho la wafugaji na wakulima wanaozunguka hifadhi. Nashauri kuwa na kikao cha pamoja kutafuta suluhisho la kupatikana kwa ardhi ni kuwa

na mpango wa kupatikana maeneo ya wafugaji na wakulima siyo kazi ya kuwakamata na kuwaua wao na mifugo yao. Topeni mpango wa kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria Namba Tano ya mwaka 2009 (Sura 283), Sheria hii inazungumzia upande mmoja wa hifadhi. Je, maeneo miliyoongeza kwa kuwaghilibu viongozi wa vijiji kwa kutumia viongozi wa Wilaya na Mkoa, inawagusa wapi?

Sheria hii inawanyanyasa wafugaji kwa kuwanufaisha viongozi wa Wilaya na Kamati zao za usalama na mikoa kwa kulazimisha kutolewa rushwa au kukandamiza wafugaji kulipa faini. Hii mifano imefanyika Tarangire katika vijiji vya Ayamango, Galapo, Mkungunero, Sangasanga, Lulenge, Pori la Wamimbiki, Utengule huko Kilombero North Safari na kadhalika. Hii sheria ifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha za kuudhi, kauli aliyoitoa Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Jumanne Maghembe katika mahojiano yaliyofanyika katika vipindi vya ITV dakika 45 ni lugha ya maudhi na dharau kwa wafugaji.

(a) Mapato yatolewayo na Maliasili na Utalii ni asilimia 22.5 huwezi kufananisha na mifugo ambayo hutoa mapato ya kiasi cha asilimia 4.5 akifananisha kuwa ukiwa na shilingi nne na ukiwa na shilingi 22 utachukua shilingi ngapi? Hiyo ni dharau, je, ng'ombe wanaochinjwa Tanzania haijachangia kutokuagiza nyama kutoka nje? Hiyo siyo dola?

(b) Wafugaji hukaa nyuma ya mikia ya ng'ombe zao tu, je Waziri alitakaje? Kuna style nyingine za kufuga ng'ombe?

(c) Ng'ombe wote walioko mipakani mwa hifadhi wana magonjwa kama kimeta, homa ya mapafu na kadhalika, hivyo nyama zao hazifai kwa kuliwa. Je, Waziri anaweza kutoa ushahidi wa magonjwa hayo kwa mifugo yote inayochinjwa?

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuwepo leo na kuchangia hotuba ya Wizara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Naibu Waziri Mheshimiwa Ramo Makani na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kubwa na ombi langu kwa Wizara hii ni kwamba naomba Wizara inipe majibu ni lini itaweka utaratibu wa kuzuia wananchi ambaa hupata kipato chao kupitia uvuvi kwenye bwawa/mabwawa yaliyopo Selous, lakini Serikali imezuia na hata kufikia kuwaua. Hili ni tatizo naomba ufanuzi.

Pia Mkoa wa Pwani kumezungukwa na misitu hivyo kwa wale ambao wanafanya biashara ya mbao (kutengeneza samani) hutozwa ushuru mkubwa wa shilingi 120,000 hata kama kitanda au samani ishatumika zaidi ya miaka 20. Naomba kauli ya Serikali lini itapunguza ushuru huo wa samani na mkaa? Naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu iliyopo Mkoa wa Pwani mingi imebaki vichaka kwa kuwa hakuna usimamizi mzuri na kupelekea ukataji hovyo wa miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mkuranga eneo la Mwandege kuna msitu ambao kwa neno msitu kwa sasa si sahihi kwani ni kichaka na kuficha wahalifu wengi, naiomba Serikali itoe maelekezo au kubadili matumizi ya eneo hilo ili kupendezesha eneo hilo, laa kama hiyo haiwezekani basi uwepo upandaji upya wa miti na ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya Serikali na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kuweza kuchangia hotuba hii kwa maandishi pia naiunga mkono na kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) katika kuunga mkono jitihada za Serikali za kutoa elimu bure kwa kuchangia madawati katika Wilaya zinazopakana na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua na kuthamini uhifadhi wa wanyamapor na faida yake kwa Taifa ambapo unachangia 25% ya Pato la Taifa katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapaswa iendelee kutoa elimu katika jamii inayoishi karibu na hifadhi na wananchi waone/wapate faida kutokana na hifadhi. Wawekezaji wamekuwa wakitoa michango ya maendeleo katika Pori la Akiba la Makao lakini mazingira yanaonesha wananchi hawaelewi mwekezaji anatoa kiasi gani cha fidia, ipo haja taarifa ya mapato na matumizi yasomwe katika vijiji vinavyounda Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapor (WMA) ili wananchi wasiendelee kumchukia mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mgogoro wa wananchi na mwekezaji wa Mwiba Holding Company katika Pori la Makao na magazeti yamekuwa yakiandika habari mbalimbali kutoka pori hilo lililopo Wilaya ya Meatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huo ukiuangalia kwa nje kuna mgongano wa maslahi hivyo kuendelea kuiathiri Wilaya ya Meatu. Mimi nikiwa Mbunge Viti Maalum kutoka Mkoa wa Simiyu na ninayehudumia Halmashauri ya Wilaya ya Meatu nilifika kuongea na wananchi (viongozi) wa kijiji cha Makao mgogoro huo unazungumzika pia zipo sheria za nchi zinaweza kutumika.

Naiomba Serikali itoe tamko kuhusu mwekezaji Mwiba Holding Company ili wananchi wa Wilaya ya Meatu waweze kupata msimamo kuhusu mwekezaji katikati ya mwezi Aprili, 2016 wakati wa kikao cha wadau wa maendeleo ya Wilaya. Baraza la Madiwani lilihindwa kupokea ahadi ya mchango katika mfuko wa maendeleo kwa kuwa bado kuna mgogoro. Serikali itakapotoa suluhu itasaidia sasa kama Wilaya kuweza kushirikiana katika shughuli za maendeleo na pia kuweza kushirikiana katika shughuli za maendeleo na pia wananchi wakazi wa Wilaya ya Meatu walioajiriwa na Mwiba Holding Company waweze kujua hatma ya ajira zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara ya Maliasili na Utalii kuharakisha mchakato wa matumizi bora ya ardi ndani ya hifadhi ili wananchi waweze kulima na kuchunga mifugo. Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu mwaka 2015 aliahidi wananchi akiwa Jimbo la Meatu kuwa tatizo hilo la malisho litapatiwa suluhisho.

Pia niishauri Serikali kutokana na ongezeko la mifugo na wananchi, athari ya mabadiliko ya tabia ya nchi maeneo mengi katika Mkoa wa Simiyu yamekuwa makame kwa kipindi kirefu hivyo Serikali iangalie upya mipaka ya hifadhi katika Wilaya ya Bariadi, Busega, Itilima na Meatu ili kupata suluhu ya migogoro ya wafugaji na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kifuta machozi/fidia; kumekuwepo na tatizo la wanyama pori kuwaua wananchi mfano; mtoto Malangwa Kasenge mwenye umri wa miaka tisa wa Kijiji cha Mwaikoli, Wilayani Meatu aliuawa kwa kuliwa na fisi mnamo tarehe 03/05/2013 lakini hadi leo familia haijalipwa kifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo uharibifu wa mazao mashambani kutokana na tembo na nyati katika maeneo tofauti na wakati tofauti katika Wilaya ya Meatu na yamefanyiwa tathimini lakini hadi leo wananchi hawajalipwa fidia au kifuta machozi na sijaona katika bajeti ya Wizara ya Fedha imetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathimini ilifanyika kwa kuzingatia Sheria Uhifadhi wa Wanyamapor Namba Tano ya mwaka 2009 (*The Wildlife Conservation Act, No. 5 of 2009*) na kanuni yake (*The Wildlife Conservation rates of Consolation Payment*). Hivyo naiomba Serikali ifanye fidia kwa wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inapaswa irejeshe asilimia 25 ya uwindaji wa kitalii ya mapato katika Halmashauri, lakini marejesho haya yamekuwa ni ya kusuasua pia yamekuwa yakinofautiana mwaka hadi mwaka, naiomba Serikali yafuatayo:-

Kwanza Halmashauri ijue ni kiasi gani kinapatikana kutoka katika hifadhi inayoizunguka Wilaya ili kuweza kujua stahili zao na pili, Serikali irejeshe kikamilifu asilimia 25 ya uwindaji wa kitalii katika Halmashauri. Naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la wafugaji na wakulima na hifadhi zetu. Tatizo hili ni kubwa sana katika nchi yetu na kama hatua za dharura hazitachukuliwa tutapeleka nchi yetu kwenye umwagaji damu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hayo baada ya kusikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge humu ukumbini. Jana michango hiyo inaligawa Taifa letu katika makundi makubwa ambao wote ni Watanzania. Mimi niiombe Serikali ichukue hatua za haraka kukaa na Wizara zake TAMISEMI, Ardhi na Maliasili kupanga maeneo kwa ajili ya wafugaji na wakulima, hii itaondoa tatizo hili kubwa, tumechoka kuona damu za Watanzania zikimwagika kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunakumbuka Operesheni Tokomeza iliyofanyika katika nchi yetu na madhara yaliyopatikana katika zoezi hilo. Serikali iliunda Tume ili kuchunguza athari na Tume hii imemaliza kazi yake, je, ni lini taarifa hiyo itatoka ili Bunge lako lipate kujua Tume imebuni nini. Lakini pia liko suala la fidia kwa wananchi walioathirika katika operesheni hiyo, je, ni lini sasa fidia hiyo itatoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuishauri Wizara kutoa elimu kwa wananchi ili wajue umuhimu wa hifadhi zetu. Naamini elimu ikitolewa wananchi wetu wataelewa na watakuwa walinzi katika hifadhi zinazozunguka. Pia nitoe ushauri mwingine ili kuondoa tatizo la mipaka na vijiji vinavyozunguka hifadhi zetu ni muhimu sana wataalam wetu wanapokwenda huko kwenye maeneo washirikishe wananchi hii itaondoa migogoro iliyopo huko nimesema hayo kwa sababu wananchi wanalamika hawashirikishwi wakati wao ni wenyeji wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lililopita tulijadili sana suala la Halmashauri zinazozunguka Mlima Kilimanjaro ambao wananchi wake pale ambapo likitokea tatizo hao ndiyo wandakuwa wa kwanza kushirikiana na hifadhi kutatua tatizo hilo. Sasa ningependa kujua ni lini Halmashauri hizo zitaanza kupokea mrabaha unaotokana na mapato ya mlima huo mzuri na wa kwanza Afrika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo mchango wangu kwa leo naomba kuwasilisha.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa mkakati madhubuti (*strategic plan*) wa kutangaza rasilimali na vivutio vyetu kunasababisha nchi nyingine kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri mwenye Wizara husika wakati atakapokuja kuhitimisha hoja aje na mpango mkakati unaoelekeza kutoa fursa kwa taasisi au watu wenyewe uwezo ili waweze kutangaza vivutio na rasilimali zetu kimkakati zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwa ni vigumu sana kuona ujangili katika nchi yetu unakuwa kwa kasi wakati kuna watumishi walioajiriwa kwa kazi ya kulinda wanyama, hata pembe za ndovu zikikamatwa mwisho wake zinapopelekwa hakujulikani, hata mrejesho wowote katika Bunge hili Tukufu ili kupata taarifa yoyote endelevu juu ya kesi endapo watuhumiwa wameshinda kesi wananchi kinyemela. Hii ndiyo sababu kubwa inayokuza kazi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali isione vigumu kutoa taarifa muhimu kama hiyo katika Bunge lako Tukufu tena taarifa hizi zinapotolewa jina la mtuhumiwa litajwe kufanya hivyo hivyo ujangili utapungua.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata majibu kuhusu suala la mjis (mabaki yake) ambayo yalichukuliwa Tendegu katika Jimbo la Mchinga na kupelekwa Ujeruman, naomba kupata majibu ya hoja zangu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inanufaika na nini kutokana na mjis huyo kuhifadhiwa huko. Mheshimiwa Waziri hii hauoni kwamba suala hili linatuletea fedheha kubwa Watanzania kwa kuonekana kwamba hatujali na kuthamini rasilimali na maliasili za nchi yetu? Kwa nini rasilimali kubwa na ya kihistoria kama hii imebaki Ujeruman bila sisi kama Taifa kunufaika kwa chochote? Kumekuwa na kauli tata kuhusu manufaa ya mjis huyu kutokana na suala hili pia kuihusisha Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANGELAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana Wizara iongeze wigo wa utalii kwani sekta hii ni sekta muhimu yenyе mchango mkubwa katika Pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Makumbusho ya Taifa, taasisi hii ikiendelezwa na kusimamiwa vizuri ikaboreshwa zaidi inaweza nayo ikatoa mchango wake. Pale katika Kijiji cha Makumbusho (*Millennium Towers*) eneo ni kubwa, lingeweza kutengenezwa na kuendelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze kwa namna tao la Mashariki (milima) inavyolindwa. Ombi langu endeleeni kuangalia milima hiyo ikiwemo Msitu wa Shengena. Naunga mkono hoja.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kunipa uzima na afya njema, na leo naomba nichangie hoja hii ya maliasili na utalii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mikindani upo Manispaa ya Mtwara Mikindani ambalo ni jimbo langu. Mji huu ni mji wa asili ambaa una magofu na vivutio vingi vya utalii ikiwemo Old Boma ambayo ilijengwa na Mjerumani kama ngome yake kuu ya ulinzi karne ya 19. Cha ajabu, mji huu umesahaulika, umeachwa na jambo la ajabu kabisa yanatangazwa maeneo ambayo hayana vivutio kama Mikindani. Namuomba Waziri aje na majibu juu ya kuutangaza mji huu kuwa ni mji wa kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara kuna fukwe nyngi nzuri sana ambazo kama Serikali ikitangaza watalii wengi wanaweza kuja Mtwara na hatimaye Taifa hili kupata kipato kikubwa kupitia sekta hii. Nimeuliza swali la utalii Mtwara tangu kipindi cha Kikao cha Kwanza katika Bunge lako hili mpaka leo sijapata majibu. Namtaka Waziri akija anieleze, yupo tayari hivi sasa kutangaza fukwe za Mtwara sambamba na kuzitambua katika Wizara yake kuwa kitovu kikuu cha utalii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msimbati, Mnazibay kuna fukwe ambayo haipo duniani na kuna maua ambayo hayapo na hayaoti popote duniani isipokuwa Mnazibay tu. Nimuombe Waziri aje Mtwara nifuatane naye kama Mbunge, na asije kimya kimya ili nimuoneshe vivutio hivi vya utalii Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Lindi eneo la Mipingo, Kata ya Nangaru alichukuliwa mjesi na Wajerumani ambaye mabaki yake yapo Ujerumani. Tangu mwaka 1907 mpaka leo Wajerumani wanapata pesa nyngi kupitia mjesi huyu

mkubwa kuliko mijusi yote duniani. Serikali hii ya CCM ni lini itaenda kumrudisha mijusi huyu na kumleta Tanzania ili tunufaike na pesa za utalii?

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuanza kwa kuunga mkono hoja. Pili, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Waziri Profesa Jumanne Maghembe na Naibu wake *Engineer Ramo Makani* kwa hotuba nzuri na yenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishauri Serikali sikuvi ya CCM kutanua wigo wa vivutio vya utalii kwa muda mrefu kumejengeka dhana kuwa utalii maana yake ni mbuga za wanyama na maeneo ya fukwe peke yake. Dhana hii si sahihi, kwani utalii una wigo mpana zaidi. Kwa mfano katika jimbo langu la Mafia (Kisiwa) kuna samaki aina ya papa mkubwa sana anaitwa Mhaleshark (*Potwe*) ni one of the species of shark, papa huyu ni adimu sana duniani, kwa sasa anapatikana Australia na Mafia tu dunia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Australia ni gherama kubwa kwa mtalii kwenda kumuona samaki huyo na moja ya sifa za whaleshark ni papa rafiki ana tabia zinazofanana na *dolphin* (pombuwe) mtalii anaweza kuogolea naye bila ya kupata madhara yoyote ile. Hivyo mtalii Australia anatumia gherama kubwa ikiwa ni pamoja na kukodi helikopta kwenda maeneo ya mbali sana kuogolea na papa. Lakini kwa upande wa Mafia papa huyu anaonekana umbali usiozidi mita 300 kutoka bandari kuu ya Kilindini Mafia. Ombi letu wana Mafia Serikali kuititia Bodi ya Utalii itsaidie kuutangazia ulimwengu upatikanaji na papa huyo ili kuongeza watalii wengi Mafia sambamba na maboresho ya hoteli zetu za kitalii na miundombinu ya kuingia na kutoka Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni uvunaji wa mikoko katika Kisiwa cha Mafia mwekezaji Tanspesca amewekeza kiwanda cha kamba katika kijiji cha Jimbo na kupewa kibali na Wizara ya Utalii kukata baadhi ya mikoko. Tunaiomba Wizara sehemu ya mapato yatokanayo na kukatwe kwa mikoko hiyo ibaki katika Halmashauri ili kuweza kusaidia shughuli za uhifadhi katika Kisiwa cha Mafia ikiwemo kupanda mikoko mingine kufidia ile iliyokatawa.

Suala lingine ni kukosekana kwa Afisa Utalii katika Wilaya ya Mafia. Pamoja na potential kubwa ya utalii katika Wilaya ya Mafia bado mpaka sasa hatuna Afisa wa Utalii wa kuratibu shughuli za utalii kisiwani Mafia, tunaomba Wizara kulifanya kazi jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyininge nawashukuru Waziri na timu yake yote na naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini naomba niwashauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha na kustawisha Wizara ambayo ni nyeti katika kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri sana inayofanywa na Mheshimiwa Waziri na viongozi wenzako nashauri kuchukua mapendekezo mazuri yaliyotolewa na Kamati pamoja na ushauri mzuri unaotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa mustakabali wa nchi.

Pia katika kutatua migogoro ndani ya hifadhi Waziri kupitia wataalam wake watatue migogoro kwa kuzingatia hekima, busara na taratibu za kisheria zilizopo, wasitumie mabavu, tunajua sheria zipo lakini tatizo ni ushirikishwaji hafifu au elimu duni ya uhifadhi ikichangiwa na rushwa.

Mheshimiwa Waziri, Shirika la Hifadhi za Taifa linalosimamia Hifadhi za Taifa 16 hadi leo halina bodi kwa mujibu wa Sheria Sura 282 ya mwaka 2002 na kama ilivyorejewa kwa Sheria ya Hifadhi za Taifa ya mwaka 1959 Sehemu ya II inayoanzisha Hifadhi ya Taifa na Bodi ya Wadhamini. Nashauri kufuatana na uzito na umuhimu wa taasisi hii Waziri umwombe Mheshimiwa Rais atue Mwenyekiti wa Bodi na wewe uteue Wajumbe wa Bodi haingii akilini taasisi kubwa kama hii kukaa miaka zaidi ya minne bila Bodi ya Wadhamini.

Naomba niulize, TANAPA kutokuwa na bodi ni nani anaamua maamuzi ambayo uamuzi wake unatakiwa uamuliwe na bodi. Mheshimiwa Waziri Chuo cha Mweka nikiwa Mjumbe wa Bodi kwa wakati huo Rais wa Awamu ya Nne alitamka kwa kumwambia Waziri wa wakati huo Mheshimiwa Mwangunga kuwa chuo hicho kiwe chuo cha mfano (center of excellence) lakini hayo hatuyaoni, kumbuka chuo hicho ndicho kiwanda cha kuzalisha wataalamu katika tasnia ya wanyamapori hasa katika hifadhi zetu zote nchini. Nashauri chuo hicho pamoja na kile cha Pasiansi visimamiwe vizuri ili kutoa wataalam na askari wanaoweza kwenda kusimamia vizuri maeneo ya uhifadhi.

Nimalize kwa kuwaomba viongozi wote walio chini ya Wizara hii kumsaidia Waziri ili yaliyoainishwa ndani ya kitabu hiki yaweze kutekelezwa. Lakini kwa pekee nimpongeze CEO wa TANAPA kwa kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa pamoja na kutokuwa na Bodi ya Wadhamini.

Mheshimiwa Waziri moja ya changamoto kubwa ni kutopata takwimu sahihi za watalii hasa katika eneo la Selous, Serikali iangaie njia nzuri zaidi hasa kwa hawa wenye hoteli ziwe na takwimu sahihi ili kudhibiti mapato ya Serikali lakini kuwe na motisha kwa wafanyakazi na Selous iimarishe usimamizi kwa kila hoteli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika pori la akiba la Selous lina jumla ya kambi za kuweka wageni (camp sites) nane na zisizopewa wawekezaji hadi leo hawajaendeleza, nashauri wanyang'anywe ili wapewe wengine na kuendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya makazi, kilimo, ufugaji na matumizi endelevu nashauri kuainisha na kuhakiki mipaka ya mapori ya akiba kwa mujibu wa GN kupitia Wizara ya Ardhi, kutoa elimu ya uhifadhi na kufanya tathmini ya mapori tengefu. Pia nashauri kuzishirikisha Wizara na taasisi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Utalii (TTB) na TANAPA kwa pamoja na NCCA hawajaonyesha jitihada za kutangaza utalii nje na ndani ya nchi. Je, ni kwa nini taasisi hizo ikiwemo Bodi ya Utalii hawatilii mkazo suala zima la kutangaza na kuondoa vikwazo vinavyokwamisha watalii hasa wa Marekani na Wafaransa ili ile idadi ya watalii iongezeke na nchi ifaidike na utalii kwa kuongeza mapato zaidi.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nkasi na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla tuna pori la akiba la ukubwa wa kilometra za mraba za 6,462.26; pori la akiba la Rukwa ukumbwa wake kilometra 4,194 na pori la Rwamfi kilometra 2,228.26 hilo pori linahujumiwa sana na majangili yaani wawindaji haramu ni kwa kuwa hilo pori la akiba limepakana na nchi jirani inakuwa vigumu sana kwa wafanyakazi wa idara kwa sababu hawana magari ya doria. Niliahidiwa kupewa gari jipya na Waziri wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Nyalandu lakini mpaka leo sijapokea hilo gari kwa ajili ya kuokoa mali kwa ajili ya wanyama na miti. Tafadhali hilo gari ni muhimu kwa doria na pia kwa upande wa Ziwa Tanganyika, kwa hiyo, usafiri wa majini ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ahadi ya aliyekuwa Waziri Mheshimiwa Nyalandu itekelezwe maana pori hilo la akiba linashambuliwa sana na wafugaji na majangili na wakata mbao. Naomba jibu kabla ya mwisho wa Bunge la bajeti kuhusu hilo gari maana ahadi ni deni na dawa ya deni ni kulipa, pori linaangamia sana sana.

Mheshimiwa Waziri gari jipya ni muhimu sana kwa ajili ya doria ya hilo pori.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nakupongeza kwa hotuba yako nzuri sana yenye ufanuzi wa masuala mbalimbali ya Wizara yako. Pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

- (i) Ufinyu wa bajeti katika Wizara hii na kusababisha kufanya Wizara kushindwa kutekeleza majukumu yake na hasa miradi mingi ya maendeleo kutojamili na kwa wakati. Fedha za miradi zitolewe za kutosha na kwa wakati.
- (ii) Serikali isitegemee sana fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kuwa hakuna uhakika kama fedha za nje zitaletwa zote au kidogo na kwa wakati gani. Fedha za ndani zitumike zaidi.
- (iii) Uhaba wa watumishi wa sekta ya maliasili na utalii na hasa katika Wilaya zetu hakuna Maafisa Misitu, magari, pikipiki na baiskeli na maslahi duni.
- (iv) Je, sababu gani zinazofanya idadi ya watalii kupungua?
- (v) Je, ni sababu gani zinazofanya Wizara ya Maliasili na Utalii kushindwa kabisa kukabiliana na ujangili na kusababisha wanyama kama tembo, vifaru wanaoendelea kupungua katika mbuga zetu, je, hakuna mbinu za kisasa za kukabiliana na majangili kwa kuwa wanaongezeka siku hadi siku.
- (vi) Serikali iijitahidi kuboresha huduma kwa watalii kama hoteli, afya, barabara na ulinzi wa watalii na viwanja vyatete.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nachukua fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Maliasili Utalii Profesa Maghembe, Naibu wake Engineer Ramo Makani kwa kazi nzuri sana wanayofanya kwa Wizara hii, kumbukeni methali ile isemayo mti wenye matunda hauishi kutupiwa mawe. Hata hivyo mmeweza na tunawataki kazi njema na ya ufanisi kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo hoja zangu kadhaa ambazo naomba mnapo-wind up mnipatie majibu.

- (i) Burunge Game Control Area iliyoko Makuyuni na Babati Vijiji ni eneo kubwa sana igawanywe ili ibakie sehemu ndogo tu na nyingine irudishiwe wananchi na hivyo sheria iliyoko ibadilishwe kuruhusu mapendekezo hayo.
- (ii) WMA iliyoko eneo la Vilima Vitatu Babati ni mateso makubwa kwa wafugaji walioko eneo lile, kiasilia eneo hilo lilikuwa la wafugaji na hata baada ya kushtakiana na WMA wafugaji walishindwa kesi. Hadi leo wananchi hao hawajapewa haki yao, naomba Wizara ilishughulikie suala hili kuwapa wananchi wa Vilima Vitatu utulivu wa maisha na usalama wa maisha yao na mifugo yao. Naomba kauli ya Wizara.;
- (iii) Vijiji 16 vinavyozunguka hifadhi ya Tarangire na Magugu walipoondolewa waliambiwa watapewa kifuta jasho hadi leo kati ya fedha walizoahidiwa

Tanzania zaidi ya shilingi milioni 100 wamepewa shilingi milioni 12 tu. Huu ni unyanyasaji wa wananchi. Naomba msaada wako Professa na naomba kauli ya Serikali.

(iv) Wananchi wanaozunguka Hifadhi za Ayamango, Gedamar na Gijgedabonga – Babati wako pale tangu Operesheni Vijiji, leo na kwa muda mrefu ndani ya hifadhi isitoshe wengi wao hawajaonyeshwa maeneo ya kuhamia kila mara ni mapambano na askari na wanyamapori. Mheshimiwa Profesa na Engineer (Wizara) naomba sana mtoe suluhu ya migogoro hii, fidia wanayopewa haijengi hata choo.

(v) Wakati wa Operesheni Tokomeza aliuwawa mwanamke kwa maelezo yaliyotolewa hata hapa Bungeni na kwenye vyombo vya habari, Serikali iliunda Tume ya Kijiji na hadi leo hii hakuna taarifa yoyote iliyotolewa na Serikali. Mheshimiwa Jitu amewaandikia barua bila majibu yoyote, naiomba Wizara itoe kauli juu ya jambo hili linalosubiriwa na wananchi wa Babati na Mkoa wa Manyara.

(vi) Halmashauri ya Wilaya zinazopaswa kupata asilimia 0.3 ya service levy za hoteli za kitalii zinazopaswa kulipa Halmashauri lakini hoteli zimegoma kulipa kiasi hicho mpaka Mahakama ya Rufaa, lakini Wizara imekaa kimya. Tunaomba ufumbuzi wa malipo haya ya asilimia 0.3 service levy kwa Halmashauri husika hapa nchini ni imani yangu Mheshimiwa Waziri utatolea kauli.

(vii) *Tanzania Forest Service* wanakusanya ushuru mkubwa kutokana na mkaa wa magogo. Naiomba na naishauri Serikali kuwa taasisi hii irudishe kiasi fulani cha mauzo haya ili kuendeleza upandaji wa miti itafika mahali misitu itaisha.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika Wizara hii muhimu kwa kukuza uchumi wa nchi yetu. Msitu wa Shagayu uliopo Wilaya ya Lushoto uliungua mwaka 2012 ambapo hekta 49 ziliungua hata hivyo mpaka sasa ni hekta 11 tu ambazo zimepandwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuungua kwa eneo la msitu huo lilsababishwa ardhi kutokuwa na vizuizi vya maji, hivyo mvua za mwaka 2015 zilisababisha maafa makubwa ya maporomoko na mafuriko katika maeneo yanayozunguka msitu huu. Mheshimiwa Waziri pamoja na eneo kubwa la msitu ambao unazungukwa na vijiji 15, lakini msitu una wafanyakazi wawili tu ilhali unazo nyumba za kutosha familia sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tunaomba Idara ya Misitu kuititia Wizara watuungezee watumishi wanne kufikia sita ili waweze kuhudumia vizuri eneo la msitu ikiwa ni pamoja na kuwapatia usafiri wa pikipiki kwani kwa sasa ipo pikipiki

moja tu. Tunaomba ziongezwe pikipiki mbili zaidi ili ziweze kuleta tija katika kuhudumia msitu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu inayozunguka maeneo ya msitu wa Shagayu sio rafiki, tunaomba Wizara kupitia Wakala wa Misitu ya Asili ili kuboresha miundmbinu hasa ya barabara ili isaidie kukabiliana na majanga hasa ya moto pale unapojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mbuga ya Mkomazi iliyopo katika Mikoa ya Tanga na Kilimanjaro, lakini Mlanga (lango) la kuingilia hifadhini lipo katika Wilaya ya Same, hivyo kuwasumbua watalii wanaotembelea Wilaya ya Lushoto na vivutio vyake kulazimika kwenda mpaka Same.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa na hususani Hifadhi ya Mkomazi kutuwekea mlango wa kuingia hifadhini kupitia Wilaya ya Lushoto katika Kata ya Lunguza, Kijiji cha Kiringo ili kukuza na kuchochea shughuli za utalii katika eneo hili la Tarafa ya Umba ili kusaidia kupunguza umaskini na kuchochea maendeleo ya watu wa Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi na ujirani bado unasuasua katika Hifadhi ya Mkomazi, hivyo kuweka mazingira hafifu ya ushirikiano baina ya hifadhi yetu na wananchi wa maeneo husika. Tunaiomba Wizara ihakikishe ile asilimia saba ya mapato yatokanayo na makusanyo ya hifadhi husika basi yaelekezwe kwenye vijiji na jamii inayozunguka hifadhi ili kuchochea shughuli za maendeleo na kupunguza uhasama baina ya hifadhi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi baina ya hifadhi zetu bado ni jambo linalosumbua sana hasa katika Kijiji cha Kiringo ambapo mpaka upo jirani sana na makazi ya watu hivyo kuleta misigano isiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Operesheni Tokomeza katika Wilaya ya Lushoto umeacha ardhi ya watu wakiwa na athari za kimwili, kiafya na kiuchumi. Silaha ambazo zimechukuliwa toka kwa wananchi waliopo jirani na hifadhi lakini hazikuhusika katika shughuli haramu za ujangili zirejeshwe kwa wamiliki halali ili waweze kujilinda kwa usalama wao kama walivyozionba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yetu kuwa uhifadhi wa misitu na mbuga zetu utaenda sambamba na ustawi wa jamii yetu ya Kitanzania kwa ajili ya vizazi vyaa sasa na vijavyo.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mgogoro katika Hifadhi ya Akiba ya Uwanda kutokana na ongezeko kubwa la watu waliopo katika vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi hiyo mipaka yake kutoeleweka, askari wanyama pori kutoza wafugaji fedha ili walische mifugo yao ndani ya hifadhi; kukodisha ardhi iliyomo ndani ya hifadhi ili wakulima waweze kulima; askari wa wanyama pori kuruhusu wananchi wasio na uwezo wa fedha walime mazao yao na mazao yakishakomaa hutumia ujeuri wa kupora mazao yao wanayauza na kuingiza fedha hizo mifukoni mwao; kuwanyang'anya pikipiki, baiskeli, majembe ya plau na majembe ya mkono, fyekeo, panga na kadhalika, jambo ambalo linahatarisha amani. Kama Serikali haitachukua hatua haraka ipo siku yatatokea mapigano kati ya askari hao na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi hiyo kwa sasa haina sifa, ni hasara tu kwa Serikali, inawanufaisha Askari tu. Hivyo kutokana na uhaba wa ardhi, nashauri, hifadhi hiyo ipunguzwe au kufutwa kabisa, wananchi wagawiwe ardhi hiyo waendeleze uchumi wao kwa kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze nini faida ya hifadhi hiyo kwa Serikali na kwa wananchi hadi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hifadhi ipunguzwe kama siyo kufutwa kabisa. Mipaka ijulikane, Serikali itoe misaada ya kuwajengea shule, zahanati na kuwapatia madawati ili kuwatia moyo wananchi. Pia nashauri Mheshimiwa Waziri atembelee eneo hili la hifadhi ili ajifunze na baadaye aweze kutoa uamuzi sahihi kuliko kusikiliza kwa mbali. Ahsante.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kumpongeza sana Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe na Naibu Waziri Mheshimiwa Engineer Ramo Makani, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara, Wakuu wa Mashirika na Taasisi zote zinazohusiana na Wizara hii. Baada ya pongezi hizo, naomba sasa kueleza yangu machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ni kati ya hifadhi chache zinazoingizia nchi yetu Tanzania pato kubwa sana la fedha za kigeni. Mlima huu unayo theluji kileleni ambayo inapungua siku hadi siku. Haya ni matokeo ya tabia nchi, lakini ukame unachangia sana. Hakuna mashaka kabisa kuwa ukame unaweza kupunguzwa kwa kuotesha miti maeneo

yanayozunguka mlima. Jambo hili linawezekana kabisa endapo wanakijiji watapatiwa miche.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalni lini Serikali itaagiza miche kwa wanavijiji hawa ili waoteshe kwa nguvu zote? Nitapenda kupata majibu wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mgao wa asilimia 25 wa mapato ya mlima kwa Halmashauri zinazozunguka mlima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ukerewe kama kisiwa inaweza kuwa chanzo kikubwa cha utalii endapo vyanzo kadhaa katika Wilaya hii vitawekwa sawa na kujengewa mazingira mazuri ya kutembelewa na watalii.

(a) Mapango ya Handebezyo ni mapango ambayo watu wa kale waliyatumbia kwa ajili ya kujilinda na kufanya shughuli nydingine mbalimbali wakati wa mashaka kiusalamu. Halmashauri ya Wilaya imekuwa ikijitahidi kuyahifadhi mapango haya yaliyoko Kata ya Nduruma.

(b) Nyumba ya Ghorofa ya Chifu Lukumbuza ni jengo lililokuwa linatumika kama makazi ya Chifu wa Wakerewe, Chifu Lukumbuza. Hiki kimekuwa kivutio kutokana na muundo wake ikilinganishwa na nyakati za ujenzi wake. Jengo hili liko katika kijiji cha Bukindo na limekuwa likivutia watu wengi, lakini faida yake kwa Taifa haina tija.

(c) Ufukwe wa Rubya ni ufukwe wa aina yake ulioko katika Kata za llangala na Muriti ambaa umekuwa ni kivutio kikubwa sana kwa watu mbalimbali, kitu ambacho kama Wizara itaweka nguvu yake, basi kinaweza kuwa chanzo kingine kizuri cha mapato kupita utalii.

(d) Katika Kisiwa cha Ukara, Wilayani Ukara kuna jiwe ambalo ni la kimila na ambalo linasimamiwa na moja ya familia zilizoko katika kijiji cha Nyamangana. Jiwe hili limekuwa ni moja ya maajabu ambayo yamekuwa yanavutia watu wengi wanoenda kushuhudia kile kinachotokea. Bahati mbaya limekuwa halitangazwi sana kiasi kwamba ukiachilia mbali watu walioko kule Ukara ni watu wachache kutoka nje ya Wilaya wanaojua jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe itumie wataalam wa utalii

utembelee vivutio hivi na kufanya maboresho na kuvitangaza ili Taifa liweze kufaidika kupitia mapato yatakayotokana na vyanzo hivi (vivutio) vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uharibifu wa wanyama kama viboko, limekuwa ni tatizo na kikwazo kikubwa cha maendeleo ya wananchi katika Kata za Nduruma, Bukindo na Kagunguli. Tatizo hili kwa kuwa ni la muda mrefu na Halmashauri imeshindwa kulidhibiti, basi naomba Wizara ichukue hatua za haraka kudhibiti na kunusuru hali hii.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja. Jimbo la Nkasi Kusini lina mbuga iitwayo Rwanmf Game Reserve. Katika mipaka ya mbuga hii kuna migogoro kati yake na vijiji jirani kwa Jimbo la Nkasi Kusini, vijiji vya King'ombe, Mlambo, Kasapa, Ng'undwe, Namansi na vijiji vya China na Nkata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vyote hivi vimekuwepo kabla ya kuanzisha Hifadhi hii, lakini wahifadhi wamekuwa wakidai kuwa wananchi wanaishi ndani ya hifadhi. Naishauri Serikali ije na mkakati mpya kuangalia kwa upya mipaka ya mbuga hii ili kuleta uelewano na vijiji jirani na kuondoa usumbufu unaotokana na wahifadhi kusumbua wananchi ikiwa ni pamoja na kuwapiga. Wananchi hawaelewi kwa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi imevikuta vijiji hivyo vyenye haki na huduma zote za kijamii ikiwa ni pamoja na shule za sekondari, zahanati na vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la vijiji hivi halitoshi pia kwa shughuli za kuendesha maisha. Tunaomba sehemu ya mbuga hii ipunguzwe kutoa eneo la kilimo kwa kilimo zaidi.

**MHE. LOESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri. Pia napongeza kwa kazi inayofanyika ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto yangu ipo katika mipaka kati ya vijiji vinavyozunguka misitu ya hifadhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Jimbo la Busanda katika kijiji cha Saragulwa; kuna mgogoro wa mara kwa mara baina ya hifadhi ya msitu wa Geita na kijiji cha Saragulwa. Mgogoro huu unasababisha kero kubwa sana kwa wananchi waishio katika kijiji kutokana na adha za kutaka kuchomewa nyumba na kufyeka mazao ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kupitia Wizara ione umuhimu wa kuangalia upya mipaka yake na kutoa elimu kwa wananchi juu ya mipaka hiyo na kuwaeleza bayana adhabu zinazotokana na kukiuka mipaka iliyowekwa.

Kijiji cha Saragulwa kimekuwepo tangu Azimio la Vijiji vya Ujamaa na kinatambulika TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni juu ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kutokuwa na Bodi. Hii ni changamoto kubwa katika utendaji wa shirika na tunakosa mapato kwa kutokuwa na Bodi. Nashauri Serikali ifanye utaratibu wa kupata Bodi mpya haraka iwezekanavyo ili kunusuru hasara tunayoipata kwa kukosa mapato kwa wakati (concession fees).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, naipongeza TANAPA kwa kutoa madawati kwa Wilaya mbalimbali hapa nchini. Hata hivyo, naomba TANAPA ituangalie Wilaya zenyе changamoto kubwa ya watoto kukaa chini. Natumia fursa hii kuiomba TANAPA mchango wa madawati katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Tuna changamoto kubwa sana, tunaomba support.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, mwisho liko tatizo la mamba katika vijiji vinavyozunguka Ziwa Victoria hasa katika vijiji vya Kasangalwa, Kageye, Bukando na Chankorongo. Mara kwa mara kunatokea matukio ya wananchi kuliwa na mamba. Naiomba Serikali ilifanyie utatuzi kwa haraka kwa sababu tunapoteza nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuwa Wizara itayafanya kazi matatizo yote niliyoyawasilisha. Naunga mkono hoja.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ifute hifadhi ambazo hazina wanyama tena na maeneo hayo yagawiwe kwa wananchi wanaoishi karibu na maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali isisitize kwa mabalozi walioko nchi za nje kufanya kazi kwa ukamilifu kutangaza vivutio vyetu na kuwe na library zao za maliasili yao katika ofisi zao zinazoelezea jinsi Tanzania ilivyo ikiwa ni pamoja na tamaduni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoteli za Tanzania ziboreshwé, pia kuwepo na vyuo vikuu vya kufundishia wahudumu wa hoteli hizo Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu ni mali, Serikali ijipange kupanda miti, pia kutoa zawadi kwa kushindanisha wapandaji bora, waweza kuwa ni Taasisi kwa Taasisi au Wilaya kwa Wilaya.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya utalii vipo Kaskazini mwa nchi yetu. Nashauri Serikali ianzishe kituo kingine cha utalii Kusini mwa nchi yetu. Utalii siyo kuona wanyama pori tu, hata bahari yetu ya Lindi na ngoma za utamaduni. Ujenzi pia wa hoteli kubwa upande wa Kusini zinaweza kufanya watu wengi kutembelea Kusini na kuja kuona mambo mbalimbali na kuliongezea Taifa letu uchumi na mapato. Pia tunayo Selous ya Liwale. Naomba iboreshwe ili watu wengi waje Liwale kwa ajili ya kuona wanyama na uwindaji halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua atakapokuja kufanya hitimisho, Mheshimiwa Waziri atueleze tunaye mjesi yule mkubwa aliyeo Ujerumani (*dinosaur*) anayeingiza mapato kule Ujerumani. Mjesi huyu aliyetoka mkoani Lindi, kijiji cha Mipingo. Sisi Tanzania tunapata nini katika mapato yale yanayoingia Ujerumani kupitia mjesi huyu? Kijiji hiki cha Mipingo kinafaidikaje na mjesi huyu? Napenda kupata taarifa ya maswali haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. QULWI W. QAMBALO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaaliwa sana kwa kuwa na vivutio vya utalii hadi kushika nafasi ya pili duniani. Hii ni zawadi na heshima kubwa aliyotupa Mwenyezi Mungu. Si watu wote nchini wanafurahi na kuwepo hifadhi za wanyama katika maeneo yao kutohuna na manyanyaso na uonevu wanaofanyiwa na hifadhi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) haitendei haki wananchi wa vijiji vinavyozunguka. Mipaka ya Hifadhi ya Ngorongoro iliwekwa tangu mkoloni na inafahamika na beacons zipo katika mazingira ya ajabu sana. Mwaka 2002/2003 NCAA walifanya uhakiki wa mipaka yao na hapo ndipo walipopora maeneo ya wananchi ya malisho ya mifugo yao katika vijiji vya Endamaghanga na Losetete. Tangu muda huo migogoro imeshamiri. Ikumbukwe wakazi wa kijiji cha Losetete walihamishiwa Lositete miaka ya 1950. Kuchua maeneo yao waliyopewa ni unyanyaswaji wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Wizara ya Ardhi imefanya uhakiki wa mipaka ya NCAA. NCAA ndio waliolipa fedha ya zoezi hilo na nitahadharishe Wizara kuwa isije ikawa uhakiki unaofanywa sasa ni kutaka kuhalalisha haramu iliyofanyika mwaka 2002/2003 walipohakiki. Nawataka NCAA wahakiki mipaka yao ya awali na siyo mipaka ya mwaka 2002/2003 waliyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni uharibifu unaofanywa na wanyama kutoka Ngorongoro (ndovu na nyati) kwenye mashamba ya wanavijiji katika vijiji vya Lositete, Kambisimba, Kambi ya Nyoka, Oldeani na Makulivomba. Wananchi wanajitahidi kulima lakini wanyama wanawatia umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la ajabu ndovu wanatoka crater hadi barabara ya lami iendayo Ngorongoro, askari wa doria hawatoshi na pia hawajawezeshwa. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha, aliambie Bunge hili Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa uharibifu wa mashamba ya wananchi unaofanywa na wanyama unadhibitiwa?

**MHE. CATHERINE V. MAGICE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) ni mionganini mwa mashirika ya umma yenyewe kulisaidia Taifa kupata fedha nyingi za kigeni. Utalii nchini mwetu unachangia asilimia 18 ya GDP na sasa kiasi hiki kinaweza kuongezeka zaidi. Jambo la ajabu, *TANAPA* kwa miaka zaidi ya mitatu sasa haina Bodi ya Wakurugenzi. Mambo yote yamekuwa yakiamriwa na viongozi wa Wizara yaani Waziri na Katibu Wakuu waliopita na waliopo sasa. Hii ni hatari kwa shirika kama hili lenye fedha nyingi zinazohitaji utaratibu wa Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujangili unashamiri, idadi ya wanyamapori ni kubwa mno. Tembo wako hatarini kutoweka licha ya juhudhi za Serikali na vyombo vya ulinzi na usalama katika kukabiliana na hali hiyo. Majangili wana silaha hasa katika mapori kama ya Ugalla, Moyowosi, Loliondo na mengine mengi. Mbaya zaidi sheria haziruhusu walinzi wa kampuni zenyeye vitalu vya uwindaji katika mapori ya akiba na WMA kuwa na silaha. Hali hiyo imesababisha majangili watambe. Kwa nini Mheshimiwa Waziri asilete sheria Bungeni ili walinzi hao wapewe silaha na kwa hiyo, wasaidiane na wale wa *TANAPA* na wa wanyamapori kukabiliana na ujangili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu kwa majangili zisiwe faini, bali ziwe hukumu za kifungo cha maisha. Kenya wana sheria kali zinazosaidia sana kulinda wanyamapori wao. Kwa mfano, wao mtu akipatikana ndani ya hifadhi kinyume cha sheria, wanampiga risasi. Sisi tunaweza tusiwe na adhabu ya aina hiyo, lakini wakati umefika kwa Serikali kuleta hapa Bungeni mabadiliko ya sheria ili majangili wajue tumedhamiria kukomesha vitendo vyao. Serikali isiwe na kigugumizi cha kuwashughulikia viongozi wanaotajwa kuwa ni washiriki wakuu wa ujangili. Yapo maneno kuwa hata mionganini mwetu Waheshimiwa Wabunge kuna majangili. Kama kweli wapo, ni vizuri sheria zikatekelezwa badala ya kuendelea kuwaaminisha wananchi kwa maneno tu kuwa kuna Waheshimiwa Wabunge majangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka kadhaa iliyopita kulitokea mvutano kuhusu ada wanazopaswa kulipa watu wenyewe hoteli (concessions fee). TANAPA walifungua kesi katika Mahakama Kuu na kushinda kesi hiyo. Ikaamuliwa wenyewe hoteli walipe, lakini utekelezaji wake ulipaswa uanze kwa Bodi kukaa na kupanga viwango vya ada hiyo. Sasa miaka zaidi ya mitano uamuzi huo haujatekelezwa na haujatekelezwa kwa sababu hakuna Bodi. Kwa kutoweza ada hizo, TANAPA wanapoteza wastani wa shilingi bilioni 10 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ahakikishe anamshawishi Mheshimiwa Rais mapema iwezekanavyo ili Bodi ya TANAPA iundwe; na kwa kufanya hivyo, iweke viwango vya ada na utekelezaji uanze mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo katika mapori ya akiba, mapori tengefu, WMA na Hifadhi za Taifa ni mingi sana. Mapori kama Maswa, Moyowosi, Kijeleshi, Ugalla yanaelekea kufa. Pori tengefu la Loliondo limevamiwa na malaki ya mifugo kutoka nchi jarani (Kenya). Loliondo ni kama imekufa. Shughuli za kibinadamu zikiwamo za kilimo ni kubwa mno. Wanyamapori wamekimbia, Loliondo hii ni buffer zone ya Serengeti na eneo ambalo ni mazalia ya nyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo imekuwa mingi sana kiasi cha kufikia hatua sasa ya kuona hatari siyo ujangili tu, ila mifugo katika mapori ya hifadhi. Pamoja na umhimu wa mifugo katika nchi yetu, Serikali isisite kutekeleza Operesheni Ondoa Mifugo ambayo imepangwa kuanza tarehe 15 Juni, 2016. Bila kufanya hivyo rasilimali wanyamapori itatoweza katika nchi yetu na hii itakuwa aibu kubwa kwa kizazi kijacho na ulimwengu kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuweke kando siasa na tujikite kwenye uhifadhi. Faida za uhifadhi ni kubwa; kwa mfano, nyati mmoja anayewindwa anaiingizia Serikali zaidi ya shilingi milioni tatu. Simba mmoja anaingiza zaidi ya shilingi milioni 10. Kwa hiyo, tusiifanye mifugo ikawa mbadala wa wanyamapori kwa sababu faida yake ni kwa wachache wenyewe kuimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Gazeti la Jamhuri lilitoa makala ikionesha vibanda vibovu kabisa vya kukusanya mapato kutoka kwa watalii katika maeneo ya Oldonyo Lengai na Engaruka. Ile ni aibu kubwa kwa sababu vibanda vyenyewe vimeshikiliwa na nguzo za miti visianguke. Hata watalii watatushangaa kuona dola zinakusanya kwao na watu walio kwenye vibanda vibovu. Ingawa vibanda hivyo vipo chini ya Halmashauri za Longido na Monduli, bado Wizara ya Maliasili na Utalii inapaswa kuitazama aibu hii na kuiondoa kwa sababu watalii hawazijui Halmashauri hizo, isipokuwa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya mkaa inashamiri sana. Misitu inamalizwa na sababu inayotolewa ni kuwa bei ya gesi au nishati mbadala ni kubwa. Ingawa suala hili la mkaa ni mtambuka Kiwizara, bado ukweli unabaki kuwa mkaa mwingu unatolewa katika mapori yanayohifadhiwa kisheria chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Mbaya zaidi, hata huo mkaa unaouzwa watu wengi hawalipi ushuru. Malori ambayo kisheria hayaruhusiwi kusafirisha mkaa, leo yanatasafirisha hadi kwenye makontena nyakati za usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pale Dar es Salaam watumishi wa Wizara wakae kwenye maegesho pale kwa Msuguri ili kuyakamata malori yote yanayopakia na kusafirisha mkaa bila vibali wala kulipa ushuru. Watumishi wa Wakala wa Vipimo wapo hapo sasa wakidhibiti upakiaji wa lumbesa kwa mazao kutoka mikoani. Sioni kwa nini Wakala wa Misitu nao wasikae hapo kwa Msuguri ili kuyadhibiti malori haya yanayotumika kutenda makosa haya ya uhifadhi.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu fidia ndogo kwa wakazi wanaoishi karibu na hifadhi na Serikali kushindwa kuwadhibiti tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyama akimuua mtu au binadamu fidia yake ni ndogo sana. Familia inalipwa shilingi 100,000 au wasipate kabisa kutokana na figisufigisu za viongozi wa eneo husika; lakini endapo mtu akikutwa kaua wanyama, fidia anayotozwa ni kubwa sana na ni kuanzia shilingi milioni sita na zaidi. Swali la kujiuliza je, kipi kina thamani kati ya binadamu na mnyama? Maana hii inaonyesha moja kwa moja kuwa Serikali yetu inathamini wanyama kuliko binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali, iangalie sheria hii kwa umakini, kwani haiwezekani hata siku moja mnyama akawa na thamani kuliko mtu au binadamu. Ni vizuri wananchi wa eneo husika wapewe elimu ya kutosha juu ya fidia wanayostahili kulipwa maana kila mwananchi akijua juu ya umuhimu wa malipo wanayostahili kulipwa, naamini hakutakuwa na kelele kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi wanaoishi karibu na maeneo ya mbuga au hifadhi wananyanyasika sana utafikiri watu hawaishi katika nchi yao (wakimbizi). Wananyanyaswa, wanafukuzwa kwenye maeneo yao wakati Serikali haijawaandalia maeneo ya kwenda kuweka makazi hayo. Ina maana wakati wananchi hao wanajenga, Serikali ilikuwa wapi? Ina maana ilikuwa inawaangalia tu wanapomaliza ndiyo iwaambie wananchi kuwa wamevamia hifadhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana na inasikitisha pia. Inabidi Serikali iwaangalie kwa upya wananchi hawa kwani wanaishi kwa hofu kubwa na maeneo hayo ni Maliwanda, Mihale, Mcharo, Serengeti, Hunyali, Kunzugu na Balili, hivyo vyote ni vijiji vya Wilaya ya Bunda. Kwa upande wa Serengeti ni Merenga, Machochwe, Nyamakendo, Mbalibali, Tamkeri, Bisarara, Mbilikiri, Bonchungu na Robanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshindwa kuwadhibiti wanyama (tembo) wanaoharibu mazao ya wananchi bila kujali hasara wanayoipata wananchi hao. Kwanza kabisa bila kuwadhibiti tembo hao umaskini hautaisha, kila siku wananchi hawa wataendelea kuwa omboomba kutokana na umaskini unaotawala kutokana na mazao yao kuliwa na tembo au kuharibiwa na tembo ama wanyama wengine waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Serikali ikajipanga upya juu ya jambo hili la kuwadhibiti tembo ili wananchi wanapolima mazao yao wavune na kupata chakula na wananchi wengine wanahamia ili wapate kuvuna mazao yao na kuyauza kwa ajili ya kusomesha watoto wao, lakini tembo wanamaliza mazao ya wananchi kabla hawajavuna na kuendelea kuwadidimiza wananchi hawa kuwa maskini. Ninaamini Mheshimiwa Waziri atalishughulikia suala hili kwa ukaribu ili kuwasaidia wananchi hawa.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mvomero ni moja ya Wilaya ambazo zimekumbwa na tatizo kubwa sana la migogoro ya wakulima na wafugaji. Zipo juhudhi mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo Halmashauri ya Wilaya Mvomero, uongozi wa Mkoa na Serikali Kuu kupitia Wizara mbalimbali. Nia na madhumuni ni kuondoa au kupunguza migogoro hii, zipo changamoto nydingi sana tunazokabiliana nazo ikiwemo uhaba wa ardhi kwa wafugaji na kwa wakulima. Mbali na hilo, lipo tatizo la bajeti, fedha hazifiki kwa wakati katika mipango yetu kama Halmashauri ikiwemo kutenga maeneo ya malisho, majosho, kupima ardhi, barabara na maeneo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lipo tatizo la watendaji wetu wa ngazi ya kijiji na kata, baadhi yao kupokea rushwa na kuongeza mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze kuhusu hifadhi iliyopo Wilayani Mvomero ya Wami Mbiki. Hifadhi hii inaunganisha Wilaya za Morogoro Vijiji, Bagamoyo na Mvomero. Kwa upande wa Mvomero baadhi ya vijiji vimetoa ardhi yao kwa lengo la kuboresha hifadhi na pia kuongeza Pato la Taifa. Tatizo lililopo sasa ni uhaba wa ardhi kwa ajili ya ufugaji na kilimo. Ombi la wananchi, baadhi ya vijiji virudishwe kwa wananchi. Vijiji hivi vikirudi vitapunguza sana tatizo la migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ndani ya hifadhi yapo makundi ya mifugo, wapo wakulima humo, yapo na makazi hewa. Tatizo kubwa ni kudorora kwa mipango ya uanzishaji wa hifadhi hii. Awali Serikali ilikuwa na nia ya dhati lakini hata wafadhili nao wamejitoa katika hifadhi na kukosa mwelekeo wa hifadhi hii. Ombi la wananchi ni kupewa maeneo yao ili wayaendeleze kwa kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata makubaliano ya awali kati ya vijiji na hifadhi hayatekelezwi na hakuna faida inayoonekana. Watu wa maeneo ya hifadhi wanafaidika na makubaliano ya kuanzisha hifadhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shamba la mitiki Mtibwa, lipo Wilaya ya Mvomero, Tarafa ya Turiani. Ni shamba ambalo Serikali inapata mapato mengi licha ya wananchi kuwa walinzi wa amani wa shamba hili. Vijiji vina miradi ya maendeleo ya elimu, afya, maji, barabara na kadhalika. Tatizo hakuna mrabaha wanaopata wanakijji wa maeneo ya jirani. Tunaomba Wizara kuitia idara yake, sasa itenye fungu la ujirani mwema ili kusaidia huduma za kijamii; hili litaleta na kudumisha mahusiano mema na pia kuongeza tija ya shamba. Pia tuna hitaji kubwa la madawati, Wizara iangalie uwezekano wa kutumia mabaki ya miti hii ya Mtibwa Teak kusaidia mabaki vijiji hivi vinavyozunguka shamba ili tupunguze tatizo la madawati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikumi National Park, inapatikana na Wilaya ya Mvomero, Kata ya Doma na Msongozi. Lipo tatizo kubwa sana la wanyama hususan tembo kuingia katika makazi na mashamba ya wananchi na kuleta athari kubwa sana ya mali na maisha ya wananchi wa Doma na Msongozi. Changamoto ni kubwa sana katika eneo hili. Wapo wananchi waliopoteza maisha yao, hadi sasa hakuna fidia iliyotolewa na TANAPA. Yapo mashamba na mali zilizoharibiwa hadi leo, hakuna fidia iliyolipwa na wanyama hawa wanatoka karika maeneo ya wananchi. Naomba kujua hatma ya malipo ya fidia za waathirika hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wananchi wa Doma na Msongozi ambao wapo mpakani na mbuga hii ya Mikumi wanahitaji madawati na kusaidia miradi ya maendeleo. Naomba TANAPA iwatupie jicho wananchi hawa katika mipango yao ya ujirani mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Bodi ya Utalii iundwe na ije Mvomero, tunazo fursa nyingi za utalii kama vile milima ya Mgeta, maporomoko ya maji Bunduki ili maeneo haya yaingizwe katika sekta hii na yaweze kuchangia Pato la Taifa.

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kuhusu suala la utalii wa Zanzibar. Utalii wa Zanzibar wageni wengi wamepungua kwa sababu mbalimbali za kisiasa na mengineyo. Sasa naomba Serikali ya Tanzania Bara iweze kusukuma utalii huu wa Zanzibar ili kupata nguvu kama utalii wa Tanzania Bara na wananchi wengi wanategemea utalii hususan vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mapato. Hii tozo inayotokana na utalii ikusanywe vizuri ili Zanzibar iweze kupata mapato vizuri. Kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 88 kuwa tufahamu wageni wanaingia na kutoka. Hiyo tozo inayopatikana ni kiasi gani ili wananchi wa Zanzibar waweze kufahamu, kwa mwaka mapato yanayopatikana, ili kusukuma maendeleo ya Zanzibar yatokanayo na utalii.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Bunge la Kumi kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali ilianzisha kauli mbiu isemeyo; "Utalii Uanzo kwa Mtanzania." Pamoja na kauli hii kuonesha msisitizo kwa Watanzania kuweza kujivunia na kunufaika na sekta hii, bado zaidi ya robo tatu ya Watanzania hawanufaiki hata kidogo na sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hii iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii wa wakati huo, ni hadaa kubwa kwa Watanzania. Inajulikana bayana kwamba kima cha chini cha mshahara wa Mtanzania hakizidi shilingi 300,000. Kutembelea mbuga zetu ni lazima kila Mtanzania kuchangia kiasi cha shilingi 5,000 mpaka shilingi 15,000, lakini pamoja na mchango huu, kama Mtanzania atalazimika kulala mbugani katika hoteli kwa usiku mmoja itamlazimu kulipa gharama mara mbili zaidi ya mshahara huo kwa kima cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Watanzania wakafahamu kuwa Mtanzania anapotaka kwenda mbugani kwa siku mmoja tu inagharimu dola za Kimarekani takribani 145 sawa na fedha za Kitanzania shilingi 316,825 kwa exchange rate ya shilingi 2,185. Hii ni kwa hoteli yenye gharama nafuu zaidi mfano Rhino Lodge. Gharama hii haijahuisha chakula wala huduma nyingine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayojipambanua na kauli ya Hapa Kazi Tu kwa nini isingeona umuhimu wa kuva viatu vya wananchi hawa wa kipato cha chini na kuona ilivyo kazi kuweza kuishi kwa kiasi hicho cha fedha kitakachomfanya Mtanzania huyu aweze na yeye kujisikia sehemu ya kulinda na kuzifahamu mbuga zetu? Ni kwa nini Serikali isifike mahali ikaona umuhimu wa dhati kuweza kumsaidia Mtanzania huyu kuweza kujisikia kuwa sehemu ya rasilimali zilizo ndani ya nchi yake kwa kuweka mazingira nafuu zaidi kwa bei ambayo Watanzania wengi wataweza kulipia na kufurahia mandhari mazuri ya mbuga zetu? Ni vyema sasa

tukaaza kujivunia vya kwetu kwa vitendo ili basi Watanzania wasiwe ni watu wa kusimuliwa au kuona mandhari ya mbuga zetu kwenye runinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali inafumbia macho malipo yanayofanywa kwa fedha za kigeni hasa kwenye sekta ya utalii? Mara nyingi tumekuwa tukilizungumzia suala la matumizi ya dola katika mzunguko wa fedha hapa nchini, lakini ni kwa nini Serikali haichukui hatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Mtanzania anayeamua kufanya utalii wa ndani na kuamua kulala kwenye hoteli zilizopo ndani ya mbuga, hasa zile zilizoko kwenye Hifadhi ya Ngorongoro, Serengeti na hata hoteli kubwa za Zanzibar, ni lazima afanye malipo kwa dola. Katika hali ya kawaida, ni Watanzania wangapi wanamiliki dola katika uchumi wao? Hii ina maana kwamba ni lazima wabadili fedha zao katika maduka ya kuza fedha ili waweze kufanya malipo. Ifike mahali hasa Serikali iijitathimini. Ukienda nchi za wenzetu walioendelea, mfano, Norway, Switzerland, German na nyingine, huwezi kununua kitu kwa fedha ya kigeni. Wanathamini fedha yao zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni aibu na ni fedheha kubwa kwa Serikali kuendelea kushiriki katika michezo ya kuua thamani ya shilingi yetu kwa kuruhusu makampuni haya kuendelea kufanya tozo mbalimbali ndani ya nchi kwa fedha za kigeni. Serikali ije na sera lazimishi ya kuhakikisha kuwa fedha yetu inatumika. Wageni waweze kununua fedha yetu ili tuwe na akiba ya dola. Tunawezaje kufikia ndoto ya kuwa na uchumi na kati wakati sisi wenyewe ndiyo tunadidimiza thamani ya shilingi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana kuwa *booking* za hoteli za kitalii kwenye hifadhi za nchi hii zinazofanywa kuitia kwa mawakala walio nje ya nchi yaani ukitaka kupata nafasi ya hoteli unapiga simu Afrika Kusini au Nairobi kwa Wakala ambaye yeye ndio atakupa nafasi au laa. Tunataka kujua ni kwa nini jambo hili linafanywa kwa namna hii? Ni kwa nini *booking* zote za hoteli zilizopo hapa nchini zisifanyike kuitia mawakala waliopo ndani ya nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Tanzania kuweza kuthamini vitu alivyotupa Mwenyezi Mungu. Inasikitisha sana kuona vyura wa kipekee kabisa duniani hawapewi nafasi ya kutosha kuweza kufahamika kwa wananchi wetu. Vitu hivi vya kipekee kabisa ambavyo duniani kote hakuna, mfano wa vyura hawa wa Kihansi wanaozaa na kunyonyesha, ni dhahiri kabisa tunakuwa hatuwatendei haki wananchi wetu na hata watoto wetu ambaa watakuwa watu wazima na hawaifahamu nchi yetu na vivutio vyetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ije na mpango mkakati wa kuhakikisha vyura kama hawa ambao ni *amphibia*, pamoja na malikale nyingine zinaingizwa katika mitaala mbalimbali ili watoto wetu waweze kuvifahamu vizuri.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendeleza maliasili zetu na watalii wanaoingia nchini mwetu wanaongezeka siku hadi siku. Ni jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kama tutajipanga vizuri kwa kutangaza utalii na vivutio tulivyonyavyo, mapato yetu yanayotokana na utalii yataongezeka zaidi. Mfano, utalii wa viungo; tuwahamasishenanchi wetu kupitia mtu mmoja mmoja au vikundi kuanzisha mashamba ya viungo (*spices*) mbalimbali na watalii wataona kitu kingine badala ya wanyama pekee na wananchi wataongeza vipato vyao moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kuwaandaa wananchi kuvutia watalii kwa utamaduni wetu wa asili, mfano ngoma zetu za asili, mila na desturi zetu za asili, mavazi, chakula, lugha, malezi na kadhalika. Kwa utalii wa historia utahusu watawala waliopita na kutawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuipongeza Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri wanayoifanya wakiongozwa na Profesa Jumanne Maghembe pamoja na watalaaam wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri na yenye ubora wanayoifanya katika kulinda maliasili ya nchi yetu, ambacho ni kivutio cha utalii ndani na nje ya nchi yetu Tanzania na ndicho kichocheo cha maendeleo ya Taifa letu. Natambua Wizara hii ni ngumu na ina changamoto nydingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii itazame vizuri kwenye maeneo ya mipaka ya Hifadhi ya Wanyamapori (*game reserves*), kwani kumekuwa na malalamiko makubwa kwa Maofisa wa Wanyamapori ikiwa ni pamoja na vitendo vya uovu kwa wananchi kwa kuwatoza faini zisizo kwenye utaratibu wa kawaida wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maofisa wamekuwa wakiwaswaga ng'ombe na kuwaingiza ndani ya hifadhi hata kama watakuwa nje ya hifadhi. Nashauri Serikali kupitia Wizara hii iweze kutatua kero hii kubwa inayosumbua wafugaji wengi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa ujumla kwa utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Mchango wangu utajikita katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ndogo ya wanyamapor/migogoro ya mipaka katika marejeo ya Sheria ya Wanyamapor ya mwaka 2009; Serikali ilielekezwa kutathmini juu ya uendelezaji wa mapori ya akiba na mapori tengefu yote yaliyoko nchini ili kubaini uendelezaji wake, aidha, marekebisho ya mipaka yake ili kuondoa migogoro ya ardhi baina ya mapori hayo na ardhi ya vijiji vinavyopakana navyo, hadi leo maelekezo hayo ya Bunge bado hayajatekelezwa na Serikali na badala yake ni kuendelea kwa migogoro katika mapori hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la migogoro ya aina hii hususan kwa pori tengefu la Kilombero na vijiji jirani, nimeliongelea sana na mara ya mwisho Serikali kupitia Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu, Aprili, 2014 alitoa agizo kwa Wizara ya Maliasili kuweka utatuzi wa kudumu katika mgogoro wa ardhi kwa pori hilo na mengine lakini hadi leo agizo hili halijatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake atoe kauli ya wazi, ni lini ardhi iliyoko katika eneo la buffer zone katika pori tengefu la Kilombero itarejeshwa katika ardhi ya vijiji ili iweze kutumika kwa matumizi ya kilimo na mifugo ambayo ndio uhai wa wananchi hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani na nitaunga mkono kama Waziri atatoa majibu ya kuridhisha katika ombi la wananchi wa Ulanga na Malinyi.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa ya kuchangia kwa maandishi. Napenda kuipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa hotuba nzuri, lakini pamoja na yote, napenda kuwataarifu Waziri na Naibu wake kwamba kwa haraka haraka inaonekana watendaji wa Wizara hii wanafanya kazi kwa mazoea na ni wakati sasa wa watendaji hawa kusimamia Katiba ya nchi pamoja na Sera Taifa zinazoigusa Wizara hii ikiwemo Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wa Wizara hii kuhakikisha kwamba utalii wa nchi yetu unaimarika kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo ile ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona nchi nyingine zikijitangaza kuwa na baadhi ya vivutio vilivyopo ndani ya nchi yetu kama come to Kenya

and see Mount Kilimanjaro. Hili ni suala la kusikitisha sana pale nchi yetu inaposhindwa kukemea masuala haya kupitia Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashangaa kwa umri wangu sikuwahi kusikia kitu chochote kuhusu mjesi wa aina ya *dinosaur* aliyewahi kupatikana hapa nchini Tanzania Mkao wa Lindi na kupelekwa Ujerumani. Nimekuwa na maswali mengi juu ya hili. Nimekuwa nikijuliza ni kiasi gani cha fedha Ujerumani inaingiza kupitia huyu mjesi? Katika hizo fedha ni kiasi gani kinalewa Tanzania na ni kiasi gani kinapelekwa Lindi kwa ajili ya maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona hata mashulenii hili halitajwi popote na kibaya zaidi hata huko Ujerumani hatuna uhakika kama hawa wanataja mnyama huyo katokea Tanzania na kibaya zaidi historia ya mjesi huyu haijulikani na ipo mbioni kupotea kabisa tukizingatia uwepo wa kizazi hiki na kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara husika kutueleza ni shilingi ngapi tunaingiza kama nchi kutokana na mjesi huyu na ni jinsi gani tunafaidi kwa yeze kuwepo huko Ujerumani? Ninaishi Serikali kumrudisha mjesi huyu nchini ili tuongeze kipato cha Serikali kupitia utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Wizara hii kuwapeleka Madiwani wa sehemu husika alipopatikana mjesi huyu na baadhi ya Wabunge wakiwemo wanaotoka Lindi kwenda kumuona mjesi huyu ili waje watuhakikishie uhai wake, lakini kikubwa zaidi tupate taarifa ya kujiridhisha juu ya kipato anachoingiza nchini humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie Wizara hii nikizingatia vitu muhimu sana ambavyo ni rasilimali zilizomo katika nchi hii ya Tanzania. Pamoja na kuingiza uchumi ili kuondokana na umaskini, jambo ambalo Wizara ya Maliasili na Utalii inafanya, nchi yetu ni tajiri sana kwa kuwa na vitega uchumi vya utalii. Tuna vivutio vingi sana na nchi yetu ni ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Serengeti, Ngorongoro, Tarangire, Momela, Mikumi, Katavi na Rubondo; tuna jiwe liko Ukerewe ambalo Serikali haijaona umuhimu wake kuipa kipaumbele ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wanajua maajabu makubwa sana ya hilo jiwe pamoja na Wabunge wa huko Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Biharamulo tuna msitu ambao kwa sasa umeingiliwa na wafugaji wengi wamevamiwa, wanashambuliwa pamoja na wachoma mkaa, hata hao wa ng'ombe wanajifanya wafugaji, tunawaogopa sana. Wanaweza kuwa sio salama; huwezi kujua kama ni Watanzania au ni wakimbizi. Matokeo yake kuanza kuteka na kurudi kwenye pori hilo. Je, msitu mkubwa kama huo wanakula nini? Tunaomba msaada wa Serikali, hata wanyama wameanza kurudi sasa, watacaa wapi kwa style hii? Je, tuna faida gani? Kwa nini wafugaji wasitengewe wakawa na mipaka? Vijiji ambavyo viko karibu na pori hilo, shida wanavamiwa na wake zao wanabakwa, wakikuta vyakula wanakula, wanaume wanapigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya Wizara iliyomo kwenye vitabu iwe ya kutekelezeka. Msitu huo uko kwenye Ziwa la Buligi ambalo lina maajabu makubwa sana. Limepakana Bukoba Vijiji, Biharamulo, Karagwe na Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana, tena sana, Serikali iweze kuweka mpango mkakati tuongeze kipato/ajira kwa vijana wetu. Vipo vitu vingi tu, ni mipango tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matangazo ya utalii wetu wa vivutio vyetu ni mdogo sana. Matangazo ya vipeperushi inafika mahali unakuta Kenya wanaongoza mbuga zetu kwa upande wao hata Mlima Kilimanjaro ni punde watasogea upande wa Kenya. Kweli tunakokwenda hili jambo mmekaa kimya, taratibu wanakuja. Hata Idd Amini alikuja hivyo hivyo kusogeza mipaka yetu ila angeingia kwenye nchi yetu, Mwalimu wetu Baba wa Taifa alipambana na Wajerumani, zimetolewa zinasogezwa matokeo yake nchi ikaingiakwenye vita. Sasa chonde chonde, Wizara iwahi mapema kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa pembe za tembo, hili suala limekuwa wimbo katika nchi hii. Ni maharamia wangapi wamefungwa? Ni kesi ngapi ambazo ziko mahakamani au zilizokwisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya vivutio ni madogo sana ukilinganisha na vivutio tulivyonyavyo vingi na kupata tofauti. Sisi tuna asili ya mali nydingi, hatupaswi kuwa hivyo, ni usimamizi siyo mzuri sana. Tuwe na usimamizi na mipango mikakati, tutaondokana na kutokuwa na plan za kudumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu kama viwanja vya ndege vinatakiwa kuboreshwa hasa vya Musoma na Kilimanjaro (KIA). Kweli viwanja vya kuingiza wageni nchini viko hivyo na kama unavyojua wenzetu wanajali maisha yao na usalama. Miundombinu inashusha utalii. Viwanja vya mbugani vyote vya changarawe viboreshwe kwa kuwekewa lami. Sasa mvua ikinyesha wasije au?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoteli zetu tukiona wazungu tunapandisha bei, siyo vizuri. Naiomba hasa Serikali iingilie, ibadili. Wizara inatengeneza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ufgaji wa nyuki. Ufgaji nyuki ni ajira kubwa sana kwa vijana. Wapewe elimu wajiajiri wenyewe. Tuhamasishe vikundi vya kufuga nyuki wafuge kiutalaam zaidi. Misitu mingi ya nchi yetu inaruhusiwa kufuga nyuki, masoko ni mengi, lakini wanaofuga hawafugi kitaalam, wala hawapati elimu. Jambo hili liangaliwe au lipewe kipaumbele. Kadri tunavyochelewa kutenga bajeti ya kutosha, wakija wawekezaji watajipangia utaratibu wao.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa uwasilishaji mzuri. Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara hii ilitoa agizo la kuwauzia MPM miti kwa nusu ya bei, *that is cubic meter* 1 – 14,000 badala ya 28,000 tangu mwaka 2007 mpaka sasa hivi Serikali inaingia hasara isiyopungua shilingi bilioni 2.8 kila mwaka. Naomba Wizara ije na mkakati wa kuondokana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa karatasi inatengenezwa Kenya, lakini misitu iko Tanzania na bado *importation* ya karatasi ina punguzo la kodi la asilimia 10 badala ya asilimia 25 ninaiomba Serikali ije na mpango wa kuhimiza viwanda vyetu kama MPM kutengeneza karatasi badala ya mifuko peke yake na tuongeze kodi ya *importation* iwe asilimia 25.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie hoja hii. Mimi ninatoka Wilaya ya Kilolo ambayo iko Mkoa wa Iringa, Hifadhi ya Udzungwa asilimia kubwa ipo katika Wilaya ya Kilolo japo Makao Makuu yapo Morogoro. Kuna vijiji ambavyo vinapakana na *Udzungwa National Park*. Vijiji vya Msosa, Ikula, Udekwa, Mahenge, Wotalisoli na kadhalika kuna tatizo kubwa la mamba, tembo hasa katika kijiji cha Msosa. Kwa sababu maji ya Mto Lukosi ndiyo yanayosababisha wananchi wengi kuliwa na mamba na pia kuuliwa na tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi:-

- (1) Tunaomba Wizara iangalie utaratibu wa kujenga post (Kituo cha ulinzi wa vijiji vile pale Msosa), kujenga miundombinu ya maji yaani tanki la maji na kusambaza kijiji kile ili kupunguza ajali za mamba.
- (2) Ujenzi wa barabara ya kutoka kijiji cha Mahenge kwenda Udekwa, kilometra 25 tu.
- (3) Kuna mapango makubwa katika kijiji cha Udekwa ambayo ni kivutio kwa watalii wa ndani na nje, ningeomba wataalam wafike waone.

(4) Kutelekezwa kwa kivutio cha Kalenga, sehemu ambayo kichwa cha Mkwawa kimehifadhiwa, familia ya Mkwawa wandalalamika na kuna uwezekano mkubwa wa kuomba kukizika kichwa kile.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa juhudzi zake za kuhakikisha Wizara inatekeleza majukumu yake kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii naishauri Wizara iweke mkakati madhubuti katika kudhibiti mapato yatokanayo na utalii. Watalii wanaotembelea Tanzania walipie hapa nchini kuepusha upotevu wa mapato. Elimu na matangazo juu ya vivutio vya utalii vilivyopo nchini ipewe kipaumbele ili kuongeza idadi ya watalii kuitembelea Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misitu, upandaji wa miti uwe mara mbili zaidi ya miti inayokatwa. Nishati mbadala ya kupikia itasaidia kupunguza matumizi ya mkaa ambapo itasaidia kupunguza miti kuchomwa kwa kutengeneza mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji wa mbao nje ya nchi udhibitiwe zaidi pamoja na kupunguza kiwango cha mbao zinazosafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya ukataji na uvunaji miti katika mashamba ya miti, kwa mfano SAO Hill na kwingineko upatikanaji wake ni wa shida sana, hata muombaji aliyetimiza masharti yote. Kuna upendeleo na wanyonge ni shida sana kupata vibali hivyo. Nashauri upangwe utaratibu mzuri katika utoaji vibali vya uvunaji miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nawatakia kazi njema.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam inaweza kuwa kivutio kwa watalii. Tuna eneo la Dar es Salaam Zoo ambalo ni eneo la mtu binafsi, Serikali inaweza pia kuanzisha eneo kama hilo kwa ajili ya kipato hasa maeneo ya Kigamboni, utalii huu utakwenda sambamba na Daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii wa majengo ya kale, Bagamoyo, historia ya Bagamoyo ikiwa promoted vizuri itaongeza tija katika *cultural tourism*; Kaole ilikuwa kivutio sana, kadri tulivyoshindwa kutangaza ndivyo utalii huu umefifia.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti yao ili tuweze kuijadili. Yapo mambo ambayo napenda kutoa ushauri na pia kupatiwa ufanuzi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mkakati wa Serikali katika kukuza na kutangaza utalii Kimkoa au Kikanda? Mko a wetu wa Iringa ni kati ya mikoa ambayo ina vivutio vingi ambavyo kama Serikali ingekuwa na mkakati wa kutosha naamini mko a wetu ungeweza kuiingizia Serikali pato kubwa sana na pia tungeweza kutengeneza ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mko wa Iringa una mbuga ya Ruaha National Park, katika Afrika ni mbuga ya pili kwa ukubwa lakini miundombinu ya barabara ni mibovu sana na bado Serikali haijaweza kuona umuhimu wa kuweka barabara ya lami ili kuvutia watalii wengi kwenda katika mbuga hiyo. Bado Serikali haiwezi kuona umuhimu wa kujenga au kukarabati kiwanja cha ndege cha Nduli, ni vema sasa Serikali ingewenza kuzifanyia upembuzi yakinifu baadhi ya miradi kama ya barabra na viwanja vya ndege ambavyo ni changamoto katika kukuza utalii wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mko a wetu eneo la Isimila Olduvai Gorge lingeweza kuongeza pato kubwa sana la utalii lakini halitangazwi na halina maboresho kabisa. Mko a wetu una kaburi na fuvu la kichwa cha Mtwa Mkwawa, bado hakuna matangazo ya kutosha ili tupate utalii wa ndani na nje ya nchi ili tuongeze utalii na vijana wetu kuitia watalii watengeneze ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu TANAPA, shirika hili ni kati ya baadhi ya mashirika na taasisi za umma zinazofanya vizuri sana katika sekta hii ya utalii lakini ni tatizo gani linasababisha Serikali kutokuweka bodi? Mambo mengi na changamoto nyingi zinakosa maamuzi kutokana na shirika kukosa bodi. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapojibu atoe ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia kwa wananchi wanaoliwa na mamba, kwa kuwa kumekuwa na vifo mara kwa mara kwa wananchi na hasa wanawake wamekuwa wakipata ajali wanapokwenda kufuata maji katika Mto Lukosi katika Wilaya ya Kilolo, Kata ya Ruaha Mbuyuni. Je, ni utaratibu gani unatakiwa kutumika ili wananchi waweze kupatiwa haki zao na je, ni kwa nini wasisaidiwe na Halmashauri kuvuta maji ya bomba katika Mto huo Lukosi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazojitokeza katika kutoa vibali vya uvunaji miti msitu wa Taifa wa Sao Hill, kumekuwa na malalamiko makubwa sana ya wananchi katika utoaji wa vibali vya kuvuna miti katika msitu wa Taifa wa Sao Hill. Ninaomba kujua utaratibu unaotumika na Serikali inatambua hilo? Je, ili kuondoa tatizo hilo nini mkakati wa Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wabunge tumekuwa tukiombwa kuchangia katika taasisi za elimu, afya na hata jamii, je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwapatia vibali hivyo vya uvunaji ili kuweza kusaidia jamii na Serikali katika kupunguza changamoto ambazo huwa zinajitokeza wakati tukiwa kwenye ziara za kikazi katika Majimbo na Mikoa kwa ujumla? Ninaomba kupatiwa jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la majengo ya kale (Miji Mkongwe); Tanzania tunaongeza pato la nchi kwa utalii kwa sababu tuna vivutio vingi lakini Serikali yetu inashindwa kukarabati baadhi ya vivutio kama magofu ya kale yaliyopo Bagamoyo, Kilwa na kadhalika. Ni lazima Serikali ikarabati magofu haya ili tuweze kuongeza mapato ya nchi katika sekta hii ya utalii ili wananchi waweze kunufaika kwa kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali itenge bajeti ya kutosha kukarabati magofu haya ya kale. Mji wa Bagamoyo ni kivutio kikubwa sana kwa watalii. Maeneo ya Bagamoyo na Zanzibar yametaka kufanana ramani ya Mji Mkongwe Bagamoyo imeanza kupotea kwa sababu wananchi wanauza maeneo hayo na wafanyabiashara wanununa maeneo haya na kujenga majengo mapya na kuondosha vivutio vya watalii. Serikali isipodhibiti hali hii ya uharibifu wa vivutio vya utalii tunaweza kupoteza vivutio vya utalii kwa miaka ya mbele na kukosa watalii katika Mji wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vituo vilivyokuwa vikipitisha watumwa (bandari) zimesahauliwa na bandari hizi ni vivutio kwa watalii. Baadhi ya watalii wanapofika Zanzibar ni lazima waende na Bagamoyo kwani Bagamoyo ni kivutio kikubwa kwa watalii. Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti majumba ya Mji Mkongwe wa Bagamoyo ambapo wananchi wamekuwa wakibomoa na kujenga majengo mapya na kupoteza ramani ya Mji Mkongwe. Je, ni lini Serikali itatenga bajeti ya kutosha katika sekta hii ya utalii na kukarabati maeneo ya Mji Mkongwe ili tuzidi kuongeza Pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la hoteli za kitalii; Tanzania tuna hoteli nydingi za kitalii lakini Watanzania wamekuwa wanapata shida wanapoenda kuomba kazi katika hoteli kwani wanaopewa kipaumbele ni wageni kutoka nchi jirani na siyo Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya wawekezaji wanaowekeza katika sekta ya hoteli wanapokuwa wamekodi hoteli wakishindwa kulipa kodi wanabadilisha majina ya hoteli hizo au hao wawekezaji wanawakodisha watu wengine na kubadilisha majina ya hoteli kwa kukwepa kulipa kodi. Wawekezaji wakija kuwekeza katika sekta ya hoteli ni lazima Watanzania wapewe

kipaumbele kwani kuna vijana wengi hawana ajira na wana uwezo wa kufanya kazi hotelini.

Je, Serikali imejipangaje kudhibiti ukwepaji wa kodi katika sekta hii ya hoteli za kitalii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Balozi zetu kutangaza utalii; nchi za wenzetu wamekuwa wakitumia Balozi zao kutangaza utalii. Kwa sababu sisi tuna vivutio vingi kuliko hizo nchi za wenzetu kama tusipotangaza utalii wetu ipasavyo hatutoweza kupata watalii wa kutosha. Kwa mfano ukitoka na ndege Uingereza ukifika Kenya watalii wengi wanashuka kiwanja cha ndege cha Kenya. Kwa maana hiyo Kenya wametuzidi kwa kutangaza utalii. Je, ni lini Serikali itatenga bajeti ya kutosha kufanya matangazo ya vivutio vyetu vya utalii nje ya nchi?

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la malisho katika Jimbo la Ushetu, napenda kushauri na kuomba Wizara iturejeshee msitu wa Usumbwa uliochukuliwa na Serikali mwaka 2002 ili wananchi wapate sehemu ya malisho na kushiriki kikamilifu kuhifadhi Mbuga ya Kigosi-Moyowosi. Ushetu tumeanza kutoa hamasa ya wananchi kushiriki katika hifadhi kwa kutozana faini za kimila ili kuzuia uharibifu, shida yetu ni eneo la malisho.

Pili niombe na kushauri tupewe eneo la msitu wa akiba wa Ushetu/Ubagwe ili tupate eneo la malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano; naomba sana Wizara itoe ushirikiano kwa wananchi na Wabunge wanaopakana na hifadhi, mashirika mbalimbali ikiwemo ya dini, vikundi na uongozi wa kimila ili tuzungumze namna bora ya kutatua migogoro katika maeneo yetu baina ya wahifadhi na wananchi ama wafugaji.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo mengi kwa wananchi hasa wakazi wa maeneo ya karibu na hifadhi. Wananchi wanataka kulima na kufuga, maeneo wanayoishi yamejaa, hayawatoshi. Wanaona kuna eneo jirani miaka yote lipo wazi na lina rutuba nzuri ya kilimo, wanaingia kulima na kufuga, wanakamatwa na kufunguliwa mashtaka ya uvamizi wa Hifadhi ya Taifa. Nini maana ya neno hifadhi ya Taifa maana isijekuwa inatumika sivyo. Hifadhi haina zuio lolote la mipaka inayojulikana kwa kijiji ikiwamo vibao vya kutambulisha hifadhi au fence.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi haina hata wanayamapor; kama ni hifadhi ya ardhi kwa wananchi kuitumia baadae basi ijulikane ni kwa matumizi yapi na hiyo baadae labda ndio imefika sasa kwa maana hifadhi nyingi za aina hiyo zimetengwa tokea ukoloni na zingine ni zaidi ya miaka 40. Je, Serikali ina mipango gani ya kutambulisha maeneo ya uhalisia wa leo na mwaka ulioanza kuwa hifadhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii; utalii unajulikana kwa matangazo. Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa vivutio vya utalii ya kwanza ikiwa ni Brazil, lakini ni nchi inayopata watalii wachache sana kulinganisha na nchi zeny vivutio vichache. Watalii milioni moja tu wakati vivutio kibao, amani na utulivu inakuwaje nchi kama Misri yeye tatizo la usalama inapata watalii zaidi ya milioni ishirini kwa mwaka? Nchi kama Mauritania yeye vivutio vichache mno nayo inatushinda? Je, Wizara kweli inafanya matangazo? Makampuni ya utalii yanajihusishaje na kuza utalii? Tunayo kweli makampuni ya utali maarufu ya kimataifa? Tunahitaji kuona utalii ukitangazwa kila kona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Ndege ni zao kubwa la utalii. ATCL haipo Kimataifa; ni nini mipango ya Serikali kufanya biashara ya utalii na ATCL kwa makampuni ya utalii kuwa na hisa ATCL? Ushauri wangu kwa Wizara ni kuhamasisha bidhaa za Tanzania hasa kazi za mikono kuuzwa kwenye maduka ya airports kubwa kama London - Heathrow, Schiphol - Amsterdam, Frankfurt - German na kadhalika. Jina Tanzania lionekane kila sehemu, linakuza hamu ya watu kuja kufanya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia unaweza kufanya mikakati ya kuandaa vijana 100 kwenye miji mikubwa yeye watalii na kumvalisha nguo zeny maandishi ya Tanzania huku wakishikilia mabango na kuzunguka mitaani. Vijana hao wanalipwa ujira mdogo tu. Wizara ihakikishe jina Tanzania linasikika kila kona ya dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi zinazotozwa kwenye *hotels* za kitalii ni kubwa au ni *hotels* zenyewe maana *hotels* ni ghali sana ikiwemo chakula. Watalii wengi wanaokuja nchini ni wale ambao wamejibana kwa muda mrefu hivyo kutokuwa na pesa nyingi kutosheleza matumizi makubwa. Tuweke bei nafuu kuvutia watalii kuja nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri Mheshimiwa Maghembe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Maofisa Watendaji wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na mipango mizuri ya kuboresha shughuli za Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina vivutio vingi vya utalii, lakini kwa uzoefu wa muda mrefu utalii huu umeonekana kuwa ni kwa ajili ya wageni tu wanaokuja Tanzania kufanya ziara za utalii nchini. Iko haja sasa kwa Wizara kuhamasisha utalii wa ndani ili na Watanzania nao wafaidi utalii na Taifa lipate kipato kutokana na hili. Serikali iweke mikakati mahsus ya kuwavutia Watanzania wengi zaidi kushiriki katika utalii wa ndani. Makundi mbalimbali ya kijamii yawekewe vivutio na mikakati ya kutembelea maeneo ya utalii. Wizara kupitia Maofisa Maliasili waandae ratiba katika maeneo waliyomo ili watembelee vivutio vilivyo karibu na maeneo yao. Hii itajenga utumiaji wa utalii kidogo kidogo hadi hili lizoeleke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wapewe hamasa wakatembelee vivutio hivyo pamoja na kupanda Mlima Kilimanjaro na kufaidi mlima wetu ulioliletea sifa kubwa Taifa letu. Niwahimize Serikali kuwekeza kwenye matangazo ya ndani kwa kutangaza vivutio vilivyomo nchini ili wananchi watamani kuvitembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuibua mazao mengine tofauti ya utalii ili kuvutia utalii zaidi, kushirikisha maeneo mengi zaidi na wadau wengi nchini kwenye shughuli za utalii na kujenga ajira na kuongeza mapato ya wananchi na Taifa kwa ujumla maeneo mengi ya Tanzania hasa ya milimani, kwenye maporomoko ya maji kuna fursa nzuri ya utalii wa jiografia kama *mountain trekking, hiking, photographic tourism, cultural tourism* na kadhalika. Utalii huu unaofanywa na jamii, vijiji na watalii wanapendelea kujifunza juu ya maisha yetu na utamaduni wetu. Ileje na Mkoa wa Songwe kwa ujumla wana fursa nyingi za *cultural geographic tourism* na Serikali iangalie jinsi ya kuboresha aina hii ya utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lleje ina misitu yenyeye aina ya nyani wa kipekee *black and white collobus* ambaye hapatikani sehemu nyingine yoyote. Mapori ya Kitulo yana aina ya maua ya *orchids* ambayo aina yake hazipatikani sehemu nyingine yoyote. Songwe, Mbeya na Nyanda za Juu Kusini kuna fursa nyingi sana za utalii kuanzia Udzungwa, Ruaha, vinajenga utalii wa *Southern circuit*, kwa hiyo Serikali sasa ihamishe nguvu kwenda kuendeleza utalii katika *Southern circuit* na ijumuishie aina zote za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Songea na Mbeya wana utamaduni wa ngoma za kimila nzuri sana ambazo zingeweza kuwa sehemu ya utalii wa kiutamaduni. Hii ni fursa ya ajira kwa wananchi na mapato kwa Taifa. Nataka kuhamasisha Serikali kupitia Maofisa Maliasili wa Wilaya kuhakikisha kuwa wanaanza kuangalia utalii vilevile kwenye maeneo yao badala ya kujikita kwenye magogo na mazao ya misitu peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mabenki kama CBA yaliyojitekeza kutoa malipo kwa wawekezaji wa ndani kwenye sekta hii ya utalii, kwa hiyo, Maafisa Maliasili waibue maeneo haya ya uwekezaji ili wananchi wayafanyie utaratibu wa kuwekeza. Watanzania wenzangu tubadilike na tuanze kushiriki utalii wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya utangazaji wa utalii ni ndogo sana Tanzania ukillinganisha na nchi jirani. Changamoto kubwa ya kukua kwa utalii nchini ni kukosa kufanya utalii vya kutosha. Vivutio vya utalii vitangazwe zaidi kwa watalii wa ndani na wa nje ili vivutio vifahamike na watalii waongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ni ndogo sana ukiitazama kuwa Tanzania inaongoza kwa vivutio vya utalii na kuliingizia Taifa pato kubwa. Inasikilitisha sana kuwa bajeti ya Wizara hii ni ndogo wakati Taifa linategemea sana sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii haipo kwenye mpango wa BRN pamoja na sekta hii kuchangia pato kubwa la Taifa. Hii ni hitilafu kubwa na inatakiwa irekebishwe haraka na Serikali itoe tamko juu ya mikakati yote hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuongeza uwekezaji katika vivutio vya utalii kwa mfano kuna huduma hafifu hasa vituo vya kufikia watalii kama hoteli, huduma ya kwanza kwenye vivutio kama Mlima Kilimanjaro. Huduma ya vyoo vizuri na sehemu za kupumzika. Gharama za kupanda Mlima Kilimanjaro ni kubwa na wananchi wa kawaida watashindwa kufaidi. Upatikanaji wa chupa za oxygen karibu na kileleni, kuwezesha Watanzania kuwekeza kwenye miradi ya utalii katika ngazi zote Wilayani. Serikali itoe tamko juu ya mkakati wa kuendeleza utalii katika ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ufinyu wa bajeti bado Bodi ya Utalii haifanyi kazi kwa kujituma, ubunifu wa maarifa yako mengi wangeweza kufanya kwa kutangaza utalii kwa kushirikisha wadau kwenye maonyesho ambayo watalipia wenyewe au kutumia fursa za maonyesho mengine na mikutano mikubwa ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe kipaumbele kwenye kujenga miundombinu mizuri katika maeneo ya kitalii. Serikali imefanya nini katika mbinu kuhakikisha wanaweka kipaumbele kuonesha miundombinu ya biashara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupendekeza kuwa Serikali iondoe kwa miaka mitatu kodi na ushuru kwenye uwekezaji katika mahotelii ya kitalii, kuruhusu wawekezaji kujenga hoteli za kitalii za kiwango cha nyota tatu hadi

tano. Katika kipindi chote cha ujenzi mwekezaji asitozwe chochote akimaliza na uendeshaji ukiaanza atozwe asilimia 15 mwaka wa kwanza na ikifika mwaka wa tatu wa uendeshaji aliye kodi zote, hii itaiwezesha Tanzania kupata vitanda vinyavyotosheleza mahitaji na kupata watalii wengi. Pia hoteli zilizopo waboreshe miundombinu na huduma kwa kupatiwa mafunzo na wafanyakazi wenye uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji wa nyuki, Tanzania ina fursa sana na nzuri za kuzalisha asali kwa wingi duniani ambayo ikitumiwa ipasavyo itasaidia kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Tanzania ni nchi ya pili Barani Afrika na inazalisha tani 56,000. Hata hivyo, kiwango hicho ni kidogo kwa sababu Tanzania ina uwezo wa kuzalisha asali tani milioni 1,038 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ninaloliona ni utashi hafifu wa jamii kujishughulisha na kazi za ufugaji nyuki na kupanda miti kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira. Serikali kupitia Maafisa Maliasili wahamasishe vya kutosha jamii juu ya faida ya ufugaji nyuki na upandaji miti ili iletu matokeo ya haraka kwa sababu asali ina faida kubwa ikiwemo ya kiafya na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe teknolojia ya kisasa inatumika kwenye ufugaji wa nyuki na kupanda miti. Idara ya Misitu iachane na shughuli za uchuuzi wa magogo na ukataji miti kiholela na badala yake wajikite kwenye upandaji miti ya kibashara na kuhifadhi mazingira na hivyo hudumisha mazingira bora ya kuishi pamoja na ufugaji wa nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkao wa Songwe na eneo lote la Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini, Rukwa kuna fursa kubwa sana kupanda miti na kufuga nyuki na hata kuendeleza utalii wa kitamaduni, kijiografia ki-photographic kuwepo kwa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Songwe ni fursa kubwa ya kuboresha utalii na uhifadhi wa misitu na kukuza utalii katika Sourthen circuit.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali kupitia Wizara hii kutumia Idara ya Misitu kutusambazia miche ya miti na mizinga ya nyuki ya kisasa. Pia kushirikisha sekta binafsi katika utalii kwa kupunguza tozo nydingi zinazowazidishia gharama na kupunguza idadi ya watalii.

Lakini pia kuunganisha watalii na wajasiriamali wadogo wadogo wanaotoa huduma na kutengeneza bidhaa za sanaa na kuwauzia watalii, kutoa mafunzo unganishi yatakayoweka programu za mafunzo, kuwatayarisha wananchi kwa pamoja kati ya sekta ya umma na binafsi ili ushiriki wa jamii ya wafanyakashara na wafanyakazi wa maeneo hayo kwenye shughuli za utalii na uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaunga mkono hoja.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na uongozi mzima wa Wizara hii kwa jitihada na kazi kubwa wanayofanya katika kusimamia majukumu makubwa ya Wizara hii. Wizara hii inasimamia majukumu ya rasilimali muhimu ya nchi yetu kwa maana mbuga zetu za wanyama, misitu yetu ya asili pamoja na vivutio vya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inachangia kwa kiasi kikubwa Pato letu la Taifa kutokana na ujio wa utalii, mazao mbalimbali ya asili mfano magogo ya mbao, lakini bado jitihada za dhati zinahitajika ili kusimamia maeneo haya pamoja na kuongeza usimamizi wa uvunaji wa misitu yetu, Serikali inapoteza fedha nyingi kutokana na watu wengi wasio waaminifu wanaoshirikiana na Watanzania wasio wazalendo kuhujumu misitu yetu. Lazima Wizara ihakikishe udhibiti mkubwa unafanyika. Mfano katika Jimbo langu la Kilindi, Kata ya Msanja, Kitongoji cha Twile kuna uharamia mkubwa wa ukataji wa miti na magogo hivi hawa Wakala wa Misitu (*TFS*) wanafanya kazi gani? Mimi nadhani kama hawashirikiani na wahalifu hawa basi hawajui makujumu yao, mara nyingi wanapokamata magogo haya yanapelekwa Handeni badala ya kusafirishwa Kilindi, huu ni utaratibu gani? Nashauri Wakala hawa pia ofisi zao zihamishwe au zianzishwe ama kufunguliwa Wilayani Kilindi, eneo hili la uharibifu wa misitu halina usimamizi wa dhati. Nashauri Wizara husika iangalie namna ya kuwa na njia sahihi ya kuwasimamia watumishi wasio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuchangia namna ambavyo Wizara inaweze kupanua maeneo ya utalii kwa kuongeza maeneo ya utalii. Mfano, katika Jimbo langu la Kilindi yapo maeneo mengi ya utalii ambayo tanaweza kuchangia pato la Wizara hii, mfano pori tengefu la Handeni milima ya asili ya Kimbe, milima ya Kilindi asilia, milima ya Lulago yenye miti na uoto wa asilia haya yote ni maeneo muhimu sana ambayo wataalam wake tuijenge nchi. Nashauri ijenge utaratibu wa kufuatilia haya tunapowaambia kwani yana lengo la kuchangia pato la nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuchangia ni upungufu wa wafanyakazi katika Wizara hii ambao wangkuwa na jukumu la kusimamia na kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa misitu na rasilimali ya nchi yetu, mfano katika Jimbo na Wilaya yangu ya Kilindi hatuna Afisa wa Wilaya anasimamia misitu, aliyepo ni Afisa katika ngazi ya Kata, Wizara ituletee mtumishi haraka kwani maeneo mengi katika Wilaya yanaharibiwa kwa kukosa usimamizi wa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni juu ya maeneo ya hifadhi za misitu yaliyopo karibu kabisa na mijini, hifadhi hizi pamoja na faida tunayopata ya kuhifadhi mazingira na kupata mvua lakini maeneo haya yamekuwa ni maficho ya wahalifu hasa majambazi. Mfano msitu wa pale Kipala mpakani Wilaya ya Mkuranga hifadhi hii majambazi yametumia kama mafichio na hata askari zaidi ya sita wameuwawa pale kwenye *check point*. Nashauri Wizara sasa isafishe kwa kukata miti kwa mita 50 ili kuleta ulinzi na usalama kwa wakazi wa eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naunga mkono hoja.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya ardhi kati ya wakulima, wafugafji na hifadhi ya Tarangire, kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu kati ya wananchi na hifadhi ya Tarangire, Mkoani Manyara jambo ambalo limewagharimu wananchi na hata kukosa makazi ya kuishi baada ya kutolewa katika maeneo yao kwa madai kuwa wamevamia Hifadhi ya Tarangire.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2007 wananchi wa vijiji vya Ayamango, Gedamara na Gijedabung' hawana makazi maalum wala maeneo ya kulima kujipatia kipato na hata chakula kwa ajili ya matumizi ya kawaida pamoja na kuwa Serikali inasema kuwa wamepata eneo mbadala ya kuwahamishia wananchi hao amba ni shamba la mmiliki Ufyomi Gallapo Estate. Shamba hilo ni dogo sana, halitoshi kukidhi mahitaji ya wananchi hao kulima na maeneo ya kujenga nyumba bora.

Pamoja na juhudi za Serikali kuwahaminisha wananchi hao hakuna makubaliano kati ya Serikali na mmiliki huyo na wala hakuna mukutano wa hadhara uliokaa kwa vijiji vyote hivyo kuwaeleza hatua zilizochukuliwa na Serikali kumfutia mmiliki wa Ufyumi Gallapo Estate. Ni lini Serikali itamaliza mgogoro huu kwa kuwakabidhi wananchi hao eneo mbadala ili waendelee na maisha ya kila siku ya kujitafutia riziki zao za kila siku katika shughuli za kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya wanyama Burunge, mgogoro wa vijiji vya Maweni Magara, Manyara Kisangaji na Kazaroho ni wa muda mrefu sana kati ya Juhibu na wafugaji pamoja na wakulima. Jumuiya ya Juhibu inaundwa na vijiji kumi ambayo ni Minjingu, Mdori, Kisangaji, Kazaroho, Maweni, Magara, Manyara, Ngole, Mwanda na Nkaiti. Huo ndiyo muunganiko wa vijiji kumi vilivyounda Jumuiya ya Hifadhi ya wanyama Burunge kwa makubaliano ya kutenga matumizi bora ya ardhi kwa kutenga maeneo ya wakulima, wafugaji na uhifadhi ambayo ndiyo Juhibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yatokanayo na Juhibu hugawanywa kwa vijiji wanachama kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya vijiji husika. Lakini cha kushangaza leo hii wakulima na wafugaji wanaondolewa katika maeneo yale kwa nguvu ya dola jambo ambalo ni la kikatili na unyanyasaji hata kufikia wananchi kuchomewa nyumba na mifugo na askari wa Juhibu na kuwataka wananchi hao kuhama ifikapo tarehe 1/6/2016 kwenda kwenye eneo mbadala la Mfula Ng'ombe amba ni eneo la madimbwi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba kuhusu wananchi wa vijiji vya Ayamango, Gidamara na Gijedabung' Serikali ifanye jitihada za haraka sana kuwapatia wananchi wale eneo mbadala lilitengwa hata kama ni vipande ili waendelee kuiamini Serikali yao na kuipa matumaini mapya ya kujikwamua kiuchumi na kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijiji vinavyounga Juhibu naishauri Serikali eneo lilitengwa kwa ajili ya wananchi wale kuhamia halifai kwani eneo lile la Mfula Ng'ombe lina historia ya kuwa na kichocho kutokana na madimbwi ya maji yaliyozunguka eneo lile. Hivyo halifai kwa makazi ya binadamu kuishi eneo lile.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja hii.

Kwa kuwa watu wanaongezeka lakini ardhi haiongezeki naomba Serikali ilite sheria Bungeni ifanyiwe marekebisho ili mipaka isogezwe ili kusudi wananchi wapate maeneo ya kulima. Mfano, katika Wilaya ya Kasulu lipo eneo la Kagera Nkanda eneo hili wananchi wanalima huko lakini mara nyingi wanaondolewa. Naomba Serikali iweze kumaliza tatizo hili la kuongeza mipaka ili wananchi wapate eneo la kulima. Ahsante.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya. Mchango wangu utakuwa katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii wa mambo ya kale ya kihistoria, maeneo mengi ya kihistoria yametelekezwa, hayana maendeleo yoyote. Yapo baadhi ya maeneo yamesambaratika kabisa. Maeneo ya kihistoria iwapo yanaboreshw na kutengenezwa vizuri yangeweza kuleta mapato makubwa kwa Taifa letu. Tunaenda katika nchi kama China watu walio wengi wanaenda kuangalia Great Wall. Serikali inapata fedha nyingi sana lakini India pia kuna Taj Mahal wanaingiza watalii wengi sana. Je, Tanzania tumejjipanga vipi katika

kutangaza maeneo yetu ya kihistoria badala ya kutegemea utalii wa mbuga peke yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali waangalie utalii wa kihistoria na tutangaze maeneo hayo ya kihistoria, matangazo ya utalii hayaonekani katika viwanja vya ndege, maeneo ya bandari na stendi kuu za mabasi. Waongozaji wetu wa watalii walio wengi wako Mkoa wa Arusha na maeneo ya Dar es Salaam na Bagamoyo siyo wengi sana. Lakini ma-tour guide wetu wanazidiwa na wale wa Kenya, Serikali imejipangaje katika kuwajengea uwezo watu wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, msitu wa Mwandege na misitu mingi iliyopo Mkoa wa Pwani imekuwa ni makazi ya majambazi na wezi. Serikali imefanya vizuri sana kutenga maeneo ya misitu kwa kusaidia kutunza mazingira na kuhifadhi ardhi kwa matumizi ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Dar es Salaam sasa idadi ya watu imeongezeka kwa kiasi kikubwa sana, Mbagala imejaa watu wanaelekea Mkuranga, msitu wa Mwandege uko katikati umezungukwa na makazi ya watu, watu wanaingilia hifadhi na Serikali hakuna wanachosema hatma yake ni kuwabomolea nyumba zao kwani wakati wanajenga Serikali ilikuwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe baadhi ya eneo la Msitu wa Mwandege wawape Halmashauri ya Temeke watengeneze kituo kikubwa cha mabasi ya Mikoa ya Kusini na eneo linalobaki liendelezwe kama msitu na litunzwe kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tozo za mazao ya misitu. Gharama za kupidisha kitanda kimoja kutoka Mkoa wa Pwani kwenda Dar es Salaam ni kubwa kuliko ulizununulia kitanda kijijini. Lakini fedha hizi wanazokusanya kweli zinaenda Serikali? Kwa kuwa tunasikia wafanyakazi wa vituo hivyo walio wengi siyo waaminifu ni vema sasa Serikali ikaangalia nidhamu na uadilifu wa wafanyakazi wa vituo vya ukaguzi wa mali na misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kutoa mchango wangu kwa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwa Mbunge wa Bunge hili. Pili nawashukuru wapiga kura wangu kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao, natambua imani kubwa walionayo kwangu na nawaahidi nitawatumikia kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kuonesha imani na uwezo mkubwa wa kuendesha nchi yetu, Mungu ampe umri na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne napenda kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa pamoja na Baraza lake la Mawaziri kwa kuonesha uwezo mkubwa wa kuongoza Wizara zao. Katika kuchangia hotuba ya Waziri napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ndogo ya ufugaji, kumekuwa na migogoro isiyomalizika kati ya sekta ya ufugaji na wakulima. Hili ni tatizo ambalo Wizara hii inapaswa kulishughulikia kwa namna ya pekee. Naomba Wizara ianzishe idara maalum ndani ya Wizara hii ya kushughulikia migogoro hii ili kuondosha kabisa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ndogo ya utalii, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 15 imeeleza hali ya sekta hii inavyochangia upatikanaji wa fedha. Takwimu zinaonesha kwenye ukurasa huu ni ndogo, hazilingani na namna uingiaji wa watalii katika nchi yetu. Watalii wanaoingia ni wengi sana hivyo nashauri Wizara ichukue mikakati zaidi ya kuziba mianya ya upotevu wa fedha za watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya usimamizi wa wanyama pori. Nachukua fursa hii kuipongeza Wizara kwa kuanzisha mamlaka hii ni jambo zuri katika kusimamia na kuwalinda wanyama pori wetu. Nashauri Wizara iharakishe kupeleka mamlaka hii katika Wilaya zote za nchi ili huduma hii ipatikane nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha utalii katika nchi yetu, nchi yetu ina vivutio vingi kama mbuga za wanyama, Mlima Kilimanjaro, maziwa na masilio ya kale. Serikali iongeze matangazo nchi za nje ili kuvutia watalii wengi zaidi pia usalama na amani ya nchi ni muhimu sana kuongeza hoteli na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna misitu mingi ambayo lazima ilindwe na kuvuna kwa utaratibu mzuri, haiwezekani nchi kukosa madawati katika shule zetu. Kuna wananchi wengi hasa katika maeneo ya Nanyara, Songwe na kadhalika wananyanyaswa sana na maliasili. Wengi wanapanda miti ambayo wanakata ili kuchomea chokaa, cha ajabu wanatozwa shilingi 15,000 kwa mti mmoja bila receipt naomba mfuutilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimondo cha Ndolezi Mbozi ni muhimu kikajengewa fence ili kukihifadhi na kuimarisha utalii katika eneo hilo ni muhimu sana.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja hii na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hoja mengi yana dira nzuri kwa maana ya msimamizi wa sheria. Tatizo langu ni namna watendaji na hasa wanaosimamia hifadhi ya maeneo wanapochukua sheria mikononi na kupigana, kushambulia wananchi. Wanahisiwa kuingia ndani ya maeneo hayo, Jimbo langu lina mgogoro katika maeneo mawili yaani Hifadhi ya Kipengere na Mpanga Game Reserve, vijiji vinavyopakana na maeneo haya vya Moronga, Kipengere, Masage, Wangana, Ikunga na Imalilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawana amani na maeneo yao, pamoja na kuwa vijiji hivi vimeidhinishwa na vina ramani ya mpaka jinsi wanavyonyanyaswa na Kipengere Forest Reserve.

Aidha, vijiji vya Malagali, Mpaga, Ludunga, Mambegu, Hamjarami, Igando, Iyayi, Mayole na Mpanga Game Reserve wananchi walihamishwa wakalipwa fidia kidogo na kuhamishwa wengi hata fidia hawakulipwa. Naomba sana viongozi walioko hifadhi hii ya Mpaga waondolewe kwani wameshindwa kabisa kufanya kazi na viongozi wa Wilaya, Serikali na Vijiji na Mbunge wa Wilaya ya Wapingale kwa namna wanavyochukua sheria mkononi kwa kuwapiga wananchi, kufyeka mazao na kuwanyang'anya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wanachukua rushwa, tumewakemea na Waziri nilikueleza, lakini mpaka leo hakuna hatua iliyochukuliwa. Naomba na wakati hilo halijafanyika wape maelezo viongozi wa hifadhi hizi, waache mara moja kuwashambulia raia kwenye nchi yao ili tulishughulikie tatizo la mpaka. Ili kuondoa migogoro hii pamoja na sheria lazima ziwe na manufaa kwa binadamu na uhifadhi ili sheria iwe endelevu. Sheria ilitungwa na Mipaka iliwekwa miaka mingi baada ya uhuru, wakati idadi ya watu ilikuwa ndogo tofauti na sasa, lazima wananchi wetu waongezewe eneo na hasa haya maeneo ya akiba ambayo hata wanyama hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 51 nimesoma kuwa Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamaporu umesaidia miradi ya kijamii kwenye Wilaya ya Wanging'ombe kwa kujenga Ofisi ya Kata ya Wanging'ombe, kuchimba kisima Mayale, na kununua vitanda 91 vya shule ya bweni sekondari llembula. Kwanza nashukuru kama kweli limefanyika, naomba kujua kiasi cha fedha zilizopelekwa au thamani ya vifaa kwa kila mradi.

Pili, utekelezaji wa msaada huu hufanyika vipi kwani mimi kama Mbunge ndiyo kwanza napata taarifa hii kwenye kitabu cha hotuba, sijawahi kushirikishwa wala kwenye Halmashauri ya Wanging'ombe hatujawahi kushirikishwa. Sasa hii kama fedha ya umma kwa nini ifanywe siri kwa ajenda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo ya kina.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uokoaji katika Mlima Kilimanjaro bado huduma ya uokoaji siyo nzuri. Gari halifiki kwenye *high altitude* na tunapoteza maisha ya watu huko mlimani, kwa nini TANAPA wasinunue helkopta ambayo inaweza kuokoa watu na wagonjwa kwenye *high altitude*? Hii inaweza kutumika kwenye park zote kwa ajili ya uokoaji pia kulinda majangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake waliopo *half mile* katika Mlima Kilimanjaro wananyanyaswa sana, wanapigwa na askari wanaolinda msituni, wanafikia hata kubakwa. Ikumbukwe kuwa wao ndiyo wanaolinda mlima, wanatumika kuzima moto unapowaka, wanasaidia watu wasikate miti na pia watu hutumia njia ili kwenda nyumbani. Kuna kijana alipigwa risasi akielekea nyumbani kutoka Kibosho anaitwa Kiwale, je, kesi yake imefikia wapi? Copy nimempa Mheshimiwa Waziri kwa reference.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Umbwe route* katika Mlima Kilimanjaro, *route* hii ni nzuri sana lakini *Umbwe cave* hakuna maji wala choo, watu wanajisaidia kwenye misitu, hii ni aibu wakati wageni wanalipa kuingia kwenye hifadhi, ni kwa nini wasifuatwe walipe *forest fees* na *park fees* wakati park ni moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine *Umbwe route* hakuna walinzi wa msituni na ukizingatia camp hii ipo karibu kabisa na Kibosho. Umbwe kwa wana vijiji ni rahisi watalii kuvamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *route* ya Old Moshi tayari Wizara ya Miundombinu imetenga fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara kutoka Kiboriloni, Kikarara, Kidia, mpaka Tsuduni na njia hii ni fupi kufika Uhuru Peak, kuna *water falls* na vipepeo, sasa ni lini *route* hii itaanza kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na wimbi la wazungu wanaojitokeza ku-volunteers kuja kufanya kazi, lakini sasa hivi wanachokifanya wanafanya biashara ya utalii na wanawalaza wageni majumbani katika mitaa ya Moshi, Soweto Rau na kadhalika, wanatumia biashara ya mlima bila kulipa

kodi, nashauri tour operators wote kuwe ni lazima wapeleke TALA licence na tax clearance ili kuonyesha wanalipa kodi. Hii itafanya kodi nyingi kukusanywa na itakuwa ngumu kubakiza fedha nyingi Ulaya.

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyeneweza na kunipa afya njema na uzima wa kuniwezesha leo hii nichangie kwa maandishi katika Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii ni moja ya sekta muhimu sana na kwa hakika ni sekta ambayo ikipewa msukumo wa nafasi ya kipekee, italiongeza Taifa letu fedha nyingi. Mbuga zetu za hifadhi ambazo ni vivutio vya watalii zinahitaji kuwekewa mazingira mazuri ambayo yatawawutia watalii, naomba nitoe mifano miwili ya mbuga za Ruaha na Saadani, barabara ya kutoka Iringa Mjini kwenda Mbuga ya Ruaha siyo ya kiwango cha lami, na vivyo hivyo barabara itokayo Tanga kwenda Pangani hadi Saadani ni mbuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii naiomba Serikali iangalie kwa jicho la kipekee kama biashara nyingine zilivyo na ushindani, Serikali iongeze kasi katika kuutangaza utalii wetu. Bodi ya Utalii ishirikiane na wadau mbalimbali wa sekta binafsi kufanya jithhada hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba nzuri yenyewe kuonesha mwelekeo, nampongeza pia Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara na nawatakia kila la kheri, wasonge mbele na kasi hii ya hapa kazi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hotuba ya Bajeti ya Wizara yako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la maliasili ni pamoja na Hifadhi za Taifa (TANAPA), bahari, mito, misitu na mbuga za wanyama au hifadhi. Tanga tunazo mbuga au hifadhi kama Mwalajembe, Kalalani, Mkomazi na Saadani, lakini bado hazijatangazwa katika medani za kitaifa, kiasi kikubwa cha kutosha. Naiomba Wizara yako ihakikishe inazitangaza mbuga za Mkomazi, Mwakijembe, Kalamani na Saadani katika viwango vya kimataifa ili ziweze kujulikana na kutembelewa na watalii wa ndani na nje na kuingiza mapato ya fedha za kigeni (*foreign currency*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapokuja watalii ajira zinaongezeka, kutajengwa hoteli, zitaajiri wahudumu pia wasafirishaji maliasili, pamoja na misitu. Napenda kuzungumzia utunzaji wa misitu ya nchi kavu na baharini.

Tanga tunayo misitu ya mikoko ambayo imewekewa utaratibu na inalindwa na coastal zone. Katika sehemu nyingine mikoko inavunwa, kukatwa kiholela, baadhi ya maeneo ya ukanda wa Pwani kuna haja ya kusimamia vizuri kwani mikoko inakatwa kwa kutumia medani/itikadi za vyama vya siasa, viongozi wanauzwa mikoko na ardhi zenyet vyano vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika biashara ya mkaa nayo itamaliza misitu yetu, nashauri Serikali na Wizara itafute njia mbadala kwa wachomaji wa mkaa. Ibibidi Wizara ikopeshe matrekta kwa wachomaji mkaa ili badala ya kuchoma mkaa waanze kujielekeza katika kilimo cha kibiashara na wakopeshwe pembejio. Katika nchi za SADC ni Tanzania pekee unaposafiri ndiyo pembezoni mwa barabara unaona magunia ya mkaa na mizigo ya kuni pembezoni mwa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo kuna shughuli za utalii au maliasili na ikiwa kuna mapato yanaingia asilimia 20 zirudi katika eneo husika. Ibibidi isiwe fedha, ziwe samani au vifaa kama madawati, ujenzi wa zahanati na kadhalika. Naomba Tanga Mjini isikose madawati ya TANAPA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumezuka tabia ya kuibwa wanyama pori wetu, ndege wetu na viumbe hai na kupelekwa nchi mbalimbali za Ulaya, Marekani na Asia, je, ni akina nani wanaofanya biashara hii haramu? Lazima nchi idai rasilimali zake na itunze viumbe hai hawa na anayehusika akipatikana hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tulitegemea labda tungepata wachangiaji wachache upande wa Serikali lakini wametimia, kwa hiyo, namuita sasa Mheshimiwa January Makamba dakika kumi, Mheshimiwa Muhongo dakika kumi, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) dakika kumi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa ya kuchangia katika hoja hii.

Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu yao nzima, kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa hotuba nzuri waliyoitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba nafarijika sana kwamba kama Taifa, sasa tumefika tuna mjadala kuhusu matumizi ya rasilimali ya asili, ikiwemo ardhi kwa maendeleo yetu. Nafarijika kwamba sasa tuna mjadala kuhusu uhusiano kati ya mazingira na maendeleo, naamini kwamba

mjadala huu unaweza kufanya kwa busara, kwa hekima, bila jazba, wala vitisho ili tuweze kupata muafaka katika jambo hili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka awali ni kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ni Serikali ya wakulima, Serikali ya wavuvi, Serikali ya wafugaji, Serikali ya watu wanaofanya shughuli zote katika nchi hii. Asiondoke mtu na dhana hapa, kwamba Serikali ya Awamu ya Tano au Waziri katika Serikali ya Awamu ya Tano anapendelea kundi moja au lingine katika Taifa letu. Hilo siyo kweli na halipo tumechaguliwa na watu wote, tumechaguliwa na kura za Watanzania wote.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1961, kwenye Mkutano uliofanyika Arusha mwezi Septemba, Rais wa Tanganyika wakati ule Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alitoa hotuba ambayo ndiyo iliweka msingi wa uhifadhi ambao tunaendelea nao leo, Mwalimu Nyerere alisema, inaitwa Arusha Manifesto, kipande kimoja kizuri sana ambacho kwa kifupi kilisema, kwamba sisi kama Taifa tumepewa dhamana ya kuhifadhi wanyama pamoja na maeneo ambayo wanyama wanaishi na tumepewa dhamana hiyo kwa ajili ya enjoyment ya hivyo vitu, lakini pia kwa sababu ya uhai na maisha yetu yanayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi wa misitu na uhifadhi wa wanyamapor, siyo kwa ajili ya misitu, siyo kwa ajili ya wanyamapor peke yake. Hifadhi ya misitu na hifadhi ya wanyamapor una uhusiano wa moja kwa moja na upatikanaji wa mvua na upatikanaji wa mvua, una uhusiano wa moja kwa moja na maendeleo ya kilimo, upatikanaji wa mvua una uhusiano na upatikanaji wa malisho. Kwa hiyo, hifadhi ya misitu ina uhusiano na ustawi wa ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu inatoa huduma za kiikolojia ambazo zinafanya nchi yetu ipumue. Sasa hapa kumekuwa na mjadala, kana kwamba uhifadhi na ufugaji ni kama lila na fila hazifungamani. Uhifadhi na ufugaji siyo dichotomous, tunaweza kufanya vyote kwa wakati mmoja na tukafanya vizuri kabisa. Kuna dhana inajengwa kwamba hapa kuna ukinzani kati ya ufugaji na utalii. Msingi premise ya huo mjadala siyo sahihi. Kama Taifa tuna uwezo wa kufuga na kunufaika na ufugaji na tuna uwezo wa kuhifadhi na kunufaika na manufaa ya uhifadhi. Isijengwe dhana kwamba hizi ni shughuli zinazokinzana kwa hiyo lazima tuchague moja siyo kweli, kwa miaka yote tumekuwa tunafanya mambo yote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio sahihi cha wafugaji ni kwamba, kila mfugaji apatiwe eneo na amilikishwe eneo la kufuga, kilio sahihi cha wakulima ni kwamba kila mkulima apatiwe eneo na amilikishwe na hii ndiyo ahadi yetu

Chama cha Mapinduzi, kwamba kila mfugaji na kila mkulima atamilikishwa eneo lake ili wafanye shughuli zao kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha migogoro inayozungumzwa siyo shughuli watu wanazofanya. Chanzo cha migogoro inayozungumzwa ni kwamba maeneo haya hayakupimwa na ndiyo maana Waziri Mheshimiwa Lukuvi alikuja katika hotuba yake na mpango mkubwa wa matumizi ya ardhi pamoja na upimaji wa ardhi ambao utapelekea kupunguza migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha msingi sisi kama Taifa ni kwamba shughuli zile ambazo tunaamini zinaharibu mazingira ni lazima zifanyike kwa tija. Inawezekana kabisa kwamba kwenye kilimo, katika heka moja kama tutaweza kupata tani nyingi zaidi za mahindi, basi haihitajiki ardhi kubwa zaidi ili kuweza kupata manufaa. Vilevile katika ufugaji inawezekana kabisa kwamba ukafuga katika eneo na hautalazimika kutafuta eneo lingine lakini ukanufaika na manufaa ya ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ufugaji udumu kwa miaka 100 ijayo, lazima tuhakishe kwamba tunalinda kile tunaita *natural capital*. Katika dunia hii nchi zinatofautiana na utajiri wa rasilimali asili. Tanzania tunayo, inawezekana hatuna mtaji mkubwa wa kifedha, lakini tunao utajiri mkubwa wa *natural capital*, tunaweza tukaamua hapa Bungeni kwamba basi tufuge vizuri kwa miaka 20 ijayo, lakini baada ya hapo hakuna ufugaji tena, hakuna kilimo tena na hakuna mazingira tena. Kwa hiyo, katika mambo ambayo Serikali inayapanga kuyafanya, ni kuhakikisha kwamba shughuli hizi watu wetu wanazofanya zinadumu katika miaka mingi ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu mfumo wake wa kiikolojia una mito na mabonde mengi ambayo ndiyo yanafanya maisha yetu yawezekane, tunayo mito mikubwa Mto Pangani, Mto Ruvu, Mto Ruaha na mingineyo. Sehemu kubwa ya vyanzo vya mito hii ni kwenye maeneo yaliyohifadhiwa. Tukitaka Taifa letu life, mito hii itoweke, mabonde haya ambayo yana-sustain uhai wetu yatoweke, basi tusijali hifadhi ya misitu na hifadhi ya maeneo haya. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kwamba watu wameongezeka, mifugo imeongezeka, kwa hiyo basi tugawe. Ukweli ni kwamba kwa sababu hiyo kwamba watu wameongezeka ndiyo uhifadhi unahitajika zaidi. Katika nchi ndogo kisiwa Uingereza wamehifadhi asilimia 25 pamoja na kuwa na tatizo kubwa la ardhi katika ile nchi, asilimia 25 imehifadhiwa na bado maisha yanaendelea nasi kadri tunavyoendelea kama Taifa, shughuli zetu zitakuwa za tija zaidi na zitaondoka katika matumizi ya ardhi zaidi, na tutaweza ku-sustain maisha yetu bila shaka yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hapa bila shaka yoyote, kwamba binadamu ndio tunasemekana kwamba ni wanyama wenyewe akili kuliko wanyama wote. Tukishindwa kuhifadhi rasilimali asili, zinazowezesha maisha yetu leo, tukishindwa kuhifadhi rasilimali asili kwa watoto wetu na wajukuu wa wajukuu wetu, basi heshima yetu binadamu kama mnyama mwenye akili kuliko wote itabidi itiliwe shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa kusema kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inawajali wakulima na wafugaji katika usawa wao. Serikali ya Awamu ya Tano haipo hapa kusema shughuli hii ni bora kuliko shughuli ile nyingine, ili mradi shughuli inaendesha maisha ya watu wetu kwetu ni shughuli muhimu na tutahakikisha kwamba wanayoifanya wananaufaika. Wakati huo tunahifadhi nchi yetu kwa sababu sisi tumekabidhiwa tunapita, kuna wajukuu wetu na wajukuu wa wajukuu zetu watakuja kupita, na watakuja kutushangaa, kwamba urithi tuliopewa sisi tulioachiwa na walioachia nchi hii, tumeuharibu kana kwamba ndiyo watu wa mwisho kuishi katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Muhongo, ajiandae Mheshimiwa AG.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utazidi kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna umuhimu wa kuunga mkono bajeti hii kwa sababu inaanza safari ambayo tulikuwa hatuna. Michango ya Wabunge wengine wamesema kwamba mjusi arudishwe, mjusi wetu, naomba niwapatie ufanuzi kidogo kuhusu huyo mjusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjusi huyu *dinosaur* ameanza kupatikana kwenye dunia yetu miaka milioni 231.4 iliyopita na yeye ndiye aliyekuwa kiumbe muhimu kwa zaidi ya miaka 135 iliyofuata. Mjusi huyu ana uzito wa kilo kati ya tani 50 na tani 70, urefu wake unatofautiana, lakini anaweza kuwa na urefu ambao unalingana na ghorofa sita. Mjusi wetu yuko Humboldt Museum ambayo zamani ilikuwa Ujerumani ya Mashariki, mimi nilikuwa naishi Berlin ya Magharibi yaani Ujerumani Magharibi. Nimeenda pale mara nyingi, nadhani zaidi ya mara mia moja.

Waheshimiwa Wabunge, nataka kuwaeleza ukweli ni kwamba hatuna uwezo wa kumrudisha na hatuna uwezo wa kumtunza, huo ndiyo ukweli kabisa. Tunachopaswa kufanya ni kujadiliana namna ya kupata yale mapato tugawane na Serikali ya Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri wengine ambao tunafahamu yote hayo, siyo kwamba majadiliano hayaajaanza, majadiliano tumeyafanya nadhani hata miezi miwili nyuma, nilikuwa najadiliana na Balozi wa Ujerumanu na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Ujerumanu namna ya kuweza kupata hilo pato. Ndugu zangu ukitaka kujua kwamba hatuwezi siyo kwamba tunahitaji muda kufikia hiyo ngazi hiyo, ukienda kwenye museum yetu Nyumba ya Makumbusho hii ukiangalia na kuangalia museum zingine duniani, utaona kuna tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo huyu mijusi tunafahamu na hawa mijusi (*dinosaurs*) wako familia zaidi ya 15, hawapatikani kwetu tu wanapatikana dunia nzima ndiyo maana kuna Jurassic Park. Kwa hiyo, tumuombe Mheshimiwa Waziri na wengine ambao tuna-connections huko tuendelee na mjadala wa kugawana yale mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mgogoro wa wakulima na wafugaji. Ndugu zangu tulioongea hapa tumeona kuna mwingine anavutia wafugaji, mwingine anavutia upande wa wakulima, vitu hivi lazima tuvikubali. Miaka 50 ijayo watakaokuwa kwenye hili Bunge, tuliyoyajadili hawatayajadili kwa namna hiyo, kwa sababu tuna imani watakuwa na kilimo bora, watakuwa na ufugaji bora, hawatakuwa watu wanajadili ukubwa wa maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sayansi inakokwenda inataka eneo linalolingana na hili Bunge letu liweze likalisha Mkoa mzima kwa mwaka mzima, ndiko huko tunakokwenda sayansi inatupeleka huko, maana yake kuna C<sub>4</sub> plants na C<sub>3</sub> ambayo inatumia carbon dioxide nyingi, mimea inakua kwa haraka sana, mtu anavuna mara tatu, mara nne, mara tano. Sasa suala siyo eneo, hapa ugomvi wetu kwa wakulima na wafugaji tatizo siyo eneo, tatizo ni matumizi madogo sana ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Watanzania mwaka 1950 tulikuwa watu milioni 7.7, mwaka jana tumefika milioni 53.5, mwaka 2050 tutakuwa watu karibu milioni 138 eneo ni lilelile la ukubwa wa 0.97 square kilometers million. Sasa tatizo hapa siyo maeneo, tatizo ni deployment of science, innovation na technologies ndiyo tatizo. Kwa hiyo, bajeti ya Mheshimiwa Profesa Maghembe tuipitishe tujipange kutumia sayansi na ubunifu zaidi kuliko kugombania ukubwa wa maeneo. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia takwimu zinavyoonesha, kilimo chetu cha pamba hekta moja Tanzania tunatoa kilo 147, Malawi kilo 269, China kilo 1,524, Brazil kilo 1,530 hapa tatizo siyo eneo. Kwa hekta moja mwingine anazalisha zaidi. Mahindi juzi Namibia ambayo ni jangwa wamefikisha tani 11 kwa hekta moja, Tanzania bado tuko chini kabisa. Mihogo nchi ya Niger ni nchi jangwa kabisa, Niger wao wanazalisha tani 22 za muhogo kwa hekta moja,

Tanzania tuko chini ya tani 10. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge tatizo hapa siyo maeneo tusimalizane, tatizo hapa ni utumizi mdogo wa sayansi, teknolojia na ubunifu, kwa hiyo Mheshimiwa Maghembe bajeti yake tuipitishe tu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maziwa, hawa ng'ombe tunaowapigania wafugaji hatuna ng'ombe wazuri. Nimechukua aina mbili tu za ng'ombe wanaojulikana duniani kwa kutoa maziwa mengi. Mmoja anaitwa holstein yeye anatoa lita 11,428 kwa mwaka, wa kwetu hapa mzee sijui lita ngapi, Mheshimiwa Nsanzugwanko wewe ndio unafahamu mfugaji.

**MBUNGE FULANI:** Lita tano. (Kicheko)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata tatizo kwa wafugaji hapa siyo eneo, tatizo ni sayansi, technology na ubunifu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyama hapa, tatizo siyo kumtengea mtu pori la kuwinda, mnyama wa kileo hii yaani tukichukua ng'ombe, unapaswa kumfuga afikishe kilo zaidi ya 500, nyama anayoweza kuitoa bila mfupa, bila makongoro, bila nini ni kilo kati ya 340 na kilo 360. Kwa hiyo, ndugu zangu hii Wizara tuipatie bajeti, sisi wenyewe tujue kwamba matumizi yetu ya sayansi ni madogo, ndiyo maana tunagombania maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (Makofii)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninashukuru kwa kunipatia fursa hii niweze kuchangia. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia hoja hii na nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hoja hii ina- cut across kwenye Wizara nyingi ndani ya Serikali naomba kuwashauri Wabunge wote wakubali kuliko kumbana Waziri tu, kwa sababu hapo yapo ya Wizara ya Katiba na Sheria, yapo ya Ardhi, yapo ya Nishati na Madini, yako ya Kilimo na Mifugo. Leo Waziri anaonekana hapa anaongelea haya lakini peke yake hayawezi akayatatua. Kwa hiyo, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wamezungumza kwa uchungu na wametoa ushauri mzuri sana kwa Serikali naomba tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri ili aweze kuyatekeleza haya. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kushauri juu ya mambo matatu hivi ambayo yamezungumzwa hapa ya kisheria. Kwanza baadhi ya Wabunge wamezungumza mambo ambayo yanagusa utendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maamuzi yanayofanywa na Mawakili wa Serikali walioko kwenye Mikoa. Naomba kushauri mambo mengine

muwe mnanishirikisha tu kule tunayamaliza, nawaomba Wabunge hawa wanilettee hizo taarifa ili tuchukue hatua, inarahisisha zaidi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni hili ambalo limezungumzwa juu ya huu mkataba mbovu wa Kiwanda cha Mgololo (*Mgololo Paper Mills*), hili naomba kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba nimeagiza wanilettee ule mkataba kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili tushirikiane ndani ya Serikali kuangalia kama kweli kuna maeneo ambayo ni mabovu yanaweza kuboreshwa tuyafanyie kazi. Kwa sababu mikataba hii yote kwa kawaida huwa ina vipengele vya marekebisho ya mikataba ile kila wakati inapotokea. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuleta taarifa hiyo humu ndani. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaomba kulitolea ufanuzi ni jambo ambalo limezungumzwa kwa hisia nzuri na kwa ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Hili suala ni la taarifa ya Tume ya Uchunguzi na asili ya taarifa hii ni kwamba kulikuwa na Kamati Teule ya Bunge, Kamati Teule ya Bunge iliundwa kuchunguza juu ya Operesheni Tokomeza na moja wapo ya maazimio ya Bunge ilikuwa ni kwamba Serikali iunde Tume ya Uchunguzi ili kulichunguza hili suala. Kwa mujibu wa sheria ya Tume za Uchunguzi Sura ya 32 ya Sheria za Tanzania, anaewunda Tume hii kwa mujibu wa kifungu cha tatu ni Rais wa Jamhuri ya Muungano na ndiyo anaipatia Tume hii hadidu za rejea. Rais wa Jamhuri ya Muungano aliunda Tume hii kupitia *Government Notice* Na. 132 ya tarehe 2 Mei, 2014 akaipa hadidu za rejea na ika-report kwake mwezi wa nane, pia akatoa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi kwa mujibu wa Kifungu cha 21 cha Sheria hii kinaeleza hivi;

“Baada ya kupokea ripoti ya Kamishna wa Uchunguzi Rais anaweza;

(a) Endapo Rais atajiridhisha kuwa upelelezi zaidi unaweza kufanyika au mashtaka kufunguliwa atamuelekeza Mkurugenzi wa Mashtaka kulishauri Jeshi la Polisi kuhusu utaratibu unaopaswa kufanyika au kuelekeza yafunguliwe mashitaka yanayostahili;

(b) Endapo Rais atakuwa na maoni kwamba hatua nyingine stahili zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya mtu au watu ataamuru kwamba hatua hizo zichukuliwe.

(2) Pale ambapo itagundulika kuwa kulikuwa na hasara baada ya uchunguzi uliotokana na mwenendo wa mtu ye yeyote Rais anaweza kuamuru mtu anayehusika kulipa fidia kwa kiasi ambacho Waziri atathibitisha kuwa ni kiasi hicho kinachostahili.

(3) Rais anaweza kuelekeza kwamba taarifa yoyote ya Kamishna izuiliwe kutangazwa au izuiliwe kwa muda ambao Rais ataelekeza."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili Rais ameelekeza kwa taasisi zote ambazo watendaji wake wamethibitika kutenda makosa au kukiuka sheria au utaratibu zote za utelekezaji wa Operesheni Tokomeza kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria. Aidha, kuzifanyia marekebisho sheria na kanuni zilizopendekezwa kufanyiwa marekebisho. Sasa kwa kuwa hatua ambazo zimechukuliwa na Rais kwa kuelekeza taasisi mbalimbali za Serikali zinahusisha uchunguzi, siyo vyema suala hili likatolewa taarifa hadharani katika kipindi hiki na sheria inamruhusu Rais nimewasomea hiki kifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo siyo vyema na kwanza hii sio Taarifa ya Bunge ni Taarifa ya Rais, tuipe Serikali fursa aifanyie kazi haya mambo haya la sivyo tutaharibu hata uchunguzi na kile ambacho Waheshimiwa Wabunge wanataka kukifikia hawatakifikia. Huo ndiyo ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo naomba kulitolea ushauri ni hili ambalo limezungumzwa juu ya kesi ya Kamran. Kamran na wenzake watumishi wa Serikali walishitakiwa kwenye Kesi ya Uhujumu Uchumi Na. 4 ya mwaka 2011 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi. Tarehe 5 Disemba, 2014 Kamran alitiwa hatiani akiwa hayupo kwa sababu yeye alipopewa dhamana alitoroka, lakini wale wenzake watatu waliachiwa hawakuonekana na hatia. Serikali imekata rufaa katika shauri la rufaa namba moja la 2016 Mahakama Kuu Moshi, kesi hiyo ya rufaa inasikilizwa kesho Moshi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba kuwaambia kwamba Serikali imechukua hatua lakini cha pili suala hili lipo Mahakamani nawapa hizo taarifa kesi hii ya rufaa ya Serikali dhidi ya hawa watu inasikilizwa kesho Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine sambamba na hili ni kwamba hatukukaa tu hivi pale, kulikuwa pia na watumishi wengine halafu pamoja na huyu Kamran Ahmed. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imechukua hatua, imeomba Serikali ya Pakstan katika utaratibu unaoitwa *mutual legal assistance* watuasadie mambo fulani kuhusiana na tukio husika ili tuchukue hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii pia Serikali inachukua hatua naomba kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali hii iko makini inajali maslahi ya wananchi kama ambavyo mnaishauri hapa, mtupe fursa tutekeleze yale ambayo tunaweza kuyatekeleza mambo mengine hayana *shortcut*, hatuwezi kuchukua bunduki tukailazimisha Serikali ya Pakstani itupatie vitu fulani ambavyo walikusudia kutupatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa ushauri huo naomba kuunga mkono hoja. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri dakika kumi na tano, jiandae Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa madhumuni ya kuchangia hoja, wakati nikifanya hivyo niweze pia kama Naibu Waziri kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakishiriki katika majadiliano ya hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa wema wake na kwa fadhili zake kutujalia afya njema ya kuwa hapa kwenye Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wetu kwa Taifa. Aidha, nachukua fursa hii muhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri wa Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nampongeza pia Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge, kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge letu la Kumi na Moja katika Awamu ya Tano ya uongozi wa nchi yetu, nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa au kuteuliwa kubeba dhamana ya kuwakilisha wananchi na kutenda kazi katika Bunge hili kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa na kuendelea kulisaidia Bunge kuitia Kamati zao, Bunge kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba na ya Kikanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya Mwenyekiti wake Mhandisi Atashasta Justice Nditi, Makamu wake Mheshimiwa Kemilemba Julius Lwota na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa namna ambavyo wameendelea kuishauri Wizara yetu ili kufanya sekta ya maliasili na utalii ifikie malengo yake ya kuchangia zaidi katika ukuaji wa uchumi, kuwaongezea wananchi kipato, kuongeza fursa za ajira na kuboresha huduma za kijamii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kunateua kubeba dhamana hii kubwa ya kumsaidia Waziri wangu kuisimamia sekta hii ya maliasili na utalii nchini. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa nitamsaidia Waziri wangu kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi katika eneo la sekta ya maliasili na utalii ili kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali itakayokuwa inatolewa mara kwa mara kuyafikia malengo yake. (Makofi)

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu nawashukuru wapiga kura na wananchi kwa ujumla wa Jimbo la Tunduru Kaskazini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na kwamba nipo njiani, mara tu baada ya kukamilisha jukumu hili la Kitaifa tutaungana pamoja katika kuendeleza utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa Jimbo na kwa Wilaya nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze katika ufanuzi wa hoja. Napenda nianze kwanza kabisa kwa kusema kwamba michango yote iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni yenye afya na ni michango yenye malengo mazuri ukiacha kasoro za hapa na pale, lakini kwa ujumla wake ni michango ambayo kweli tunaipokea na mingi tutaifanya kazi ili iweze kuongeza tija katika mafanikio ya Wizara. Jukumu letu kama Wizara au jukumu letu kama Serikali katika sekta hii ni kupokea na kuyafanya kazi maoni hayo na ushauri wote tuliuopokea kwa sababu huko ndiko kukubali kushauriwa na kusimamiwa kwa mujibu wa Katiba hiyo ndio kazi ya Bunge.

Maliasili na utalii ajenda yake kubwa ni uhifadhi. Napenda nirudie katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii ajenda kubwa ni uhifadhi. Tunapaswa kuhifadhi tulichonacho, tunapaswa kukilinda tulichonacho kinachotutofautisha sisi na nchi zingine au na maeneo mengine ambayo ni nje ya Tanzania na hilo ndilo linalotufanya sasa hata tuzungumzie utalii kwa sababu wanaokuja hapa wanakuja kuona vitu ambavyo kwao havipo na vinaweza vikaendelea kuwepo na kuboreshwa ili tuweze sasa kuweza kufikia malengo ya kukidhi haja ya watalii.

Sasa wakati tukiwa tunajipanga upya kwenye maeneo ambayo yana kasoro na mapungufu ya hapa na pale, kwa sababu haiwezekani kuwa hakuna maeneo ambayo yanahitaji kufanya vizuri zaidi. Mimi nina msemo wangu siku zote huwa naurudia mara kwa mara, huwa nasema hakuna mwisho wa kufanya vizuri, kila wakati utakapodhani umefanya vizuri bado kuna namna bora zaidi ya kufanya vizuri zaidi. Sasa kwa sababu hiyo, tunataka tubaki pale pale kwenye lengo la kwamba kwa sababu sekta hii ina husisha makundi mbalimbali kama ambavyo yamekuwa yakijadiliwa tangu pale mwanzoni. Ustawi wa sekta hii unahitaji wafugaji, ustawi wa sekta hii unahitaji pia wakulima wa mazao, ustawi wa sekta hii unahitaji pia wavuvi na watu wengine wote

ambao wataweza kuorodheshwa kulingana na shughuli zao mbalimbali wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati tukiwa tunazingatia maslahi ya kila kundi, lakini maslahi ya Taifa ndiyo yatayotakiwa kupewa nafasi kubwa zaidi. Kwa hiyo, tunajipanga katika kuzingatia zaidi maslahi ya Taifa kwa sababu maslahi ya Taifa yanazidi au yanavuka ukomo wa umuhimu kwa mahitaji ya makundi moja moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaya fikaje maslahi ya Taifa? Sisi kama nchi tunayo *vision*, tuna dira; dira yetu ni dira ya 2025. Ukitoma dira utakutana na masuala yote yanayohusiana na uhifadhi, utakutana na masuala yote yanayohusiana na tabianchi kwenye dira ile, tuna kawaida ya kusoma kwa kwenda kwenye *search engines* na kusoma mambo ya mataifa mengine lakini natoa wito tusome pia na nyaraka ambazo ni za kwetu tulizoziaandaa wenye we na nyingine tumeziandaa humu Bungeni au kuziidhinisha, tusome *vision* lakini pia tuangalie namna ambavyo tunaweza tukasoma mipango tuliojiwekea kwa mfano, tuna mipango ya miaka mitano mitano, tuna mipango ya kila mwaka, lakini pia tunayo Katiba yetu, tunazo sheria, tunazo kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa tumeshakubaliana juu ya yote hayo na hasa tunapokubaliana juu ya sheria, kanuni, taratibu na miongozo, basi wajibu wetu baada ya pale hatuna uchaguzi isipokuwa ni kufuata na kutii. Pale ambapo tunaona kwamba kuna sababu yoyote ile ya msingi ya kuweza kubadilisha au kufanya marekebisho kulingana na wakati au kwa sababu nyingine yoyote tutakayoona inafaa, basi tunapaswa kufuata utaratibu ule ule na kuweza kufanya marekebisho ya sheria au hata kufuta kabisa sheria kwa sababu taratibu zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja kubwa ambayo imebeba mjadala au imefanya mjadala wa Bunge jana na leo uweze kuwa mzito zaidi, watu wamechangia kwa hisia mbalimbali, watu wamechangia wengine baadhi yao kwa jazba tunawasemehe, lakini nataka nisisitize tu kwamba suala la migogoro ya ardhi, migogoro ya mipaka limebeba uzito mkubwa. Napenda niseme kwamba Wizara kwa kuzingatia pia andiko ambalo limeandikwa na Wizara ya Ardhi na ambapo nimekwenda kuchukua takwimu kama ifuatavyo tunaweza kutoa jibu moja tu hapa ambalo ni la mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba kwanza tuna jumla ya migogoro 281 kwa kadri ambavyo takwimu zimekusanya na Wizara ya Ardhi, lakini miongoni mwa migogoro hiyo; migogoro ambayo inahusu hifadhi ni migogoro 35 tu ambayo hii ni asilimia 12.5. Mikoa inayoongoza kwa migogoro ambayo inahusiana na hifadhi na Mikoa yote inayoongoza kwa migogoro yote kwa

ujumla ni Kagera, Mara, Tanga na Tabora ambayo inabeba karibu asilimia 50 ya migogoro yote. Mkoa wa Tabora ambao wenyewe ni wa nne kwa idadi ya migogoro kwa ujumla yenyewe migogoro yake asilimia 40 ni migogoro ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudie hapa sasa baada ya takwimu hizi hoja ya Mheshimiwa Profesa Muhongo kwamba tatizo siyo eneo, tatizo siyo ukubwa wa ardhi na mimi tayari nilikwishaliona hilo kupitia takwimu hizi zilizokusanywa na Wizara ya Ardhi kwamba Mkoa wa Tabora ambao ni mionganini mwa mikoa minne yenyewe maeneo makubwa lakini ambao una asilimia 40 ya migogoro inayohusiana na hifadhi ndiyo unaoongoza kwa kuwa na eneo kubwa nchini. Tabora wana kilometra za mraba 760,151.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzoni tutakachofanya sasa hivi ni kuhakikisha kwamba migogoro yote hii sasa Wizara zote zinazohusika zinakwenda kukaa kwa sababu tayari tuna agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusiana na kushughulikia migogoro hii. Wizara zote sita ambazo naweza kuzitaja hapa haraka haraka ni Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maliasili na Utalii, TAMISEMI, Wizara ya Maji, Wizara ya Nishati na Madini lakini pia Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) wote tunakwenda kukaa pamoja kwa ajili ya kwenda kushughulikia migogoro yote kwa ujumla. (Makofij)

Kuhusu migogoro ya ardhi nimekwishamaliza kwa namna hiyo. Lakini nzungumzie ujangili kidogo kwa sababu muda umeshakimbia sana. Masuala yote yaliyotajwa kuhusu ujangili kwanza tumeunda chombo kipyka kinachoitwa TAWA (*Tanzania Wildlife Authority*), Mamlaka ambayo inakwenda kuchukua maeneo ambayo yanahusiana na uhifadhi wa mbuga za wanyama zile ambazo zipo nje ya zile zilizopo chini ya TANAPA na Ngorongoro. TAWA inakwenda kuboresha zile mbuga ambazo zilikuwa hazina uongozi wa pamoja kama ilivyokuwa TANAPA na Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake sasa sekta ndogo ya wanyamapori inakwenda kuwa bora zaidi, inakwenda kuboreshwa zaidi baada hasa kuhusiana na masuala ya uhifadhi mambo yanayohusiana na askari wa hifadhi, tunaanzisha chombo kinaitwa Jeshi Usu ambalo ni *Paramilitary* kwa namna ile sasa tunakwenda kukusanya kwa namna bora zaidi ya kuweza kuboresha mapato ili tuweze kushughulikia zaidi maadili ya askari hawa, mmetaja mambo mengi yanayohusiana na matendo ambayo yasiyofaa ya ukosefu wa maadili, kuyataja moja moja muda hautoshi kama mnavyoona, lakini kwa kuanzisha Jeshi Usu tunakwenda kuimarishe zaidi maadili, nidhamu lakini pia tunakwenda kushughulikia zaidi pia maslahi ya hawa askari, *incentives* zao, lakini pia tunakwenda kuwafanya waweze kuwa manageable zaidi kuliko ilivyo sasa. Kwa hiyo, kwa njia hii tunaweza kuondoa changamoto nydingi zaidi

zinazohusiana na ujangili kwa maana ya eneo hili. Yapo mengine mengi lakini kwa sababu muda hautoshi labda pengine naweza kuishia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii, kila mmoja amezungumza hapa juu ya mapungufu kwenye sekta ya utalii na kwamba kunahitajika uboreshaji. Wanazungumzia vivutio vipyta, kwanza kuboresha vivutio vilivyopo pia kwa kubuni vivutio vipyta, lakini pia kutangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe taarifa kwenye Bunge lako Tukufu kwamba katika ziara zangu nilizofanya kwenye baadhi ya Wilaya nimetoa maelekezo na huu ndiyo msimamo wa Wizara kwamba vivutio vyote vinavyoweza kuorodheshwa kwenye vivutio vya utalii nchini, Wilaya zote tunakwenda kuziagiza ziweze kuorodhesha kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wanasema hapa, waende wakashirikiane na Halmashauri zinazohusika waorodheshe kwa sababu tunakwenda kuandaa directory ya vivutio vyote vinavyoweza kuwa na sifa ya utalii nchini na ambavyo sasa tutaweza kuvi-market kwa maana ya kuvifanya utangazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia miundombinu mbalimbali kwenye maeneo ya utalii. Ni kweli lipo suala la miundombinu ndani ya hifadhi zenyewe kwa maana jinsi ya kuweza kutembelea hifadhi, masuala ya hotels mle ndani lakini pia kuna suala la miundombinu ambayo inakufikisha kwenye hifadhi zenyewe kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Sasa huku upande ambako tunazungumzia miundombinu ambayo inakufikisha kwenye hifadhi, kama barabara, Wizara hii haifanyi kazi peke yake, tunakwenda kushirikiana na Wizara inayohusika, inayoshughulika na mambo ya ujenzi pamoja na mawasillano na mambo yanayohusiana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la *Southern Circuit*, (Utalii wa Kusini). Tuna mradi mkubwa sana unaitwa REGROW (Mradi wa Kuboresha Utalii Kusini) wa makusudi kabisa chini ya Benki ya Dunia wenye dola za Kimarekani zaidi ya milioni 210. Tunakwenda kufanya vitu vingi sana. Kwanza kuboresha vivutio vyenyewe, lakini pia kwenda kuzitambua mbuga, hifadhi na vivutio vingine vyote vilivyo katika ukanda wa kusini ili kuwe na maana ya circuit kweli kweli, kwa sababu mtalii akifika sehemu moja aweze kupata value for money, kwa sababu anaweza kutembelea zaidi ya kivutio kimoja kwa wakati mmoja kwa sababu ya ukaribu na vitu kama hivyo. Ndani kuna viwanja vya ndege vya ndani ya hifadhi na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema muda hautoshi, nakwenda mbio lakini nataka kusema kwamba wote ambao wameguswa na suala la kuimarisha utalii ukanda wa kusini, nataka kuwaambia kwamba Serikali tayari ina mpango mahsusini kwa ajili ya hilo.

Pia hata kuhusiana na vivutio, tumekuwa na vivutio vya aina iliyozoeleka, wanyama; na Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema hapa. Ukweli ni kwamba tunakwenda sasa kuimarisha utalii wa kihistoria, utalii wa kiutamaduni, utalii wa starehe labda (*leisure tourism*), zote hizi ni aina tofauti za utalii ambazo tunakwenda kuziboresha kwa kutekeleza miradi mbalimbali, lakini kwa mipango mbalimbali ambayo kulingana na wakati na kulingana na jinsi fedha zitakavyopatikana tunaweza kwenda kuufanya utalii ukawa bora zaidi kuliko hivi sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, dakika 35.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda niwashukuru sana ndugu zangu mnaotutia moyo. Napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Chama changu na Wabunge wa Upinzani. Tangu jana hapa hoja zilizotolewa, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, unaweza kuziita very constructive. Zilikuwa hoja nzuri sana za kujenga. Zilikuwepo chache ambazo zina miiba, miiba, ndiyo ubinadamu, lakini hoja ambazo zimetolewa hapa kwa kiasi kikubwa zimetujenga, nasi tunatoka hapa tukiwa tumejjamini zaidi katika kazi ambayo tunaifanya ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inafaidika zaidi na maliasili ambazo tunazo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge 90 wameleta michango yao kwa maandishi. Na mimi nawaheshimu na ninawashukuru sana. Nimesoma michango ile, kama ingesemwa hapa, pangkuwa na hewa nzuri zaidi, maana ilikuwa ni michango mizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuongea hapa Bungeni ni Waheshimiwa Wabunge 55; kwa kweli hii ni faraja kubwa sana na muda kama mlivyoelezwa, siyo rafiki sana. Nitajaribu kutoa majibu kwa upana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Makamba, Mheshimiwa Profesa Muhongo, Mheshimiwa AG na wengine wote ambao mmetusaidia katika kujibu maswali kwa utangulizi mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi, maliasili zetu na sisi wanadamu na wanyama na viumbe vingine vilivyo chini ya group kubwa la wanyama, tunaishi na mimea yetu kwa mtindo unaoweza kuuita *symbiotic*, yaani tunaishi kwa kusaidiana. Bila rasilimali zetu hizi za maliasili, tusingweza kuishi na bila sisi, hizi

rasilimali zisingekuwepo. Ninaposema sisi, nina maana ya sisi binadamu na viumbe wote ambao wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maliasili zetu za misitu na nyuki, wanyamapor na utalii zinatuwekea mfumo wa ikolojia ambao ndiyo unakuwa muhimili mkubwa wa maisha yetu. Hewa tunayotoa sisi kama hewa chafu ili tuweze kuishi inavutwa na majani na kutumika kuzalisha chakula cha majani. Mimea yetu, miti na mimea mingine ndiyo chanzo kikubwa cha kurekebisha mvua yetu, kurekebisha joto katika dunia.

Katika Tanzania, Mwenyezi Mungu ametujalia, tumekuwa na aina tofauti sana, nyingi za mimea na viumbe wengine ambazo zinapatikana Tanzania peke yake na hazipatikani mahali pengine popote duniani na ndiyo maana tuna msingi mkubwa wa utalii kupita nchi zote duniani ukiacha Brazil. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ambayo ndiyo uhai wetu yanatoka kwenye misitu yetu na hifadhi zetu nyingine. Maji haya ndiyo tunayotumia nyumbani, ndiyo tunatumia kwa kilimo cha umwagiliaji, tunazalishia umeme kwa miaka mingi katika nchi yetu na ndiyo inaendesha viwanda vyetu. Maliasili hizi tumeelezwa hapa mara nyingi, ni msingi mkubwa wa pato letu la Taifa na zinatuletea asilimia 25 ya fedha zote za kigeni tunazopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia hapa na Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri, kwamba tuna mradi wa zaidi ya dola milioni 200 wa kujenga misingi ya utalii Kusini mwa Tanzania. Tutaviboresha viwanja vya ndege, tutabioresha barabara kutoka kwenye viwanja hivyo mpaka kwenye hifadhi zetu na kwa sababu hiyo, wale ambao wamepisha Ruaha ili iwe mbuga yetu kubwa, waliopisha Kitulo, waliopisha Katavi wakae mkao wa kula, maana tunatengeneza mradi ambao utabioresha utalii katika maeneo haya ambayo yana sifa nzuri sawa sawa au hata kuzidi hizi mbuga nyingine ambazo tunazitumia kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya matatizo makubwa ambayo tunayo katika kuboresha utalii Kusini mwa Tanzania, ni bei ya tiketi za ndege. Kutoka Arusha mpaka Kigoma dola 1,800 kwenda na kurudi kwa dola 1,800 unaweza kutoka Dar es Salaam ukaenda New York na kurudi. Kutoka Dar es Salaam kwenda Mpanda; kutoka Dar es Salaam kwenda Iringa ni ajabu bei za ndege zilivyo kubwa.

Kwa hiyo, hatua ya kwanza ambayo tunachukua, tunaanzisha vituo vya kuzipa ndege mafuta katika viwanja hivyo vya ndege ili kuhakikisha kwamba hakuna kisingizio kwamba lazima tutue Tabora kwanza, tutue Dodoma kwanza ndipo twende, kwa hiyo, ni lazima bei ipande. Pia tumeishauri Serikali inunue

ndege ndogo kama hizi Fokker Friendships ambazo zinaweza ku-service viwanja vyetu hivi ambavyo ndiko watalii wetu watakapokuwa wanakwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi zetu ndiyo kiini cha utalii wetu na zinalindwa kwa sheria kama ambavyo tumesema na kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mmetueleza, mmerudia; Sheria ya Wanyamapori hasa sehemu ile ya 18(2), Sheria ya Misitu na Sheria ya Mazingira. Sheria hizi zinatutaka tulinde, tuhifadhi na tuendeleze maliasili zetu. Hizi siyo sheria za kwanza ambazo zinatulazimisha tuangalie shughuli zetu; wote tunajua watu ambaao wamejenga kwenye hifadhi za barabara katika maeneo mengi nchini kwetu wameondewa na hata bila fidia kwa sababu wameingilia hifadhi ya barabara na watu ambaao wamejenga kwenye mabonde. Kwa hiyo, siyo mara ya kwanza kuhakikisha kwamba tunasimamia Sheria za Uhifadhi kama ambavyo zimetungwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niliambia Bunge lako Tukufu kwamba japo nchi nyininge za jirani zina sheria na zinavyozitekeleza zinakuwa za imla sana; kwa mfano, nchini Kenya ukiingia kwenye Hifadhi ya Taifa na huna sababu ya kuwa hapo, wanapiga risasi bila kukuuliza swali na nchini Botswana, hivyo hivyo. Nchini Tanzania hatuwezi kufanya hivyo, hata kama tunaingia kwenye matatizo ambayo wakati mwingine tunakuwa nayo.

Kwa hiyo, nimesikiliza kwa makini na nimesikia kwamba wafanyakazi wa wanyamapori, wafanyakazi wa misitu na walinzi wa hifadhi zetu wakati mwingine wanakuwa na roho mbaya sana. Wanapiga raia, hatukuwatuma kuwapiga raia; wanapiga mifugo risasi, hatukuwatuma kupiga mifugo risasi. Pia hatukuwatuma kuchoma nyumba za watu; hatukuwatuma kuwaumiza watu. Kwa hiyo, Wizara yangu itachukua hatua kali pale ambapo tutathibitisha kabisa kwamba askari alipiga watu, tutamchulia hatua kali sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, baada ya kikao hiki cha Bunge, tutawaita wahifadhi wote tuangaliane kwenye macho, tuelezane tabia nzuri ya kufuata huko kwenye hifadhi zetu na wale ambaao hawatafikia kiwango cha weledi tunachokitaka, tutakapobadilisha hili Jeshi la Uhifadhi hatutawaingiza kwenye *Paramilitary Force* ambayo tunaijenga. Tutapeleka wale tu ambaao wana weledi na uaminifu wa kutosha wa kuhakikisha kwamba Watanzania wamewaaajiri ili walinde maliasili zetu, lakini hawakuwaaajiri ili wawapige, wawaumize, wapige risasi ng'ombe zao au wapasue nyumba zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mjadala ambaao umeendelea hapa, nimeelewa kwamba katika maeneo mengi bado wakulima wanavuna mazao yao. Kwa sababu hiyo, ninawaomba wenzangu huko, Wakuu wa Mikoa kwamba wasiwabughudhi watu wakati wanapovuna mazao yao; na hivyo

wawaache hao ng'ombe kwanza mpaka watu wamalize kuvuna ndipo watekeleze agizo la Waziri Mkuu ambalo amelitoa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala ambalo lisememwa hapa la huyu mtu anayeitwa *Green Miles Safari* ambaye alifutiwa leseni, akafutiwa na vitalu vyake vyote; kwa nini Serikali imemrudishia leseni na kitalu chake?

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Bunge lako Tukufu likajua kwamba katika eneo la Natron kabla ya mwaka 2011 kulikuwa na vitalu viwili; *Natron North* na *Natron South*; na kwamba baada ya kuweka tathmini katika vitalu hivi, vitalu vile vilionekana ni vikubwa sana na kwa hiyo, vikagawanyawa tukatoa vitalu vinne. Majina yake siyo muhimu, lakini moja ya hicho kitalu kilipewa *Green Miles* na kingine akapewa *Wengert Windrose Safaris*. *Green Miles Safari* ni Mwarabu na *Wengert Windrose* ni Mmbarekani. Kwa hiyo, siasa za Kimarekani na Kiarabu zimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule Mmarekani aliyejewa na hicho kitalu chote kikubwa alisema eneo alilopewa *Green Miles* ndilo eneo zuri zaidi na yeye amewekeza zaidi hapo, kwa hiyo, hataki kuondoka. Anataka abaki na hicho kitalu chake hata kama hakupewa na Serikali. Idara ya Wanyamaporimejaribu kusuluhisha jambo hilo ikashindwa. *Wengert Windrose* akaenda Mahakamani kupinga jambo hilo kisheria. Kabla kesi hiyo haijamalizika, ikatolewa DVD hapa ambayo inaonesha watu waliokuwa wanawinda katika kitalu kimoja cha *Green Miles* huko Selous, siyo *Lake Natron*; huko Selous walifanya makosa na kuwinda kinyume na kanuni za uwindaji zilivyowekwa. Wale wote ambao mtapenda kuiona hiyo DVD tutakuwa tayari ku-share tuwaoneshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ile DVD kuoneshwa hapa, Mheshimiwa Waziri aliongea na vyombo vyaa habari, akasimamisha leseni, akasimamisha na vitalu vyote vyaa *Green Miles Safaris*. Tarehe 30 Machi, 2015 Mahakama ikaamua, ikasema kitalu alichopewa *Green Miles* ni haki yake. Mahakama Kuu ya Tanzania sehemu ya biashara, ni haki yake, kwa hiyo, aruhusiwe kuendelea na kazi yake.

Kwa hiyo, ukiangalia ile Sheria ya Wanyamaporimifungu cha 38(12)(c) ndiyo inayompa Waziri mamlaka ya kugawa vitalu, lakini pia mamlaka ya kumnyang'anya mtu kitalu. Hata hivyo ukiangalia ile mamlaka ya kunyang'anya kitalu inasema; "Waziri hatamnyang'anya mtu kitalu kama mtu huyo hakuonekana ana hatia na Mahakama ya Tanzania." Sasa huyu mtu hakuonekana ana hatia na Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulichofanya ni kutekeleza sheria na kutekeleza maamuzi ya Mahakama yetu. Kwa hiyo, hakuna jambo ambalo limefanyika hapa ambalo halikufanyika kwa utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huyu bwana, alirudishiwa kitalu chake na amerudishiwa leseni ya kuwinda. Hata hivyo, wale wafanyakazi wa Serikali walioshiriki na wafanyakazi wa Green Mile Safaris na kuonekana kwenye ile DVD, tunaandaa utaratibu na charges tumeshapeleka kwa DPP ili waweze kufunguliwa mashitaka kwa kosa la kuwinda kinyume cha Kanuni. Sasa huwezi kwenda kumnyonga baba kama mtoto wake ndio ameua mtu. Kama mtoto wake ameua mtu na ni mtu mzima, yule mtoto ana-face makosa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niongee kidogo kuhusu TANAPA. Nawashukuru sana wengi ambao mmewapongeza TANAPA kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Napenda pia niseme, sentensi moja moja kwamba, Serikali haichukui mapato ya TANAPA na kuyaweka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, kilichobadilishwa ni TANAPA na mashirika mengine yote ya umma, zile akaunti zake zote za makusanyo, zinafunguliwa Central Bank. Kwa hiyo, wakishapokea pesa kwenye Commercial Bank, ile Commercial Bank ina-transfer mapato yale kwenye Central Bank. Wakifanya matumizi, wanachukuwa fedha kule kwenye Central Bank na kutumia kama kawaida. Cha muhimu ni kutaka kujuu kwa uhakika mashirika haya yote tulionayo, mapato yake ni kiasi gani, yanatumikaje na kwa wakati gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya madawati ya thamani ya shilingi bilioni moja, ambayo ni madawati 16,500, ambayo tulimkabidhi Mheshimiwa Makamu wa Rais wiki iliyopita, yametoka kwenye bajeti ya TANAPA ya Corporate Social Responsibility, siyo kwamba tumechukuwa fedha za mipango ya kazi ya TANAPA na kutengenezea madawati, hata kidogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda *at this juncture* nieleze kidogo kuhusu haya madawati yote ambayo yatabolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Shirika la TANAPA limechangia madawati 16,500, katika Wilaya 55 na kila Wilaya itapata madawati 300 ambayo yatakaliwa na wanafunzi 300 mara tatu; na hizi ni zile Wilaya zinazozunguka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, imechangia madawati 2,000 katika Tarafa ya Ngorogoro yenyе thamani ya shilingi milioni 140 na itatoa madawati mengine 10,000 kuchangia Mfuko wa Madawati wa Wizara; TFS itatoa madawati 20,000 na kutoa meta za ujazo za magogo 15,000 za misitu kama mgao maalum kwa kikosi cha Magereza na madawati mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zitaruhusiwa kuyanunua kutoka kwenye mashamba yetu mbalimbali bila kutoa mrahaba, lakini kulipa asilimia 25 ya mrahaba kwa ajili ya fedha zinazotakiwa katika kurudishia kupanda miti katika meneo hayo yatakayokatwa. Jumla ya madawati 168,500 yataolewa na haya yana uwezo wa kukaliwa na wanafunzi 505,050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niende kwa haraka katika suala la concession fees. Ni kweli kwamba mwaka 2007 nilipokuwa Waziri wa Maliasili na Utalii tulitangaza concession fee ya kitanda dola 50. Baadaye watoa huduma wakakataa mchango huo, wakaenda Mahakamani mwaka 2007 na mwaka 2008 ndiyo Mahakama ikahamua. Kwa hiyo, kilichotokea hapo katikakati, Mahakama ilikuwa haijaamua. Sasa hivi tunangojea Bodi ya TANAPA ikamilike kuteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya TANAPA ni tofauti kabisa katika kuunda Bodi na sheria nyingine. Wizara imefanya inayotakiwa kufanya na tunangojea hatua ya mwisho ya kukamilisha uteuzi huo na baada ya uteuzi huo, Bodi itapitia concession fee mpya na ikishapitia tutai-gazette na kuanza kutumika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine liliosemwa hapa na nafuu niliseme linahusu *lodge* ya Mikumi. Tender ilishatangazwa, mjenzi ameshapatikana na tunangoja mjenzi huyo ajikusanye, aanze kujenga *lodge* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wabeba mizigo, wapishi na waongoza misafara katika Mlima Kilimanjaro; Wizara ya Kazi, Wizara ya Maliasili tulikutana na Vyama hivi na wale wenyewe wanaohusika, wakatengenezeana mkataba wa malipo na tukaweka msimamo. Wale watoa huduma, lazima wawalipe wale wabeba mizigo, wapishi na waongoza misafara kabla hawaajaanza kupanda mlimani na wasiwarushe pesa zao. Kwa hiyo, tunangoja tuone utekelezaji unavyokwenda na hivi sasa wana mikataba na bei ya kupanda ni dola 10 kila siku kwa mbeba mizigo; dola 15 kila siku kwa mpishi, nadhani na dola 30 kwa mwongoza msafara. Kwa hiyo, hilo liko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mlima Kilimanjaro ni kweli kwamba kuna uchafu sana katika njia ya kupanda na njia zote zile. Suala la kutengeneza vyoo na maeneo mengine ya kupumzika liko mikononi. Tender ya Kimataifa ilitangazwa ili kupata vyoo ambavyo vinageuza kinyesi kiwe vumbi (*powder*) ili kupunguza uchafu kule juu ya mlima. Kwa sababu vyoo vyenyewe vinavyotakiwa ni vingi na bei ya kuvijenga vyote ni zaidi shilingi bilioni moja, ilitangazwa Kimataifa na tender ilikwishatolewa kwa Kampuni ya Korea ya Kusini, lakini Bodi ikija, Mwenyekiti ndio atasaini hiyo. Maana tender ya zaidi ya shilingi bilioni moja ni lazima isainiwe na Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kuliongelea hapa linahusu Watanzania wanaopewa ruhusa wenyewe au kampuni zao kufanya biashara ya wanyama hai. Wanyama hai wanaoruhusiwa kwa sasa, baada ya ile scandal ya kubeba twiga ndani ya ndege na kusafirisha nje ya nchi, wanyama wanaohurusiwa sasa ni *primates* hawa wadogo wadogo; nyani, tumbili na hawa wanyama wadogo, aina ya kenge, *reptiles*, ndege aina mbalimbali pamoja na wadudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeonekana kila siku tunapata taarifa ya Watanzania kusafirisha Wanyama nje ya nchi bila utaratibu; bila vibali, bila ruhusa, bila kitu chochote. Wanyama wanakamatwa Hong Kong, Thailand, *Eastern Europe*, wanakamtwa kila mahali! Hawa waliokamatwa na tumbili juzi, siwezi kusema jambo hilo kwa sababu liko mahakamani, lakini limefikishwa mahakamani kwa sababu kuna ushahidi kabisa kwamba walikuwa wanafanya michezo. Halafu wanyama hawa wanaosafirishwa nje, hata wale ambao wanakatazwa na conference of parties, wanapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna jina chafu huko kwa sababu ya watu ambao wanapeleka wanyama hai bila utaratibu. Hakuna utaratibu mzuri uliowekwa kuhakikisha kwamba tunaweza kudhibiti biashara hata hii biashara hii ikaipatia Taifa pesa, wale tumbili walikuwa wanapelekwa *for medical research*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anayekuja kupeleka wale wanyama wala hafanyi *declaration* ya aina yoyote kwamba wale wanyama wanakwenda kutumika kwa ajili gani? Kama wanaenda kutumika kwenye zoo, unaweza kuelewa; hawana faida kubwa sana ambayo unaweza kusimama imara ukasema hakuna ruhusa kupeleka; lakini wengine wanapelekwa kwa ajili ya utafiti wa dawa. Kwamba huyu nyani ni jamii ya mtu, tukitumia dawa ya namna hii kutibu hiki, inaweza kuponya au haiwezi kuponya? Tutumie kiasi gani? Tumtibu kwa muda gani ili huu ugonjwa upone? Dawa ikipatikana, ile kampuni inapata *billions of dollars* na sisi tunabaki na nyani aliyeuzwa kwa dola 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuanzia leo hivi nilivyosimama hapa, ninasimamisha kwa muda wa miaka mitatu usafirishaji wote wa wanyama hai kutoka Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, wanyama wakubwa, swala, pundamilia, twiga, hawakubaliwi, lakini bado wanasafirishwa, bado wanaibiwa, kwa hiyo, tunasimamisha. Hata chawa wa Tanzania hatasafirishwa nje ya Tanzania. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha miaka mitatu, Idara ya Wanyamapori itajipanga na kuweka utaratibu unaofaa ili Serikali ikiangalia na wenyewe unafaa, ndiyo biashara hiyo iweze kuruhusiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo la Sao *hill*. Muda hauko rafiki sana, lakini mradi wa misitu ya kupanda wa Sao *Hill* ulianzishwa kwa minajili ya kujenga kiwanda cha karatasi. Wakati umeanzishwa, ulianzishwa pia mradi wa kujenga kiwanda cha karatasi pale Ruvu, Kongowe. Kiwanda kilipangwa kijengwe Morogoro, unapoingilia Mto Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi ule wa Ruvu ulikuwa umepangwa kwa pine ile ya Caribbean ambayo haikuweza kukua katika mazingira yale. Pine ilioanzishwa kule Sao *Hill*; pine ya Ellioti iliota na kukua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya magogo kukua, kiwanda cha Sao *Hill* kikajengwa kama Kiwanda cha NDC, SU (Shirika la Umma). Tulipoendesha kikatushinda, tukakuza kama ambavyo sasa kinamilikiwa na mtu binafsi. Sasa wakati tunacho kiwanda chetu, mi-pine ambayo tulikuwa tunatumia ya miaka 14, hiyo ndiyo inatumika kuzalisha paper, ndiyo kawaida, dunia nzima! Unaangalia ule mti, uone wakati ambao fiber ile ya kutengenezea paper ni ndefu kupita wakati wote; na kwetu hapa Tanzania, pale Sao *Hill* ni miaka 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, miti ile ya miaka 14, haifai kupasua mbao. Ndiyo maana wao walikuwa na mkataba na Serikali wa kuuziwa miti ile ambayo ni michanga na midogo ambayo huwezi kupasua mbao kwa shilingi 14,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, actually mwaka 2007, ukiangalia bajeti ambayo tulisoma hapa, yale magogo ya kutengeneza karatasi yalikuwa yanauzwa shilingi 1,700. Tuli yapandisha bei hapa mwaka 2007, ndiyo ilifika hapo; na magogo yale ya kupasua mbao yalikuwa shilingi 18,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mtu aliyenunua kiwanda hicho, naye alinunua kwa lengo lile lile, kutengeneza karatasi. Kile kiwanda ambacho kilijengwa pale na NDC, kilijengwa kutengeneza *craft paper*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango iliyokuwepo ni kwamba kile ambacho kitajengwa pale Bagamoyo, ndiyo kitamalizia *craft paper* kuwa karatasi hii nyeupe ambayo tunatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana unaona yanayotokea pale. Kwanza wamepewa bei ile ya chini ya pulp na bei hiyo ni tofauti na wale ambao wanatengeneza mbao. Kwa sababu bei ya paper na mbao ni tofauti

kabisa. Ukiwa na kiwanda cha karatasi kinachonunua magogo kwa bei ya timber, hakiwezi kuza karatasi barabarani, ndiyo jambo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilichotufikisha pale ambapo wanatumia magogo makubwa kama wale wanaopasua mbao, ni ule muda uliotumika kuanzia tuliposhindwa kukiendesha mpaka tulipopata mwekezaji. Ile miti yote ambayo ilikuwa kwa ajili ya kuzalisha paper, ikawa imekuwa magogo makubwa, lakini hakuna eneo kubwa zaidi ambalo lilipandwa.

Kwa hiyo, ile yote ikawa lazima igawanywe, nyingine itengenezwe paper kwa bei ya *paper and pulp* na nyingine itengeneze mbao na ndiyo sad story ya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa cha muhimu wananchi wa Mufindi, Njombe, Mbeya na Morogoro mpande miti kwenye mashamba yenu. Pale Sao Hill penye kuna *four thousand hectors* ambazo wananchi wanaweza kupanda miti yao. Mpande miti ile, ikiwa midogo, mnaweza kuiiza kama *pulp and paper*, lakini mkiacha ikiwa mikubwa mnaweza kujikwamua kiuchumi kama Mheshimiwa Mbunge wangu wa Viti Maalum alivyosema kwa uchungu sana na mimi namuunga mkono. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kuwapa Miche bure ili muweze kupanda miti katika eneo lote hilo na mjitegemee hapa badaye, mijkwamuwe kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme kwamba suala hili la migao ambalo limelalamikiwa hapa, na mimi nimelalamikiwa. Nimesema mgao mpaka kwanza tuupitie ule utaratibu wake na ndiyo tutatoa mgao. Mwaka huu hakuna mgao mwezi wa sita na labda hata mwezi wa saba hautatoka mpaka tumejua namna ya kuugawa vizuri. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, una dakika mbili tu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa bado nina karatasi nyingi hapa, lakini muda ndiyo umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kifungu 1001 – Administration and HR Mgt.....Sh. 3,720,187,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilishapewa majina ya Vyama, nina majina ya CCM, CHADEMA na CUF. Tunaanza na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Serikali inayoteklezwa na Wizara hii ya Maliasili na Utalii ime-introduce kodi ya kitanda katika Tangazo la Serikali Namba 324, tarehe 14 Agosti, 2015. Kwa kuwa sheria hii inatekelezwa kwa maeneo ya Pwani, nikizungumzia Rufiji, inawataka wananchi wangu kulipia kodi ya kitanda ya shilingi 120,000 kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 13(4) inayozungumzia ubaguzi na Ibara ya 13(5) inayotoa tafsiri ya neno ubaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi hii ya kitanda haijatoa tafsiri ya nini kitanda na ni nani anapaswa kulipia kodi hii ya kitanda? Iwe ni Mtanzania wa Rufiji umekilalia kitanda miaka 20, miaka 30, ukitoka nacho sehemu moja kwenda nyingine, Maliasili wakikukamata unalipia kodi ya shilingi 120,000; iwe mfanyakazi wa Serikali unayehama kutoka Rufiji kwenda Kibiti, kutoka Rufiji kwenda Dar es Salaam, unapaswa kulipa kodi hii ya kitanda ya shilingi 120,000. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi hii ni baguzi na ninaomba unipe ridhaa ya kusoma Ibara ya 13(5) kuonyesha ni namna gani Serikali imeamua kuwabagua wananchi wa Jimbo langu la Rufiji kwa ku-introduce kodi hii ya kitanda. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchengerwa, samahani, una simu umeweka hapo karibu na microphone yako?

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Hapana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ya neno ubaguzi limetafsiriwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 13(5) ikimaanisha kwamba kutimiza haja kwa kuwabagua watu kutokana na kabile lao, mahali wanapotoka, maoni yao ya kisiasa, rangi, dini, hali yao ya maisha ili watendewe tofauti na Watanzania wengine. Kodi hii utekelezaji ni Rufiji na Serikali imedzirisha mageti zaidi ya 20 ili kuwakandamiza wananchi wa Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, vinginevyo nitasimamia haki ya wananchi wangu wa Jimbo la Rufiji, Kibiti na maeneo mengine ya Mkoa wa Pwani na nitatoa shilingi kutokana na hili. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ipo tozo ya kitanda katika Wilaya za Rufiji, Kisarawe, Mkuranga na hata Mheshimiwa Mariam Kisangi alii taja huko kwenye eneo lake la kule Temeke. Hii tozo inatozwa kwa vitanda ambavyo vimetumia mbao ambazo hazikufuata utaratibu wa kuzipata zile mbao kule kwenye...

**MBUNGE FULANI:** Umejuaje?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Ngojeni basi. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tozo ambayo ilikuwa ni shilingi 8,000 sasa ni shilingi 120,000. Shilingi 8,000 imepanda mpaka shilingi 120,000, hii haikubaliki.

Kwa hiyo, tutaiangalia hii tozo kwa sababu hailingani na hali halisi ya eneo lile na tutaiipunguza ili isizidi shilingi 20,000. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wenzangu tusaidiane kuwahimiza hawa watu ambao wana viwanda vidogo wapate malighafi kwa kutumia utaratibu wa kawaida uliowekwa. Wasiende misituni na kuchukua mali bila kufuata utaratibu na kuwa na leseni ya kufanya kazi hiyo. *The bottom line*, hiyo tozo kubwa namna hiyo tutaiondoa na haitakuwa zaidi ya shilingi 20,000. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shilingi ili Waheshimiwa Wabunge wawzeze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Endelea, wengine kaeni, ye ye mwenyewe ndiyo anatoa mchango wake. (Kicheko)

**MHE. MOHAMED O. MCHENERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 30(5), inatoa maelekezo kwa taasisi zetu pamoja na Mahakama ya Tanzania kuondoa sheria kandamizi, sheria baguzi, sheria ambazo zinakinzana na Katiba. Kodi hii kuwekwa kwa wananchi wa Jimbo la Rufiji ni ubaguzi wa hali ya juu. Tafsiri ya neno ubaguzi nimeizungumza katika Ibara ya 13(5), ikimaanisha kuwabagua wananchi wa Jimbo langu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, misitu haipo Rufiji peke yake katika nchi yetu hii ya Tanzania, yapo maeneo makubwa yenye misitu mikubwa, misitu mingi. Nikizungumzia mfano Iringa kule, lakini hakuna kodi hii, utekelezaji wake haufanyiki katika maeneo yale, tofauti na eneo letu la Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Mheshimiwa Waziri anieleze, je, kodi hii iliwekwa kwa ajili ya kuwakandamiza watu wa Mkoa wa Pwani ili washindwe na wakose haki zao za msingi zilizoainishwa katika Ibara ya 13 mpaka Ibara ya 29 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? (Makofi/Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa Shilingi, ili Waheshimiwa Wabunge wengine waweze kuchangia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, tulia kwanza. Mheshimiwa Ulega; hatuwezi wote tukawatooa Pwani. (Kicheko)

Mheshimiwa Lusinde, Mheshimiwa Tizeba, Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Millya na Mheshimiwa Kuchauka. (Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Ulega.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, bado tuna mjadala mrefu.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ulega.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Niseme kwanza namuunga mkono Mheshimiwa Mohamed Omari Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, kwenye hoja hii na namuomba sana ndugu yangu asiirudishe kwanza shilingi mpaka

kauli ya Mheshimiwa Waziri kufuta kodi hii hapa. Asiirudishe shilingi mpaka kodi hii ifutwe. Maana siyo watu wa Rufiji tu, wale ndugu zangu peke yake, lakini hata watu wa Mkuranga tumekutwa na adha hii kwa kiasi kikubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la ajabu sana watu kutozwa kodi kubwa kiasi hiki na wanatozwa siyo hiyo tu, maana mtu huyu akishalipa kodi hiyo anakwenda kulipishwa na kodi nyingine za kitanda hicho hicho. Imekuwa ni kero kubwa sana. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri wala asisubiri, atuambie hapa leo anatufutia kodi hii ya kitanda.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lusinde!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuunga mkono Mheshimiwa Mchengerwa kwa hoja yake. Hii siyo sheria ya Bunge, iko katika uwezo wa Waziri, ni kanuni ndogo. Kwa hiyo, hata Mheshimiwa Waziri anaposema anapunguza kutoka sijui laki na ngapi hadi shilingi 20,000, hii inaonyesha Waziri hakumsikia sawasawa mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoa hoja amenekuu Katiba kwamba tozo ile inakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri, badala ya kupaka mafuta, aifute moja kwa moja tozo hiyo tuweze kuendelea. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tizeba.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia namuunga mkono Mheshimiwa Mchengerwa katika hoja yake hii, kwa sababu kodi hii ni hizi kodi kandamizi kama niliyoisema jana kwamba watu wanatozwa square metre moja, wavuvi wanalipishwa shilingi 74,000. Hizi ni kodi ambazo ziko katika kanuni za Waziri na siyo sheria ya Bunge. Kwa hiyo, kama alivyosema Mheshimiwa Lusinde hapa, hizi kodi jana nilimwombwa Mheshimiwa Waziri azifute na leo narudia, zifute tu Mheshimiwa Waziri, zitatupaka matope sana Chama chetu. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Milly, ajiandae Mheshimiwa Heche.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi kandamizi zote nchi hii hazikubaliki. Mtoa hoja amenekuu Ibara ya 13 na ya 14 - haki ya kuishi; wakati jana Mheshimiwa Waziri akiwasilisha hoja yake kwenye Bunge hili aliwabagua wafugaji. Kwa hiyo, mara nyingine...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Milly!

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni kwamba kabla hujatetea haki yako, tetea na watu wengine. Kwa hiyo, akikumbuka kwamba...

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. JAMES K. MILLYA:** No, no, no! Issue ni kwamba Wakili ni mbaguzi, lakini kodi hiyo Mheshimiwa Waziri aifikirie kwa sababu kodi kandamizi na unyanyasaji kwenye nchi hii haikubaliki hata kidogo. Yeye mwenyewe aangalie mikono yake kama ni safi, aendelee kuleta hoja hiyo ya msingi anayoileta. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Heche, ajiandae Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Waziri, watu wamezungumza na umesikia. Haya maumivu wanayopata watu wanaochajiwa shilingi 20,000 ni makubwa zaidi ukiua ng'ombe wetu mmoja.

**WABUNGE FULANI:** Eeeeh!

**MHE. JOHN W. HECHE:** Kwa hiyo, mimi nafikiri, hakuna sababu ya kuzomea...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, order please!

**MBUNGE FULANI:** Wanazomea kule!

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kuna nia njema hapo kwa Serikali kutunza misitu, kwa sababu wamesema ng'ombe anaharibu misitu. Ng'ombe haharibu misitu wowote, wakataji hawa ndio wanaharibu misitu. Kwa hiyo, nilichokuwa nasema ni vyema ikawekwa njia nyingine ya kuzuia hawa wasikate miti, lakini kodi kwa wananchi maskini kuwawekea shilingi 20,000 hizi ziondoke na ng'ombe wetu mhakikishe hamuwaui. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi nataka niende moja kwa moja kwamba namuunga mkono Mheshimiwa Mchengerwa aliyetoa hii hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa sababu hii kodi imebagua, ni Kilwa Road peke yake ndiyo hiyo kodi ipo. Sasa sijaelewa kwa nini imewekwa kwa ajili

ya watu wa Kilwa Road tu. Halafu isitoshe, kule tuna vijana ambao wanajijiri na wanachukua mikopo wanatengeneza vitanda na nini, hatuwezi kununua kitanda pale ukaja nacho Dar es Salaam. Kwa hiyo, wale wanakosa soko kule. Kwa hiyo, tunadidimiza uchumi wa watu wa kule. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri hii kodi aiondoe, kwa sababu kwa nini haipo nchi nzima? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, kubali yaishé. (Kicheko)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu viwili; cha kwanza hii ni *government notice* ambayo inahusu Jamhuri ya Muungano yote, siyo *government notice* ya Kisarawe, Rufiji na Mkuranga peke yake, hata kidogo. Hizi bei ambazo zimebekwa hapa ni kwa Tanzania nzima. Kwa hiyo, huwezi kusema kwamba *government notice* imebagua watu; hata kidogo, hiyo moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimesema hapa kwamba hii *Punitive Levy* iliyopandishwa kutoa shilingi 8,000 mpaka 120,000 ni kubwa sana. Maana kuna utaratibu wa kutengeneza hizi, huwezi kutoa tangazo tu hivi ukasema nimefuta, maana yake ni Serikali. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kitu ambacho naweza kusema hapa ni kwamba tutaiangalia hii *government notice* na tunatoa *commitment* ya kuiangalia vizuri Serikali nzima. Ninasema hapa mbele ya Serikali yote, tutaiangalia vizuri na kuiweka kwa *level* ambayo haiwezi kumuumiza mlaji mdogo. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Safi sana. (Makofi)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Hii Mheshimiwa Mchengerwa, naomba urudishe tu hiyo shilingi maana nitashughulika na hii. *I give you my commitment and I will do it.* (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waziri wa Katiba na Sheria, Kaimu Waziri Mkuu, *commitment!* (Makofi)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri napenda tu nisisitize kwamba kwanza hii GN siyo *unconstitutional*, hapana, kwa sababu haimuonei mtu wa sehemu moja tu, ni kwa nchi nzima. La msingi hapa, Waziri pamoja na Serikali nzima tumeona kwa kweli hii tozo imepitwa na muda wake. Tutaiangalia, *this is the commitment tunai-make* hapa kwamba tutaiangalia, lakini hatuwezi tukatamka hapa kuifuta GN, ina procedure yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni *commitment*, naomba mniangalie machoni, mumwangalie Mheshimiwa Profesa Maghembe machoni, tutaishusha, tutaibadilisha hii na nina uhakika wote mtaikubali. Ahsante. (Makofi/Kicheko)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mchengerwa. *Commitment* ya Serikali ndiyo hiyo na wewe ni Mwanasheria, procedure za sheria unazifahamu. (Makofi)

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza naomba ndugu zangu watambue, vinginevyo wapitie hotuba yangu ya jana, mimi sikumzungumzia mfugaji kwa ubaya wowote, hilo ni moja. Nilichofanya ni kutoa tafsiri za kisheria ambazo zimekuwa zikikiukwa katika nchi hii, hicho ndicho kikubwa nilichokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametoa *commitment* na ameliahidi Bunge hili kwamba suala hili litashughulikiwa haraka, basi naomba *commitment* hiyo iletwe ndani ya Bunge hili baada ya kushughulikia suala hili na ninarudisha shilingi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Cosato Chumi!

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri kuhusu *Sao Hill*, hoja yangu nilizungumzia kuhusu MPM. Ni kweli kabisa shamba la *Sao Hill* lilipandwa kwa madhumuni aliyoyleza Mheshimiwa Waziri, lakini MPM wanauziwa nusu ya bei, kama nilivyosema katika mchango wangu. Nikasema kwamba kama hawa wanauziwa nusu ya bei ambayo as of now tunapoteza kiasi cha 2.8 billion; hizi fedha ukienda kwenye hii karatasi tuliyogaiwa ambapo TANAPA wametoa shilingi bilioni moja kwa ajili ya madawati, tumepata madawati 16,500. Hii 2.8 billion tungeweza kupata madawati 46,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *but not only that*, kwa muda ambao wameuziwa nusu bei kuna loss Serikali imepata karibu shilingi bilioni 15, tungeweza kupata madawati 247,000. Sasa nia yangu, kama sitapata maelezo mazuri naomba kutoa Shilingi katika suala hili. *Unless otherwise na watu wetu wauziwe nusu ya bei kama MPM.* (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kutoa jibu ambalo haliendani na ule utaalam wenyewe wa misitu. Nimeeleza kwamba magogo yanayotengenezea *pulp* na yale ambayo ndiyo yanatengeneza karatasi ni tofauti na magogo yale ambayo unatengenezea mbao yaani sawn

timber na kwamba ukitengeneza karatasi kwa bei ya mbao utafunga tu kiwanda hicho, hakitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba bei ya magogo yale ambayo yanauzwa pale *Sao Hill* ukachukua ile bei ya shilingi 28,000 ukagawanya kwa 2,100 ambayo ndiyo dola ya sasa; na magogo haya yanauzwa kwa pulp ama kwa timber bei ni karibu sawa, ni *the same* dunia nzima. Utakuta kwamba cubic meter moja ya *sawn timber*, hii ya mbao ni kama dola 12; na katika soko la dunia cubic meter moja ni dola 20 mpaka 25. (*Makofii*)

Kwa hiyo, bado mbao zetu kwa bei hiyo ya kupasua mbao iko chini sana, lakini pia vijiji ambavyo vinafaidika na bei ya chini sana ya mbao ile ambayo wanapewa kama huduma ya Shirika lile kwa vijiji ni fedha nyingi sana. Ukikubali Mheshimiwa Mwenyekiti naweza kuisoma, nina page tano hapa ya idadi ya vijiji ambavyo vimepewa zaidi ya shilingi bilioni mbili.

**MWENYEKITI:** Hiyo utamsomea baadaye. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii napenda baadaye nimpe Mheshimiwa Mbunge. Misitu hii iko *Sao Hill* kweli lakini ni kama mgodi wa Watanzania wote. Hawa ambao tunawapa fedha hizi zote wanakaa pale, wanaulinda ule msitu, moto ukiwaka wanazima na ndiyo maana huduma yote hii inatolewa pamoja na *five percent cess* ambayo inatolewa kwenye Halmashauri za Mafinga na Mufindi. (*Makofii*)

Kwa hiyo, namuomba sana rafiki yangu akubali hali hii kwamba siyo faida yetu sisi kama Taifa kufunga kile kiwanda cha karatasi na kwamba bado mbao zile tunapeana na kupasua kwa bei ya chini sana na wewe unajua pia kwamba wale watu wanaopewa kibali, wakishapewa kile kibali tu, wakigeuka nyuma tayari wameshalipwa hela yao ambayo wanahitaji, wala hawahangaiki kwenda kukata huko.

Kwa hiyo, ninyi mna bahati hii ya kuwa na shirika hili pale, linatoa misaada mingi kwa Wilaya zenu na Halmashauri zenu. Tumuombe Mungu shirika hili liendeleee, lakini pia nimesema Wizara yangu itaendelea kuvipa vijiji miche ya kupanda, wapande wenyewe miti ya *Eucalyptus* unapata boriti hii ya umeme kwa miaka sita mpaka nane hii ya pine kwa miaka 20 unaweza kupata mbao ukauza.

Kwa hiyo, tuweke juhudhi, tutawapa haya magogo mwendelee kukata kwa miaka 10 au 15 ijayo, lakini ni vizuri kwamba na ninyi wenyewe mjitegemee na mwendeleeze upandaji wa misitu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umeeleweka. Nakushukuru sana, ahsante. Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sipingani na Mheshimiwa Waziri kuhusu *social responsibility* ambayo shirika linafanya, ni wajibu. Tumeona hapa Mheshimiwa Muhongo akiwasilisha hotuba yake, watu walioko kwenye madini wanapata hizo huduma na kadhalika. *It's corporate social responsibility, sipingani naye. Hoja yangu ya msingi, there is a lot of huge amount ya pesa kutokana na nusu ya bei kwa MPM.* Sasa labda Mheshimiwa Waziri tukubaliane. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hiyo miti, ni kweli umri wa miaka mpaka 12 au 14, vyovoyote vile ambavyo Mheshimiwa Waziri anaona, je, yuko tayari pia na sisi wavunaji? Kwa sababu kama na wao watauziwa nusu bei, itakuwa pia siyo *loss* kama ambavyo siyo *loss* kwa MPM. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani sisi tunamwonea huruma mwekezaji; *well and good analipa kodi na kadhalika, lakini hata hao wavunaji pia wanalipa hizo kodi. But good enough, hii ardhi sisi tumetoa.* Jana nilisema, mimi babu yangu alikuwa *sub-chief tume-sacrifice hundred of acres.* Kwa hiyo, lazima tuwe beneficiary. Kweli msitu ni wa Taifa, sipingani na hilo, lazima u-benefit Taifa lakini na sisi pia tuwe beneficiary wa kwanza. (Makof)

Kwa hiyo, kwenye hili naomba kutoa hoja na naomba Waheshimiwa Wabunge muweze kunielewa na kuniunga mkono. Nimetaa tu hesabu ndogo, fedha hizi zinazopotea kwa mwaka mmoja tungepata madawati 46,000, ukichukua hii hesabu ya TANAPA. Naomba kutoa hoja, naomba mniunge mkono. (Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chumi, kaa kwanza. Mheshimiwa Waziri amekueleza kwamba mbao zinazotumika kwenda kwenye kiwanda cha karatasi ni tofauti na mbao zinazouzwa kwenye *furniture.* Kwa maana hiyo, hesabu zako ziko sahihi na sisi tunakubaliana na wewe; lakini Serikali inapata revenue kwenye makaratasi, kwenye eneo lingine na ndiyo hicho anachokwambia Mheshimiwa Waziri.

Sasa unaweza ukatoa hoja, tukapiga kura, hoja yako itakufa humu ndani. Mimi ninachokuomba, nakusihi nakubali hoja yako ni ya msingi, kaa na Mheshimiwa Waziri akupe orodha ya vijiji, tazameni njia gani ya kupata muafaka ili baadaye sasa mjue kwa siku za mbele ni kitu gani, wewe na yeze na vijiji vyako vita-benefit. Nakuomba nakusihi sana Mheshimiwa. (Makof)

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo yako hayo, tumetoka mbali llala kule nikiwa ofisi ya DC pale, naomba kwa heshima hiyo nipate tu *commitment* na hilo ulilolisema. Najua wataalam na watendaji wa Wizara wako hapa, Mheshimiwa Waziri akubali kukutana na sisi Wabunge tunaotoka eneo lile *immediately* tujadili hili suala. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari kabisa kukutana na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Iringa kujadili jambo hili. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda nipate majibu ya kina kwa ninachoenda kukiongelea, nisiporidhika nitatoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba ujangili kwenye nchi yetu umekithiri na ulipelekea siku ya tarehe 4 Oktoba, 2013 Serikali ikaunda kikosi maalum na wakakipa jina la Operesheni Tokomeza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua yaliyojiri kwenye Operesheni Tokomeza. Target ambayo iliundiwa kile kikosi haikufanyika, badala yake walienda kupiga wananchi ambao wanaishi kando kando na zile hifadhi. Wananchi walinyanyaswa na walidhalilishwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishuhudia baba amekaa pemberi na mama mtu yupo anaambiwa afanye tendo la ndoa na mti. Tukashuhudia Bi Emiliana wa Babati na kesi ilikuja hapa, tukashuhudia Peter, kaka yangu wa Mrito alipigwa akawa anachomwa chomwa na vitu vya ajabu na picha nafikiri Mheshimiwa Heche amezileta. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua yale maazimio ya Bunge yametekelezwa kwa kiwango gani, ikiwepo fidia? Wananchi wamelipwa fidia zao kama ambavyo walitamka hapa? Ni kiasi gani mmetekeleza kulipa fidia kwa wale waliofiwa, familia zikawa affected kisaikolojia kwa wale ng'ombe ambao mliwaua, punda sijui mbuzi kondoo; wananchi wanaenda sokoni wanakutwa barabarani wanatobolewa bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua government commitment, wamelipwa fidia kiasi gani mpaka sasa hivi; hiyo status? Nisiporidhika, nitatoa shilingi. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri na AG.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri na nimeshauri hapa hili Bunge Tukufu tena kwa ufasaha kabisa.

Kwanza, Serikali imeji-commit, iliunda Tume ile ya Uchunguzi ikafanya kazi, ikatoa ripoti. Mheshimiwa Rais, ametoa maelekezo kitu cha kufanyiwa kazi na nimewasomea hapa. Kwa sababu inafanyiwa kazi, haiwezi ikawa public, haiwezi kuletwa hapa. Kwanza hiyo haikuwa Tume ya Bunge, ni Tume ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sitaki kwenda mbali, kwa sababu kulikuwa na maelekezo hayo, ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wavute subira, la sivyo hatutaki kurudi kule nyuma tukasema kwamba aah, hili suala limepita na uhai wa Bunge lile lingine. Kama wanataka, walilet kwa hoja mpya. Hatutaki kufika huko, kwa sababu kuna Tume ya Rais ambayo ilifanya kazi na Serikali inalifanya kazi. Sasa kama ni mambo ya uchunguzi, leo huwezi kwenda Mahakamani ukapeleka ripoti ya ile Tume. Mahakamani unapeleka statement iliyoandikwa na Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ripoti imeona hiki, Mheshimiwa Rais akaelekeza hapa kuna watu itabidi wachukuliwe hatua za kisheria, wengine walipwe fidia na kadhalika na kadhalika kwa mujibu wa maagizo yake pale. Kuna kazi inafanyika kule.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwashauri, tuliache hili suala, Serikali ilifanyie kazi hatimaye mtaona matokeo yake. Mnachoking'ang'aniza hapa, *at the end of the day* ni kuharibu hata huo uchunguzi na hakuna kitakachofanyika.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Matiko, nakuheshimu sana na naomba kwa sababu hayo mnayoyasema unawezaje kuyathibitisha? Kwa sababu ni issue za picha. *How can you prove this, that this picture emanates from the allegation?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana naomba kushauri, Waheshimiwa wawe na subira, waipe fursa Serikali ifanye kazi, hili lilikuwa ni Azimio la Bunge. Naomba kuhakikisha kwa sababu haya mambo ni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye aliyependekeza ndani ya Bunge hili Tukufu kwamba iundwe pia mbali ya mapendelekezo yale ya Kamati Teule ya Bunge, pia liongezwe pendelekezo, ni azimio lingine kwamba iundwe Tume ya Uchunguzi? Sasa Tume ya Uchunguzi ndiyo itakayokuja kuleta justice hapa Waheshimiwa Wabunge, naomba mvute subira. Kwa hiyo, ndiyo ushauri ambao naweza kuutoa mbele ya Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko, ushauri huo.

Mheshimiwa Matiko kaa kwanza, kulikuwa na issue mbili; kulikuwa na Kamati ya Bunge na baadaye Mheshimiwa Rais akaunda Tume. Tume ya Rais kwa mujibu wa sheria siyo lazima iwe *public, unless yeye mwenyewe atake iwe public*. Ameshatoa maagizo Serikalini hatua zichukuliwe. Sasa anachokuomba uwe na subira. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa masikitiko makubwa sana and *it can only happen in Tanzania; only in Tanzania!* Leo Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kaka yangu unasema nini? Ina maana hata Kamati ya Bunge iliyoundwa ikatembea Tanzania nzima, ikashuhudia yaliyotendeka, leo hata yule Bi. Emiliana wa Babati, yule mama, mnasem *it's a matter of picture*. Leo ndugu zetu wa wameteswa na wana ushahidi upo. Leo huyu baba na picha mmepewa; where is my picture? (Makofii)

Leo huyu baba mnasema *it's a matter of picture*; huyu marehemu aliyeseswa hivi, kudhalilishwa, what? Mmemtesa hivi na familia yake imenyanyasika, leo mnasema *it's a matter of picture*. We are not serious. Ninachosema, kwenye hili Bunge ndiyo tuliazimia tukasema pia na Mheshimiwa Rais aunde Tume, akaiunda hiyo Tume, imetoa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kama kweli Rais Mstaafu Mheshimiwa Kikwete, aliyejewa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaweza akachukulia mambo easy, asifanye *implementation* eti wanasesma ushahidi, mnafanya uchunguzi wa muda gani? Naomba nitoe hoja, Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono maana yake siyo Mara tu, ni Tanzania nzima. Wale asilimia 30 waliokuwa hapa Bunge lililopita mlisshuhudia picha za Kamati, leo Serikali mnasema nini? Naomba kutoa hoja mniunge mkono. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Haya. Mheshimiwa Paresto, Mheshimiwa Bulaya, Mheshimiwa Albeto, Mheshimiwa Gekul, Mheshimiwa Anatropia, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa AG na Mheshimiwa Kairuki.

Waheshimiwa Wabunge, naongeza nusu saa kwa mujibu wa Kanuni. Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja ya Mheshimiwa Esther.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yanayotolewa na AG katika Bunge hili kuhusu hili la Operesheni Tokomeza hayawezhi kuvumilika hata kidogo. Hizi familia zimeteseka na ninamshukuru Mheshimiwa Esther amekumbuka na familia

za Babati; mpaka leo wale watoto hawana pa kwenda. Serikali iliahidi humu ndani italipa fidia baada ya Azimio la Bunge. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati tulimbana Mheshimiwa Waziri na kama hoja ni Tume ya Mheshimiwa Rais, ilishatoa majibu. Pesa zilizotoka ni shilingi bilioni saba za kuwalipa askari waliokaa mwezi mzima kule wakati wamestopishwa kwenye operesheni, wananchi wa kawaida pesa zao hazipo. Ni kwa nini Serikali mnadanganya Bunge hili ilhali mkijua pesa za askari shilingi bilioni saba mmezitenga, askari walioua watu wetu mnawalipa, wananchi wetu hamuwalipi? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti tutakuwa Wabunge wa namna gani kama tunawalipa watu waliotesa watu wetu shilingi bilioni saba lakini wananchi wetu hawalipwi! Hili halikubaliki na Mheshimiwa Waziri usitudanganye; ultunganya kwenye Kamati kwamba fedha za fidia za watu hawa ziko kwenye Mfuko wa Hazina Kuu. Waziri wa Fedha yupo atuambie ni kiasi gani kwa ajili ya kulipa watu wetu, vinginevyo msituchezee humu ndani, tupeni majibu. (Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Albeto.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kweli inahuzunisha sana katika *level* ambayo tumefikia. Tungetarajia katika jambo hili tungepata huruma ya Serikali kwa raia wake, kwa sababu mambo haya yametokea na sisi ambao hatukuwepo Bungeni tulikuwa tukiona kama yaitokea. Nasikitika kumwona AG anataka kwenda katika excuse ya kwamba yale yalikuwa ni maamuzi ya Bunge lililopita na kwa hiyo, haihusiani na Bunge hili. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndiyo naona Serikali kwa kiasi gani hata pale tulipotetea kwamba Tume ya Haki za Binadamu iongezewe fedha, basi haikuungwa mkono. Kwa hiyo, nafikiri kuna haja ya jambo hili kutolewa suluhu, nchi yetu inaharibika kwa mambo ya haki za binadamu kama ambavyo yamefanyika Zanzibar hivi karibuni. Kwa hiyo, tunasema haya ili kuisaidia Serikali kujenga taswira nzuri, tusiharibu jina letu. Tumalize hili wananchi wapate haki zao, ili nchi iende salama. Ahsante. (Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kairuki.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokisema Mheshimiwa AG, nianze labda na hoja ya kuhusiana na picha. Picha tumeionta hapa. Alichokisemea siyo kwamba ameikania, ila alichosema, huwezi kuthibitisha tu kwa picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko hatua mbalimbali zinaweza zikafikia mpaka kuweza kuthibitisha. Wanasheria wanalelewa hilo; halina ubishi na sidhani kama kuna haja ya kuweza kubishania hilo. Tayari picha imeletwa hapa na ninaamini kuna michakato mbalimbali.

Mheshimiwa Heche alisema ataipeleka mezani, sijajua kama aliipeleka au laa. Kama imefika kuna utaratibu wake na kwa kuangalia kwa macho hapa hapa huwezi ukasema kilichotolewa hapa ni kweli na kama kweli kimefanyika au laa. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Tume ya Operesheni Tokomeza, tayari utekelezaji umekwishaanza katika ngazi mbalimbali. Tulijionea hapa wako viongozi wa kisiasa ambao tayari walishawajibishwa; lakini vilevile katika watumishi wa umma ambao imethibitika kwa mujibu wa Tume ile, pia na wenyewe wameweza kuchukuliwa hatua, tuendelee kuomba kama ambavyo AG amesema tuvute subira, utekelezaji utaanza. Ukitisema ripoti ya Tume ile uiletete hapa leo hii, kwa kweli haitawezekana kwa sababu aliyeiunda haikuwa ni Bunge hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwigulu.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza jambo hili tunaloliongelea ni jambo ambalo Wabunge tulikubaliana na Serikali ikapokea; na kwa kuwa Serikali ilishapokea na Tume ile ikaundwa, kilichokuwa kinafuatia sasa hivi baada ya kazi ya Tume kuwa imemalizika ni utekelezaji wake.

Kwa hiyo, kile ambacho Mheshimiwa AG amesema cha kumwombwa Mheshimiwa Mbunge avute subira, ni sahihi kabisa kwa sababu kwa mazingira ya sasa ambayo ndiyo Serikali mpya imeingia madarakani, nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge wa-take commitment kwamba yale ambayo tayari Tume itakuwa ilipendekeza yatafanyiwa kazi kwa sababu moja ambalo linatupa uhakika, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, kwanza ameshasema na amewaambia Watanzania na ametupa maelekezo wasaidizi wake kwamba hatataku kuona manyanyaso yanatokea kwa wananchi wasio na hatia kama ilivyokuwa imetokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa commitment hiyo hiyo, na kwa huruma hiyo hiyo, kwamba amewahurumia watu waliopata mateso na hataki yajitokeze ya aina hiyo; kwa maana hiyo, yale ambayo yameshakuwa proven na yameshatolewa mapendekezo na Tume yatafanyiwa kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili tunalolisema la kuvuta subira ni kwa sababu hatuwezi tukafanya kazi hiyo hapa kwa muda huu. Ndiyo essence ya kusema kwamba tuvute subira ili kile ambacho kilikuwa kinastahili kiweze kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo ambayo naomba Waheshimiwa Wabunge waridhie.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu. (Kicheko)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namuomba Mheshimiwa Matiko aelewé kwamba suala aliloliletá hapa hatujalichukulia kiurahisi, ni suala zito, limewagusa Watanzania. Ni Watanzania walioumia na wewe mwenyewe unaelewa kabisa mapendekezo yaliyotolewa na Tume tulishaanza kuyatekeleza. Kuna watu wameshawajibika kisiasa; na sasa kinachoendelea ni sehemu ya pili ya wale wale watu ambao hawako katika nafasi za kisiasa ni kuchunguza kuhusu *responsibility* yao na hilo litafikishwa tu hatma yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sidhani kama *solution* ni leo hii wakati wa bajeti ya Mheshimiwa Maghembe ndiyo upate *solution* yote, hapana! Ni *commitment* ya Serikali kwamba hili suala tunalifikisha kwenye hatima yake. Tunashukuru kwamba ume i-raise hapa kwa nguvu sana, tunalielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kusema zaidi ya hapo, ni kwa sababu tayari tuko kwenye mchakato as *government* kwamba kuweza kuhakikisha kwamba hili suala tunalifikisha kwenye hatma yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko, nakusihi, najua una hoja *valid*, lakini kuna watu wamefanya makosa Vita Kuu ya Pili, ya Kwanza mpaka leo wanasakwa. Karibu Mheshimiwa Matiko. (Kicheko)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza kabisa nasikitika kwamba wote waliosimama kwa upande wa Serikali hawajanibu hoja yangu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyouliza *in particular* nilitaka nijue fidia, *status* ya fidia kwa wananchi. Wenyewe wanakurupuka wananiambia mambo ya ripoti ya Tume ya Rais. Nilipoomba siku ile, nilisema azimio mojawapo la Bunge, Tume ya Rais ilipendekeza fidia, nikataka nijue *status* sasa ya fidia, lakini wenyewe wananiambia kwamba watu wanawajibika kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisiasa waliwajibika humu humu kabla ya Tume ya Rais kuundwa, Mawaziri wale walioondoka kabla ya Tume ya Rais kuundwa. Kwa hiyo, Tume ya Rais so far, *there is no any implementation that has been done.* (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sirudishi shilingi, ninachotaka kujua ni fidia ya watu wetu walioleteseka, wakauawa mifugo ikauliwa vibaya. Nataka nijue hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi; na kuhusu hii picha ya Mheshimiwa Heche, kwa kumbukumbu tu, siku nachangia hapa, miaka mitatu nyuma, Mheshimiwa Angellah Kairuki ulikuwepo, nilitoa hii picha ya huyu baba aliyeuawa na kuteswa. Kwa hiyo, you could have taken measures since then.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua shilingi bado. Hii ndiyo ile contradiction hata Serikali leo Mheshimiwa Maghembe ameonesha hapa kuhusu Green Miles, wale walinyang'anywa leseni kwamba uwindaji mbovu; leo unawarudisha ruhusa ya court, ndiyo contradiction. Kwa hiyo, naomba niingie kwenye kumbukumbu na Bunge hili amba maeneo yenu yote siyo kwamba ni Upinzani tu waliathirika, wananchi wa Tanzania wote waliteseka. Tupige kura kwamba hawataki kuona wananchi walionyanyaswa wanalipwa fidia kwa yale madhara waliyoyapata. Ila nataka kuona wale waliotumika kuwauwa ndugu zetu wanapewa seven billion shillings na wale walionyanyaswa hawalipwi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba twende kwenye shilingi, wafanye maamuzi. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi ndio nimempa nafasi Attorney General. Mimi ndiye ninaye-control kikao. Hoja ya Mheshimiwa Matiko haijafungwa.

**MBUNGE FULANI:** Tulieni ninyi.

**MWENYEKITI:** Haijafungwa! Mheshimiwa AG, kuna commitment ya Serikali?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, commitment naomba...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, subirini basi! No, no, no, subirini kwanza. Mheshimiwa Matiko, you will get your day, subiri. Mheshimiwa AG.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge wanisikilize vizuri nilichokisema. Nilisema hivi kwa sababu suala la utekelezaji haliwezi tukaliampilia hapa leo, ni mambo yako kwenye hatua mbalimbali.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niseme nilichokisema kwa kumbukumbu za Bunge. Nilisema hivi, baada ya kupokea ile taarifa ya Tume, Rais alitoa maelekezo kwa taasisi zote ambazo watendaji wake wamethibitisha kutenda makosa au kukiuka sheria au taratibu zote za utekelezaji wa Operasheni Tokomeza, kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuzifanya marekebisho sheria na kanuni zilizopendekezwa kufanyiwa marekebisho. Maelekezo ya utekelezaji wa mapandekezo hayo kwa taasisi na vyombo vya umma husika, yamewekewa muda maalum wa utekelezaji. Hatua hizo zimechukuliwa na zimeendelea kuchukuliwa kama ilivyoelekezwa na Serikali. (Makofij)

Kwa hiyo, haya anayoyasema Mheshimiwa Mbunge, yatakuwa ni sehemu ya utekelezaji.

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa AG, nimekuelewa. Mheshimiwa Matiko endelea kufunga hoja yako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu nilishaifunga.

**MWENYEKITI:** Basi kaa chini.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Naomba tu uende kwenye shilingi.

**MWENYEKITI:** Kaa chini.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** AG amerudia yale yale aliyoysasema mwanzo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kaa chini.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Hajatoa solution yoyote ambayo inaweza ikanishawishi vinginevyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wabunge, sasa...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Naomba uende kwenye shilingi ili wananchi wajue nini kitakuwa mwisho wa hatma yao.

**MWENYEKITI:** Sasa kaa chini basi Mheshimiwa Matiko.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

**MWENYEKITI:** Haya tunaendelea.

**MBUNGE FULANI:** Siyo.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigola.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ndiyo utaratibu wa kura, wachache mnasema, wengi wanapitisha. Mheshimiwa Kigola.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwenye hotuba yangu jana wakati nachangia hoja, nilimuomba Mheshimiwa Waziri kwamba katika ile hela aliyoitenga shilingi bilioni sita kwa ajili ya kusaidia jamii, naomba angalau atenge hata shilingi bilioni nne kwa ajili ya madawati. Tanzania nzima tuna shortage kubwa sana ya madawati katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwombwa Mheshimiwa Waziri kwamba katika ile shilingi bilioni sita, ukisoma amesema ni kwa ajili ya matayarisho ya makaratasi, machapisho na vitu kama vile; lakini kwa mwaka huu tungeachana na machapisho, shilingi bilioni tano tupeleke kwenye madawati ili tuweze kusaidia watoto wanaokaa chini. Sasa nilimuomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe jibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu; commitment ya madawati!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisoma hapo, commitment yetu ya kutoa magogo ambayo yataweza kuzalisha madawati 168,000; ambayo yatahakikisha kila Wilaya Tanzania nzima maana misitu hii ni ya Watanzania wote ipate madawati 1000. Huu ni mchango wa TFS.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kutakuwa na maombi mengine ya Wilaya na tumeshaanza kupata, kwa mfano, tumepata maombi kutoka Wilaya ya Tarime ambayo tayari tumeyapa mgao; na Halmashauri nyingine ambazo zitataka magogo au mbao kwa urahisi wanaweza kuleta maombi kama ambavyo walileta Wilaya ya Tarime Jimbo la Profesa Muhongo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kigola, peleka maombi.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Waziri ni mazuri, na sisi Wilaya yetu ya Mufindi tutaleta maombi. Sasa naomba tukileta maombi yetu yapokelewe. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tangu tumeanza kujadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri kumekuwa na hoja kubwa na nyeti kwa Taifa juu ya suala la mapato ya Serikali ya Tanzania yanayotokana na fedha za mjusi aliyepo Ujeruman. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais anayeongoza Taifa hili kwa sasa, kama nilivyoeleza wakati ninachangia, alitoa commitment kubwa sana alipokuwa kwenye Jimbo la Mchinga kwamba atahakikisha fedha zinazotokana na mjusi zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kushangaza, kumekuwa na sintofahamu na kuna usemi unasema kwamba nani atamfunga paka kengele? Mheshimiwa Muhongo amelieleza hili, sijajua alitolea maelezo kama Waziri wa Nishati, ama kwamba suala hili liko kwenye Wizara yake; lakini nilionesta utata wa majibu ambayo niliyapata kutoka kwenye Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, nilijibiwa hivi hivi. Kwa hiyo, ni danadana ambazo zinaendelea; na Mheshimiwa Muhongo ameendeleza danadana la namna gani Serikali ya Tanzania inakosa mapato kutokana na fedha za mjusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala sikusudii kutoa shilingi kwa sababu najua kutapigwa kura za ndio na hapana, ninachotaka commitment ya Serikali, ni lini mtamaliza kufanya calculation, maana majibu niliyojibiwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, ni kwamba mpaka sasa hamjafanya calculation, hamjui Serikali ya Ujeruman inapata kiasi gani? Nisipopata majibu ya kuridhisha...

**MWENYEKITI:** Aaah!

**MHE. HAMIDU HASSAN BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba commitment ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Eeeh! Na wewe usilete danadana tena humu! Mheshimiwa Waziri, commitment!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Muhongo kwa jibu zuri alilotoa, kwa sababu amesema kwa niaba ya Serikali, siyo kama liko Wizarani kwake au liko Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba nchi zote ambazo zilitawaliwa na Ujerumani, ambapo Ujerumani ilichukua vitu vyatuhii wa Mataifa hayo, vilivyoko Ujerumani. Nchi zote tumeanza majadiliano na Serikali ya Ujerumani ili vige vitu ambavyo vinafaa kuletwa, wakati huu viletwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana pia katika hatua hii ambapo tumefikia, kwamba ile Museum ambayo ni ya *natural history*, Profesa aliita Humboldt Museum. Ile museum itasomesha Watanzania watatu na mmoja tayari yuko pale, anafanya utafiti ndani ya ile museum, kwa vitu vilivyoko pale, kujua vyatuhii Tanzania ni vige na vige vinavyoweza kuletwa haraka viletwe. Yule mjisusi ni mkubwa sana ni kiumbe wa kilo zaidi ya sabini.

**MWENYEKITI:** Kilo! Ni tani!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Eeeh, tani zaidi ya 70. It's a big animal! Ni mnyama mkubwa na alichimbwa kutoka ardhini. Kwa hiyo, maeneo mengine yameunganishwa na pop ili iweze kukaa pamoja. Ile mijusi actually wako watano; yuko mmoja mkubwa huyo na mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaendelea na mazungumzo nao na kuendelea kufanya utaratibu ambao utatumika ama kulirudisha, ama kutufidia. Kwa hiyo, ni kazi ambayo tunafanya na siyo danadana. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bobali kwa mujibu wa Kanuni zetu, Waziri Mkuu, Waziri, Mwanasheria Mkuu, wanaweza kujibu swali lolote ndani ya Bunge. Kwa hiyo, alipojibu Mheshimiwa Profesa Muhongo alikuwa ni sahihi na amelijibu sababu amelielewa vizuri na majibu yake ni sahihi.

Mheshimiwa Bobali, hoja yako ni ya msingi, unaweza ukauliza, wakati Serikali imefanya mazungumzo, je, kutakuwa na *retrospective*? Je, *royalty* hizi zitalipwa kuanzia lini? Toka waanze kuzipata wao ili na Tanzania nao wafaidike? Karibu Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri akachukue Hansard ya Bunge; mwaka 2008 ndani ya Bunge hili, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mchinga Mheshimiwa Mudhihiri Mohamed Mudhihir, alimwuliza swali Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wa wakati huo Mheshimiwa Bernard Membe, akajibu ndani ya Bunge hili kwamba Serikali ya Ujerumanu imekubali kujenga Chuo cha Utafiti wa Viumbe katika eneo la Tendeguru kule Mipingo na kwamba Serikali ya Ujerumanu itajenga barabara kutoka pale Mkwajuni mpaka kwenda Tendeguru ambapo mhusi alichukuliwa, mwaka 2008. Nendeni mkachukue Hansard muone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu haya ndiyo maana nasema danadana, Mheshimiwa Membe alijibu kwa niaba ya Serikali, na leo naambiwa ndio kwanza *decision inaanza*, ameanzisha mazungumzo Profesa Muhongo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Membe alidanganya humu? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema hivi, juu ya suala hili kwanza ni aibu. Mheshimiwa Waziri unasi mama unasi fia ukubwa, hivi haujui kama mabilioni ya shilingi yanapotea, Wajerumanu wanachukua, sisi hatunufaiki? (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mbona hatuwi wazalendo?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Hamna taarifa sasa hivi, nani huyo?

**MBUNGE FULANI:** Hii Serikali mpya! (Kicheko)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali endelea.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naomba tuwe wazalendo, tunapoteza fedha! Nimiambie Mheshimiwa Waziri, hivi sasa ninavyoongea kuna Wazungu wanakwenda kule kufanya utafiti; hakuna barabara hata njia ya kuwapitisha, tunawabeba mgongoni tunawavusha kwenye Mto Mbemkulu tunawafikisha kule, hamuoni aibu? Wanakuja kutoka Ulaya kufanya utafiti ili waone alipochukuliwa. Sisi mpaka leo tumelala usingizi tu kwamba tunaendelea kufanya mazungumzo; miaka 55 ya Uhuru! Mheshimiwa

Waziri naomba fuatilia ujibu. Sitoi shilingi, lakini nataka commitment ya nguvu na hili suala mllichukulie very serious tunapoteza fedha. Mimi nimezungumza nao, hayo anayoyasema Profesha Muhongo hayo mengine hatutaki kusema, nina details za kutosha. Ukizihitaji nitakuja kukupatia ili uone wapi kwa kuanzia pia. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri ni kweli, hili suala ni la miaka mingi sana. Alikuwa nalo Mheshimiwa Mudhihir, akaja Mbunge mwingine yule mama akaitwa jina hapa Mheshimiwa Mjusi kwa hili suala. (Kicheko)

Kama kuna hoja hiyo, Serikali ya Ujerumani iko tayari ku-offer vitu hivyo, then you have to work on that. Sasa chukua hiyo Hansard ifuatilie and then wafuate Ujerumani mlete hizo barabara. (Makofi/Kicheko)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaiangalia hiyo Hansard.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Nitafuatilia jambo hilo.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1002 - Finance and Accounts .....Sh. 1,491,330,000  
Kifungu 1003 - Policy and Planning.....Sh. 1,015,860,000  
Kifungu 1004 - Gvt. Communication Unit.....Sh. 303,120,000  
Kifungu 1005 - Internal Audit Unit.....Sh. 415,480,000  
Kifungu 1006 - Procurement Mgt. Unit.....Sh. 516,744,000  
Kifungu 1007 - Legal Unit.....Sh. 378,188,000  
Kifungu 1008 - Mgt. Inf. System.....Sh. 465,240,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 2001 - Wildlife Development.....Sh. 23,825,603,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihoji kifungu kidogo cha 229900 - Other Operating Expenses. Fedha hizi zimeongezeka kutoka shilingi milioni 110 kwenda shilingi milioni 257. Nimesoma kwenye

randama ni kwa ajili ya kuwaongezea hawa askari wanaofanya doria. Sasa naomba tu nisikie commitment ya Waziri kwamba kwenye kitabu cha development pia mmetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya askari hao hao. Naomba tu nifahamu mmewaongezea pesa kiasi hiki, fidia hamjalipa watu wetu, kwa hiyo, mnaendelea kuwaongezea nguvu waendelee kuwaua watu wetu, au tuchukue hizo shilingi milioni 500 na hizi tuwalipe watu wetu fidia?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeeleza hapa kwamba ujangili ni tatizo kubwa sana na tumekubaliana kwamba tuanzishe tower; na katika tower tuanzishe Jeshi Usu (Paramilitary Force) ya kupambana na ujangili. Fedha hizi zitatumika katika kazi ya kuanzisha Jeshi hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 3001 - Forestry and Beekeeping..... Sh. 71,551,162,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 4001 - Tourism Development..... Sh. 9,711,820,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nipate maelezo katika kifungu kidogo 22100 na 221100...

**MWENYEKITI:** Soma kimoja tu kwanza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Fedha za ndani...

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Kifungu 221000 - Travel In Country mmetenga shilingi milioni 526, lakini fedha za safari za nje imetengwa shilingi milioni 54, wakati huku tunatarajia utalii utangazwe kwa nguvu kubwa, lakini inaonekana fedha za nje zimetengwa kidogo kuliko fedha za ndani. Nataka nipate maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kifungu kwa ajili ya safari za nje kimepungua. Jambo la kwanza, huo

ndio mwelekeo sasa hivi wa kitaifa kwamba safari za nje zitakuwa ni zile tu ambazo ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutangaza utalii, bajeti ya kutangaza utalii haipo kwenye Wizara Makao Makuu, bajeti hiyo iko kwenye Bodi ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la mawasiliano, communication and information tunahitaji sasa hivi kuweza kuimarisha zaidi masuala yote yanayohusiana na ujangili, kwa maana ya kukamilisha taratibu za kuwasiliana ili kuweza kupata taarifa kwa wakati ili tuweze kukabiliana na ujangili kwa ubora zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa Kanuni ya 104, tunaingia kwenye guillotine.

Kifungu 4002 - Antiquities Unit.....Sh. 4,656,371,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **Fungu 69 - Maliasili na Utalii**

Kifungu 1002 - Finance and Accounts.....Sh. 0

Kifungu 2001 - Wildlife.....Sh. 8,294,791,000

Kifungu 3001 - Forestry and Beekeeping.....Sh. 8,451,891,000

Kifungu 4001 - Tourism.....Sh. 1,000,000,000

(Vifungu vilivyo tajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

(Bunge lilirudia)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa Hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu likaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja lliaamuliwa na Kuafikiwa)

(Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017 – Wizara ya  
Maliasili na Utalii ilipitishwa na Bunge)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nachukua nafasi hii kwanza kumpongeza Waziri na timu yako na vilevile kupongeza Wabunge wa pande zote, kwa kazi kubwa mliyoifanya humu ndani. Ndiyo Bunge livilyo, wachache waseme, wengi wanapitisha, ndiyo demokrasia. Kwa hiyo, wengine mlion wageni huu ndiyo mchezo wenyewe humu ndani. (Makofii)

Mheshimiwa Waziri hii ni Wizara yako mpya, tunaamini kipindi hiki na Serikali hii itafanya mabadiliko makubwa sana. Utalii unaweza tusijivunie au tukajisifia tuna watalii milioni moja kwa mwaka, wawekee malengo. Nitaiomba Kamati inayohusika mkae na Serikali muweke malengo, angalau tupate watalii milioni tatu kwa mwaka ili tuweze kupata mapato mengi.

Hoja aliyoitaoa Mheshimiwa Albeto ya wachezaji wetu wa Tanzania ambao wana majina duniani, watumiwe na wao kuvuta watalii nchini mwetu. (Makofii)

Hoja ya mifugo na wakulima; tunaitaka mifugo, wakulima na mazingira bora kwenye nchi yetu. Hivi wenzetu wa Ethiopia wamefanya vipi? Ethiopia wana mifugo zaidi ya sisi Tanzania.

Sasa katika fedha hizo za safari za nje, nendeni Ethiopia mkajifundishe, mwone wenzeni wamefanya nini. Kwa hiyo, nawashukuru. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo lingine muhimu, tena nalisema kwa kujivunia, kwa kuipongeza Klabu ya Yanga kuchukua tena ushindi leo, wamewafunga Azam goli tatu kwa moja. Penye ukweli, tutasema ukweli. (Kicheko/Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

**MBUNGE FULANI:** Sema na *birthday* yako!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

(Saa 2.27 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 26 Mei, 2016 Saa Tatu Asubuhi)

